

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 24 Aprili, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI WA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 143

**Ujenzi wa Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Wilaya ya Nyamagana ambayo ni kongwe imeanza kujenga jengo la Wilaya takribani miaka 6 sasa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha jengo hili ili Mkuu wa Wilaya apate mahali pa kufanyia kazi zake kwa uhuru na eneo rafiki hata kwa watu wenye ulemavu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana ulianza katika mwaka wa fedha 2008/2009 chini ya Mhandisi Mshauri Wakala wa Majengo Tanzania - TBA kwa gharama ya Sh.1,836,843,148. Hadi Machi, 2020

kiasi cha Sh.1,714,812,276 kimetolewa na kutumika katika kazi za ujenzi. Ujenzi wa ofisi hii umekamilika na Mkuu wa Wilaya alikabidhiwa jengo tarehe 23/09/2019 na kuhamia rasmi tarehe 01 Oktoba, 2019.

Na. 144

### **Kuzipandisha Hadhi Zahanati za Mji wa Tarime kuwa Vituo vya Afya**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Zahanati nyingi zilizoko Halmashauri ya Mji wa Tarime zimekuwa zikihudumia wananchi wengi kutoka ndani ya Mji wa Tarime na wengine kutoka Jimbo la Tarime Vijijini na Wilaya ya Rorya, mfano Zahanati ya Gamasara iliyopo Kata ya Nyandoto inahudumia wananchi kutoka Kijiji cha Kongo na Kitere vya Wilaya ya Rorya na Vijiji vya Kewamba na Nyangisya vya Jimbo la Tarime Vijijini kwa zaidi ya 50% na zahanati hiyo ina upungufu mkubwa wa watumishi, dawa pamoja na vifaa tiba:-

(a) Je, nini mkakati wa Serikali katika kujenga na kuzipandisha hadhi zahanati hizi kuwa vituo vya afya ili kukidhi mahitaji ya watu wa Tarime Mjini na Majimbo ya jirani?

(b) Je, nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha zahanati hizi zinakuwa na watumishi wa kutosha, vifaa tiba pamoja na dawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali ni kuimarisha huduma za afya ya msingi kwa kuhakikisha zahanati na vituo vya afya vinajengwa kwenye mamlaka za

Serikali za Mitaa ili kuwawezesha wananchi kupata huduma za afya katika umbali mfupi na kupunguza vifo hasa vinavyotokana na uzazi.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imepanga kujenga zahanati tatu (3) katika Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa gharama ya shilingi milioni 150 ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Hivyo, mpango wa Serikali siyo kupandisha vituo vya zahanati kuwa vituo vya afya badala yake imejielekeza katika kujenga zahanati na vituo vya afya katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2019/2020, Serikali imeajiri na kuwapanga watumishi 35 wa kada za afya katika Halmashauri ya Mji wa Tarime. Aidha, OR-TAMISEMI, imepata kibali cha kuajiri madaktari 610 ambao watapangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuweka kipaumbele katika vituo vyenye upungufu mkubwa wa watumishi.

Na. 145

### **Migogoro ya Wakulima na Wafugaji Kilwa**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Wafugaji katika Wilaya ya Kilwa wapo katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa ufugaji ikiwemo Vijiji vya Nakiu, Kikole, Nanjirinji na Kiranjeranje hali inayosababisha migogoro ya wakulima na wafugaji:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kulishughulikia suala hili kabla halijaleta uvunjifu wa amani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kudhibiti uingizaji wa mifugo kiholela Wilayani Kilwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 60 vikiwemo Vijiji vya Nakiu, Kikole, Nanjirinji na Kiranjeranje.

Aidha, limewekwa zuiu la uingizaji wa mifugo kwenye vijiji pasipo kibali kutoka Halmashauri na kuondoa mifugo iliyolingia pasipo kufuata taratibu. Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imekuwa ikitenga fedha ili kufanya mapitio ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Vijiji ambavyo mipango yake iliandaliwa zaidi ya miaka 10 iliyopita ili iweze kuendana na hali halisi ya sasa na kuepuka mwingiliano wa matumizi ya ardhi kwenye maeneo hayo.

Na. 146

### **Kuboresha Vituo vya Afya – Ngara**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Kituo cha Afya Nyamaga kinakabiliwa na changamoto ya miundombinu ikiwemo ukosefu wa jengo la utawala, jengo la upasuaji, jengo la *X-Ray*, jengo la wazazi na mochwari:-

(a) Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuboresha hospitali hiyo ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Ngara haina Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kumaliza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Nyakisasa, Kata ya Nyakisasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za afya Wilayani Ngara kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Machi 2020, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kiasi cha shilingi milioni 690 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya Mabawe, Kiinga na Zahanati ya Nyakisasa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa zahanati tatu (3) katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara utakaogharimu shilingi milioni 150. Serikali itaendelea kuzingatia na kuweka kipaumbele cha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya ikiwemo ukarabati wa Hospitali ya Nyamaga ambayo ndiyo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kadri fedha zitakavyopatikana.

Na. 147

### **Kujenga Kiwanda cha Samaki Kanda ya Ziwa**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Mkoa wa Geita umepakana na Ziwa Victoria na Wananchi wa maeneo hayo hujishughulisha na uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha samaki kwenye maeneo hayo ili kutoa fursa za ajira?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina jukumu la kuweka mazingira wezeshi ili kuwezesha sekta binafsi kufanya shughuli za maendeleo ikiwemo kujenga viwanda. Tanzania ina viwanda kumi na nne (14) ambavyo huchakata samaki wastani wa tani 350.3 kwa siku. Uchakataji huo wa samaki unahusisha Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika. Kwa hivi sasa kuna viwanda vitano (5) Ukanda wa Pwani; viwanda nane (8) Ukanda wa Ziwa

Victoria; na kiwanda kimoja (1) na viwanda vidogo 34 vya kuhifadhi samaki hai Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Samaki wanaochakatwa na viwanda hivyo ni pamoja na pweza, ngisi, kaa, kambamiti na kambakochi (Ukanda wa Pwani), sangara (Ziwa Victoria) na migebuga (Ziwa Tanganyika). Aidha, kuna maghala 33 ya kuhifadhi mazao hayo ya uvuvi yaliyokaushwa na maghala 23 ya kuhifadhi mazao yaliyogandishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuwahimiza wavuvi na wafanyabiashara wa samaki Mkoa wa Geita kutumia fursa za viwanda vya kuchakata samaki vilivyoko Kanda ya Ziwa Victoria na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kujenga kiwanda cha kuchakata samaki nchini ukiwemo Mkoa wa Geita ili kuongeza fursa za ajira.

Na. 148

### **Hitaji la Soko la Ndizi na Viazi Mviringo**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatafuta soko la uhakika la zao la viazi mviringo na ndizi ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda kwa ajili ya mazao hayo katika Halmashauri ya Busekelo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busekelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na uhamasishaji wa uwekezaji katika sekta ya viwanda nchini ili kuongezea thamani mazao ya kilimo vikiwemo viazi na ndizi. Lengo ni kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi na pia kupata mapato zaidi. Katika zao la ndizi, kuna viwanda vya usindikaji vya *Mazimba Company Ltd* na *Matunda Mema Tanzania Ltd* vilivyopo Wilayani Karagwe Mkoani Kagera; Kibo

*Alex Banana Wine Ltd* kilichopo Wilayani Rombo, Mkoani Kilimanjaro; *Kilimanjaro Banana Wine Ltd* na *Lumbugani Banana Enterprises Ltd* vilivyopo Mwanjelwa katika Jiji la Mbeya; *Kasuku Banana Wine Ltd* kilichopo Wilayani Rungwe, Mkoani Mbeya na *Arusha Banana Investment Ltd* kilichopo Jijini Arusha. Hivyo, nawashauri wakulima wa ndizi kutoka Halmashauri ya Busekelo watumie fursa ya uwepo wa soko la viwanda hivyo kuuza mazao ya ndizi katika viwanda hivyo ili yaongezewe thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kituo cha Utafiti cha Uyole imeingia ubia na Serikali ya Uholanzi ili kuleta mbegu mpya za viazi mviringo, mbegu hizo zitaongeza uzalishaji wa viazi. Kwa sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo inafanyia majaribio mbegu hiyo na endapo italeta matokeo chanya, Serikali ya Uholanzi imetuhakikishia soko la uhakika la zao la viazi hivyo. Soko hilo litaleta chachu ya uwekezaji katika eneo la uongezaji thamani kwa viazi vinavyozalishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo na maeneo mengine yanayolima zao la viazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa mazao ya viazi, matunda na mbogamboga yanafikia soko la nje yakiwa na ubora na tija kwa wasafirishaji, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli akiwa ziarani Mkoani Mbeya aliwahakikishia wakulima wakiwemo wa maparachichi kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege na bandari ikiwemo kuweka vyumba vya baridi (*cold rooms*) na maeneo maalum kwa ajili ya uhifadhi na usafirishaji wa mazao hayo. Wizara yangu itaendelea pia kushauriana na wamiliki wa viwanda kuona kama wanaweza kuwekeza huko Busekelo.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo kuendelea na matumizi ya soko lililojengwa katika Kata ya Lupala. Soko hilo linaweza kuwa kiungo muhimu kati ya wakulima, wenye viwanda na wafanyabiashara wa ndizi na viazi mviringo wa ndani na nje ya nchi.



Na. 149

## **Kupambana na Tatizo la Ugonjwa wa Fistula**

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO** aliuliza:-

Tanzania ni moja ya nchi duniani zenye wagonjwa wengi wa Fistula.

Je, Serikali inaweza kutueleza namna ilivyojipanga kupambana na ugonjwa wa Fistula?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fistula ni shimo ambalo hutokea kati ya kibofu cha mkojo na sehemu ya siri (uke) au katikati ya njia ya haja kubwa na uke kwa mwanamke ambaye amejifungua kwa shida ya uchungu pingamizi. Shimo hutokea pale ambapo kichwa cha mtoto ni kikubwa kuliko njia ya uzazi. Fistula inasababishwa na kusukuma mtoto wakati wa kujifungua kwa muda mrefu bila usaidizi au matibabu yoyote na anachanika katika njia ya uzazi na kusababisha shimo, hivyo husababisha uvujaji wa haja kubwa au mkojo bila kujizuia. Aidha, kujifungua mapema kabla ya umri kumekuwa chanzo kikubwa cha kutokea fistula, hilo linatokana na kutopevuka kwa njia za uzazi pamoja na nyonga. Wataalamu wa afya wanabaini kwamba fistula mara nyingi hutokea kwa wanawake wanaojifungulia majumbani baada ya kukosa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la fistula, Wizara imetoa mafunzo juu ya namna ya kutibu matatizo yatokanayo na uzazi na hasa namna ya kumhudumia mama mjamzito mwenye uchungu pingamizi kwa watoa huduma za afya 676 katika Mikoa yote ikiwemo

Mwanza, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Kigoma, Kilimanjaro na Dar es Salaam. Aidha, Wizara imetoa mafunzo maalum juu ya namna ya kufanya upasuaji wa kurekebisha tatizo la fistula kwa madaktari 32 (*Vesco and Recto Vagina Fistula Surgeons*). Hii imesaidia kupunguza matatizo mengine yanayotokana na fistula kama vile unyanyapaa pamoja na sonona. Aidha, ongezeko la vituo vya afya vilivyoboreshwa na mwamko wa kina mama kwenda kliniki na kujifungua kwenye vituo vya afya vimesaidia kupunguza sana tatizo hili.

Na. 150

### **Matumizi ya Tambuu, Mirungi na Kungumanga**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je matumizi ya tambuu, mirungi na kungumanga yana madhara gani kiafya?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya tambuu (*areca catechu*), mirungi (*cathaedulis*) na kungumanga (*myristicafragrans*) ni miongoni mwa vilevi ambavyo vimekuwa vikitumika kwa wingi hasa na watu wanaoishi maeneo ya Ukanda wa Pwani ya nchi yetu. Kungumanga (*myristicafragrans*) imekuwa maarufu kama kiungo (*spice*) katika baadhi ya tamaduni hususani watu wenye asili ya kiasia, lakini imekuwa pia ikitumika kama kilevi kichangamshi kwa baadhi ya watu.

Kwa upande wa tambuu na mirungi hivi vimekuwa vikitumika kama vilevi vichangamshi muda wote na mara nyingi watumiaji wamekuwa wakitumia ili kuwafanya wasilale na kufanya kazi muda mrefu na kuleta hali ya uchangamfu

ndani ya mwili hata pale miili yao inapochoka kupita kiasi na huleta madhara makubwa kimwili na kisaikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kungumanga inaonesha kuwa na madhara machache zaidi ikitumika katika kiasi kidogo, matumizi ya muda mrefu kwa kiwango cha uzito wa mg 120 inaweza kuleta madhara kama kuchanganyikiwa (*psychosis*), kichefuchefu, kizunguzungu, matatizo kwenye mapigo ya moyo na hata kupelekea kifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, matumizi ya mirungi na tambuu uhusishwa na kutopata usingizi, kuchanganyikiwa (*hallucinations*), presha kupanda (*High BP*) na moyo kusimama ghafla (*heart attack*). Matumizi ya tambuu pia yanahusishwa na ongezeko la saratani ya kinywa na njia ya chakula, pia ugumba au utasa, matatizo ya moyo, kisukari, ongezeko la ugonjwa wa tezi dume na matatizo ya ini na figo.

Na. 151

### **Hifadhi ya Bahari ya Mafia**

**MHE. MBARAKA K. DAU** aliuliza:-

Je, hifadhi ya Bahari Mafia ilianza na vijiji vingapi?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Hifadhi ya Bahari ya Mafia lilianza na vijiji 10 ambapo takribani wakazi 20,000 wanaishi katika vijiji hivyo. Hifadhi hiyo ilianzishwa kwa kutangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali (*Government Notice*) Na. 200 la tarehe 6 Septemba, 1996 na ina jumla ya kilomita za mraba 822. Kati ya hizo asilimia 75 ni eneo la bahari na asilimia 25 ni nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla eneo lililotangazwa mwaka 1995 na mipaka yake kutangazwa mwaka 1996 kama hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia ndilo ambalo linasimamiwa na kutumika kama Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia na mipaka yake haijabadilika.

Na. 152

### **Mitamba na Madume ya Ng'ombe kwa ajili ya Mbegu**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

(a) Je, nini mkakati wa Serikali katika kutoa mitamba na madume ya mbegu kwa Tarafa ya Chamiho yenye wafugaji wengi?

(b) Je, nini mahusiano ya kiuchumi kati ya Ranchi za Taifa na jamii zinazozunguka Ranchi hizo kulingana na malengo tarajiwa?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia mashamba yake imeendeelea kusambaza mitamba kwa wananchi ili kuwapatia mbegu bora za mitamba ya maziwa. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi sasa, mitamba 1,062 imezalishwa na kusambazwa kama ifuatavyo:- Sao Hill 212, Mabuki 175, Ngerengere 93, Nangaramo 8, TALIRI 260, LITA 164 na mitamba aina ya Friesian 150 kutoka Shamba la Kitulo. Aidha, jumla ya madume 134 ya mbegu yamezalishwa na kusambazwa ambapo madume ya Friesian 40 ni kutoka katika Shamba la Kitulo na madume aina ya boran ni kutoka katika mashamba ya *Sao Hill* 74 na *NARCO* 20.

Pia, kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango Kabambe wa Mifugo (*Tanzania Livestock Master Plan 2017/2018 – 2021/*

2022) ambao unalenga kuboresha koosafu kwa kuzalisha ndama kwa lengo la kuboresha na kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa na nyama kwa kuzalisha ng'ombe (ndama) 1,000,000 walioboreshwa wa nyama na maziwa kwa mwaka kwa kutumia uhimilishaji ili kuweza kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama kufikia uhitaji uliopo. Katika kutekeleza Mpango huo, kambi za uhimilishaji zimeanzishwa katika Mikoa ya Simiyu (Bariadi na Meatu), Geita (Bukombe na Chato), Dodoma (Kongwa), Katavi (Mpanda na Tanganyika) na Kagera (Missenyi na Kyerwa). Katika maeneo haya, Serikali inahamasisha uhimilishaji ambapo hadi sasa wamehimilishwa jumla ya ng'ombe 4,990 bure.

Baada ya Mikoa hii, utafuata Mkoa wa Mara katika Wilaya ya Bunda kwa Mheshimiwa Boniphace Mwitwa Getere lengo likiwa ni kuendelea kuzalisha ng'ombe bora wenye uwezo wa kutoa maziwa mengi na nyama kwa wingi. Serikali inatekeleza mkakati huu kwa kuzingatia dhana ya ushirikishwaji wa sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa mantiki hiyo, Tarafa ya Chamihio yenye wafugaji wengi itashirikishwa katika mkakati wa uhimilishaji ili kutoa mitamba na madume bora ya mbegu.

(b) Serikali imeendelea kudumisha mahusiano ya kiuchumi yaliyopo kati ya Ranchi za Taifa *NARCO* na jamii zinazozunguka Ranchi hizo. Serikali ilianzisha mashamba ya *NARCO* kwa madhumuni ya kuendeleza na kueneza ufugaji bora, hususan ufugaji wa ng'ombe bora wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi kwa kutumia mbinu za ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, jamii zinazozunguka mashamba hya ya *NARCO* hupata faida za:-

(i) Kutumia masamba ya *NARCO* kama mashamba darasa; na

(ii) Wakati wa kiangazi kikali hupatiwa fursa ya kulishia mifugo kwa njia ya kukodishiwa vitalu na hivyo kunenepeshea mifugo yao.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha  
2020/2021- Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**NAIBU SPIKA:** Nimuite Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutimiza majukumu yetu hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa letu na Dunia kwa ujumla inakabiliwa na janga la ugonjwa wa homa kali ya Mapafu inayotokana na virusi vya *Corona* yaani *Covid-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa, natoa shukurani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini katika dhamana ya kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naendelea kumuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa moyo wa dhati, kwa umakini wa hali ya juu na kwa uadilifu mkubwa huku nikimtanguliza Mwenyezi Mungu muweza wa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza kwa dhati Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake thabiti na kwa uzalendo mkubwa ambao ameonyesha katika kusimamia rasilimali za Nchi yetu. Watanzania wote wanashuhudia miradi mikubwa ya maendeleo ikitekelezwa katika sekta zote muhimu hapa Nchini. Tuendeleo kumuunga mkono Rais wetu ili aendelee kufanikisha azma yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu mchapakazi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wao makini. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na nakupongeza wewe Naibu Spika Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuliongoza Bunge letu kwa umakini wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge kwa kumpoteza Mheshimiwa Mchungaji Getrude Pangalile Rwakatare, aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020. Marehemu Rwakatare alikuwa ni mmiliki wa Shule za St. Mary's na pia mmiliki wa Chuo cha Ualimu cha St. Mary's kilichopo Tabata. Ni dhahiri kuwa, Wizara imepoteza mdau muhimu sana katika sekta ya elimu. Mchango wake katika kutoa elimu Nchini tutaendelea kuenzi na kuuthamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kuwa shule pamoja na vyuo vimefungwa ikiwa ni hatua muhimu ya Serikali kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa *Corona*. Wizara yangu imeanzisha vipindi maalum vya Redio na Televisheni ili wanafunzi waendeleo kupata elimu wakiwa nyumbani hivyo, natoa wito kwa Wazazi na Walezi kuendelea kuwasimamia Watoto wao ili kuhakikisha wanaendelea kujisomea.

Aidha, nawasihi wazazi na walezi waendeleo kuwakinga watoto wao na wasiwaruhusu kutoka na kuzurura hovy hovy bila ya kuwa na sababu za msingi. Napenda pia kuwasihi wanafunzi, walimu na wadau wote wa elimu kwa ujumla kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam wa afya ili kujikinga na kuepuka na maambukizi ya ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kutoa shukurani za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri ambao wamekuwa wakitoa kwa Wizara ambao umechangia katika kuongeza tija. Nawashukuru sana pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, hakika wamekuwa na mchango wenye tija sana katika Wizara yangu. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa ambao mmekuwa mkinipatia katika kipindi cha uhai wote wa Bunge hili. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu hayo kwa utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe Taarifa ya utelekezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na naomba hotuba yangu yote iingie katika *Hansard* za Bunge.



Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi 1,386,508,723,272.00 kwa ajili ya Fungu 46. Aidha, Bunge lako liliidhinisha kiasi cha shilingi 2,156,017,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa ajili ya Fungu 17 ambayo ni Tume ya Taifa ya *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makusanyo ya Maduhuli; Wizara ilipanga kukusanya Maduhuli yenye thamani ya shilingi 553,739,899,119.13 na hadi kufikia Mwezi Machi, Wizara ilikuwa imekusanya Maduhuli yenye thamani ya shilingo 335,148,981,970.31 ambayo ni sawa na asilimia 60.5 ya Makadirio na kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO*, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya shilingi 27,000,000.00 na hadi kufikia mwezi Machi, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ilikuwa imekusanya shilingi milioni 8.5

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida; hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi 396,788,907,260.36 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na asilimia 75.8 ya Bajeti iliyotengwa. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO*, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 1,176,454,000 sawa na asilimia 54.56 ya fedha zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo; hadi kufikia mwezi Machi Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 734,890,659,288.20 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 80.2 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji; sasa naomba nitoe Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Taarifa hiyo imeelezwa kwa kina katika kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa sita hadi ukurasa wa 63 naomba nieleze kwa uchache mambo ambayo nitaweza kuyazungumza kwa kuzingatia muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za uongezaji fursa za upatikanaji wa elimu:-

- (i) Wizara imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9712;
- (ii) Matanki ya maji 911 pamoja na miundombinu ya maji ya kunawia katika shule za msingi 602 kupitia mradi wa huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni;
- (iii) Wizara imesajili shule 395 zilizokidhi vigezo kati ya 407 zilizotuma maombi;
- (iv) Wizara imetoa jumla ya leseni 253 za kufundishia;
- (v) Wizara imenunua na kusambaza vifaa maalum vya kielimu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule maalum na vitengo 424;
- (vi) Wizara imetoa mafunzo kazini kwa walimu 269 kuhusu matumizi ya lugha ya alama;
- (vii) Wizara imeimarisha elimu ya ualimu kwa kuhakikisha kwamba tunaimarisha michezo ikiwa ni pamoja na kuendesha mashindano ya michezo katika vyuo vya ualimu ambayo yanajulikana kama UMISAVUTA;
- (viii) Wizara imenunua magari 39 kupitia program ya “Lipa kulingana na matokeo” ambapo Magari 35 yamegawiwa katika vyuo vya ualimu vyote vya Serikali Nchini;
- (ix) Wizara pia imesamba za aina 449 za vitabu. Nakala zake jumla ni 25,709 kwa ajili ya masomo yote ambayo yanafundishwa katika vyuo vya ualimu;
- (x) Ili kuimarisha TEHAMA, Wizara imenunua *computer 480, UPS 480, photocopy machine 35, computer mpakato 43* na *server* mbili kwa ajili ya ufundishaji TEHAMA katika vyuo vya ualimu vyote vya Serikali;
- (xi) Wizara imetoa mafunzo ya TEHAMA kazini kwa wakufunzi 550, imetoa mafunzo ya TEHAMA na mafunzo ya usaidizi kwa walimu wenye mahitaji maalum 125 na wakufunzi tisa;

(xii) Imetoa mafunzo kazini kwa walimu 771 katika halmashauri 20 zenye ufaulu mdogo katika somo la Hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia ubora wa elimu katika vyuo vya walimu; Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Taasisi zinazopata ithibati na Usajili zinatoa elimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika Mwaka 2019/2020:-

(i) Serikali imefanya tathmini ya mazingira ya utoaji wa elimu katika Asasi 4,102;

(ii) Imekagua ukaguzi maalum asasi 548;

(ii) Imeongeza Wathibiti Ubora wa shule wapya 400 katika Ofisi za Kanda pamoja na Ofisi za Wilaya;

(iii) Imekamilisha ujenzi wa Ofisi za wadhhibi ubora 100 katika halmashauri 100 ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 15.2;

(iv) Imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kuongeza madarasa, maabara na Ofisi za walimu;

(v) Lakini pia imewezesha vijana 2534 kupata mafunzo ya uanagenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Juu kama nyenzo muhimu kuifikisha Nchi yetu katika uchumi wa kati na katika Mwaka 2019/2020 Serikali:-

(i) Imeendelea kugaharmia wanataaluma 620 ambapo 196 wanasoma shahada za umahiri na 424 shahada za uzamivu kwa lengo la kuwa na Wahadhiri waliobobea katika fani zao;

(ii) Serikali imeratibu ufadhili nje ya Nchi kwa wanafunzi 115 wa Kitanzania na imefadhili wanafunzi 10 Rais wa China kusoma lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es

salaam ikiwa ni sehemu ya kuendeleza uhusiano mzuri na kuendeleza lugha yetu adhimu ya Kiswahili;

(iii) Lakini pia Serikali imefadhili wanafunzi 207 kupitia mradi wa vituo vya umahiri vya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia; katika kuratibu, kusimamia kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu:-

(i) Serikali imetambua na kuhakiki teknolojia 231 zilizoanzishwa Nchini kwa lengo la kuwa na kanzidata ya Kitaifa. Aidha, Serikali imepata ufadhili wa jumla ya Euro 965,220 sawa na Fedha za Kitanzania bilioni 2,414,045,190 kwa ajili ya miradi mipya mitano ya utafiti katika sekta za maji, afya, kilimo na mifugo;

(ii) Serikali imewaendeleza wabunifu 60 waliopatikana katika mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya mwaka 2019. Na kati ya wabunifu hao, bunifu za wabunifu 12 zipo katika hatua ya kutengeneza bidhaa za mfano kwa ajili ya kuingia sokoni yaani *prototypes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika shughuli ambazo zimefanywa na Taasisi, mamlaka na wakala zilizo chini ya Wizara ya Elimu; Wizara imeendelea kuratibu majukumu ya Taasisi, mamlaka na wakala zilizo chini yake ili kuhakikisha kwamba Nchi yetu inazalisha raslimali watu wenye weledi kwa kuzingatia mahitaji ya nchi, soko la Kikanda na soko la Kimataifa. Shughuli zilizofanywa na kila Taasisi ilito chini ya Wizara ya Elimu zimeainishwa kuanzia ukurasa wa 16 hadi ukurasa wa 63 wa kitabu cha hotuba. Nitaeleza kwa uchache baadhi ya shughuli kama ifuatavyo:-

(i) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeendelea na ukarabati wa Bweni namna moja, kitalu G linalotumika na wanafuynzi wenye mahitaji maalum ambalo linaweza kuchukua wanafunzi wenye mahitaji maalum 63 pamoja na ukarabati wa majengo ya ndaji ya uhandisi na teknolojia;

(ii) Pia Chuo Kikuu kinaendelea na ukarabati mkubwa wa bweni namna mbili na namba tano yenye uwezo wa kuweka wanafunzi 788 ambapo ukarabati huu ukikamilika, Chuo Kikuu cha Dar es salaam kitakuwa na uwezo wa kulaza wanafunzi 11,103;

(iii) Chuo Kikuu kimeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano na kituo cha wanafunzi ka lengo la kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi na kimeendelea pia na kutatua changamoto ya maji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo kinajenga mfumo mpya wa maji katika *campus* ya Mwalimu Julisu Nyerere unaohusisha kuweka upya mabomba makubwa mapya, kujenga tanki lenye ujezo wamita za ujazo 500,000 na kufunga mashine zitakazoweza kusafirisha maji kiasi cha shilingi 360,000 kwa saa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine; katika kipindi cha mwaka 2019/2020 kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine, Serikali imeanzisha *campus* mpya katika Mkoa wa Katavi iliyopewa jina la Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Peter Kayanza Pinda ambayo itatoa masomo ya Astashahada, Shahada na Stashahada katika Nyanja za kilimo na mifugo. Nadhani sasa tumemuezi mtoto wa mkulima kwa vitendo sasa ana Chuo Kikuu chake cha Kilimo kule Katavi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine pia kimeimarisha hospitali ya rufaa ya wanyama kwa hiyo wale wenye mifugo tuna hospitali ya wanyama pale Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine lakini pia imeimarisha Taasisi ya elimu ya kujiendeleza, kumbi za mikutano na idara ya huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu ca kilimo cha Sokoine pia kinaimarisha ufundishaji na kinajenga maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2400 kwa wakati mmoja na maabara hii inajengwa kwa fedha za ndani. Nashukuru Wizara ya Fedha mpaka sasa hivi Maabara inagharimu shilingi bilioni 11.9 na mpaka sasa Wizara ya fedha imeshatupatia bilioni tisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inaendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu lakini Chuo Kikuu cha kilimo cha Sokoine kimeboresha pia shamba darasa kwa ajili ya kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati. Uboreshaji wa shamba hilo umechochewa na kuwepo kwa matrekta 10 yaliyolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli baada ya kutembelea Chuo hicho cha Kilimo cha Sokoine mnamo tarehe 07 Mei, 2018 akaona jinsi ambavyo walikuwa na vifaa duni akatoa ahadi ameitekeleza na ahadi yake inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo pia kimeboresha shamba darasa wka kufunga vifaa vya kisasa vya kilimo na kupanda mazao ya Kitaifa ya kimkakati kama vile Zabibu, Pamba, Katani, Kakao, Kahawa, Mananasi, Migomba na mazao ya mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha afya na Sayansi Shirikishi - Muhimbili kinaendelea na ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Ardhi kinaendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalam hususani usanifu wa majengo, utayarishaji wa mipango na kuendeleza Miji na uthamini. Pia chuo cha Ardhi kinaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 ili kuongeza malazi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Mzumbe kimeendelea na ujenzi wa madarasa 10 na mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na ofisi yenye uwezo wa kuchukua wafanyakazi 50 katika kampasi kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma kinaendelea na ujenzi wa Kitengo cha Huduma za Mionzi katika Hospitali ya Chuo kwa lengo la kuongeza wigo wa hutoaji huduma. Chuo cha Ushirika Moshi kimetoa mafunzo kwa vyama 101 vya ushirika katika wilaya 61 za Tanzania Bara, kimefanya ukarabati na upanuzi wa mabweni tisa na hivyo kuongeza nafasi ya malazi kwa wanafunzi 460 na

kimekamilisha ujenzi wa *cafeteria* yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania imeimarisha mtandao wa kujifunzia kwa njia ya masafa kwa kutengeneza programu mpya 35 ambazo zimepitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu, lakini pia kimeimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kuzindua maabara tatu za Sayansi. Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia kimeendelea na jitihada za upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo ya chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Mafunzo ya Ufundi, kinakarabati nyumba 68 za watumishi pia kinaendelea na ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 800. Chuo cha Ufundi Arusha kimekamilisha ujenzi wa jengo la kufundishia kuhusu matumizi ya nishati jadidifu ya umeme wa jua na kinaendelea na ujenzi wa miundombinu katika kituo cha mafunzo ya nishati jadidifu ambayo (*renewable energy*) katika Kituo cha Kikuletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimeendelea na ujenzi wa bweni katika kampasi ya Zanzibar lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha malazi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa Elimu ya Watu Wazima na elimu nje ya mfumo rasmi ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wa Kitanzania wanapata stadi, ujuzi na maarifa stahiki. Katika mwaka 2019/2020, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeboresha Mkakati wa Kuendeleza Kisomo na Elimu kwa Umma ili uendane na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kimeendelea na ujenzi wa maktaba utakaogharimu kiasi cha shilingi bilioni 5,523 ambazo zinatolewa ni fedha za ndani na maktaba hiyo ikikamilika

itaweza kuchukuwa wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja. Vile vile chuo kinakamilisha ujenzi wa madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja. Kimekarabati ofisi 80 ambazo zilikuwa ni *basement* na ofisi hizo zimewesha kupatikana kwa nafasi 320 za wafanyakazi. Chuo kimeendelea kutoa huduma za ushauri na kitaalamu kwa jamii na kushiriki katika kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi mikubwa ya kimkakati ambayo ni mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere *Hydropower Project* na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa. Kwa hiyo, tunafurahi kwamba taasisi zetu za elimu ziko pia katika kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania Baraza la Mitihani la Tanzania limekamilisha Uchapaji, Usafirishaji na Usahihishaji wa mitihani ya Kitaifa kwa ngazi zote ambazo inazisimamia kwa mujibu wa sheria. Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu imeratibu maombi 99,014 ya wanafunzi walioomba kujiunga na masomo katika mwaka 2019/2020. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Taasisi nyingine zote zilizoko chini ya Wizara ambazo zimeorodheshwa katika kitabu change, zimetokeleza shughuli ambazo zimeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania imekamilisha uchapaji na uzambazaji wa vitabu vya Darasa la Sita nakala 2,962,000 zimetolewa lakini pia imechapisha vitabu ambavyo vinatumia lugha ya Kiingereza. Sasa tumetatua changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa vitabu kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze katika Mpango wa Wizara katika mwaka wa fedha 200/2021. Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeelezwa kupitia Idara, Vitengo kama ambavyo imeainishwa na kuanzia ukurasa wa 64 mpaka 112 wa kitabu cha hotuba yangu. Aidha, Wizara itendelea kuratibu miradi mbalimbali katika Wizara ambayo imeainishwa kwenye kitabu cha hotuba, lakini niseme tu kwamba tunategemea kwamba Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya Juu itatoa mikopo kwa wahitaji 54 ikilinganishwa na wanufaika wa mwaka wa kwanza 49,799.



Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinategemea kuongeza ghorofa mbili kwenye hostel za Dkt. John Pombe Magufuli na hivyo ghorofa mbili zikiongezwa zinataweza kuchukua wanafunzi 1,280 na kwa ujumla zile *hostel*/zitaweza kuchukua wanafunzi 5,120.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO*, shughuli ambazo zitatekelezwa zimeainishwa katika ukurasa wa 19 mpaka wa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua mchango mkubwa sana ambao unatolewa na viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara. Kipekee kabisa namshukuru kwa dhati Mheshimiwa William Tate Olenasha, Mbunge na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo; Naibu Makatibu Wakuu; Profesa James Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wa karibu ambao wananipa katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, walimu, wanafunzi na wadau wa elimu kwa ujumla kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani za kipekee kabisa kwa wamiliki wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao hakika wamekuwa wakishirikiana sana na Serikali katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha mpango wa elimu na wote wametambulika kwenye kitabu ukurasa wa 120 mpaka 121.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nayashukuru mashirika ambayo yamechangia kufanikisha kuchangia *Program* za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo pia yametambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa 2020/2021, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,348,563,375,000/= kwa mchanganuo ufuatao: shilingi 491,049,151,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 457,514,224,000/= zinaombwa kwa ajili ya miradi na maendeleo. Kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* Wizara inaomba jumla ya shilingi 2,239,181,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mafungu yote mawili, yaani fungu 46 na fungu 18 yenye jumla ya shilingi 1,350,802,556,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukurani za dhati kabisa kwako wewe na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB)  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21 -KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka

wa fedha 2019/20. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**2. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutimiza majukumu yetu hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa letu na Dunia kwa ujumla inakabiliwa na janga la ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu inayotokana na virusi vya Corona (COVID-19). Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa namna ya pekee na kwa unyenyekevu mkubwa, natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini katika dhamana hii aliyonipa ya kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa moyo wa dhati, kwa umakini na uadilifu wa hali ya juu huku nikimtanguliza Mwenyezi Mungu.

**3. Mheshimiwa Spika**, sina budi kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kwa uongozi wake thabiti na kwa uzalendo alionao katika kulinda na kusimamia rasilimali za nchi yetu. Watanzania wanashuhudia miradi mikubwa ya maendeleo ikitekelezwa katika sekta zote muhimu. Tuendeleo kumuunga mkono ili aendeleo kufanikisha azma yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu.

**4. Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi wao makini, miongozo wanayotoa na ufuatiliaji wanaofanya katika kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliotukuka.

**5. Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze kwa dhati wewe Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuliongoza Bunge kwa umahiri wa hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu.

**6. Mheshimiwa Spika**, napenda kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki tarehe 20 Aprili, 2020. Marehemu Rwakatare alikuwa ni mmiliki wa Shule za St. Mary's ambazo zinatoa elimu kuanzia ngazi ya Awali mpaka Elimu ya Sekondari. Pia alikuwa ni mmiliki wa Chuo cha Ualimu cha St. Mary's kilichopo Tabata ambacho kinafundisha walimu wa shule za Awali na Msingi. Ni dhahiri kuwa, Wizara imepoteza mdau muhimu sana katika Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mchango wake katika kutoa elimu tutaendelea kuuthamini na kuenzi. Pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kumpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Akbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**7. Mheshimiwa Spika**, sote tunatambua kuwa shule pamoja na vyuo vimefungwa ikiwa ni hatua muhimu ambayo Serikali imechukua kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Corona. Wizara yangu imeanzisha vipindi maalum vya Redio na Televisheni ili wanafunzi waendeleo kupata elimu katika kipindi ambacho wapo nyumbani. Hivyo, natoa wito kwa Wazazi na Walezi kuendelea kuwasimamia Watoto wetu ili kuhakikisha wanaendelea kujisomea na kwamba hawatoki nyumbani bila kuwa na sababu za msingi. Aidha, napenda kuwasihani wanafunzi, walimu na wadau wote wa elimu kwa ujumla, kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Wataalam wa Afya ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa wa Corona.

**8. Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mbunge wa Kibakwe) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira.

**9. Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb), na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na mapendekezo yao, ambayo yamechangia kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri mlinipa kwa kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**10. Mheshimiwa Spika**, naishukuru kwa dhiti familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu.

**11. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21.

**B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20  
TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI**

**12. Mheshimiwa Spika** katika mwaka wa fedha 2019/20 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,386,508,723,272.00** kwa ajili ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 523,788,923,012.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 862,719,800,260.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO -

Fungu 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,156,017,000.00** ambapo **Shilingi 1,532,293,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 623,724,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume.

### **Ukusanyaji wa Maduhuli**

**13. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 553,739,899,119.13** ambapo kiasi cha **Shilingi 13,942,894,000.00** kilipangwa kukusanywa na Idara na Vitengo, na **Shilingi 539,797,005,119.13** zilipangwa kukusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 335,148,981,970.31** sawa na asilimia **60.5** ya Makadiri.

**14. Mheshimiwa Spika**, kupitia Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 27,000,000.00** kutokana na malipo ya mrabaha kutoka katika uchapishaji wa Jarida la Tume. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, kiasi cha **Shilingi milioni 8.5** sawa na asilimia **31.48** ya lengo kilikuwa kimekusanywa.

### **Matumizi ya Kawaida**

**15. Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea Jumla **Shilingi 396,788,907,260.36** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na asilimia **75.8** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,176,454,000** sawa na asilimia **54.56** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

### **Miradi ya Maendeleo**

**16. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 30, 2020 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 734,890,659,288.20** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **85.20** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi**

459,937,828,356.68 ni fedha za ndani na **Shilingi 274,952,830,931.51** ni fedha za nje.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU

**17. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2019/20.

### Uongezaji Fursa za Upatikanaji Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu

**18. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kuhakikisha Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu inaendelea kutolewa kwa ubora kwa kuzingatia fursa sawa kwa wote ili kuwawezesha wahitimu kukabiliana na mazingira pamoja na kuwa na utayari wa kuendelea na ngazi za elimu zinazofuata. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 9,712 (Wasichana - 5,539, Wavulana - 3,645 na Walimu - 528) miundombinu ya maji, matanki ya maji 911 pamoja na miundombinu ya kunawia mikono katika shule za Msingi 602 kupitia **Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni**;

(ii) imekamilisha taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari inayojengwa eneo la Iyumbu – Dodoma kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R;

(iii) imeendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020 kupitia **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu**;

(iv) imeendelea kuboresha miundombinu na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kukarabati Vyuo vya Ualimu 9 kupitia Mradi wa Lipa kulingana na Matokeo. Vyuo hivyo ni:

Singachini, Monduli, Mamire, Bustani, Bunda, Katoke, Vikindu, Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi

(v) imeendelea na Ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ualimu Mpuguso, Ndala, Kitangali, na Shinyanga kupitia **Mradi wa Uboreshaji Vyuo vya Ualimu – UTC**.

### **Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

**19. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la upatikanaji wa fursa ya Elimu na Mafunzo, Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imesajili jumla ya shule 395 zilizokidhi vigezo kati ya 407 zilizoomba kwa mchanganuo ufuatao: Awali Pekee 15 (Zisizo za Serikali), Awali na Msingi 265, (Serikali 144, Zisizo za Serikali 121) na Sekondari 115 (Serikali 87 na Zisizo za Serikali 28);

(ii) imeendelea kutengeneza mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi ili kuwezesha usajili wa shule kufanyika kwa uwazi na kwa wakati; na

(iii) imetoa jumla ya leseni 253 za kufundishia zikiwemo 240 kwa walimu wa kigeni na 13 kwa wataalam raia wasio walimu.

### **Utoaji wa Miongozo ya Uratibu wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu**

**20. Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia na kuratibu utoaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu, katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imehuisha Mwongozo wa Mafunzo ya Malezi, Unasahi na Ulinzi wa Mtoto kwa Walimu wa Shule za Msingi, Sekondari na Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu;

(ii) imehuisha Mwongozo wa utoaji wa Huduma za Elimu kwa Wanafunzi wenye Ualbino ili kuongeza uelewa wa wadau



kuhusu wajibu wao na mahitaji ya kielimu kwa wanafunzi hao;  
na

(iii) imeandaa Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (*Teachers' Continuous Professional Development Framework*) ambacho kitakuwa nyenzo ya kuwaendeleza walimu kitaaluma na kitalaamu ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

### **Kusimamia Utoaji wa Elimu Maalum**

**21. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua zenye kuhakikisha elimu yetu inakuwa jumuishi, Serikali imetekeleza yafuatayo;

(i) imenunua na kusambaza vifaa maalum vya kielimu katika shule maalum na vitengo 424 ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 269 kutoka shule 23 za sekondari nchini kuhusu matumizi ya Lugha ya Alama na mbinu za kufundishia. Aidha, imetoa mafunzo kazini ya Lugha ya Alama kwa walimu 183 wanaofundisha shule zenye wanafunzi Viziwi; na

(iii) imenunua na kusambaza Vifaa vya Wanafunzi na Wakufunzi wenye mahitaji maalum katika vyuo vya Ualimu Patandi, Mpwapwa na Mtwara Kawaida ili kuwawezesha kufundisha na kujifunza kikamilifu.

### **Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu**

**22. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa walimu katika kuinua ubora wa elimu nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali imeendelea kuhakikisha inaimarisha elimu ya ualimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ambapo yafuatayo yametekelezwa:

(i) kugharamia chakula na malazi kwa wanachuo wote katika vyuo vyote 35 vya Serikali;

(ii) kuimarisha elimu ya michezo ikiwa ni pamoja na kuendesha mashindano ya michezo na sanaa katika Vyuo vya Ualimu (UMISAVUTA). Mashindano hayo yamefanyika kuanzia ngazi ya Vyuo, Kanda na Taifa na kuhusisha michezo ya riadha, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu na mpira wa wavu. Vilevile, mashindano ya sanaa za maonesho (nyimbo, michezo ya kuigiza na ngoma), uchoraji na utengenezaji wa zana za kufundishia na kujifunzia yalifanyika.

(iii) kununua magari 39 kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo – EP4R, ambapo magari 35 yamegawiwa katika Vyuo vyote vya Ualimu vya Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi katika vyuo hivyo na magari 4 ni kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini;

**23. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu imetekeleza yafuatayo:

(i) imenunua na kusambaza katika vyuo vya Ualimu vya Serikali aina 449 za vitabu zenye jumla ya nakala 25,709 kwa ajili ya masomo yote yanayofundishwa vyuoni;

(ii) imeendelea kuimarisha mafunzo kwa njia ya TEHAMA katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali ikiwa ni pamoja na kununua *Servers* mbili kwa ajili ya kuweka mfumo wa ufundishaji na ujifunzaji (Learning Management System).

(iii) imenunua na kusambaza katika Vyuo vya Ualimu, kompyuta 480, *UPS* 480, *Photocopy Machines* 35, kompyuta mpakato 43 ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA;

(iv) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA kwa wakufunzi 530 wa kutoka katika vyuo 17 vya Ualimu (Butimba, Murutunguru, Bunda, Tarime, Katoke, Ndala, Tabora, Kasulu, Shinyanga, Kabanga, Mamire, Monduli, Patandi, Singachini, Marangu, Mandaka na Korogwe) ili kuwajengea uwezo wa kutumia TEHAMA kama nyenzo ya ufundishaji na ujifunzaji;

(v) inaendelea na uunganishaji wa Vyuo vyote 35 katika Mkongo wa Taifa kwa lengo la kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu;

(vi) imetoa mafunzo kazini ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Walimu 125 na Wakufunzi 9 wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kutumia TEHAMA;

(vii) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 771 (Msingi 451 na Sekondari 320) katika Halmashauri 20 zenye ufaulu wa chini katika somo la Hisabati kwenye mitihani ya Kitaifa kwa lengo la kuwapa Walimu mbinu na njia fanisi zaidi kufundishia na kujifunzia somo hilo. Halmashauri zilizopewa mafunzo hayo ni: Korogwe, Chemba, Gairo, Momba, Nyasa, Madaba, Rufiji, Ruangwa, Nanyamba, Butiama, Nachingwea, na Tandahimba kwa shule za sekondari na Mkalama, Simanjiro, Meatu, Chemba, Ukerewe, Kilindi, Musoma na Lushoto kwa shule za Msingi;

(viii) imeandaa miongozo ya mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia saidizi kwa Wakufunzi na Walimu wenye mahitaji maalumu ili waweze kufundisha na kujifunza kwa urahisi zaidi;

(ix) imeandaa miongozo ya mafunzo kazini kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji; na

(x) imefanya ufuatiliaji kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopata Mafunzo ya ufundishaji wa Hisabati ili kutathmini tija ya mafunzo waliyopata.

**Kusimamia Uboru wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu**  
**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizopata Ithibati na Usajili zinatoa elimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Kutokana na azma hiyo, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini ya mazingira ya utoaji wa elimu katika asasi 4,102 zikiwemo Shule za Msingi 3,251, Sekondari 837 na

Vyuo 14 vya Ualimu na kutoa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha utoaji wa elimu;

(ii) imefanya ufuatiliaji katika asasi 516 zikiwemo Shule 428 za Msingi, Sekondari 76 na Vyuo vya Ualimu 12. Ufuatiliaji huo ullenga kufanya tathmini ya jumla ya shule ili kubaini kama wamiliki wa asasi hizo wametekeleza ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Wathibiti Ubora wa Shule;

(iii) imefanya ukaguzi maalum katika asasi 548 zikiwemo shule 363 za Msingi na 185 za Sekondari kwa ajili ya kupewa kibali cha Usajili, ambapo shule 395 zikiwemo za Msingi 280 na za Sekondari 115 zilikidhi vigezo na kupatiwa usajili;

(iv) imeongeza Wathibiti Ubora wapya 400 wa Shule katika ofisi za Kanda na Wilaya;

(v) imenunua kompyuta na *printer* 153 na kuzisambaza katika Ofisi mbalimbali za Uthibiti Ubora ili kurahisisha utendaji kazi kwa Wathibiti Ubora wa Shule;

(vi) imekamilisha ujenzi wa ofisi mpya 100 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya na inaendelea na ujenzi wa ofisi nyingine mpya 55 ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Wathibiti Ubora; na

(vii) inaendelea na utaratibu wa ununuzi wa magari 65 ya Uthibiti Ubora wa Shule ili kuimarisha ufuatiliaji.

### **Kusimamia Ubora wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**25. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inatolewa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na kuwafikia walengwa kwa ufanisi. Ili kufikia azma hiyo yafuatayo yamefanyika:

(i) kufanya ufuatiliaji wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ikiwemo programu ya Elimu Changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi

(Intergrated Programme for Out of School Adolescents - IPOSA); na

(ii) kutoa elimu ya katika Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa vijana 13,036 (Wanawake 7,625 na wanaume 5,411).

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**26. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imewezesha ununuzi wa vifaa vya ufundi vya kufundishia na kujifunzia (Technical Equipments) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika vyuo hivi; na

(ii) imewezesha ujenzi wa mabweni mawili (2) katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro (MVTC) ili kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa wakufunzi wa vyuo vya ufundi stadi;

(iii) imegharamia chakula cha Wanachuo 5,520 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(iv) imewezesha mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (*Folk Education*) kwa washiriki 7,079 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwapa ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira;

(v) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (Folk Education) kwa washiriki 1,079 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwaongezea ufanisi katika shughuli mbalimbali za uzalishaji katika maeneo wanayoishi;

(vi) imeratibu uanzishwaji wa vituo vinne (4) vya umahiri kwenye nyanja za TEHAMA, Usafiri wa anga, Nishati jadidifu na Mazao ya ngozi katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Usafirishaji cha Taifa na Chuo cha Ufundi Arusha

kupitia mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project* (EASTRIP);

(vii) imewezesha ushiriki wa wabunifu katika Mashindano ya Ubunifu – *African Challenge Tech Awards* yaliyofanyika Kenya - Nairobi na kuhusisha nchi 8 ambapo Timu ya Tanzania iliibuka mshindi wa pili na kupata zawadi ya \$100,000, pamoja na ufadhili wa kusoma nchini China;

(viii) imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(ix) imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi stadi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza awamu ya pili ya ukarabati na upanuzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 20 (FDCs); na

(x) imewezesha vijana 2,534 kupata mafunzo ya uanagenzi.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**27. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa Elimu ya Juu katika juhudi za kuifikisha nchi yetu katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea kugharamia wanataaluma 620 katika ngazi za Shahada ya Umahiri 196 na Uzamivu 424 kutoka Vyuo Vikuu vya Serikali kwa lengo la kuboresha Elimu ya Juu kwa kuwa na wahadhiri waliobobea katika fani zao;

(ii) imeratibu ufadhili nje ya nchi wa wanafunzi 115 wa Kitanzania (China 61, Hungary 29, Uingereza 7 na Algeria 18);

(iii) imeratibu uchambuzi wa wanafunzi watakaonufaika na ufadhili kwa mwaka wa masomo 2020/21 kutoka Jumuiya ya Madola - Uingereza, China, Hungary, Malaysia na Venezuela;

(iv) imefadhili wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mujibu wa mkataba uliopo na kwa lengo la kukuza Lugha yetu adhimu ya Kiswahili; na

(v) imefadhili wanafunzi 207 (Umahiri 107 na Uzamivu 100) kupitia Mradi wa Vituo vya Umahiri vya Africa (African Centres for Excellence ACE II) katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM-AIST).

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**28. Mheshimiwa Spika**, katika kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imetambua na kuhakiki teknolojia 231 zilizozalishwa nchini kwa lengo la kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa kuhusu teknolojia hizo.

(ii) imeendelea kuandaa mahitaji ya mfumo wa kanzidata ya teknolojia zinazozalishwa nchini kwa kushirikiana na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu (NIDC)

(iii) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi saba (7) ya utafiti inayofadhiliwa na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo na kubaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kulingana na makubaliano; na

(iv) imeshiriki Mkutano Mkuu wa 63 wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria Septemba, 2019 ambapo miradi mipya mitano (5) ya utafiti katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo imepata ufadhili wenye jumla ya **Euro 965,220** sawa na **Shilingi 2,414,045,190.13**.

**29. Mheshimiwa Spika**, katika kuwajengea uwezo wabunifu kuhusu kulinda na kuendeleza ubunifu kuwa fursa za kiuchumi, Serikali imewaendeleza wabunifu 60 waliopatikana katika

Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka 2019. Aidha, bunifu za wabunifu 12 zipo katika hatua ya kutengeneza bidhaa za mfano (prototypes) tayari kwa kuingia sokoni.

**30. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeratibu mashindano ya MAKISATU kwa lengo la kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu na wagunduzi nchini. Mashindano yalihusisha wabunifu kutoka Makundi 7 ya wabunifu ambayo ni: Wanafunzi wa Shule za Msingi; Shule za Sekondari; Vyuvo vya Ufundi Stadi; Vyuvo vya Ufundi wa Kati; Mfumo usio Rasmi; Vyuvo Vikuu; na Taasisi za Utafiti na Maendeleo. Jumla ya wabunifu 621 walijitokeza kushiriki mashindano ambapo wabunifu mahiri 70 (10 kutoka katika kila kundi) walipatikana na kushiriki kilele cha mashindano hayo. Wabunifu watatu mahiri kwa kila kundi walipewa tuzo mbalimbali na ubunifu wao utaendelezwa ili kufikia hatua ya kuwa bidhaa na kubiasharishwa.

## **SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI, MAMLAKA NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**31. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuratibu majukumu ya Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizo chini yake ili kuhakikisha nchi inazalisha rasilimaliwatu yenye weledi kwa kuzingatia mahitaji ya Mipango ya ndani ya nchi, Soko la Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizofanyika kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**32. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 28,511 wakiwemo Astashahada 483, Stashahada 802, Shahada 24,368, Stashahada ya Uzamili 191, Shahada ya Umahiri 2,300, Shahada ya Uzamivu 320 na kozi za muda mfupi wanafunzi 47 katika Kampasi Kuu ya Mwl.

J.K. Nyerere;



(ii) imeongeza idadi ya miradi ya utafiti ili kutatua changamoto mbalimbali katika jamii kutoka tafiti 135 hadi 173;

(iii) imeongeza idadi ya machapisho katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa kutoka machapisho 735 hadi 1,048 (Kitaifa) na 11 hadi 13 (Kimataifa) kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii, kuelimisha na kujitangaza kimataifa;

(iv) inaendelea na mradi wa ufungaji gesi asilia kwenye nyumba 35 za wafanyakazi na Kafeteria zote za chuo, Kampasi ya Mwalimu Nyerere ili kuhakikisha mazingira ya chuo yanahifadhiwa; na

(v) imegharamia masomo ya uzamili kwa wanataaluma 35 (31 – Uzamivu na 4 Umahiri) ili kupunguza changamoto ya upungufu wa Wahadhiri.

**33. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi, Serikali imetekeleza yafuatayo;

(i) imekarabati Bweni Na. 1 Kitalu G linalotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalum lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 63. Aidha, inaendelea na ukarabati wa majengo ya Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia;

(ii) imeendelea na ukarabati mkubwa wa mabweni Namba 2 na 5 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788 kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo. Kukamilika kwa mradi huu kutakiwezesha chuo kufikia jumla ya wanafunzi 11,103 wanaopata malazi katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere;

(iii) imekamilisha ukarabati mkubwa wa nyumba 5 za watumishi kwa lengo la kuboresha mazingira ya makazi;

(iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano la kituo cha wanafunzi kwa lengo la kutoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma za kujisomea, kupumzika, kufanya michezo

ya ndani, migahawa, benki, maduka ya vitabu na ofisi za Serikali ya wanafunzi na Mshauri wa wanafunzi;

(v) imeendelea na ujenzi wa mfumo mpya wa maji katika Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere ambapo inahusisha kuweka upya mabomba makubwa mapya na kujenga tenki la maji lenye mita za ujazo 500,000, mashine kubwa nne (4) za kusukuma maji na ulazaji wa bomba jipya la inchi 16 lenye uwezo wa kusafirisha maji kiasi cha lita 360,000 kwa saa; na

(vi) imeendelea na ujenzi wa Jengo la huduma katika Hosteli za Dkt. J. P. Magufuli ambapo jengo hilo linahusisha maduka, *ATM, Hair Salons, Dry cleaner, Dispensary, Mgahawa na Supermarket.*

### **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**34. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 4,873 kati yao Shahada za awali 4,208 (Wanawake 1,361 na Wanaume 2,847) na Shahada za Umahiri wanafunzi 194 (Wanawake 79 na Wanaume 115) na masomo yasiyo ya Shahada (*Non-degree Programme*) wanafunzi 471 (Wanawake 192 na Wanaume 279);

(ii) imeanzisha kampasi mpya iliyopewa jina la Waziri Mkuu mstaafu Mhe. Mizengo Peter Kayanza Pinda katika Mkoa wa Katavi ambayo itatoa masomo ya Stashahada, Astashahada na Shahada katika nyanja za Kilimo na Mifugo. Uanzishwaji wa Kampasi hiyo unalenga kutekeleza malengo ya Serikali ya awamu ya tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda. Kampasi hii itasogeza huduma za kitaalamu kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi na Mikoa ya jirani;

(iii) imeendelea kuviongezea uwezo vitengo vyake vya uzalishaji vikiwemo: Vitengo vya kuzalisha mikate, maziwa na mbogamboga; na

(iv) imeimarisha Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza, kumbi za mikutano na Idara ya Huduma za Afya kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani ya chuo na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

**35. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la Tafiti na Ushauri elekezi, Serikali kupitia Chuo imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na miradi mipya 13 ya utafiti yenye lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi ili kuwezesha wananchi kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda;

(ii) imetoa huduma ya elimu ya ushauri wa kitaalamu kwa wakulima 9,500 kwa kutumia vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija na kupunguza umaskini kwa wananchi. Mafunzo hayo yametolewa kwa wakulima katika mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Iringa, Dodoma, Tabora, Tanga, Pwani na Morogoro;

(iii) imeandaa na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa ya: kilimo *Nane Nane* yaliyofanyika kitaifa Mkoani Simiyu na kuwafikia takribani wadau 8,000; Kamisheni ya Tume ya Vyuo Vikuu; Kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine na Maonesho ya zana za Kilimo kwa lengo la kutoa elimu kuhusu kilimo na ufugaji; na

(iv) imepima jumla ya sampuli 1,553 zikiwemo sampuli za udongo 1,180, za mimea 297, za mbolea za viwandani 20, za samadi tisa (9) na sampuli za maji 47 kutoka kwa watafiti, Mashirika ya kilimo, Viwanda na Taasisi mbalimbali pamoja na wakulima binafsi kupitia maabara yake ya udongo iliyopo Idara ya Sayansi ya Udongo na Jiolojia.

**36. Mheshimiwa Spika**, ili kujenga uwezo wa wafanyakazi na wanafunzi katika kufanya tafiti za kisayansi na kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi, Serikali imeingia mikataba mipya 13 ya mahusiano na Taasisi nyingine za ndani

na nje ya nchi. Taasisi hizo ni pamoja na: Chuo Kikuu cha Sophia kilichopo Japan; *National Institute of Health - Korea*; *Foundation Pierre Fabre - France*; *Kunming Institute of Zoology, Chinese Academy of Science*; *Silverlands Tanzania Limited - Iringa, Tanzania*; *College of Animal Science and Technology Nanjing Agricultural University - China*; *Agronomos Sin Fronteras Foundation (ASFF) - Iringa Tanzania*; *University of Leeds – UK*; na *Wuhan University (WHU) – China*.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imejenga jengo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja litakalokuwa na maabara nane (8) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kila moja na madarasa nane (8) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kila moja kwa gharama ya **shilingi bilioni 11.5**. Kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza changamoto ya ufinyu wa nafasi za kufundishia na kujifunzia uliopo chuoni;

(ii) imenunua vifaa mbalimbali vya maabara, kemikali za kufundishia na samani za ofisi;

(iii) imekamilisha ujenzi wa jengo la utafiti wa wanyama na wadudu - *Animal House* kwa ufadhili wa mradi wa *Eastern and Southern Africa Centers of Excellence for Innovative Rodent Pest Management and Biosensor Technology Development (ACE II, IRPM and BTD)*;

(iv) imeendelea na ukarabati wa madarasa likiwemo jengo la *Hay Building* kwa lengo la kuongeza nafasi za kufundishia na kujifunzia;

(v) imeendelea na ukarabati wa karakana za uhandisi kilimo ambao umelenga kuboresha karakana za uhandisi kilimo hivyo kukamilika kwake kutawapa fursa wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo kwa kutumia vifaa vya kisasa; na

(vi) imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufunga mfumo wa mawasiliano - *wireless point* kwenye kumbi za mikutano na maeneo yanayozunguka chuo. Aidha,

chuo kinaendelea kuboresha mifumo ya kurusha matangazo kwa njia ya runinga na redio ili "SUA *media*" iweze kuwafikia wananchi wengi.

**38. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeboresha shamba kwa kupanda mazao ya Taifa ya kimkakati kwa kuandaa eneo lenye ukubwa wa hekari 200 kwa ajili ya kupanda zao la katani ambapo hekari 80 zimepandwa na zoezi la upandaji linaendelea. Uboreshaji wa shamba hilo umechochewa na matrekta yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, chuo kimeboresha shamba darasa kwa kufunga vifaa vya kisasa vya kilimo na kupanda mazao ya kitaifa ya kimkakati kama vile zabibu, pamba, katani, kakao, kahawa, mananasi, migomba na mazao ya mbogamboga.

**39. Mheshimiwa Spika**, ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali imeanzisha Programu zifuatazo;

(i) Shahada za Umahiri tisa (9) ambazo ni: *MSc. Seed Technology and Business; MSc. Horticulture; MSc. Environmental Sciences, Management and Technology; MSc. Hydrogeology and Water Resources Management; MSc. Public Health Pest Management; MA. Development Planning and Policy Analysis; MSc. Acquacture; PhD. Agribusiness na PhD. Agro-ecology;*

(ii) Shahada za kwanza mpya nne (4) ambazo ni: *Bachelor of Agricultural Investment and Banking; BA Human Resources, Management and Labour relations; BA in Development planning and Management na BSc in Bee Resources management;* na

(iii) Programu zisizo za Shahada katika fani mbili (2) ambazo ni *Certificate in Tour Guiding and Hunting Operations na Diploma in Crop Production and Management.*

## **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,329 wa Shahada na Stashahada na kuongeza fursa za elimu kwa wanafunzi;

(ii) imeongeza idadi ya moduli kutoka 40 hadi kufikia 155 zinazotolewa kwa kutumia jukwaa la TEHAMA. Vilevile, imeongeza usajili wa wanaotumia jukwaa la TEHAMA kutoka wanafunzi 715 hadi kufikia wanafunzi 2,597 kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa elimu;

(iii) inaendelea na ujenzi wa kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu - *Center of Excellence in Cardiovascular Sciences* ambapo kazi ya kimuundo, *skimming* ya jengo na uwekaji wa dari katika chumba cha mikutano umekamilika na uwekaji wa umeme na mifumo ya mtandao unaendelea;

(iv) inaendelea kutekeleza tafiti 102 ambapo 31 ni mpya na zimepata ufadhili. Tafiti hizi zimejikita katika maeneo mbalimbali ya magonjwa ambukizi, yasiyoambukiza na magonjwa yasiyopewa kipaumbele; na

(v) imefanya maboresho katika "Shule ya Tiba Meno" ikiwemo kufanya ukarabati wa chumba kwa ajili ya kutolea huduma binafsi na mchakato wa kupatikana kwa vifaa tiba unaendelea.

## **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,393 kwa lengo la kutoa fursa ya elimu ambapo wanafunzi wa Shahada ya kwanza 4,127, Shahada ya Umahiri 200 na Shahada ya Uzamivu 66;

(ii) imeendelea kufanya miradi ya tafiti 43 yenye lengo la kutatua changamoto katika jamii ili kuboresha maisha yao kwa ujumla;

(iii) imeandaa jumla ya machapisho 37 ya tafiti zilizokamilika kwa ajili ya kuongeza maarifa katika jamii kuhusu kutatua changamoto katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, uboreshaji wa makazi na usanifu wa majengo;

(iv) imetoa mafunzo kwa jamii kuhusu usimamizi bora wa Ardhi na Sheria za Ardhi kwa wakazi wa Wilaya za Mkuranga, Kisarawe na Nachingwea yaliyolenga kupunguza migogoro ya ardhi. Aidha, imetoa mafunzo kuhusu utengenezaji wa mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo kwa wakazi wa kata za Igawa, Mabadaga, Uburaku, Igurusi, Ruiwa, Utengule, Rujewa, Mswiswi na Madibira katika Wilaya ya Mbarali;

(v) imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kuhusu usanifu majengo, utayarishaji wa mipango ya kuendeleza miji na uthamini ikiwemo ujenzi wa Shule ya Mfano Dodoma na jengo la ofisi za Uhamiaji Dodoma, jengo la Mahakama ya Wilaya ya Chato na kuandaa *Master Plan* ya Mji wa Mafinga;

(vi) inaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 ili kuongeza sehemu za malazi; na

(vii) imewezesha wafanyakazi 48 kwenda masomoni wakiwemo wanataaluma 37 (Uzamivu 25 na Umahiri 12) na wafanyakazi waendeshaji 11.

## **Chuo Kikuu Mzumbe**

**42. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Mzumbe imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya wanafunzi 11,967 na kati ya hao, wanafunzi 5,310 ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza

(Astashahada 411, Stashahada 598, Shahada ya Kwanza 3,587; Shahada ya Uzamivu 14);

(ii) imegharamia masomo kwa watumishi 103 wakiwemo wa Shahada ya Uzamivu 67, Shahada ya Umahiri 27 na Shahada ya Kwanza 9;

(iii) imeandaa na kuchapisha Makala 104 katika majarida mbalimbali ya ndani na nje ya nchi; sura za vitabu ("book chapters") 10, pamoja na kitabu kimoja kwa lengo la kusambaza matokeo ya tafiti na kazi mbalimbali za kitaaluma ili kutoa maarifa yanayolenga kutatua changamoto katika jamii. Aidha, utekelezaji wa miradi 26 ya utafiti katika maeneo mbalimbali ikiwemo uchumi wa viwanda unaendelea; na

(iv) imeendelea na ujenzi wa madarasa na kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na ofisi zenye uwezo wa kuchukua wafanyakazi 50 katika Kampasi Kuu; ukarabati na uwekaji wa samani katika majengo ya Tegeta, Kampasi ya Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchukua takribani wanafunzi 1,500 pamoja na maktaba, maabara ya kompyuta na ofisi za wafanyakazi. Aidha, imekamilisha ukarabati wa hosteli mbili (2) katika Kampasi ya Mbeya, pamoja na hosteli tatu (3) na nyumba saba (7) za watumishi katika Kampasi Kuu.

## **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**43. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 27,133 wakiwemo wapya 10,447 na 16,686 wanaoendelea na masomo;

(ii) imejengea uwezo wafanyakazi 441 ambapo wafanyakazi 234 walipata mafunzo ya muda mfupi na 207 mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Astashahada (10), Stashahada (22), Shahada ya kwanza (11), Shahada ya Umahiri (77) na Shahada ya Uzamivu (87);



(iii) imeajiri wafanyakazi 61 wa kada tofauti ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi;

(iv) inaendelea na ujenzi wa jengo la kitengo cha huduma za mionzi katika hospitali ya chuo kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji huduma za mionzi kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii; na

(v) imeendelea na ukarabati wa majengo ya ofisi, makazi, mabweni, madarasa, miundombinu ya barabara pamoja na viwanja vya michezo ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

**44. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la Tafiti na Ushauri Elekezi, Serikali kupitia Chuo imefanya jumla ya tafiti 11 katika maeneo ya Elimu, Mazingira na TEHAMA. Vilevile, imetoa huduma za ushauri nne (4) katika nyanja za TEHAMA na elimu ili kuongeza ufanisi wa huduma mbalimbali zinazotolewa katika jamii. Aidha, imejenga mahusiano na taasisi nyingine 49 katika nyanja za ubunifu, Afya na Elimu.

### **Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 7,231 wakiwemo Astashahada 1,363, Stashahada 1,148, Shahada ya kwanza 4,448 na Shahada za uzamili 272. Aidha, imepata ithibati ya programu mbili (2) za Shahada ya Umahiri;

(ii) imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 64 (wahadhiri 55 na wafanyakazi waendeshaji 9) ambapo Shahada ya Uzamivu ni 42, Shahada ya umahiri 20, Shahada ya Kwanza mmoja (1) na Stashahada mmoja (1);

(iii) imetekeleza mradi wa kutoa mafunzo ya kilimo, biashara na ujasiliamali (Skills Development Fund) kwa wanafunzi wa mwaka wa pili na wa tatu wa shahada za kwanza ili

kuwajengea uwezo wa kujiajiri pindi watakapomaliza masomo;

(iv) imeandaa machapisho manne (4) ya utafiti yanayohusu ushirika na biashara, sayansi jamii, sheria na mazingira kwa lengo la kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau mbalimbali; na

(v) imetoa mafunzo kwa vyama 101 vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) katika wilaya 61 za Tanzania Bara yaliyofadhiliwa na "*Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance* (MIVARF)". Mafunzo hayo yalilenga kuvijengea uwezo Vyama vya Ushirika katika usimamizi na uendeshaji.

**46. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ukarabati na upanuzi wa mabweni tisa (9) ambapo mabweni sita (6) yapo katika Kampasi Kuu ya Moshi na matatu (3) katika kituo cha Kufundishia Kizumbi kilichopo Shinyanga. Ukarabati huo umewezesha upatikanaji wa nafasi mpya 460, matundu ya vyoo 40 na mabafu 38 na kufanya mabweni hayo kuwa na jumla ya nafasi 962, matundu ya vyoo 68 na mabafu 66; na

(ii) imekamilisha ujenzi wa kaferia yenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza maeneo ya utoaji wa huduma ya chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi pamoja na ukuta wenye urefu wa mita 200 kwa lengo kuimarisha usalama wa wanafunzi na mali za chuo.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**47. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,198 wakiwemo wanafunzi wa mafunzo ya awali 1,009, Astashahada 517, Stashahada

175, Shahada ya kwanza 1,532, Shahada ya Umahiri 903 na Shahada ya Uzamivu 62 kwa lengo la kuongeza fursa za elimu;

(ii) imekamilisha uwekaji wa kompyuta 20 katika maabara ya kituo cha mkoa wa Geita na kompyuta mpakato 20 katika Mkoa wa Mara na kufunga mfumo wa mawasiliano kwa lengo la kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA;

(iii) imeimarisha mtandao wa kujifunzia kwa njia ya masafa kwa kutengeneza programu mpya 35 ambapo kati ya hizo 30 zilipitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu;

(iv) imefanya ukarabati wa ukumbi wa Mitihani katika Kituo cha Mkoa wa Mwanza na kuendelea na miradi ya ujenzi katika vituo vya mikoa ya Manyara na Geita;

(v) imeendesha mafunzo ya wiki mbili kwa walimu 837 wa Shule za Msingi wanaosomea Stashahada ya Ualimu wa Shule za Msingi ' *Diploma in Primary Teachers Education – DPTE* ' kwa mwaka wa kwanza na wa pili katika vituo vifuatavyo: Chato (237), Korogwe (145), Mtwara (85), Njombe (130) na Singida (240) ili kuwaongezea ujuzi wa utendaji kazi;

(vi) imeunganisha mfumo wa kujifunzia (OUTLeMS) na mfumo wa rejesta ya wanafunzi (SARIS) ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ambapo kwa sasa mifumo hii inafanya kazi pamoja; na

(vii) imeimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kuzindua maabara tatu (3) za Sayansi katika masomo ya Kemia, Fizikia na Bailojia zilizopo katika kituo cha Kinondoni.

### **Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia**

**48. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa mitaala 35 ikiwemo Shahada za Sayansi 26 na Astashahada za taaluma za Sayansi za kilimo tisa (9);
- (ii) imeajiri watumishi 82 kati yao wahadhiri ni 42 na waendeshaji ni 40; na
- (iii) imeendelea na jitihada za upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo ya chuo kama ifuatavyo:
  - (a) imepata hatimiliki ya ekari 231 zikiwemo ekari 95 katika kampasi ya Kinesi Halmashauri ya Rorya na ekari 136 kampasi ya Kisangura Wilaya ya Serengeti;
  - (b) inaendelea kukamilisha taratibu za kupata umiliki wa ekari 61 kutoka eneo la Oswald Mang'ombe ambapo awali lilikuwa ni shule ya sekondari;
  - (c) inaendelea kukamilisha umiliki wa eneo la BAIC lenye ukubwa wa ekari 1,512 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Butiama ambalo litakuwa makao makuu ya chuo; na
  - (d) inaendelea na majadiliano ili kupata eneo katika Hospitali kuu ya Rufaa Mkoa wa Mara na eneo la Kwangwa kwa ajili ya Stadi za Afya na Sayansi shirikishi.

## **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**49. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,943 kati ya hao Shahada ya kwanza ni 1,878 na Stashahada ya Uzamili 65;
- (ii) imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (iii) imefanya jumla ya Tafiti 14 za sayansi na teknolojia zenye lengo la kutatua changamoto za kijamii; na

(iv) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 6,315 (Wanaume 3,535 na Wanawake 2,780) ili kuongeza fursa za elimu;

(ii) imetoa mafunzo kwa wahadhiri kuhusu namna ya kuandaa mihtasari ya sera - *Policy brief writing*, usimamizi wa wanafunzi wa shahada za juu - *Postgraduate supervision* na namna bora ya kubadilisha maudhui ya kwenye Tasnifu (*Dissertation*) kuwa Machapisho (*Journal Paper*) katika majarida ya kitaifa na kimataifa ili kuongeza maarifa, weledi na ufanisi katika utendaji kazi;

(iii) imeendelea kutekeleza miradi mitano (5) ya utafiti na imeanza utekelezaji wa miradi saba (7) mipya katika nyanja za kilimo, afya, na mabadiliko ya tabia nchi. Tafiti hizo zinalenga kutafuta njia salama za kukabiliana na wadudu waharibifu wa mazao;

(iv) imetoa jumla ya machapisho 24 katika nyanja mbalimbali za kitaaluma zenye lengo la kuongeza maarifa, weledi na ufanisi katika utendaji kazi; na

(v) imewezesha jumla ya wafanyakazi 75 kwenda masomoni wakiwemo wanataaluma 71 (Wanaume 46 na Wanawake 25) na waendeshaji wanne (4) kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

### **Chuo cha Ufundi Arusha (ATC)**

**51. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo cha Ufundi Arusha imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 1,129 wa mwaka wa kwanza ambapo ngazi ya Astashahada na Stashahada ni 911 na Shahada 218 (NTA Level 4-8);

(ii) imeendelea na ukarabati wa nyumba 68 za watumishi zilizojengwa mwaka 1975 wakati chuo kinaanzishwa pamoja na ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira wanayoishi wafanyakazi na wanafunzi;

(iii) imekamilisha ujenzi wa jengo la kufundishia matumizi ya nishati jadidifu ya umeme wa jua lenye uwezo wa kuchukua washiriki 20 na ufungaji wa mtambo wa uzalishaji wa Umeme wa jua wa kilowati moja, ambapo vijana 98 wameshapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya nishati hiyo;

(iv) imekamilisha ujenzi wa tanki kubwa la kuhifadhia maji lenye uwezo wa mita za ujazo 675 pamoja na nyumba ya pampu na mifereji ya umwagiliaji. Kukamilika kwa miundombinu hiyo itaongeza ufanisi katika utoaji wa mafunzo kwa vitendo inayohusisha teknolojia za umwagiliaji na hivyo kuzalisha wataalamu wa umwagiliaji wenye uzoefu;

(v) imekamilisha ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*) cha Kikuletwa kwa asilimia 40. Mradi ukikamilika utaweza kuzalisha umeme wa kW 70 na utachangia katika uzalishaji wa wataalam wa umeme utokanao na nguvu za maji (Hydropower) wanaohitajika katika miradi ya uzalishaji umeme wa nguvu ya maji. Kazi zilizokamilika ni pamoja na:

(a) ujenzi wa barabara (access roads) zenye jumla ya urefu wa kilometa 4.3 kwa kiwango cha changarawe (gravel standards) na kuwezesha kituo kufikika kwa urahisi;

(b) ujenzi wa nyumba mbili (2) za kisasa zenye uwezo wa kuchukua familia nne (4) zitakazotumiwa na wataalam watakaokuwa wanafanya tafiti mbalimbali kuhusiana na nishati jadidifu; na

(vi) imesanifu na kutekeleza mradi wa kufunga taa za kuongozea magari barabarani katika Jiji la Arusha kwa kushirikiana na ofisi ya TANROADS kwa lengo la kuongeza usalama kwa watumiaji wa barabara katika jiji hilo.

**52. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimeendelea kutoa Ushauri wa Kitaalamu katika miradi ifuatayo:

(i) usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi katika Vyuo vya VETA (Kasulu, Ruangwa, Kongwa na Nyasa); Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ishirini (20) na Vyuo vya Ualimu tisa (9);

(ii) upimaji wa udongo katika miradi ya Upanuzi wa Maji Safi na Taka katika Jiji la Arusha; Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Arusha, ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati na ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji Kivingo – Lushoto, Tanga; na

(iii) upimaji lami katika miradi ya ukarabati wa barabara Bariadi – Slama A, Lamadi – Wigelekelo na Bariadi – Kisesa na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Arusha.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**53. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,142 wakiwemo Astashahada 368, Stashahada 719 na Shahada 3,055;

(ii) imefunga viti 326 visivyohamishika katika jengo jipya la mihadhara hivyo kuimarisha na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iii) imegharamia mafunzo kwa watumishi 10 wakiwemo Shahada ya Uzamivu saba (7) na Umahiri watatu (3) katika vyuo vya ndani; na

(iv) imeendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika kampasi ya Zanzibar lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha malazi kwa wanafunzi.

## **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**54. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili wanafunzi 302,626 katika kozi ndefu na fupi kwenye Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kati yao wanafunzi wa kike ni 112,453 sawa na asilimia 37;

(ii) imefanya upanuzi na ukarabati wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 11 katika mikoa ya Pwani, Manyara, Lindi, Singida, Arusha, Mbeya, Mara, Mwanza pamoja na Halmashauri ya Karagwe, Makete na Kituo cha Dakawa;

(iii) imefunga vifaa na mitambo ya kisasa kwenye karakana za Mtwara, *Morogoro Vocational Teacher Training Center (MV TTC)*, Kihonda, na Arusha kwa lengo la kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iv) imeendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi 42 ambavyo vinajumuisha: Vyuo vipya vitatu (3) vya Mikoa ya Kagera, Geita, Rukwa; na kufanya upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi kumi (10) ambavyo ni; Kitangali, Ileje, Nkasi, Ndolage, Kanadi, Samunge, Nyamidaho, Mabalanga, Gorowa, Simanjiro; pamoja na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vipya 29 vya Wilaya za Kongwa, Kasulu, Ruangwa, Nyasa, Chunya, Kilindi, Korogwe, Ukerewe, Butiama, Igunga, Pangani, Kishapu, Rufiji, Uyui, Kwimba, Bahi, Mafia, Longido, Nkinga, Uvinza, Ikungi, Isimani, Lushoto, Mbalali, Monduli, Buhigwe, Ulanga, Masasi na Butiama kwa utaratibu wa *Force Account*;



(v) imeboresha karakana na kuweka zana za kisasa za kilimo katika Chuo cha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) cha Arusha kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo na hivyo kuwaongezea wanafunzi stadi na uwezo wa kiutendaji;

(vi) imeendelea kuongeza fursa kwa watoto wa kike kujiunga na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga bweni la wasichana na nyumba ya mtumishi katika chuo cha Wilaya ya Makete;

(vii) imeendelea kuongeza fursa za mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga Karakana za ufundi magari, bomba na uashi katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Lindi;

(viii) imeboresha utoaji mafunzo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuunganisha Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi 27 katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na

(ix) imefanikiwa kupata Hati Miliki za maeneo ya Vyuo vya Wilaya vya Ufundi Stadi vya Ukerewe, Ulanga, Chunya, Babati na Kwimba kwa lengo la kulinda maeneo hayo yasivamiwe na jamii inayozunguka.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

**55. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi ili kuhakikisha kuwa vijana wengi wanapata Stadi, Ujuzi na Maarifa stahiki. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili jumla ya wanafunzi 3,062 (Wanaume 1,184 na Wanawake 1,878) wa Astashahada 99 (wanaume 22 na wanawake 77), Stashahada 2,867 (wanaume 1,121 na Wanawake 1,746) na Shahada 96 (Wanaume 41 na wanawake 55);

(ii) imesajili wanafunzi 13,036 wa sekondari wanaosoma Nje ya Mfumo Rasmi wakiwemo Wanaume 5,411 na Wanawake 7, 625;

(iii) imeendelea kusimamia ubora katika uendeshaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi ambapo mitihani ya utamilifu ilifanyika katika mikoa 21 ya Tanzania Bara;

(iv) imefanya mapitio ya mitaala ya programu tatu (3) za Usimamizi wa Elimu Masafa (*Management of Distance Education*) NTA level 4 - 8; Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii (Adult Education and Community Development NTA level 4 - 8) na Usimamizi na Utawala wa Elimu ya Watu Wazima (Adult Education Management and Administration NTA level 4 - 8); na

(v) imeboresha Mkakati wa Kuendeleza Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy - NALMES) ili uendane na mahitaji ya sasa.

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imekarabati madarasa mawili (2) na kuweka viti 173 katika kituo cha Luchehele Mwanza ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, imenunua vifaa kwa ajili ya kufanya mafunzo ya uongezaji thamani mazao ya samaki katika kituo cha Luchehele Mwanza.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**57. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 5,738 (Wanawake: 1,182 na Wanaume: 4,556) kati ya wanafunzi hao Stashahada 2,680, Shahada 3,043, Shahada ya Umahiri ya Uhandisi Ujenzi 6, Stashahada ya Juu ya Elimu ya Ufundi 2 na Shahada ya Uzamivu ya Uhandisi Ujenzi 6;

(ii) imeendelea na tafiti na bunifu zilizofadhiliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) zinazohusu kutengeneza ndege inayoendeshwa bila rubani (*Drone*), 3D Printa pamoja na programu ya simu inayoonesha na kutoa maelezo ya maeneo na mitaa ambayo huduma za kijamii na kiuchumi zinatolewa;

(iii) imeendelea na ujenzi wa maktaba itakayogharimu kiasi cha **Shilingi 5,523,685,496.00** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi imekamilika na jengo limeanza kutumika hivyo kupunguza changamoto ya nafasi ya maktaba katika chuo;

(iv) imefunga jumla ya taa 20 za kisasa zinazotumia nishati ya jua kuzunguka eneo la chuo, kampasi ya Mbeya na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kupunguza gharama za nishati;

(v) imetathmini eneo lenye hekta 511 kupitia Mamlaka ya Ardhi, Nyumba na Makazi ikishirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya ikiwa ni hatua za kupanua eneo la chuo;

(vi) imetathmini hekta 500 kuzunguka Kampasi ya Rukwa kupitia Mamlaka ya Ardhi, Nyumba na Makazi ikishirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga kwa lengo la kuongeza ukubwa wa eneo la kampasi ya Rukwa;

(vii) imekamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja na hivyo kupunguza changamoto ya madarasa inayotokana na ongezeko la wanafunzi;

(viii) imekamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la vyumba viwili (2) vya mihadhara na vyumba vya madarasa vitatu (3) litakalokuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 800; na

(ix) imekarabati ofisi 80 zilizo chini ya majengo ya chuo (basements offices) ili kuongeza nafasi za ofisi kwa

wafanyakazi 320 pamoja na kufunga viti visivyohamishika katika madarasa matano (5) ili kuboresha mazingira ya kusomea kwa wanafunzi.

### **Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

**58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 2,025 wakiwemo Stashahada 956, Shahada ya Kwanza 1,027 na Shahada ya Umahiri 42. Aidha, imeendelea kuhudumia wanafunzi 2,309 wanaondelea na masomo na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 4,334; na

(ii) imefanya mashindano ndani ya Taasisi ya kuwatambua wanafunzi wabunifu 26 na kuwazawadia wanafunzi bora zaidi katika ubunifu. Aidha, bunifu zilizofikia hatua ya kuendelezwa kwa lengo la kubiasharishwa ni pamoja na uundaji wa gari aina ya "buggy" (Manufacturing of a buggy vehicle), teknolojia ya ufuatiliaji wa ndege angani (Aircraft Tracking System) na mashine ya kutengenezea vitofali vya vitalu (Manufacture of a Concrete Paver Making Machine).

**59. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto mbalimbali Taasisi imeendelea kutekeleza miradi saba (7) ya tafiti za kijamii ambayo ni:

(i) kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini;

(ii) kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa kilimo cha umwagiliaji unaotumia nguvu za jua kwa kutumia maji ya kisima;

(iii) kutengeneza mfumo wa kuhifadhi, kusambaza na kuchakata taarifa za bioanwai nchini;

(iv) kuboresha teknolojia ya mfumo wa usimamizi wa hospitali na vituo vya afya ambao kwa sasa unatumika katika hospitali ya Amana kwa majaribio;

(v) kutengeneza mfumo wa Mawasiliano yasiyotumia nyaya kwenye magari yasiyo na dereva;

(vi) kukamilisha kusanifu na kutengeneza mashine ya kuchakata kahawa kwa kigezo cha rangi utakaosaidia wakulima wa kahawa kuongeza mnyororo wa thamani; na

(vii) kutengeneza injini itakayotumia mfumo wa gesi asilia.

**60. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii ili kutatua changamoto za kijamii kwa kukamilisha miradi 12 na kuendeleza miradi 38. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) kufanya upembuzi yakinifu na usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu mbalimbali katika Vyuu 12 vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Pwani, na Rufiji;

(ii) kutoa ushauri wa kitaalamu wa kuandaa mkakati wa kuboresha mawasiliano wa kitaifa (National Broadband Strategy) chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;

(iii) kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la kufanyia matengenezo ya ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius K. Nyerere; na

(iv) kupima ubora wa vifaa vya ujenzi katika miradi miwili mikubwa ya kimkakati ambayo ni mradi wa kufua umeme wa maji (Julius Nyerere Hydropower Project) na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway).

**61. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Taasisi imejenga, imekarabati na kufanya upanuzi wa majengo katika kampasi zake tatu kama ifuatavyo:

(i) upanuzi wa jengo la maktaba (Vertical Extension of DIT Library) pamoja na kuweka samani na miundombinu ya TEHAMA katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na hivyo

kuongeza uwezo wa matumizi ya Maktaba kutoka wanafunzi 150 hadi 450 kwa wakati mmoja;

(ii) ukarabati wa miundombinu ya Kampasi ya Mwanza ikiwemo maabara na ununuzi wa mashine ya kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi kupitia mradi wa "Skills Development Fund (SDF)" kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA);

(iii) ujenzi wa jengo la maabara ya Kompyuta, darasa na bwalo la chakula katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe;

(iv) imeendelea kupitia na kuboresha Mitaala 14 kwa ngazi za Stashahada, Shahada na Shahada ya Umahiri ambapo mitaala nane (8) ni maalumu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ajira Kitaifa na kikanda katika fani ya TEHAMA na teknolojia za ngozi;

(v) imepata ithibati ya mtaala wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Madini na ya Umahiri wa Uhandisi katika Nishati Endelevu ambapo wanafunzi 59 wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Madini na wanafunzi 9 wa Shahada ya Umahiri wa Nishati Endelevu wamedahiliwa; na

(vi) imeanza utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa miaka mitano ujulikanao kama "*East Africa for Transformation and Regional Integration Project – EASTRIP*". Mradi huu una lengo la kuanzisha vituo vya umahiri vya kikanda katika fani za TEHAMA na teknolojia ya uzalishaji wa bidhaa za ngozi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao ulitekeleza kazi zifuatavyo:

(a) kuwajengea uwezo wasimamizi na watekelezaji wa mradi;

(b) kuratibu ujenzi wa mabweni manne (4) ya wanafunzi na majengo mawili (2) ya vituo vya umahiri katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam;

(c) kuandaa miongozo ya utekelezaji wa mradi; na

(d) kuratibu ununuzi wa magari manne (4) ya mradi.

**62. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kutekeleza miradi mikubwa mitatu (3) ya kubiasharisha bunifu ambayo ni: ufungaji wa taa za barabarani katika eneo la daraja la Ruvu mkoani Pwani; ufungaji wa taa za kuvukia waenda kwa miguu mkoani Manyara na kuhuisha mfumo wa miito ya huduma kwa wateja (call center) wa TANESCO. Aidha, imeandaa maandiko manne (4) ya miradi ya utafiti kwa ajili ya kupata fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi. Miradi hiyo ni pamoja na:

(i) Elimu ya Nishati Jadidifu (Education for Renewable Energy Technology Center);

(ii) Uendelezaji vipaji vya uvumbuzi katika mafunzo ya uhandisi (Leading Invention in Engineering Education);

(iii) Uboreshwaji wa uongozi wa elimu ya juu katika Bara la Afrika (African Higher Education Leadership in Advocacy (AHEAD)); na

(iv) Uandaaji wa Kanzidata ya vifaa vya utafiti katika taasisi za elimu ya juu na utafiti (Development of Equipment catalogue of higher learning and Research and Development institutions).

### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM- AIST)**

**63. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha imetekeleza yafuatayo:

(i) Imeongeza udahili kutoka wanafunzi 116 hadi 602 sawa na ongezeko la asilimia 24;

(ii) imeandaa sera mbalimbali za chuo ikiwa ni pamoja na Sera ya Utafutaji Rasilimali na Uwekezaji, Sera ya Utafiti na Ubunifu na Sera ya Hatimiliki kwa lengo la kuboresha utendaji wa Taasisi na ukusanyaji maduhuli; na

(iii) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti katika kilimo, maji, TEHAMA na usalama wa chakula kama vile uzalishaji wa miche bora ya ndizi inayohimili magonjwa ya kitropiki na kuondoa sumu kuvu katika nafaka na kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa kimeta kwa wanyama pori na wanaofugwa.

**64. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imetekeleza tafiti na bunifu mbalimbali ambapo baadhi ya tafiti zimeonesha matokeo chanya kwa kuja na teknolojia mbalimbali zinazoweza kutumika katika maendeleo ya viwanda nchini ambazo ni:

(i) kanuni ya madawa asilia yatokanayo na magome ya miti yanayoweza kutumika katika uchakataji wa ngozi ili kuengeneza bidhaa mbalimbali (kama vile viatu, mikamba na mikoba);

(ii) kiuatilifu cha kumdhibiti mdudu maarufu kwa jina la kanitangaze '*Tuta absoluta*' ambaye hushambulia nyanya na mahindi shambani; na

(iii) kanuni ya utengenezaji wa unga lische '*Nutritional formulation*' ili kutatua changamoto za utapiamlo kwa mama na mtoto.

#### **Tathmini ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo**

**65. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha elimu yetu inaendana na mahitaji ya mipango ya nchi yetu na soko la ndani, kikanda na kimataifa, Serikali imeendelea kuziwezesha taasisi zetu zenye majukumu ya kutathmini ubora na utoaji wa elimu kama ifuatavyo.

#### **Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA**

**66. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania imetekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha Uchapaji, Usafirishaji na Usahihishaji wa mitihani ya Kitaifa ya Darasa la Nne ambapo jumla ya



watahiniwa 1,667,552 walifanya upimaji kati ya watahiniwa 1,787,034 waliokuwa wamesajiliwa; Kidato cha Pili ulijumuisha Watahiniwa 571,670 kati ya 609,386 waliokuwa wamesajiliwa na Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) ulikuwa na jumla ya Watahiniwa 933,369 kati ya 947,077 waliokuwa wamesajiliwa. Aidha, Mitihani ya Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT) ilifanyika ambapo jumla ya Watahiniwa 473,724 wa Kidato cha Nne walifanya mtihani kati ya 485,737 waliokuwa wamesajiliwa na jumla ya Watahiniwa 11,985 walifanya Mtihani wa Maarifa (QT) kati ya 12,985 waliokuwa wamesajiliwa;

(ii) imekamilisha Usajili wa Watahiniwa wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2020 ambapo jumla ya Watahiniwa 85,525 wamesajiliwa;

(iii) imekamilisha usajili wa Watahiniwa wa Mtihani wa Ualimu kwa mwaka 2020 ambapo jumla ya Watahiniwa 8,574 wamesajiliwa kufanya Mtihani huo; na

(iv) imekamilisha Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Sampuli ya wanafunzi 33,313 wa Darasa la Pili (2019) uliofanyika tarehe 28 hadi 29 Januari, 2020.

## **Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania - TCU**

**67. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Vyuu Vikuu imetekeleza yafuatayo:

(i) imeratibu maombi 99,014 (Wanaume 57,328 na Wanawake 41,686) ya wanafunzi walioomba kujiunga na masomo ya Shahada ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2019/20. Kati ya maombi hayo, waombaji 87,813 wamedahiliwa katika vyuu mbalimbali vya Elimu ya Juu hapa nchini;

(ii) imepokea maombi 457 ya waombaji wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi ambapo maombi 393 yaliidhinishwa na maombi 64 yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo;

(iii) imeandaa Mwongozo wa waombaji wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi ili kuhakikisha wanafunzi kutoka Tanzania wanaenda kusoma vyuo vinavyotambulika. Aidha, imefanya ukaguzi wa Taasisi saba (7) zinazoshughulikia usajili na upelekaji wanafunzi kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzisajili;

(iv) imeratibu programu mbalimbali za kuwajengea uelewa wanaotaka kujiunga na Elimu ya Juu nchini kupitia vyombo vya habari na kambi za Jeshi la Kujenga Taifa Tanzania Bara na Visiwani ambapo jumla ya Vijana 19,196 walifikiwa;

(v) imetoa ithibati ya Chuo cha Tumaini Ndaki ya Dar es Salaam (TUDARCo) na ithibati 170 za Programu kati ya hizo 93 ni mpya na 77 zilipitiwa upya na kuridhiwa;

(vi) imetathmini na kutambua tuzo 1,502 zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nje ya nchi;

(vii) imefanya ufuatiliaji wa masuala ya ubora katika vyuo vikuu nane (8) ili kijiridhisha kama vinafuata miongozo ya Tume;

(viii) imeratibu mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu (3) wanaoendelea na masomo ya Shahada za Umahiri na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 26 kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa watumishi;

(ix) imeratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 604 wa taasisi nufaika wa mradi wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi (ESPJ) kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wa uzalishaji kwenye sekta sita za kipaumbele (Kilimo Biashara, Utalii na Ukarimu, Ujenzi, Uchukuzi, Nishati na TEHAMA). Aidha, mafunzo haya yalihusu Usimamizi wa Programu mbalimbali katika Taasisi, Utunzaji Kumbukumbu, Mfumo wa Bajeti na Masuala yahasuyo Ukaguzi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa watumishi;

(x) imechapisha kitabu kinachoeleza “Hali ya Elimu ya Juu nchini, 2018” ili kutoa taarifa mbalimbali kuhusu vyuo, wanafunzi na watumishi wa vyuo vya Elimu ya Juu;

(xi) imeendelea kufanya maboresho ya mfumo wa kukusanya taarifa uitwao *University Information Management System - UIMS* ambapo Bodi za Mikopo za Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania Bara na Visiwani ziliunganishwa ili kurahisisha utoaji wa taarifa mbalimbali za Taasisi za Elimu ya Juu nchini;

(xii) imeratibu maonesho ya 14 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu mambo mbalimbali yahasuyo elimu ya juu ambapo jumla ya taasisi 84 za ndani na nje ya nchi zilishiriki; na

(xiii) imeshiriki kwenye mikutano kuhusu masuala ya uthibiti ubora katika Elimu ya Juu iliyoratibiwa na Umoja wa Afrika na IUCEA.

### **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

**68. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa elimu ya ufundi, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2019/20 imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya ufundi 109 ambapo vyuo 103 vilipatiwa ushauri kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo, Vyuo viwili (2) vilifutiwa usajili, na vyuo vinne (4) vilizuliwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika;

(ii) imesajili vyuo 24 katika bodi za masomo katika fani zifuatazo:- Afya na Sayansi Shirikishi - 12, Biashara, Utalii na Mipango - 9, Sayansi na Teknolojia Shirikishi - 2 na Elimu na Uwezeshaji wa Kujifunza - 1;

(iii) imehakiki Mitaala 65 iliyokuzwa na vyuo vya ufundi, imeidhinisha programu 7 na kukagua vyuo 17 ili kuhakikisha elimu na mafunzo yanayotolewa yanalingana na vigezo vilivyowekwa na Baraza;

(iv) imeratibu na kuhakiki udahili wa Wanafunzi 151,969 (Wanaume 81,523 na Wanawake 70,446) katika ngazi ya

Astahada ya Awali, Astahada na Stahada katika fani za Sayansi na Teknolojia Shirikishi; Afya na Sayansi Shirikishi; Biashara, Utalii na Mipango; na Uwezeshaji wa Ufundishaji na Kujifunza;

(v) imefanya tathmini ya vyeti vya wahitimu 16,549 vilivyopokelewa kwa ajili ya kutoa namba ya uthibitisho (*Award Verification Number* - AVN) ili kudhibiti uendeshaji wa mafunzo bila kufuata kanuni na sheria zilizowekwa na Baraza. Aidha, utoaji wa AVN umesaidia kuepusha udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na elimu ya juu;

(vi) imetoa mafunzo kuhusu Mitaala inayozingatia Umahiri kwa wakufunzi 608 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi yatakayosaidia wahitimu kuwa mahiri katika ujuzi uliokusudiwa;

(vii) imetoa ithubati kwa vyuo 19 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi vyuo 11, Biashara, Utalii na Mipango vyuo vinne (4) na Sayansi na Teknolojia Shirikishi vyuo vinne (4);

(viii) imefanya utafiti katika sekta 6 ambazo ni *Construction, Agribusiness and Agroprocessing, Energy, Tourism and Hospitality, Transport and Logistics* na *ICT* kwa lengo la kubaini pengo la ujuzi lililopo ili kuviwezesha vyuo na taasisi kutoa elimu na mafunzo yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira; na

(ix) imeunganisha mifumo ya udahili na mitihani ili kuwezesha kuwasiliana na mifumo ya vyuo 32 vya elimu ya ufundi iliyotengenezwa kwa lugha mbalimbali (*Coding Language*) ambayo itarahisisha mawasiliano kati ya Baraza na vyuo.

## **Uwezeshaji wa Utoaji wa Elimu na Mafunzo**

**69. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha elimu yetu inatolewa kwa ufanisi na tija, Serikali imeendelea kuwezesha Taasisi zenye majukumu ya kuwezesha mifumo ya elimu na ujifunzaji kuhakikisha unafanyika katika mazingira yenye

kuleta tija na ufanisi na kuhakikisha na vitabu vyenye kufaa katika shule zetu. Taasisi hizo zimetokeleza yafuatayo.

**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)**

**70. Mheshimiwa Spika**, kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Taasisi ya Elimu Tanzania imetokeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha kazi ya uandishi, kuchapa na kusambaza aina nane (8) za vitabu vya kiada vya Darasa la VI kwa masomo ya Kiswahili, Hisabati, English, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na Kifaransa kwa kuzingatia mtaala wa mwaka 2015 unaolenga umahiri. Jumla ya nakala 2,962,155 zimesambazwa katika Halmashauri za Mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa uwiano wa 1:3;

(ii) imeandaa na kusambaza nakala 272,000 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote nane (8) kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ufundishaji wa masomo husika;

(iii) imechapa na kusambaza nakala za vitabu 1,359,350 vya masomo yote kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I-V kwa matumizi ya shule zinazotumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia yaani *English Medium Schools* na hivyo kuondoa changamoto ya upatikanaji wa vitabu kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza;

(iv) imekamilisha uandishi wa vitabu vya kiada kwa Darasa la VI kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Vitabu hivyo vinapatikana katika maktaba mtandao na nakala ngumu ipo katika hatua ya uchapaji;

(v) imechapa na kusambaza katika Halmashauri zote nakala 440,000 za kitabu cha kiongozi cha mwalimu kwa Darasa la I na II nchini ili kumwezesha Mwalimu kuutekeleza mtaala wa Darasa la I na II kwa ufanisi zaidi;

(vi) imechapa na kusambaza nakala 719,905 za vitabu vya kiada vya Elimu ya Awali na kufikia uwiano wa 1:3 pamoja na nakala 41,642 za Mwongozo wa Mwalimu wa kufundishia Elimu ya awali;

(vii) imekamilisha kazi ya uandishi, kuchapa na kusambaza aina 15 ya vitabu vya kiada kwa masomo ya Historia na Jiografia ngazi ya Sekondari (O-level), pamoja na masomo ya Sayansi (Biology, Chemistry, Physics na Basic Mathematics) na Kiswahili kidato cha 5 na 6 ili kurahisisha upatikanaji wa vitabu. Jumla ya nakala 1,567,537 zimesambazwa kwa (uwiano wa 1:3) katika Halmashauri za Mikoa 26 ya Tanzania Bara;

(viii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu. Jumla ya nakala 8,750 za vitabu hivi zimegawanywa katika Halmashauri zote zenye wanafunzi wenye uoni hafifu kwa uwiano wa 1:1;

(ix) imeandika, kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada vya nukta nundu (Braille) aina 18 kwa Darasa la I, II, na V kwa ajili ya wanafunzi wasioona. Jumla ya nakala 11,402 za vitabu vya nukta nundu (braille) na Mchoro mguso (embossed drawing) vimesambazwa kwa uwiano 1:1 katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara;

(x) imechapa katika maandishi ya nukta nundu (braille) na kusambaza nakala 200 za Mtaala wa Darasa la I – VII katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara;

(xi) imefanya tathmini ya machapisho 80 ya kielekroniki yaliyopokelewa ambapo machapisho 11 yalipewa ithibati yakiwa na maboresho madogo, 38 yalikuwa na maboresho makubwa na machapisho 31 yalikalaliwa;

(xii) imeandaa na kusambaza aina 47 za vitabu vya ziada vya nukta nundu kwa ajili ya masomo ya sekondari kwa kushirikiana na Shirika la *Siloam International for Blind*. Jumla ya nakala 5,100 zimesambazwa katika shule zote zenye wanafunzi wasioona Tanzania Bara na Visiwani;

(xiii) inaendelea kufanya mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Ualimu kupitia **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya**

**Ualimu** ili uendane na mtaala wa Elimu ya msingi na mahitaji ya sasa;

(xiv) inaendelea kuimarisha upatikanaji wa vitabu kupitia huduma ya maktaba mtandao (TIE- online library) ambapo wanafunzi wanapata vitabu vya kiada, ziada, na machapisho mengine ya TET kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na vyuo vya Ualimu. Maktaba hii inawawezesha wanafunzi kujisomea na hivyo kuimarisha utamaduni wa kujisomea.

**71. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeendelea kuandaa na kusambaza miongozo na mihtasari mbalimbali yenye lengo la kuimarisha ufundishaji wa wanafunzi kwa kuzingatia vitabu vinavyotolewa na taasisi kama yafuatayo:

(i) imeandaa Mwongozo wa Mwalimu Mshauri wa Darasa la Elimu ya Awali, Darasa la I na II ambao utatumika kutoa mafunzo kwa walimu kazini;

(ii) imeandaa miongozo mitano (5) ya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia mbinu ya michezo kwa Darasa I – IV itakayosaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuibua udadisi wa wanafunzi;

(iii) imeandaa mwongozo wa kutekeleza mtaala wa Elimu ya Sekondari unaozingatia mahitaji ya wanafunzi viziwi na kusanifisha Lugha ya Alama nchini ili kuboresha ufundishaji kwa wanafunzi hao;

(iv) imeandaa mwongozo wa mafunzo ya Lugha ya Alama ili kuwawezesha wakufunzi kutekeleza Mtaala wa Astashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum; na

(v) imetafsiri mtaala na mihtasari ya Astashahada ya Ualimu kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza ili kuwezesha vyuo vya Serikali na vyuo binafsi kuandaa walimu wa ngazi ya Astashahada wenye uwezo wa kufundisha shule za msingi kwa kutumia lugha ya Kiingereza.

**72. Mheshimiwa Spika**, uboreshaji wa mitaala ni moja ya majukumu ya Taasisi ya Elimu Tanzania wenye lengo la kuhakikisha nchi inakuwa na mitaala yenye kuwanda vijana wetu kuendana na mahitaji ya mipango ya nchi, kikanda na kimataifa. Utekelezaji wa jukumu hili unahusisha pia uelimishaji wa watumiaji wa mitaala husika ili waweze kuzingatia maboresho wakati wa utoaji wa elimu. Katika kufikia azma hiyo, Serikali kupitia Taasisi imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha mafunzo kwa wathibiti ubora, Maafisa Elimu na Maafisa Elimu Kata kuhusu mtaala ili kuwawezesha kufuatilia utekelezaji wa mtaala shuleni na vyuoni;

(ii) imetoa mafunzo kabilishi kwa walimu 592 wa Shule Zisizo za Serikali, kwa ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi yaliyolenga kuwawezesha kutekeleza kwa ufanisi mtaala ulioboreshwa; na

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 431 wa Shule Zisizo za Serikali kwa ngazi ya Elimu ya Sekondari ambayo yatawawezesha walimu kutekeleza mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri kwa ufanisi.

### **Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania imetekeleza Miradi ifuatayo:

(i) inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 81 (madarasa matatu (3) kwa kila shule) katika shule za msingi 22 na shule za sekondari tano (5) zenye uhitaji mkubwa. Aidha, inajenga mabweni 16 ya wasichana katika shule 16 za sekondari (kidato cha 5 na 6) zilizo katika mazingira hatarishi;

(ii) inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 40 za walimu; (Nyumba 4 kwa kila shule) katika shule za sekondari 10;



(iii) inajenga mabweni matatu (3) katika shule 3 za msingi na ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa, chumba maalum (Audiology room); na

(iv) inaendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 528 (matundu 24 kwa kila shule) katika shule za msingi 18 na shule za sekondari nne (4) zenye uhitaji mkubwa.

## **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**74. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Taasisi za Elimu nchini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu imetekeleza yafuatayo:

(i) imesajili walimu 2,806 kati ya walimu 2,521 waliopangwa kusajiliwa, sawa na ongezeko la asilimia 11, katika kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA), Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule (DSI), na Astashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (CELMA). Lengo ni kuwajengea uwezo wa kuthibiti utoaji wa elimu bora shuleni, kuongoza na kusimamia rasilimali katika taasisi za elimu, hususan shule za msingi na sekondari;

(ii) imetoa Mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 yaliyolenga kuboresha utendaji katika kuongoza, kusimamia na kuendesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(iii) imetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Taaluma (Pedagogical Leadership) **kupitia mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu** kwa wajumbe 245 wa Menejimenti za Vyuo kutoka vyuo vya Ualimu 35 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia utoaji wa elimu bora kwa Wanachuo tarajali;

(iv) imetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu ngazi ya Mkoa na Wilaya (Sekondari na Msingi) 383 ambayo yalilenga kuwapatia uwezo wa kuongoza, kupanga, kusimamia na kufanya tathmini ya shughuli za elimu katika maeneo yao ya kazi;

(v) imetoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Sekondari pamoja na Maafisa Elimu Kata 985 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Mwanza, Geita na Kilimanjaro kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuongoza, kupanga, kusimamia na kufanya tathmini ya shughuli za elimu katika maeneo yao ya kazi;

(vi) imetoa mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Shule kwa Wakuu Shule 89 za Sekondari zilizo chini ya madhehebu ya Kikristo (CSSC) kutoka mkoa wa Arusha, Kilimanjaro na Manyara pamoja na Wakuu wa Shule 20 kutoka shule zinazomilikiwa na BAKWATA kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuongoza, kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa shughuli za utoaji elimu katika ngazi ya shule;

(vii) imetoa mafunzo kwa wawezeshaji wa kitaifa 74 (Trainer of Trainers) kwa lengo la kuwapatia uwezo wa kuwezesha Wajumbe wa Kamati za Shule za Msingi katika mikoa minne (4) ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe kwa ajili ya kusimamia utoaji wa elimu kwa shule za msingi;

(viii) imetoa mafunzo kuhusu Kupambana na Rushwa, Kujikinga na Maambukizi ya UKIMWI na elimu kuhusu kuzuia Majanga kwa watumishi 67 na Wanachuo 2,324 katika Kampasi za Bagamoyo, Mbeya na Mwanza;

(ix) imeandaa moduli ya uendeshaji mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Shule za Msingi pamoja na Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule kwa lengo la kutoa mwongozo wa utoaji wa elimu bora ngazi ya shule; na

(x) imeimarisha mazingira ya kufundishia, kujifunzia na mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu - ADEM kwa kukarabati nyumba nne (4) za watumishi, ofisi tatu (3) na madarasa manne (4).

## Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**75. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetekeleza yafuatayo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 132,119 hadi kufikia Machi, 2020 wakiwemo 49,799 wa mwaka wa kwanza na 82,320 wanaoendelea na masomo ili kutoa fursa ya wahitaji wa Elimu ya Juu;

(ii) imefanya ukaguzi kwa waajiri 2,406 nchi nzima na kutambua wanufaika wapya 14,731 wenye mikopo iliyoiva yenye thamani ya Shilingi Bilioni 100.7 ambapo kati yao wanufaika 13,969 (94%) wameanza kulipa. Aidha, hadi kufikia Disemba, 2019 idadi ya wanufaika wanaorejesha mikopo ilikuwa imefikia 176,952 kati ya 184,166 waliotarajiwa sawa na asilimia 96 ya lengo;

(iii) imetoa jumla ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 449.99** kwa wanafunzi 132,119 kati ya **Shilingi bilioni 450** iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 sawa na asilimia **99**.

(iv) imeendelea na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 144.3** kati ya **Shilingi bilioni 166.1** zilizolengwa katika kipindi cha mwezi Juni 2019 hadi Machi 2020 sawa na asilimia 86.9 zimekusanywa. Lengo la makusanyo kwa mwaka ni **Shilingi bilioni 221.5**;

(v) imefungua ofisi ya Kanda katika Mkoa wa Mtwara na kufikisha jumla ya ofisi sita (6) za Kanda ambazo ziko katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na Zanzibar ili kusogeza huduma za mikopo ya Elimu ya Juu karibu na wananchi pamoja na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mikopo iliyoiva;

(vi) imeendelea kuboresha mifumo ya uendeshaji ili kuongeza uwazi na ufanisi wa utoaji huduma katika upangaji, utoaji na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva. Aidha, mifumo imeboreshwa

na kumuwezesha mwanafunzi kupata taarifa za mkopo wake kupitia simu ya mkononi au mtandaoni (Student's Individual Permanent Account – SIPA) na kuondoa usumbufu wa wanafunzi kufuatilia taarifa hizo kwenye ofisi za Bodi; na

(vii) imebuni mfumo unaoviwezesha vyuo kuambatisha nyaraka muhimu kama vile matokeo ya mitihani kupitia mtandao badala ya kutuma nakala ngumu. Vilevile, uboreshaji wa mifumo umehusisha uunganishaji wa mifumo ya TEHAMA ya Bodi ya Mikopo na ya Tume ya Vyuo Vikuu ambapo taarifa za udahili za waombaji wa mikopo zinapatikana kwa urahisi na kwa wakati.

**76. Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha jamii kupata taarifa za huduma zinazotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Serikali imeendelea na kampeni za uelimishaji kuhusu mikopo kama ifuatavyo:

(i) imeendesha programu za elimu katika shule na kambi 17 za Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu sifa, vigezo na taratibu za uombaji wa mikopo kwa wanafunzi waliomaliza masomo ya kidato cha sita (6) na kujiandaa kujunga na taasisi za Elimu ya Juu; na

(ii) imeandaa na kuendesha vipindi 30 vya Redio na Televisheni kuhusu umuhimu wa kurejesha mkopo wa Elimu ya Juu ambapo waajiri, wanufaika na wanafunzi walipata fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)**

**77. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 551 katika Chuo cha Ukutubi, Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu (*School of Library Achieves and Documentation Studies - SLADS*) ili kiongeza upatikanaji wa wataalamu Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka nchini; na

(ii) imewezesha upatikanaji wa jumla ya vitabu 310,490 ambapo vitabu 1,673 vilipatikana kwa mujibu wa sheria, vitabu 308,801 vilipatikana kwa msaada na vitabu 16 kwa fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya magazeti na majarida 4,906 yalipatikana (magazeti 4,788 na majarida 118). Upatikanaji wa vitabu, magazeti na majarida hayo vimeongeza fursa kwa wasomaji katika maktaba za Mikoa 22, Wilaya 19 na Tarafa 2.

### **Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)**

**78. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imetekeleza fuatayo:

(i) imebaini mahitaji ya ubunifu na namna ya kujenga uwezo kwa wabunifu 60 wa MAKISATU na kuwapatia mafunzo katika nyanja za ulinzi miliki bunifu, ujasiriamali, ubiasharishaji na usimamizi wa mikataba;

(ii) imeandaa siku maalum ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo watafiti, wabunifu, wawekezaji, watunga sera na wananchi 207 walikutanishwa na kujadili namna ya ukuzaji na uendelezaji wa bidhaa za wabunifu kibiashara;

(iii) imeendesha kongamano la ubunifu lijulikanalo kama *AfricaLICS* lililofanyika Novemba, 2019 ambapo washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni walihudhuria. Kongamano hilo lililenga kutoa elimu kuhusu masuala ya ubunifu;

(iv) imeshiriki katika maonesho na mikutano mbalimbali ambapo kazi za wabunifu na watafiti zilioneshwa na kusambazwa kama ifuatavyo:

(a) Watafiti na wabunifu 26 walionesha kazi zao na wananchi 576 walitembelea banda katika viwanja vya maonesho ya Sabasaba - Dar es Salaam;

(b) imetoa elimu kuhusu *biotechnology and biosafety* na kupokea maoni kutoka kwa washiriki 800 wakijumuisha Wakulima, Watafiti, NGOs na Wananchi katika maonesho ya Nanenane katika mikoa ya Dodoma, Simiyu na Morogoro;

(c) imetoa elimu kuhusu majukumu ya Tume kwa wageni 456 waliotembelea banda la Tume katika maonesho ya vyuo vikuu (Wageni 300) na maonesho ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Wageni 156); na

(d) imetoa mafunzo kwa Washiriki 230 kutoka nchi 29 ulimwenguni kuhusu masuala ya utafiti na matumizi ya ushahidi wa kisayansi katika kutunga sera na kutoa maamuzi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mafunzo hayo yalitolewa katika mkutano wa Mabaraza uliofanyika Novemba, 2019 uliokuwa na kaulimbiu "Sayansi Wazi na Shirikishi katika Utafiti na Ubunifu kwa Maendeleo."

(v) imeelimisha na kuhamasisha matumizi ya tafiti, sayansi, teknolojia na bunifu kwa umma wa watanzania kwa kuandaa na kusambaza machapisho ya tafiti na bunifu yakiwemo *promotional materials* 2,000, mabango 8, vijitabu 500 na vipeperushi maalum 1,000. Aidha, ilifadhili makala za magazeti 212, vipindi 211 vya redio na runinga, Makala maalum (*documentary*) tatu (3) na vipindi mubashara vinne (4) vya runinga na redio kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya tafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu;

(vi) imeendelea kugharamia uanzishaji wa Kituo cha Teknolojia cha mfano *pilot technology station* kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje;

(vii) imeratibu na kufadhili zoezi la kuwapata na kuwawezesha wabunifu wawili (2) kushiriki katika mashindano ya kimataifa ya ubunifu (SLUSH 2019) yaliyofanyika nchini Finland;

(viii) imeboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini na kuwawezesha kusajili na kutoa jumla ya vibali vya utafiti 449 kati ya maombi 580 ikilinganishwa na vibali 406 vilivyotolewa mwaka wa fedha 2018/2019;

(ix) imetathmini na kufanya ufuatiliaji wa miradi 12 ya utafiti na ubunifu (kutoka watafiti wa nje wakishirikiana na watafiti wazawa) iliyopewa vibali vya utafiti kutoka COSTECH ili kujiridhisha na utekelezaji wa taratibu za vibali na misingi ya ushirikiano wa utafiti kwa maendeleo na kuainisha mapungufu yaliyoshughulikiwa; na

(x) imeendesha Mikutano minne (4) na wadau muhimu wa utafiti nchini ambao ni Vyuu Vikuu, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za utafiti na OR - TAMISEMI na kuweka mikakati ya pamoja ya utaratibu wa kieletroniki inayounganisha taasisi za utafiti na waratibu wa tafiti nchini.

### **Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)**

**79. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2019/20, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki imetekeleza yafuatayo:

(i) imepokea na kutathmini maombi 469 ya leseni za kutumia, kumiliki, kusafirisha na kuingiza nchini vyanzo vya mionzi ambapo leseni 447 sawa na asilimia 95 zimetolewa. Aidha, maombi 22 hayakukidhi vigezo;

(ii) imekagua migodi mitano (5) ambayo ni Buzwagi Gold Mine, North Mara Gold Mine, Bulyankulu Gold Mine, Mkuju River Project na Oceanic na kubaini kuwa haina madhara ya mionzi kwa mazingira na wafanyakazi;

(iii) imekagua na kuhakiki vituo 384 vya vyanzo vya mionzi nchi nzima ambapo ukaguzi huo ulibaini kuwa vituo 369 vilikuwa vinaendeshwa kwa kufuata taratibu husika na vituo 15 vilikuwa vinatumia vyanzo vya mionzi bila kufuata utaratibu wa kiusalama. Aidha, vituo vitano (5) vilitimiza masharti na hivyo vimeruhusiwa kuendelea na kazi zake;

(iv) imesajili vituo vipya 58 kwa ajili ya kuanza kutumia vyanzo vya mionzi na hivyo kufikia jumla ya vituo 985 vilivyosajiliwa;

(v) imewapima wafanyakazi 1,743 kwenye vituo 400 sehemu

mbalimbali nchini. Upimaji huo ulibaini kuwa katika vituo vyote viwango vya mionzi vilikuwa kati ya 0.1mSv hadi 4.5mSv ambavyo ni salama kwa binadamu;

(vi) ilisafirisha vyanzo vya mionzi 14 vilivyokwisha muda wa matumizi kutoka Wakala wa Barabara Tabora na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa lengo la kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na vyanzo hivyo vikiachwa kuhifadhiwa bila utaratibu;

(vii) ilipima sampuli 19,462 na kutoa vibali 29,613 vilivyojumuisha sampuli za vyakula 16,563, mbolea 363, na sigara pamoja na matumizi mengine kama chakula cha mifugo zilikuwa sampuli 2,536. Sampuli zote zilizopimwa hazikuwa na mionzi hatarishi;

(viii) imeendelea kuratibu miradi mitano (5) ya kitaifa na kushiriki katika miradi 45 ya kikanda ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu. Miradi hii inanufaisha sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Maji, Elimu na Mifugo;

(ix) ilinunua vifaa viwili (2) vya kupima mionzi (Sodium Iodide Detector) kwa ajili ya ofisi mbili (2) za kanda na vifaa vingine mbalimbali vya maabara kwa ajili ofisi 18 za mipakani vyenye thamani ya Shilingi 227,949,660.00. Vifaa hivi vimesaidia kuongeza kasi ya utoaji wa vibali ndani ya siku moja ili kulinda usalama wa wananchi, mazingira na kulinda masoko ya bidhaa zetu nje ya nchi;

(x) imeendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma na ufanisi katika utendaji wa kazi za Tume. Vilevile, Tume imepata mshauri elekezi kwa ajili ya michoro ya maabara za kanda zilizopo Dodoma, Zanzibar na Mwanza;

(xi) imeendelea na upimaji wa mionzi kwenye mazingira katika vituo 14 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine. Pia, imepima usalama wa mionzi kwenye ofisi za wizara zote na makazi ya viongozi



pamoja na maeneo yatakayokuwa na miradi mikubwa ya maendeleo kama vile maeneo ya ujenzi wa uwanja wa ndege jijini Dodoma;

(xii) imeendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZPRN64) kilichopo kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*. Upimaji wa usalama wa mionzi kwenye anga ni muhimu kwa kuendelea kulinda usalama wa mazingira yetu dhidi ya uchafuzi wa mionzi;

(xiii) imekagua vituo 41 vinavyotoa mionzi isiyoayonishwa (Non- Ionizing Radiation) kama vile minara ya simu, redio, runinga, na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika;

(xiv) imeendelea kujitangaza kwa kutumia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na vipindi vya Televisheni na Redio pamoja na mitandao ya jamii. Vilevile, Tume ilishiriki katika maonesho matano (5) pamoja na vipindi 24 vya redio na 26 vya runinga. Aidha, vipeperushi na vijarida 3,000 vilisambazwa kwa lengo la kuelimisha wananchi na kuongeza uelewa kuhusu kazi za Tume, usalama wao na faida za matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia; na

(xv) ilitoa mafunzo kwa maafisa 137 wa vyombo vya ulinzi na usalama na kuendesha mafunzo 14 ya muda mfupi ya kinga na udhibiti wa mionzi kwa taasisi na vituo mbalimbali vinavyotumia vyanzo vya mionzi ambapo wafanyakazi 270 walipatiwa mafunzo.

## **C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**80. Mheshimiwa Spika**, Mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 itatekelezwa kupitia Idara, Vitengo na Taasisi kama ilivyofafanuliwa katika majukumu ya Wizara. Malengo yatakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

## Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuvo vya Ualimu

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la kusimamia Sera na kuongeza upatikanaji wa fursa za Elimu na Mafunzo, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 zilizopatiwa usajili ili kuhakiki uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za usajili wa shule;

(ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 100 zilizosajiliwa kwa masharti ili kuona kama zimekamilisha miundombinu iliyokuwa haijakamilika;

(iii) itafanya ufuatiliaji na tathmini kwa shule 200 ili kuhakiki kama walimu wa kigeni wanafundisha kwa mujibu wa leseni zao;

(iv) itaandaa “Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ujenzi na Ukarabati wa Shule” ili kuwezesha wadau wote wa shule kufuatilia na kutathmini maendeleo ya ujenzi; na

(v) itakamilisha uandaaji wa mfumo wa Kieletroniki wa usajili wa shule za Awali na Msingi, Vyuvo vya Ualimu na Vituo Nje ya Mfumo Rasmi ili kuhakikisha usajili wa shule unafanyika kwa uwazi na wakati.

## Usimamizi wa Elimumsingi na Sekondari

**82. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha Elimumsingi na Sekondari, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa vituo Shikizi vya shule katika mikoa 15 ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kuchukua hatua stahiki;

(ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za Ufundi, Kilimo na shule za Michezo ili kutathmini hali ya miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) itaratibu mashindano ya insha ya nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC) kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kuandika na kujieleza;

(iv) itatoa mafunzo ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni kwa walimu 200 wa shule za sekondari ili kuwajengea uwezo na kuimarisha stadi za utoaji wa huduma za malezi shuleni;

(v) itasambaza Mwongozo wa “Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu” ili kuimarisha utoaji wa huduma za malezi shuleni;

(vi) itahuisha Miongozo na Nyaraka ya utekelezaji wa Programu ya MEMKWA Kudirika la II ili kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa vijana ambao hawakumaliza elimu ya msingi wenye umri kati ya miaka 14-18;

(vii) itachapisha na kusambaza Miongozo na Vitabu vya MEMKWA Kudirika la I ili kuimarisha/kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa wanafunzi nje ya mfumo rasmi (MEMKWA Kudirika la I) ili kuendana na mabadiliko ya Mtaala mpya wa mfumo rasmi wa shule darasa la I – IV;

(viii) itawezesha Vituo vya Walimu kutekeleza Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa kuandaa mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu ili kuendana na Mpango wa mafunzo endelevu kazini;

(ix) itaandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa shule za msingi kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;

(x) itawajengea uwezo Waratibu wa Vituo vya Ualimu na Maafisa Elimu Kata 966 kuhusiana na Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa kuzingatia Kiunzi cha Mafunzo Endelevu Kazini kwa Walimu (Teachers’ Continuous Professional Development Framework);

(xi) itaandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa wawezeshaji wa MEMKWA kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;

(xii) itawajengea uwezo wawezeshaji wa MEMKWA na mahitaji maalum ngazi ya Mikoa na Halmashauri; na

(xiii) itawajengea uwezo Maafisa Elimu Mikoa, Halmashauri, Kata na Walimu Wakuu kuhusu miongozo mipya ya usimamizi wa shule katika utekelezaji wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule.

### **Usimamizi wa Elimu Maalum**

**83. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu maalum, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21 imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendesha Mafunzo kazini kwa walimu wenye taaluma ya elimu maalum 350 wa shule za msingi na 150 wa shule za sekondari kuhusu Lugha ya Alama, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, na TEHAMA ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji shuleni;

(ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika shule za Sekondari 26, Msingi 52, Vyuo vya Kati vitatu (3) na Vyuo vikuu saba (7) vinavyopokea wanafunzi wenye ulemavu ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kutoa ushauri wa kitaalamu;

(iii) itawezesha ununuzi wa vifaa maalum vya kielimu na saidizi katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

(iv) itahamasisha jamii kupitia vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, na vikao maalum kuhusu utambuzi wa mapema, uandikishaji katika shule na utoaji wa huduma za kielimu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi zote za elimu.

## Usimamizi wa Elimu ya Ualimu

**84. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mafunzo ya Elimu ya Ualimu, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21 itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu zoezi la udahili, ufundishaji na ujifunzaji wa walimu tarajali pamoja na uendeshaji wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ili kubaini upungufu na kufanya maboresho; na

(ii) itaratibu na kusimamia mashindano ya michezo na Sanaa katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali (UMISAVUTA) ili kuimarisha elimu ya michezo na sanaa vyuoni.

## Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu

**85. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 6,020 zikiwemo shule za Msingi 4,700, Sekondari 1,200 na Vyuo vya Ualimu 120 pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu;

(ii) itawajengea uwezo wathibiti ubora wa shule wapya 200 watakaoteuliwa kujiunga na idara ya uthibiti ubora wa shule katika ngazi ya kanda na wilaya; na

(iii) itafanya tafiti tatu (3) za kielimu katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ili kubaini mafanikio na changamoto za utoaji wa elimu nchini na kutoa mapendekezo stahiki.

## Baraza la Mitihani la Tanzania

**86. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza la Mitihani la Tanzania litatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,825,387;
- (ii) kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,009,938;
- (iii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa watahiniwa 612,745;
- (iv) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 495,207 na Mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,044;
- (v) kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 90,182;
- (vi) kuendesha Mitihamu ya Ualimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa watahiniwa 8,135; na
- (vii) kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK kwa sampuli ya watahiniwa 33,350 wa Darasa la Pili mwezi Januari, 2021.

## **Taasisi ya Elimu Tanzania**

**87. Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) kuandaa aina nane (8) za vitabu (book titles) vya kiada Darasa la VII pamoja na viongozi vya mwalimu ili kutatua changamoto ya uwepo wa vitabu hivyo vinavyoendana na mtaala ulioboreshwa;
- (ii) kutafsiri aina tano (5) za vitabu vya kiada Darasa la VII kwa ajili ya matumizi ya shule zinazotumia lugha ya kiingereza;
- (iii) kuandaa vitabu vya kiada Darasa la VI na VII kwa matumizi ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona ili kuwawezesha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(iv) kuandika aina 40 za vitabu vya kiada ngazi ya sekondari ili kukidhi mahitaji ya mtaala;

(v) kuandaa vitabu vya kiada aina 40 kwa matumizi ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasioona kwa ngazi ya sekondari ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanajifunza kwa ufanisi;

(vi) kuandika miongozo 12 ya ufundishaji kwa njia ya vitendo (*practical manuals*) kwa kidato cha kwanza mpaka cha sita;

(vii) kutathmini vitabu vya ziada na maudhui ya kielektroniki yanayoandaliwa na wadau ili kuhakikisha kama vinakidhi mahitaji ya mtaala;

(viii) kuandaa maudhui ya kielektroniki kwa ngazi ya Elimu ya Msingi ili kurahisisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji; na

(ix) kuboresha mitaala ya Elimu ya Ualimu ngazi ya Astashahada na Stashahada na elimu ya sekondari ili kukidhi mahitaji ya sasa.

**88. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaandaa mfumo wa mafunzo ya walimu kazini kwa njia ya mtandao ili kukuza stadi na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) itaendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wathibiti ubora wa shule kuhusu mtaala ulioboreshwa ili kukuza stadi na mbinu za ufundishaji;

(iii) itafanya ufuatiliaji wa matumizi ya vifaa vya utekelezaji wa mtaala kama vile vitabu, mihtasari na viongozi vya mwalimu ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji mtaala;

(iv) itafanya tafiti za utekelezaji wa mtaala zitakazosaidia kuboresha ufundishaji na ujifunzaji; na

(v) itaandaa matini ya kidigitali na kurekodi vipindi vya redio na television ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji.

## **Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu-ADEM**

**89. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala utatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili walimu 2,483 watakaosoma kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule ili kuwapa ujuzi na maarifa katika utoaji na Usimamizi wa Elimu;

(ii) kujenga jengo la utawala, madarasa, maktaba na kompyuta katika Kampasi ya ADEM-Mbeya ili kuwezesha kuhudumia wanachuo 421 na kukarabati jengo la Kihistoria la zamani la ADEM pamoja na nyumba nne (4) za wafanyakazi kampasi ya Bagamoyo;

(iii) kutoa mafunzo kwa ngazi ya Astashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu (CELMA) kwa Wakuu wa Shule za Msingi 32 ili kuwajengea uwezo wa kuongoza na kusimamia Shule zao kwa ufanisi;

(iv) kuratibu mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa washiriki 250 ambao ni Wakuu wa Vyuo vya Ufundi Stadi (VET) na Wasaidizi wao, na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) kwa lengo la kuimarisha uongozi na usimamizi wa taasisi zao;

(v) kuratibu mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa viongozi 4,548 wakiwemo Wakuu wa Shule za Sekondari, Maafisa Elimu katika ngazi ya kata hadi Mkoa ili kuimarisha mbinu bora za uongozi na usimamizi wa Elimu;

(vi) kufanya tafiti tatu (3) kuhusu Uongozi na Usimamizi wa Elimu katika maeneo yenye changamoto na kutoa ushauri; na



(vii) kufadhili watumishi sita (6) katika mafunzo ya muda mrefu katika maeneo ya taaluma na 20 katika mafunzo ya muda mfupi.

### **Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**90. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (NALMES) ili kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika kwa kuwajengea uwezo maafisa na wataalamu wa kisomo;

(ii) itaboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi kwa mikoa 24 na kuongeza udahili kutoka wanafunzi 13,036 hadi 14,930;

(iii) itafanya utafiti wa kitaifa juu ya hali ya kisomo na elimu kwa umma utakaoboresha utekelezaji wa Mkakati wa Kisomo na Elimu kwa Umma;

(iv) itatekeleza miradi ya Elimu ya Watu Wazima ikiwemo: Mradi wa Elimu ya Sekondari kwa Wanafunzi walio Nje ya Mfumo Rasmi, Mpango wa Elimu changamani kwa vijana walio Nje ya Mfumo Rasmi (IPOSA) na Mradi wa kuwawezesha vijana na watu wazima kielimu;

(v) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Astashahada, Stashahada na Shahada kutoka 3,062 hadi kufikia 3,200; na

(vi) itajenga na kukarabati miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika vituo vilivyoko katika mikoa minne (4) ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro - WAMO na Mwanza.

### **Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)**

**91. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaongeza vitabu 40,000 na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya watu wazima na watoto ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii;
- (ii) itaendelea kutoa ushauri wa Kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo na Halmashauri za Miji na Wilaya nchini;
- (iii) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka katika ngazi ya Cheti cha Msingi (NTA 4) wanafunzi 400, Cheti (NTA 5) wanafunzi 300 na Stashahada (NTA 6) wanafunzi 300;
- (iv) itanza taratibu za ujenzi wa maktaba katika Mikoa ya Singida, Shinyanga, Simiyu na Dodoma pamoja na Wilaya ya Chato, na Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka – Bagamoyo na;
- (v) itakarabati majengo ya Maktaba za Mikoa ya Ruvuma, Songwe, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Rukwa, Kagera, Iringa na Tabora.

### **Mamlaka ya Elimu Tanzania**

**92. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itawezesha ujenzi wa madarasa 180 katika shule za Msingi 50 na Sekondari 10 zenye uhaba wa vyumba vya madarasa ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu;
- (ii) itawezesha ujenzi wa nyumba 100 za walimu katika Shule za Sekondari 25 zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu ili kuongeza ufanisi kwa walimu;
- (iii) itawezesha ujenzi wa mabweni 15 ya wanafunzi wa kike katika shule 15 za sekondari zenye mazingira magumu. Kukamilika kwa mradi huu kutanufaisha wanafunzi wa kike 1,200;
- (iv) itawezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 432 katika shule za msingi 13 na sekondari tano (5) zenye upungufu ili

kuboresha mazingira kwa wanafunzi na kupunguza magonjwa ya mlipuko;

(v) itawezesha awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule ya msingi ya kisasa inayotumia Kiingereza kufundishia katika jiji la Dodoma;

(vi) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na uboreshaji wa miundombinu katika Chuo Kikuu kimoja kutoka Zanzibar ili kuboresha upatikanaji wa Elimu ya Juu; na

(vii) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za Msingi nne (4) na Sekondari nne (4).

#### **Kituo cha Maendeleo Dakawa**

**93. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kupanda miti ya mbao aina ya mitiki 9,240 kuzunguka eneo lenye ukubwa wa ekari 140 ili kuhifadhi mazingira ya kituo;

(ii) kukarabati nyumba tano (5) za watumishi (2 in 1) zenye uwezo wa kubeba familia 10 na kuendeleza ujenzi wa nyumba mbili (2) ili kuboresha mazingira ya makazi kwa watumishi;

(iii) kuendeleza, kuhifadhi na kutunza kumbukumbu adhimu za nyaraka, majengo na makaburi ya makumbusho ya wapigania uhuru wa ANC; na

(iv) kupima eneo la kituo lenye ukubwa wa ekari 7,500 kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na kulipatia hati.

#### **Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**

**94. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itatoa mafunzo ya muda mrefu ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi (Folk Education) kwa washiriki wapatao 10,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuongeza ujuzi utakaowawezesha wahitimu kujijiri na kuajiriwa;

(ii) itawezesha mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 24,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza miradi na shughuli katika maeneo wanayoishi;

(iii) itawajengea uwezo wakufunzi 670 kutoka katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuwaongezea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na soko la ajira;

(iv) itaendelea kuratibu uhamasishaji kwa wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya Sayansi kwa lengo la kuwaongezea sifa za kujiunga na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(v) itaendelea kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuhakikisha elimu itolewayo inaendana na soko la ajira;

(vi) itawezesha maafisa 7 kushiriki mikutano ya ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwenye maeneo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nje ya Nchi ili kuwajengea uwezo wa kuratibu na kusimamia Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini;

(vii) itawezesha mkutano wa kimkakati wa Taasisi nne (4) ambazo ni Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu mafunzo na uandaaji wa Mitaala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(viii) itagharamia upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kote nchini

kwa lengo la kuhakikisha kuwa maeneo hayo hayavamiwi na wananchi wanaozunguka vyuo hivyo;

(ix) itaendelea kugharimia chakula katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54;

(x) itaendelea kuratibu ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 25 vya Wilaya (DRVTSC) kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Ufundi; na

(xi) itaendelea kuratibu uanzishwaji wa vituo vinne (4) vya umahiri kwenye nyanja za TEHAMA, Usafiri wa anga, Nishati jadidifu na Mazao ya ngozi katika Taasisi za DIT, NIT na ATC kupitia mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project* (EASTRIP) kwa lengo la kuviongezea vyuo hivyo uwezo wa kutoa mafunzo kwa vitendo yanayoendana na soko la ajira.

### **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itadahili jumla ya wanafunzi 2,800 wakiwemo wanafunzi 400 wenye mahitaji maalum na vijana 2,400 kutoka kwenye mazingira magumu ifikapo Juni, 2021;

(ii) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 370,000 hadi 700,000 ifikapo Juni, 2021 ikiwemo ongezeko la wanafunzi wa kike kutoka asilimia 35 hadi asilimia 45;

(iii) itatoa mafunzo kwa wajasiriamali 3,000 wa Sekta isiyo rasmi kupitia programu ya *INTEP* (Intergrated Training for Entrepreneurship Promotion) kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa uendeshaji wa shughuli zao za kiuzalishaji; na

(iv) itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Ufundi Stadi wa vyuo vya VETA na FDC kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa kufundisha kwa kupitia mradi wa SET (Skills for Employment Tanzania) unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi.

**96. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha utawala na usimamizi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mamlaka itatekeleza yafuatayo:

(i) itaboresha utendaji kazi kwa kutekeleza Muundo wa Mamlaka na *Scheme of Service* mpya na kuajiri watumishi wapya ili kuziba nafasi zilizo wazi;

(ii) itawajengea uwezo watumishi katika taaluma zao;

(iii) itaendelea kutangaza shughuli za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii kuhusu huduma zinazotolewa na mamlaka; na

(iv) itajenga nyumba 23 za watumishi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi kama ifuatavyo: Makete (6); Ulyankulu (10); Busokelo (2) na Namtumbo (5) pamoja na kukarabati nyumba saba (7) za watumishi wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizopo Tabata Dar es Salaam.

**97. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi itaendelea kuimarisha Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) kuimarisha mfumo wa utafiti pamoja na kufanya utafiti wa soko la ajira kwenye sekta tatu (3) za uchapishaji vitabu, biashara na sekta ya umeme;

(ii) kuanzisha kitengo cha unenepeshaji Ng'ombe kwenye Kituo cha Mafunzo na Kiwanda cha Nyama katika Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Dodoma pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Kituo cha Uchapaji kwenye Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Chang'ombe, Dar es Salaam;

(iii) kutoa elimu kwa wadau kuhusu matumizi ya taarifa za soko la ajira na kuratibu ukusanyaji wa taarifa za Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini; na

(iv) kuratibu utekelezaji wa mpango wa kukuza ujuzi viwandani - *Skills Enhancement Programme* (SEP) katika makampuni 60 ambao utawajengea uwezo wafanyakazi na kuwapelekea teknolojia mpya bila kulazimika kuhudhuria mafunzo vyuoni.

**98. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi na Huduma vya mikoa ya Kagera, Geita, na Rukwa. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa vyuo 30 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Wilaya za Monduli, Buhigwe, Butiama, Chemba, Chunya, Ikungi, Igunga, Kishapu, Kwimba, Chato, Mbarali, Mafia, Pangani, Ulanga, Uvinza, Kilindi, Korogwe, Longido, Masasi, Mkinga, Ukerewe, Uyui, Bahi, Iringa, Lushoto, Kongwa, Ruangwa, Nyasa, Kasulu na Rufiji ili kutoa fursa za mafunzo kwa jamii.

**99. Mheshimiwa Spika**, Serikali itajenga mabweni sita (6) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 kila moja, katika Vyuo mbalimbali vya Ufundi Stadi kama ifuatavyo: Namtumbo (2), Mbeya (1), Mara (1), Dakawa (1), na Makete (1) ili kutatua changamoto ya malazi. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa madarasa sita (6) katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Makete yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 160.

**100. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo vya ufundi stadi, Serikali itanunua na kuweka vifaa vipya vya kujifunzia katika vyuo vikongwe 29 vya Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini pamoja na kuvifanyia ukarabati. Aidha, itajenga karakana 12 kwenye Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma vya Mikoa ya Lindi, Pwani, Manyara, Kihonda, Kipawa na Mwanza. Aidha itakarabati karakana mbili (2) za Useremala na Uchomeleaji Vyuma katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Arusha.

## **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**101. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza litatekeleza kazi zifuatazo:

(i) litafuatilia na kutathimini Vyuo 200 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vya ubora;

(ii) litakagua na kuhakiki Vyuo 60 kwa ajili ya usajili wa Vyuo vitakavyokidhi sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, pamoja na kutoa miongozo itakayoviwezesha Vyuo kupata ithibati kamili endapo vitakidhi vigezo vilivyowekwa;

(iii) litahakiki na kuidhinisha Mitaala 150 ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira; na

(iv) litaratibu na kuhakiki udahili wa wanafunzi wapatao 150,000 katika programu za Astashahada na Stashahada.

## **Chuo cha Ufundi Arusha**

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo cha Ufundi Arusha kitatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kitadahili wanafunzi 1,390 wa mwaka wa kwanza kwa ngazi za Stashahada na Shahada (NTA level IV-VIII) na wanafunzi 1,000 wa ngazi ya Ufundi Stadi (NVA level I-III);

(ii) kitajenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja na maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ili kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) kitakarabati madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa maji safi na majitaka, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iv) kitakamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja litakalokuwa na maabara, madarasa na ofisi za walimu kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa lengo la kuboresha mazingira ya kusomea;



(v) kitaendeleza Kituo cha Mafunzo ya Nishati Jadidifu cha Kikuletwa ili kiwe Kituo cha Umahiri (Centre of Excellence) kupitia mradi wa EASTRIP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia;

(vi) kitafanya utafiti juu ya matumizi bora ya maji katika kilimo cha mpunga kwa kushirikiana na shirika la utafiti kutoka Japan (JIRCAS) ili kuwezesha wananchi kuongeza uzalishaji wa zao hilo kwa kutumia maji kidogo; na

(vii) kitaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa walengwa mbalimbali kuhusu uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara, kupima ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi wa aina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi wa taasisi husika.

### **Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

**103. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itatekeleza yafuatayo:

(i) itadahili wanafunzi 9,389 kwa mwaka wa masomo 2020/21;

(ii) itafanya tafiti 10 zenye lengo la kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili jamii katika maeneo ya Maendeleo ya uchumi 3, Jinsia na Maendeleo (2), Taaluma za jamii (3) na Maadili na Uongozi (2). Aidha, itaandika maandiko ya miradi ya utafiti mawili (2) kwa ajili ya ufadhili kutoka nje ya Chuo;

(iii) itafadhili watumishi wanataaluma 10 kwenda masomoni katika ngazi za Uzamivu na Uzamili ili kuongeza idadi ya wahadhiri;

(iv) kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Karume litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000

kwa wakati mmoja na jengo la Maktaba katika Kampasi ya Kivukoni kwa lengo la kuongeza udahili na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Aidha, itakarabati madarasa na nyumba za watumishi, barabara za ndani ya chuo, umeme pamoja na mifumo ya maji safi na majitaka; na

(v) itahuisha mitaala 34 ya chuo ili iendane na mahitaji ya soko. Aidha, itaboresha mfumo wa TEHAMA katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

### **Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu**

**104. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kuratibu maendeleo ya udahili, uandikishaji na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi katika Taasisi za Elimu ya Juu;

(ii) itaendelea kuratibu ufadhili wa masomo wa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka mashirika na nchi rafiki;

(iii) itaratibu ufadhili wa wanafunzi 10 raia wa China kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(iv) itafanya ufuatiliaji wa utendaji wa Vituo vya Umahiri vya Afrika katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini (African Centre of Excellence- ACE II) ambavyo vipo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;

(v) itaendelea kuratibu ufadhili wa masomo ya wanataaluma 68 kutoka Vyuo Vikuu vya Umma katika shahada za umahiri kwenye nyanja za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati;

(vi) itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa 'Higher Education for Economic Transformation' (HEET); na

(vii) itaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Vyuo Vikuu ili waweze kujifunza kwa ufanisi.

## Tume ya Vyuho Vikuu Tanzania

**105. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itakagua Vyuho Vikuu 25 kwa lengo la kuhakiki ubora wake;

(ii) itafanya tathmini ya programu 200 za masomo mbalimbali katika Vyuho Vikuu nchini na kuzisajili zile zitakazokidhi vigezo;

(iii) itafanya tathmini na kutambua tuzo 5,000 zilizotolewa katika Vyuho Vikuu nje ya nchi;

(iv) itaratibu udahili na kuhakiki maombi ya wanafunzi takribani 100,000 wa mwaka wa kwanza watakaooomba kudahiliwa katika Vyuho vya Elimu ya Juu katika programu mbalimbali;

(v) itaandaa miongozo ya ulinganifu (Benchmarks Standards) kwenye programu za masomo ya Uhandisi na Sayansi ya Tiba ya Binadamu;

(vi) itafanya utafiti ili kuweza kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yenye lengo la kufanya maboresho kwenye mfumo wa utoaji Elimu ya Juu nchini;

(vii) itakagua Asasi/Kampuni zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili;

(viii) itaboresha mfumo wa kutumia TEHAMA katika utoaji na ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji;

(ix) itashiriki katika makongamano na mikutano inayohusu uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini; na

(x) itaratibu maonesho ya 15 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na programu mbalimbali zinazotolewa.

### **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itatoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji **54,000** wa mwaka wa kwanza yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 199.8** ikilinganishwa na wanafunzi **49,799** waliopata mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 173.2** katika mwaka 2019/2020. Lengo la utoaji mikopo ni kuwawezesha wanafunzi wengi zaidi wa Kitanzania kupata Elimu ya Juu bila kuathiriwa na hali zao za kiuchumi na kijamii;

(ii) itatoa mikopo kwa wanafunzi 91,000 wanaoendelea na masomo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 264.2** ikilinganishwa na wanafunzi 82,320 waliopata mikopo katika mwaka wa fedha 2019/20;

(iii) itakusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 190** ili zitumike kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji na kuwa na sifa ya kupata mikopo;

(iv) itaendesha programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi katika shule 300 za sekondari na vyuo 70 ili kupunguza makosa yanayofanywa na waombaji wa mikopo wakati wa uombaji na hivyo kuwakosesha mikopo; na

(v) itatoa elimu kwa waajiri na wafanyabiashara katika mikoa 20 kuhusu umuhimu wa urejeshaji wa mikopo kwa wakati ili kuwezesha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo.

### **Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**107. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili wanafunzi 29,056 wa shahada za awali pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka 12,129 hadi 12,735 ambapo ufadhili wa masomo utatolewa kwa wanafunzi 50 wa kike wanaosomea masomo ya sayansi;

(ii) kuongeza idadi ya miradi ya tafiti kutoka 173 hadi 221 kwa kuwafadhili watafiti 40 katika maeneo yanayolenga uchumi wa viwanda na kuzingatia Ajenda ya Utafiti ya Taifa;

(iii) kuongeza idadi ya machapisho ya CKD katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 1,048 hadi 1,103;

(iv) kuongeza idadi ya majarida ya CKD ya kimataifa kutoka 13 hadi 16 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao ifikapo Juni 2021;

(v) Kugharamia wanataaluma 112 kusoma masomo ya uzamili katika fani mbalimbali; na

(vi) kukamilisha upanuzi wa Hosteli za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ghorofa mbili zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 hivyo kufanya Hosteli hizo kuweza kuchukua jumla ya wanafunzi 5,120.

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu tarajiwa ya Uchumi katika kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lenye ghorofa sita (6) ambalo litakuwa na ofisi 50 za wafanyakazi; ofisi za kukaa wanafunzi 60 wa masomo ya uzamili, kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 80 na sehemu ya huduma ya chakula yenye uwezo wa kuhudumia watu 120 kwa wakati mmoja.

**109. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya watumishi na wanachuo, Serikali itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la kituo cha wanafunzi ambapo kukamilika kwa jengo hili kutasaidia kuwa na sehemu za kujisomea, sehemu za kibenki, maduka, *saloon* za kike na

kiume, sehemu za vinywaji, kumbi za burudani na ofisi ya Mlezi wa Wanafunzi.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam**

**110. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili wanafunzi wa mwaka wa kwanza 1,900 kati yao 600 ni wa fani ya Sayansi;

(ii) kugharamia uendeshaji wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,850 ili kukazia maarifa yatolewayo kwa njia ya nadharia;

(iii) kuimarisha ufundishaji na utoaji wa huduma kwa kuajiri jumla ya wafanyakazi 164 kati yao wanataaluma ni 45 na waendeshaji ni 119;

(iv) kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kugharamia ununuzi wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi 68 pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma ili kuhakikisha kuwa watu wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa za elimu;

(v) kuandaa mitaala minne (4) mipya ya Stashahada za Uzamili, Shahada za awali na Uzamivu ili kuongeza fursa za wanufaika na Eimu ya Juu;

(vi) kufanya tafiti 20 zinazotatua matatizo ya jamii na kutoa huduma tano (5) za ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya elimu, sayansi na sayansi za jamii;

(vii) kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la utawala ili kuongeza ofisi hamsini (50) za wafanyakazi na vyumba vya utafiti na kujenga jengo la maabara za sayansi na vyumba vya kujifunzia ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa vitendo;

(viii) kuimarisha miundombinu kwa kukarabati mabweni na kumbi za mihadhara, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na ujenzi wa mfumo wa ukusanyaji wa maji taka ili kuhakikisha kuwa miundombinu ya chuo ni rafiki kwa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji;

(ix) kupunguza tatizo la uhaba wa malazi kwa wanafunzi kwa kujenga hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na kuiwekea samani. Vilevile, itaboresha hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi) zenye uwezo wa kuchukua jumla wanafunzi 500; na

(x) kujenga madarasa katika shule ya Msingi ya Mazoezi Chang'ombe na Shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe pamoja na maabara nne (4) za sayansi ili kuongeza fursa za kupata elimu.

### **Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa shahada za awali na uzamili kutoka 6,315 hadi kufikia 6,635;

(ii) itaanzisha shahada mpya tatu (3) za awali na tatu (3) za umahiri ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu;

(iii) Itaongeza machapisho 20 katika Nyanja za Insia na Sayansi ya Jamii, Elimu na Sayansi;

(iv) itaratibu makongamano mawili (2) ya kitaaluma na kutekeleza miradi 10 ya utafiti na ushauri ili kuongeza wingi na ubora wa kazi za kitafiti na kiugunduzi;

(v) itafadhili mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi 75 katika ngazi za Shahada ya kwanza, Umahiri na Uzamivu ili kuongeza weledi na ufanisi katika utendaji wa kazi;

(vi) itanunua vifaa vya TEHAMA, vitabu 2,000 pamoja na vifaa vya maabara za Fizikia, Baolojia na Kemia; na

(vii) itaimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kupanua maabara ya Baiolojia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 120 kwa wakati mmoja kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa vitendo. Baada ya upanuzi maabara itaweza kuchukua wanafunzi 240 kwa wakati mmoja.

## **Chuo Kikuu Mzumbe**

**112. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Mzumbe itatekeleza yafuatayo:

(i) itasajili wanafunzi wapya 5,864 (Astashahada 747, Stashahada 760, Shahada ya kwanza 3,631, Shahada ya Umahiri 716 na Shahada ya Uzamivu 10) kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu;

(ii) itaandaa programu 10 mpya za masomo kwa lengo la kuongeza fursa za masomo;

(iii) itafadhili masomo kwa watumishi 66 wakiwemo Shahada ya Uzamivu 44 na Shahada ya Umahiri 22. Aidha, itawezesha watumishi 40 kuhudhuria warsha, semina na makongamano ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi na ufanisi katika kazi; na

(iv) itachapisha machapisho 35 katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa na kuchapisha jarida la “Uongozi” la Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo kuwezesha jamii kupata maarifa. Aidha, itaandaa mapendekezo 15 ya kazi za utafiti na mapendekezo 30 ya kazi za ushauri wa kitaalamu.

**113. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itaendelea na ujenzi wa madarasa, ofisi, ukumbi, uwekaji wa samani na miundombinu ya TEHAMA katika jengo la Kampasi Kuu (Maekani). Aidha, itajenga bwalo la chakula na kuweka samani katika majengo yaliyopo Kiwanja Na. 300 Kitalu D Tegeta, Kampasi ya Dar es



Salaam pamoja na kukarabati na kuweka samani katika jengo la wanafunzi wa Shahada za Uzamivu (PhD).

### **Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)**

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, wakiwemo wanafunzi wa Shahada za Kwanza kutoka 4,526 hadi 4,845, Shahada za Juu (Umahiri na Uzamivu) kutoka 195 hadi kufikia 245;

(ii) itaanzisha shahada mpya za awali mbili (2) na shahada za uzamili tatu (3) katika fani tatu (3) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira;

(iii) itaanzisha tafiti mpya 45 na kuendelea kufanya tafiti zilizopo 103 kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi ili kuhuisha elimu na uwezo wa wananchi katika kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda;

(iv) itaongeza utoaji wa elimu na ushauri kwa washiriki 2,500 wakiwemo wakulima, maafisa ugani na watafiti kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile vituo atamizi, mashamba darasa, semina, kozi fupi, runinga na redio ili kuongeza uzalishaji na tija na hatimaye kupunguza umaskini kwa wananchi;

(v) itaboresha na kuongeza mahusiano na taasisi nyingine ndani na nje ya nchi ili kuleta tija katika tafiti na shughuli mbalimbali za maendeleo;

(vi) itajengea uwezo vitengo vya uzalishaji ili kuongeza mapato ya ndani ya chuo kwa asilimia ishirini; na

(vii) itaajiri wafanyakazi 238 kwenye maeneo yenye upungufu na kuwaongezea elimu.

**115. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza fursa za udahili ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali itajenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000, pamoja na chanzo kipya cha maji na mfumo mpya wa maji taka na itaboresha miundombinu ya maji iliyopo katika kampasi ya Solomon Mahlangu.

**116. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itakarabati vyumba 17 vya madarasa Kampasi kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu, majengo ya ofisi na maabara katika idara za DFRAM na DEC, majengo ya idara ya mimea vipando (Crop Science), mabweni na hosteli tano (5), *Horticulture shed house* (Crop museum) pamoja na kukarabati majengo na kununua samani kampasi ya Tunduru.

**117. Mheshimiwa Spika**, Serikali itakarabati miundombinu kampasi ya Katavi, kituo cha mafunzo ya kilimo kwa wakulima kilichopo Mgeta, kiwanda cha samani Vuyisile SMC pamoja na mabweni matano (5), nyumba 30 za wafanyakazi katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.

**118. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kutoa huduma katika jamii, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itapanua misitu ya mafunzo iliyopo Madaba – Songea kwa kupanda miti hekari 300 pamoja na shamba la mkonge Morogoro kwa kuongeza hekari 200;

(ii) itafufua kitengo cha ufugaji wa ng'ombe na nguruwe pamoja na maghala ya kuhifadhia chakula cha mifugo katika shamba la mifugo la Solomon Mahlangu;

(iii) itaanzisha malisho ya asili (natural pastures) Kampasi Kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu; na

(iv) itafunga mfumo wa kisasa wa umwagiliaji (traveller irrigation gun) kwenye shamba la mafunzo lililopo Kampasi Kuu.

## Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

**119. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya kwanza na Stashahada kutoka udahili wa sasa wa wanafunzi 4,051 hadi kufikia wanafunzi 4,500;

(ii) itaongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka asilimia 29 hadi asilimia 40, ili kuongeza rasilimali watu iliyo na uwiano wa kijinsia;

(iii) itahakikisha asilimia 40 ya idara zote za kitaaluma zinaanzisha angalau kozi tatu za muda mfupi kwa ajili ya mafunzo ya kuendeleza ueledi na maadili (professionalism and ethics) kwa wafanyakazi wa kada ya afya kote nchini ili kuboresha utendaji katika kutoa huduma za afya;

(iv) itaongeza matumizi ya TEHAMA katika kujifunzia na kufundishia kutoka asilimia 25 hadi kufikia asilimia 40, ili kuongeza ufanisi wa kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi kwa wakati mmoja; na

(v) itafanya kongamano la tisa (9) la kisayansi (9<sup>th</sup> MUHAS Scientific Conference) na kuboresha semina za kitafiti za ndani ya chuo ili kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau ikiwemo watunga sera za afya.

**120. Mheshimiwa Spika**, ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika jamii pamoja na kutoa huduma za ushauri, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenye tija katika kutatua changamoto za afya;

(ii) itaanzisha miradi mipya miwili (2) ya tafiti na kutoa huduma tano (5) mpya za ushauri wa kitaalamu pamoja na kuanzisha mahusiano na wenye viwanda watatu (3) ili kuongeza uwezo wa kuzalisha rasilimali watu katika kada ya afya watakaoleta tija katika kuendeleza viwanda; na

(iii) itaongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya chuo ikiwemo shule ya meno na kuanza mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic), ili kuimarisha mazingira ya kufundishia, kutafiti na kutoa huduma za tiba; na

**121. Mheshimiwa Spika**, ili kuzalisha rasilimaliwatu wenye utaalamu wa kutafiti, kutibu na kuinga magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya tafiti kwa kukamilisha kituo cha Umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu (Center of Excellence in Cardiovascular Sciences) katika kampasi ya Mloganzila.

## **Chuo Kikuu cha Dodoma**

**122. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili jumla ya wanafunzi 31,604 ambapo Shahada za awali ni 27,379; Astashahada na Stashahada 3,471 na Shahada za Umahiri 754;

(ii) kufanya mapitio ya kozi 10 katika Ndaki tano (5) ili ziendane na uhitaji wa wataalamu na soko la ajira;

(iii) kuajiri watumishi 850 ili kuweza kuziba mapengo ya uhaba wa wafanyakazi sambamba na kuendana na ongezeko la wanafunzi;

(iv) kushiriki katika maonesho ya Nane Nane, Sabasaba na Tume ya Vyuo Vikuu ili kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na chuo;

(v) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara na vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji; na

(vi) kukarabati majengo ya ofisi, hosteli za wanafunzi, madarasa pamoja na nyumba za makazi pamoja na mifumo ya maji na umeme katika majengo hayo.

**123. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza ufanisi wa kazi, chuo kitawajengea uwezo watumishi ili kuboresha utendaji kazi kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa jumla ya watumishi 850 kwa mchanganuo ufuatao: Viongozi waandamizi 40, ngazi ya Astashahada, Shahada na Shahada za Umahiri 250, Mafunzo ya ustadi wa kufundisha 450 na watumishi 110 watejengewa uwezo kulingana na uhitaji.

**124. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza idadi ya tafiti na Huduma za Ushauri (Consultancy Services) chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitaratibu mashindano ya wanataaluma katika kufanya tafiti ambapo tafiti bora tano (5) zitachapishwa;

(ii) kitachapisha machapisho 400 ya wanataaluma katika majarida (peer reviewed journals) ambayo yatatokana na uhamasishwaji kwa wafanyakazi wanataaluma;

(iii) kitahamasisha wafanyakazi wanataaluma kutumia majarida ya nje na ndani katika kuchapisha tafiti zao;

(iv) kitawezesha wafanyakazi wanataaluma 50 kushiriki katika makongamano ya kisayansi ya Kitaifa na ya Kimataifa; na

(v) kitawajengea uwezo wafanyakazi wanataaluma 400 katika eneo la kutoa huduma za ushauri ili kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye uwezo wa kuendesha huduma hizi sambamba na kukiwezesha chuo kuongeza idadi ya huduma za ushauri na kupanua wigo wa mapato kupitia huduma hizi.

**125. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kitajenga nyumba sita (6) za wafanyakazi zenye uwezo wa kuchukua familia 33;

(ii) kitaboresha huduma za Maktaba kwa kununua vitabu 2,000 pamoja na kuboresha miundombinu ya mfumo wa TEHAMA ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iii) kitaanza awamu ya pili ya ujenzi wa Ndaki mbili (2) ambazo ni; Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati na Ndaki ya Sayansi za Ardhi na Uhandisi. Majengo haya yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 yatakapokamilika na kutoa nafasi za maabara za kutosha kujifunzia;

(iv) kitajenga hosteli za wanafunzi katika Hospitali za Rufaa za Iringa na Singida kwa ajili ya wanafunzi wa Shahada za Udaktari na Ukunga wanaopata mafunzo kwa vitendo. Hosteli hizi zitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 pindi zitakapokamilika. Kukamilika kwa ujenzi huu kutasaidia kupunguza gharama za kupanga majengo ya watu/Taasisi binafsi kwa ajili ya malazi ya wanafunzi hao;

(v) kitajenga kiwanda cha utengenezaji maji tiba ya hospitali (Intravenous-IV fluids) kwa ajili ya matumizi ya hospitali ya chuo na kuziuzia hospitali nyingine za umma ambazo kwa sasa zinaagiza maji tiba nje ya nchi pamoja na kutumika kama sehemu ya mafunzo;

(vi) kitakarabati ukumbi wa mihadhara wa Chimwaga kwa kuweka samani mpya na kuboresha miundombinu yake ili kuufanya uwe wa kisasa kwa ajili ya matumizi ya Chuo na Taasisi mbalimbali; na

(vii) kitanunua magari matano (5) yatakayosaidia katika shughuli za kila siku za uendeshaji za chuo.

## Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

**126. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili wanafunzi wapya 4,415 (Astashahada 1,480, Stashahada 695, Shahada za awali 2,100 na Shahada za Uzamili 140);

(ii) kuandaa programu nne (4) za mafunzo ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika fani za Ushirika na Biashara, Huduma za Kibenki, Usimamizi wa Fedha na Ushirika wa Mazao na Masoko;

(iii) kitafanya miradi ya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuchapa makala mbalimbali kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;

(iv) kitatoa na kueneza elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC); Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO); Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na vyama vya ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(v) kitaendelea kuwezesha mafunzo ya wafanyakazi 64.

**127. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira ya kujifunzia;

(ii) kitajenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; na

(iii) kitakarabati kumbi za mihadhara tatu (3), vyumba vya mihadhara 12, vyumba vya semina 9, jengo la maabara ya kompyuta na nyumba 10 za makazi.

### **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**128. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili jumla ya wanafunzi 16,650 (Cheti 3,000, Stashahada 4,000, Shahada ya kwanza 7,000, Shahada ya Uzamili 2,500 na Shahada ya Uzamivu 150);

(ii) kufanya utafiti katika maeneo ya mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano pamoja na tafiti katika lugha na fasihi;

(iii) kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika Nyanja za mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo; na

(iv) kujenga jengo Makao Makuu ya Nchi Jijini Dodoma na majengo ya ofisi za wafanyakazi katika vituo vya mikoa ya Geita, Simiyu, Manyara, Lindi na Kigoma. Pia utafanyika ujenzi wa ukumbi wa mitihani mkoani Morogoro. Vilevile, katika kipindi hiki Chuo kinatarajia kufanya ukarabati katika majengo ya ofisi za vituo vya Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Shinyanga, Kilimanjaro, Tabora na Kagera. Aidha, Chuo kitajenga uzio katika viwanja vya vituo vya Mtwara, Arusha na Rukwa. Pia utafanyika ukarabati wa vituo vya uratibu vya Zanzibar, Mafia na Tunduru.

### **Chuo Kikuu cha Ardhi**

**129. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi itatekeleza kazi zifuatazo:



(i) kudahili wanafunzi 5,255 wakiwamo ngazi ya shahada ya kwanza 4,955, ngazi ya shahada ya uzamili 215 na ngazi ya Shahada ya Uzamivu 85;

(ii) kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 31; wakiwemo 17 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na 10 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na 4 katika ngazi ya Stashahada;

(iii) kufanya miradi ya tafiti 50 zinazolenga kutatua changamoto za jamii hususan katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na majenzi. Aidha, Chuo kitaandaa machapisho 150 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo;

(iv) kutoa mafunzo ya aina tano (5) ya kitaalam kwa jamii (outreach training) kuhusiana na matumizi bora ya ardhi, kujikinga na majanga, kutengeneza bidhaa kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo, kutunza kumbukumbuku za biashara ndogondogo na utunzaji wa mazingira;

(v) kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa jamii kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na ujenzi;

(vi) kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (Lands Building), ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na kuweka samani katika mabweni ya wanafunzi; na

(vii) Kuendeleza ujenzi wa mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592.

## **Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Sayansi, Teknolojia na Ubunifu itaendelea kuibua, kutambua, na kuendeleza ubunifu, ugunduzi na teknolojia zinazozalishwa nchini kupitia Mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuchangia katika kuzalisha

ajira mpya. Aidha, itaratibu shughuli za Sayansi Teknolojia na Ubunifu katika ngazi za mikoa na mamlaka za Serikali za mitaa ili kuwafikia wabunifu katika ngazi zote hususan vijijini.

**131. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaainisha matokeo ya utafiti hususan yale yenye manufaa ya moja kwa moja kwa jamii, pamoja na kubaini uwezo wa vifaa na wataalam katika taasisi za utafiti na Elimu ya Juu ili kuimarisha ushirikiano baina ya Taasisi za utafiti. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi na manufaa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi; na

(ii) itafanya mapitio ya Mwongozo wa Kitaifa wa Kutambua na Kuendeleza Ugunduzi, Ubunifu na Maarifa Asilia ili uendane na wakati na uweze kutumika na wadau wengi.

### **Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – COSTECH**

**132. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kubaini na kugharamia miradi mipya 8 ya utafiti yenye kulenga kutatua matatizo ya wananchi katika sekta za Kilimo na Mifugo; Viwanda; Mafuta na Gesi; Uvuvi; Elimu; Afya na Mazingira;

(ii) kufungasha na kusambaza matokeo ya utafiti kwa wadau ikiwemo viongozi, watunga sera na wananchi, kupitia machapisho, runinga na radio pamoja magazeti ili kuelimisha jamii kuhusu ufumbuzi wa matatizo kutokana na utafiti uliofanyika; na

(iii) kubiasharisha matokeo matano (5) ya tafiti nchini yanayolenga kutatua matatizo kwa jamii ili kuthibitisha uzalishaji, muendelezo na utumiaji wa matokeo ya utafiti

katika mifumo ya kibiashara kwa kutumia viwanda na masoko.

**133. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu pamoja na kuboresha mifumo ya ubunifu kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) kugharamia kazi za wabunifu ili kuwajengea uwezo, kuwahamasisha na kuendeleza ujuzi na umahiri wao;

(ii) kuratibu mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya mwaka 2021 ili kutambua, kuendeleza na kurasimisha matokeo ya ubunifu kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya nchi;

(iii) kuboresha mifumo ya ubunifu na kuendeleza wabunifu nchini ili kuhamasisha na kuongeza matumizi ya ubunifu katika mifumo rasmi ya uchumi na viwanda kwa maendeleo na ushindani wa kibiashara;

(iv) kusimamia uanzishwaji wa mifumo na miongozo ya kuzijengea uwezo taasisi zinazofanya tafiti nchini katika kulinda viwango vya utekelezaji wa utafiti kulingana na weledi na ubobezi wa taaluma ili kupata matokeo ya utafiti yanayotatua matatizo ya nchi kijamii na utamaduni, kiuchumi na kisiasa;

(v) kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi inayofadhiliwa na Tume ili kuboresha mfumo wa udhibiti na utoaji vibali vya utafiti nchini kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji na uendelezaji wa tafiti unafuata sheria na taratibu; na

(vi) kuchangia shughuli za ubunifu kupitia mradi wa *South African Innovation Support (SAIS)* unaotekelezwa katika nchi tano kusini mwa bara la Afrika ili kuhamasisha ushindani, ujuzi na ubora wa ubunifu wa wabunifu nchini na katika nchi hizo tano za Bara la Afrika.

**134. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia COSTECH itaandaa mwongozo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji

wa nje, pamoja na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia kwa lengo la kurasimisha uratibu na kulinda haki miliki na hati miliki. Aidha, itasimamia na kuhakikisha kuwa elimu ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu inatekelezwa kukidhi mipango ya taifa ya maendeleo iliyowekwa (TDV 2025) na ile ya kimataifa (STISA 2063 na Malengo 17 ya Maendeleo endelevu).

### **Tume ya Nguvu za Atomiki**

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kuendelea na ujenzi wa maabara changamano kwa awamu ya pili na maabara za kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Zanzibar, Dodoma na Mbeya ambazo zitaboresha na kusogeza huduma kwa wananchi; na

(ii) kuanzisha ofisi za Tume katika kanda ya Kati - Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya na Kanda ya Kusini -Mtwara ili kusogeza huduma kwa wananchi.

**136. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Tume imefanya upembuzi yakinifu wa miradi miwili (2) ambapo utekelezaji wake utasaidia kuhifadhi mazao yanayoharibika haraka (perishables) kurefushwa muda wa kuhifadhi bila kuharibika. Aidha, itawezesha tafiti za kisayansi kwa wadau katika uzalishaji wa dawa za mazao ya kilimo na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza madawa ya kutibu saratani kutoka nje ya nchi. Miradi hiyo ni:

(i) Mradi wa uanzishwaji wa kinu cha kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi (perishable) kwa kutumia mionzi (Multipurpose Irradiator Facility); na

(ii) Mradi wa kinu cha tafiti za kinyuklia (Research Reactor) wa kutengeneza madawa ya kutibu saratani kwa viwanda vya madawa.

Aidha, Serikali itaratibu miradi mipya mitano (5) ya kitaifa na miradi 26 ya kikanda ambayo itagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (International Atomic Energy Agency (IAEA).

**137. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha afya za wafanyakazi wanaotumia teknolojia ya nyuklia zinakuwa salama, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) itaanzisha kituo cha mafunzo cha usalama na kinga ya mionzi katika ngazi ya diploma, cheti na mafunzo ya muda mfupi ambayo yatalenga kuiweka nchi katika usalama zaidi dhidi ya mionzi na nyuklia kwa ujumla;

(ii) itaendelea na upimaji wa viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,200 wanaofanya kazi kwenye vyanzo vya mionzi Hospitali katika, Viwanda na Migodi ili kuhakikisha afya zao zinakuwa salama; na

(iii) itaendelea kufanyia matengenezo na kusimika mitambo inayotumia teknolojia ya nyuklia pamoja na kuhakiki ubora wa vifaa/mitambo vinavyotumia teknolojia ya nyuklia katika hospitali, viwanda, migodi na kampuni za ujenzi wa barabara.

**138. Mheshimiwa Spika**, ili kulinda umma wa Tanzania na mazingira yake yasichafuliwe na mabaki ya vyanzo vya mionzi ambavyo havitumiki tena kutokana na nguvu yake kupungua au teknolojia kubadilika, Serikali itaendelea kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo sita na kuyahifadhi katika jengo maalumu (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF) lililopo Arusha ambapo ukusanyaji na uhifadhi unafanyika.

**139. Mheshimiwa Spika**, katika kuwalinda watanzania na kulinda bidhaa zetu kwenye masoko ya nje, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) itapima kiasi cha mionzi katika sampuli zipatazo 20,000 za vyakula, tumbaku na mbolea zinazotoka na kuingia nchini ili kubaini endapo hazina madhara ya mionzi;

(ii) itapima mionzi kwenye mazingira katika vituo 50 ili kubaini iwapo kuna uchafuzi wa mazingira utokanao na mionzi; na

(iii) itasimamia kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZPRN64) kilichopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya mkataba wa kimataifa wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons*.

**140. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Tume itafanya tafiti kuhusu matumizi ya teknolojia ya nyuklia na kuchapisha matokeo yake ili kuhamasisha matumizi ya matokeo hayo. Aidha, itaanzisha, itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa tafiti na miradi ya kitaifa na kikanda inayotumia sayansi ya nyuklia na teknolojia yake ili kuendelea kuleta faida kwenye sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo, Mifugo na Maji ikiwa pamoja na kujijengea uwezo katika ubunifu na matumizi ya teknolojia hii.

**141. Mheshimiwa Spika**, katika kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi na vituo vya mionzi, Serikali kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:

(i) itakagua migodi sita (6) (Geita Gold Mine, Bulyanhulu Gold Mine, North Mara Gold Mine, Buzwagi Gold Mine, Williamson Gold Mine, na Stami Gold Tulawaka;

(ii) itatathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni za usalama wa mionzi ili kubaini kama yanakidhi matakwa ya Sheria na Kanuni zake;

(iii) itakagua vituo 500 vyenye vyanzo vya mionzi ayonisha (Ionizing Radiation) ili kubaini hali ya usalama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma; na

(iv) itakagua vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyo ayonisha (Non-Ionizing Radiation) mfano minara ya simu, redio, runinga na vifaa vingine vya mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika.

## Taasisi Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Kampasi Kuu ya Dar es Salaam itatekeleza yafuatayo;

(i) itadahili wanafunzi wapya 2,400 na kuhudumia wanafunzi 3,300 wanaoendelea na masomo na kufanya Taasisi kuwa na jumla ya wanafunzi 5,700;

(ii) itakamilisha tafiti saba (7) zinazoendelea na kuanza kufanya tafiti mpya tatu (3) na kutekeleza miradi 25 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii. Tafiti hizo ni kuhusu:

(a) kutengeneza mtambo maalumu wa kuwezesha mazingira rafiki ya kilimo mjini;

(b) kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa kutumia nguvu za jua kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya kisima;

(c) kutengeneza mfumo wa kuhifadhi, kusambaza na kuchakata taarifa za bioanwai hapa nchini kwa kushirikiana na COSTECH unaofadhiliwa na Shirika la kimataifa la *JRS Biodiversity Foundation* la Marekani;

(d) kuboresha teknolojia ya mfumo wa usimamizi wa hospitali na vituo vya afya ambao kwa sasa unatumika katika hospitali ya Amana kwa majaribio;

(e) kutengeneza mfumo wa mawasiliano yasiyo tumia nyaya kwenye magari yasiyo na dereva;

(f) kukamilisha utengenezaji wa mashine ya kuchakata kahawa kwa kigezo cha rangi utakaosaidia wakulima wa kahawa kuongeza mnyoro wa thamani; na

(g) kutengeneza injini itakayotumia mfumo wa gesi asilia.

(i) itaendelea na utekelezaji wa mradi wa 'East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)' kama ifuatavyo:

(a) kujenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 na jengo la ghorofa 12 la kituo cha umahiri wa TEHAMA katika Kampasi ya Dar es Salaam;

(b) kuanza ujenzi wa mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 na jengo la ghorofa sita (6) la kituo cha umahiri wa teknolojia ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi katika Kampasi ya Mwanza; na

(c) kuhuisha mitaala ya programu 14 (Stashahada 10, Shahada 3, na Umahiri 1) na kuanzisha mitaala ya programu 8 (Stashahada 6, Shahada 1, na Umahiri 1).

**143. Mheshimiwa Spika**, Taasisi itaanza utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa *Tanzania Education Labour Market Survey (TELMs)* awamu ya pili unaofadhiliwa na Serikali ya Italia. Mradi huu una lengo la kuvijengea uwezo vyuo vinne (4) vya ufundi nchini (DIT, KIST, ATC na MUST) ili kuzalisha wataalamu waliobobea katika fani za ufundi na teknolojia ambapo yafuatayo yatatekelezwa:

(i) kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa majengo ya vituo viwili vya ujasiriamali, ubunifu na usambazaji wa teknolojia (Centres of Entrepreneurship, Innovation and Technology Transfer) katika kampasi za Mwanza na Dar es Salaam;

(ii) kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa jengo la ghorofa nne la kufundishia katika Kampasi ya Myunga iliyopo mkoani Songwe;

(iii) kufanya ununuzi ya magari matatu (3) ya mradi;

(iv) itaendelea kushiriki kwenye zabuni za miradi ya kitaifa minne (4) kwa lengo la kujengea Taasisi uwezo wa kifedha na kutatua changamoto za jamii kupitia Kampuni ya Taasisi iitwayo "DIT Company Limited"; na



(v) itaendelea kushiriki katika kusimamia mchakato wa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wa Taasisi na kitaifa.

### **Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

**144. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kudahili jumla ya wanafunzi 7,150 (Stashahada 3,327, Shahada ya Kwanza 3,705 na Shahada za Uzamili 118);

(ii) kununua vifaa vya kisasa vya maabara na karakana kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani za Sayansi na Teknolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia;

(iii) kufanya tafiti 120 zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za sayansi na teknolojia ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda;

(iv) kuboresha mnyororo wa thamani wa zao la viazi kwa kushirikiana na *Hanze University of Applied Sciences (Netherlands)* na MATI Uyole kwa kujenga uwezo kwa wanataaluma na kutoa mafunzo kwa wakulima;

(v) kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi kwa kukamilisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na jengo la madarasa la Ndaki ya Usanifu na Teknolojia ya Majengo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800 kwa wakati mmoja;

(vi) kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, itakarabati madarasa, hosteli na nyumba za watumishi;

(vii) kuongeza matumizi ya nishati mbadala ili kuwa na vyanzo endelevu vya nishati kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za

Chuo kwa kufunga taa 30 zinazotumia umeme wa jua na hivyo kupunguza gharama za umeme;

(viii) kuanzisha Kituo cha Teknolojia Vijijini katika Kampasi ya Rukwa ili kuchochea matumizi ya teknolojia stahiki (appropriate technology) katika maeneo ya vijijini; na

(ix) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Ufundi kwa wanafunzi 400, Shahada ya Ualimu wa Ufundi kwa wanafunzi 400 na Stashahada ya Uzamili ya Ualimu wa Ufundi wa wanafunzi 50 ili kukidhi mahitaji ya Walimu wa Ufundi katika Shule na Vyuo vya Ufundi nchini.

### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (NM- AIST)**

**145. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha itatekeleza yafuatayo:

(i) itadahili jumla ya wanafunzi 125 ambapo wanafunzi 100 ni wa ngazi ya Shahada ya Uzamili na wanafunzi 25 wa ngazi ya Shahada ya Uzamivu;

(ii) itakamilisha utafiti katika miradi 21 ya kitafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi sanjari na kulipa gharama za utafiti kwa wanafunzi na wanataaluma ili kuzalisha bunifu katika maeneo ya TEHAMA, sumu kuvu, uchakataji wa ngozi, viini lishe kwa watoto wenye udumavu na ugonjwa wa kimeta kwa mifugo na wanyamapori;

(iii) itaratibu shughuli za utafiti na ubunifu kwa kuzalisha bunifu mbili (2) zitakazofikia katika hatua ya atamizi na hatimaye bidhaa kamili; na

(iv) kutatua changamoto ya makazi kwa wanafunzi kwa kuanza ujenzi wa bweni litakalokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500.

## Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu

**146. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia idara ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimaliwatu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kukamilisha taratibu za ujenzi wa jengo kuu la ofisi za Wizara Mtumba - Dodoma kulingana na miongozo na maelekezo za Serikali;

(ii) itakamilisha mpango wa utumiaji wa Mfumo wa mawasiliano wa Kielektroniki (E-office) wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi, kupunguza gharama na kuongeza kasi ya mawasiliano katika ofisi; na

(iii) itasimamia na kuhakiki Rasilimaliwatu kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto za kiutendaji na kuzipatia ufumbuzi.

**147. Mheshimiwa Spika**, katika kuleta ufanisi na weledi kwa watumishi, Serikali itaendelea kufanya mapitio ya Mpango wa Mafunzo wa Wizara pamoja na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi yakiwemo: Mafunzo Elekezi; Maadili katika Utumishi wa Umma; Haki na Wajibu wa Watu Wenye Ulemavu; UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukizwa; na Utumiaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (Open Performance Review and Apraisal System – OPRAS). Aidha, itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wanaokaribia kustaafu ili kujiandaa na maisha baada ya kustaafu.

## Usimamizi wa Rasilimali za Wizara

**148. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia idara ya Usimamizi wa Rasilimali za Wizara itatekeleza yafuatayo:

(i) itakagua matumizi ya fedha katika Taasisi za Wizara;

(ii) itaendelea na ukaguzi wa ukusanyaji wa maduhuli na matumizi katika Taasisi za Wizara;

(iii) itafanya ukaguzi wa taratibu za ununuzi na usimamizi wa Mikataba inayotekelezwa na Wizara ikiwemo mikataba ya Ujenzi na ukarabati; na

(iv) itafanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara (Expenditure Management) Makao Makuu ya Wizara.

### **Uendelezaji na Uboreshaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu**

**149. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali itaendelea kuendeleza na kuboresha Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu kama ifuatavyo:

(i) itahuisha Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu - Education Sector Development Plan (ESDP) wa Miaka Mitano 2020/21- 2025/26 na Mpango Mkakati – Strategic Plan (SP) wa Wizara 2020/21-2025/26 ili kuweka mwelekeo wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kutekeleza Mipango ya Kitaifa na Kimataifa;

(ii) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera, Mpango na Mkakati ya Wizara 2016/17 - 2020/21;

(iii) itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu sera, nyaraka, miongozo na mikakati ya Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa taasisi zilizo chini ya Wizara;

(iv) itaendelea kutoa ushauri kuhusu mikataba na itifaki za mashirika ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo nchi inapaswa kuridhia pale inapojitokeza; na

(v) itakamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 ili kuwa na Sera ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inayoendana na mahitaji ya sasa.

## USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA

**150. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Wizara itatekeleza miradi ifuatavyo;

### **Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Programme for Results – EP4R)**

**151. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2020/21 itatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuboresha Vyuo vya Ualimu vya Mhonda na Dakawa kwa kukarabati na kujenga miundombinu katika vyuo hivyo ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) kukamilisha ujenzi wa Hosteli, Bwalo la chakula na mifumo ya maji katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ili kuwezeshaji upatikanaji wa malazi na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) Kukarabati Nyumba za Wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu;

(iv) kuendelea kutoa motisha kwa Halmashauri 184 kutokana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika kati ya Serikali na wafadhili;

(v) kuwezesha ukaguzi wa nje wa Programu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi; na

(vi) itaendelea kuratibu ujenzi wa ofisi 55 za Uthibiti Ubora wa Shule ngazi ya wilaya;

### **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)**

**152. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi unatakelezwa kwa utaratibu wa Lipa Kulingana na Matokeo - *Payment for Results* (P4R). Katika mwaka wa

fedha 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa ESPJ itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kuwezesha Karakana na Maabara za Wabunifu kwa kuzipatia vifaa vya kisasa ili kuboresha mazingira ya uendelezaji ubunifu na ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo;

(ii) kuendelea na utekelezaji wa Mfuko wa Kukuza Stadi za Kazi kwa kutoa fedha za kuziwezesha taasisi za mafunzo ya ufundi kununua vifaa na kuboresha mitaala kupitia maandiko ya kiushindani ili kuendana na mahitaji ya kijamii;

(iii) kuboresha miundombinu ya Taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi ikiwemo VETA kwa ujenzi na ukarabati;

(iv) kujengea uwezo Wizara na Taasisi kwa kununua vifaa na kutoa mafunzo ili kuwawezesha kusimamia ubora wa elimu ya ufundi na stadi za kazi;

(v) kutoa ufadhili kwa Vijana ili kuwawezesha kupata ujuzi kupitia Mwongozo wa Mamlaka ya Elimu Tanzania;

(vi) kuwezesha ujenzi wa Maktaba mpya 5 katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Simiyu, Dodoma na katika Chuo cha Maktaba - Bagamoyo. Aidha, Ukarabati wa Maktaba 9 za mikoa utafanyika; na

(vii) kuimarisha Vyuo vya VETA na Elimu ya Ufundi kwa kufanya mafunzo kwa njia ya Uanagenzi (Apprenticeship).

### **Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu**

**153. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa kuimarisha Elimu ya Ufundi, Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Ualimu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kuwezesha uendeshaji na maendeleo ya Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(ii) kuwezesha wanafunzi wa vyuo vya ufundi stadi kupata ujuzi wa kujiri na kuajiriwa; na

(iii) kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi.

**Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEMM) – Kuimarisha Mafunzo ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK**

**154. Mheshimiwa Spika**, Serikali imesaini mkataba wa makubaliano na wadau wa Maendeleo - GPE tarehe 15 Januari, 2020 kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Programu hii inalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wenye umri wa miaka 5-13 walio ndani na nje ya mfumo rasmi. Mpango huu unafadhiliwa na Mfuko wa Ushirika wa Kimataifa wa Elimu (*Global Partnership for Education-GPE Fund*). Katika mwaka 2020/2021, itatekeleza kazi zafuatazo:

(i) kuwezesha Vituo vya Walimu (TRC) kutekeleza Mpango wa mafunzo endelevu kazini (CPD);

(ii) kuandaa mwongozo kwa ajili ya Waratibu wa Vituo vya Walimu (TRC) ili kuendana na Mpango wa mafunzo endelevu kazini (CPD);

(iii) kuwezesha mafunzo ya Waratibu wa TRC na Maafisa Elimu kata 966;

(iv) kuwezesha Tathmini na Ufuatiliaji wa Mradi;

(v) kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa shule za Msingi kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;

(vi) kuandaa moduli za mafunzo endelevu kazini kwa wawezeshaji wa MEMKWA kuhusu mtaala mpya, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu;

(vii) kuwezesha uandaaji, uchapaji na usambazaji wa vitabu vya wanafunzi wa Darasa la VI na VII pamoja na kiongozi cha mwalimu kwa masomo yote;

(viii) kuandaa miongozo na kuboresha mihtasari kwa ajili ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) na kufanya upimaji;

(ix) kuwezesha mafunzo kazini kwa walimu wenye mahitaji maalum kuhusu mtaala, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na upimaji endelevu; na

(x) kuwezesha mafunzo kwa Wawezeshaji wa MEMKWA wenye mahitaji maalum ngazi ya Mikoa na Halmashauri.

### **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP)**

**155. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/2021, Wizara kupitia Mradi wa TESP itatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara ya Sayansi, TEHAMA, vitabu vya kiada vya shule za Msingi na Sekondari pamoja na vitabu vya kiada na ziada kwa Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;

(ii) kuwezesha Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali kuunganishwa katika Mkongo wa Taifa;

(iii) kukarabati Maabara za Sayansi nne (4), za TEHAMA tano (5) na Maktaba sita (6) katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali; na

(iv) kuwezesha mapitio ya mtaala wa Elimu ya Ualimu, uchapaji na usambazaji na miongozo kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo kazini kwa masomo 21 na moduli 6 za mkakati jumuishi. Aidha, itawezesha uandaaji, usambazaji, ufuatiliaji na tathmini wa Kionzi cha Ujuzi wa Mwalimu na Mkufunzi.

**156. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha utendaji kazi wa watumishi, Serikali kupitia mradi wa TESP itatoa mafunzo kazini katika maeneo yafuatayo:-



- (i) utawala na matumizi ya TEHAMA kwa watumishi 1,300 kutoka Vyuo vya Ualimu;
- (ii) usimamizi wa fedha za miradi kwa watumishi 50 wa makao makuu ya Wizara;
- (iii) matumizi ya TEHAMA kwa watumishi 210 wa vyuo vya ualimu wakiwemo Wakutubi na Makatibu muhtasi;
- (iv) usimamizi na ufuatiliaji kwa Bodi za Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;
- (v) matumizi ya vifaa visaidizi na TEHAMA kwa Walimu na Wakufunzi 300 wenye mahitaji maalumu;
- (vi) matumizi ya Lugha ya Alama kwa walimu wa shule za Msingi 350 na Sekondari 150; na
- (vii) mbinu za ufundishaji kwa Wakufunzi 570 wakiwemo wa masomo ya Sayansi, Hisabati, Biashara, Kilimo, *Development Studies*, Elimu ya Michezo, Uraia na Sanaa.

### **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC)**

**157. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC), itatekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) Ujenzi wa kumbi za Mihadhara, ununuzi wa vifaa vya Maktaba na ukarabati wa jengo la utawala katika Kampasi ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Morogoro; na
- (ii) Kuendelea na Ujenzi na Ukarabati wa vyuo vya Ualimu vinne (4) vya Shinyanga, Mpuguso, Ndala na Kitangali.

### **Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni**

**158. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni itatekeleza yafuatayo:

(i) kufuatilia na kutathmini ujenzi wa miundombinu ya vyoo na maji awamu ya pili katika Shule za Msingi 946 kwa kushirikiana na Wizara zinazotekeleza Programu Endelevu ya Usambazaji wa MajiVijijini na Usafi wa Mazingira ili kubaini mafanikio, changamoto na kutoa ushauri stahiki;

(ii) kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji na vyoo vya mfano katika Vyuo vya Ualimu vitano (5) vya Katoke, Nachingwea, Kinampanda, Shinyanga na Murutunguru ili kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu;

(iii) kutoa elimu elekezi kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira shuleni kwa Maaafisa Elimu na Wathibiti Ubora wa Shule ili waweze kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni; na

(iv) kununua magari matatu (3) ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu katika Mikoa na Halmashauri nchini.

### **Mradi wa Kuimarisha Ubora Elimu ya Sekondari - SEQUIP**

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) kuandaa moduli na Mwongozo wa Elimu Jumuishi pamoja na kutoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa walimu wa Shule za Sekondari za Serikali ili kuwajengea uwezo katika kazi zao na kupata uelewa zaidi kuhusu elimu jumuishi;

(ii) kuandaa na kutekeleza mkakati wa upatikanaji wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa walimu na kuongeza ufaulu wa wanafunzi;

(iii) kuandaa mwongozo kwa ajili ya kufanya tathmini ya ujifunzaji kwa Elimu ya Sekondari;

(iv) kuandaa mwongozo wa ufundishaji wa TEHAMA na kutoa mafunzo kwa walimu 1,000 kutoka shule za Sekondari 500 kuhusu moduli za TEHAMA; na

(v) kuainisha na kuboresha vituo vya kutolea Elimu nje ya mfumo rasmi ili kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu.

### **Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - *East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)***

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - EASTRIP itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itawajengea uwezo wanataaluma 100 pamoja na kuandaa na kutoa ithibati ya mitaala ya Umahiri ya Elimu ya Ufundi (Competence Based Curricular); na

(ii) itajenga uwezo kwa vyuo vya ufundi kwa kutoa mafunzo ya kufundisha elimu ya ufundi ya ujuzi (Competece Based Training) kwa wanataaluma 400 na kuanzisha *National TVET Resource Centre*.

### **TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)**

**161. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO itatekeleza yafuatayo:

(i) Itafanya tathmini ya mikataba ya UNESCO iliyoridhiwa na Serikali;

(ii) itasimamia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali iliyopitishwa katika mpango wa UNESCO wa mwaka 2020/22;

(iii) itashirikiana na wadau katika kutumia fursa mbalimbali zinazotokana na uanachama wa Serikali katika shirika la UNESCO;

(iv) itachangia upatikanaji wa Elimu bora kwa wote kwa kujenga utamaduni endelevu wa kujifunza;

(v) itatoa mafunzo ya uelewa kwa masuala ya UKIMWI na rushwa katika mazingira ya kazi; na

(vi) itaimarisha mazingira ya utendaji kazi katika kwa kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na upatikanaji vitendea kazi.

#### D. SHUKRANI

**162. Mheshimiwa Spika**, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa William Tate Olenasha (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu; Profesa James Epiphan Mdoe na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo, na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao wa karibu katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**163. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi na Wadau wa Elimu, kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki wa Shule, Vyuo na Taasisi Binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu hapa nchini.

**164. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Washirika mbalimbali wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Algeria, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Malta, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Netherland, New Zealand, Norway, Palestine, Romania, Saudi

Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

**165. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuyashukuru mashirika yaliyochangia kufanikisha programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na; Benki ya Dunia, *Department for International Development (DfID)*, *Swedish International Development Agency (SIDA)*, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, *Global Partnership in Education (GPE)*, *United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF)*, *United Nations Development Programme (UNDP)*, *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO)*, USAID, *Inter University Council for East Africa (IUCEA)*, *Human Development Innovation Fund (HDIF)*, *Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD)*, *British Council*, *Campaign for Female Education (CAMFED)*, *Commonwealth Secretariat*, *Aga Khan Education Services*, *Japan International Cooperation Agency (JICA)*, *Karibu Tanzania Organization (KTO)*, *Korea International Cooperation Agency (KOICA)*, *WaterAid*, *Plan International*, *Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET)*, *Christian Social Services Commission (CSSC)* na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

#### **E. MAOMBI YA FEDHA WA MWAKA 2020/21**

**166. Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,348,563,375,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

**(i) Shilingi 87,361,755,810.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya idara na vitengo vilivyoko Makao Makuu ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 61,802,934,325.00** ni Mishahara na **Shilingi 25,558,821,485.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) **Shilingi 403,687,395,190.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 356,908,438,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 46,778,957,190.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(iii) **Shilingi 857,514,224,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo a m b a p o **Shilingi 606,715,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 250,799,224,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**167. Mheshimiwa Spika**, naliomba pia Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 2,239,181,000.00** kwa ajili ya Fungu 18 Tume ya Taifa ya UNESCO. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 706,888,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,532,293,000.00** ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 706,888,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

**168. Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**169. Mheshimiwa Spika**, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni <http://www.moe.go.tz>.

**170. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kwa sababu ya muda, naomba *speech* yangu yote iingie kwenye *Hansard* za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ina wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia kama ilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchambua Bajeti, Kamati ilipata wasaa wa kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha ulioisha kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo. Shughuli hiyo ilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) ilijiwekea makadirio ya kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 553.739. Hadi kufikia Februari, 2020, Wizara ilikuwa imekusanya asilimia 52.9 ya makadirio ya makusanyo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Fungu 18 (Tume ya *UNESCO*) katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiria kukusanya shilingi milioni 27 hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ilikusanya shilingi 8,500,000/= sawa na asilimia 31.48 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Elimu ya

Juu (Fungu 46) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya kutekeleza mipango na majukumu yake. Hadi kufikia Februari, 2020 Wizara ilifanikiwa kupokea jumla ya shilingi bilioni 808.63 sawa na asilimia 57.5 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika fedha za Miradi zilizopatikana, shilingi bilioni 421.953 sawa na asilimia 91.9 ni fedha za ndani. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha zake za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malelezo na matokeo ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kuanzia tarehe 13 - 17 Machi, 2020; Kamati ilifanya ziara ya kutembelea, kukagua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ziara za Kamati kwa kipindi hiki zilifanyika katika Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro ambapo jumla ya miradi miwili ilitembelewa na kukaguliwa na Kamati pamoja na kupokea taarifa ya mradi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilishindwa kufanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam kufuatia kuahirishwa kutokana Ugonjwa wa Mafua unaotokana na Virusi vya *Corona*. Miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni 12 yaliyotolewa na Kamati Mwaka 2019 na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maoni hayo. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa utekelezaji huo. Pamoja na utekelezaji huo mzuri, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya maoni, utekelezaji wake unahitaji uwepo wa wa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani ya Kamati kuwa maoni hayo yatafanyiwa kazi hasa ikizingatiwa kuwa bado hatujafika mwisho wa mwaka wa fedha. Wizara ya Fedha



isaidie kutoa fedha za Wizara hii kwa kuzingatia kuwa elimu ni kila kitu kama ambavyo mwanazuoni Benjamin Franklin alivyowahi kusema *“An Investment in Knowledge Pays the Best Interest.”* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Wizara imepanga kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi bilioni 525.93 kutoka katika vyanzo mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Fungu 46 inakadiria kutumia Jumla ya shilingi trilioni 1.24. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 491.04 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Idara na Taasisi na shilingi bilioni 750.65 ni kwa ajili ya kutekeza miradi ya maendeleo, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO (Fungu 18), katika mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha shilingi bilioni 2.23 kinaombwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume. Kati ya Fedha hizo, mishahara inaombewa kiasi cha shilingi milioni 706.88 na matumizi mengineyo yanaombewa kiasi cha shilingi bilioni 1.53. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Tume imeongezeka kwa asilimia 3.7. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Tume hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya uhaba wa Watumishi katika Sekta ya Elimu ni kubwa kwani karibu kila Taasisi ambayo Kamati iliitembelea kwa ajili ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilieleza changamoto hii. Uhaba huu umefanya taasisi hizi na sekta kwa ujumla kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa vibali vya ajira vya watumishi wa Sekta ya Elimu na hususan wa Taasisi ya

Nelson Mandela, Chuo cha Ushirika Moshi na Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha kama ilivyoonyeshwa kwenye uchambuzi wa Kamati. Kamati imekuwa inashauri mara kwa mara ni bora kutenga miradi michache ambayo itakuwa na uhakika wa upelekaji fedha. Kamati inaendelea kushauri utekelezaji wa ushauri huu ni muhimu ili kuondoa changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi Nyingi za Elimu zinakumbana na uhaba na uchakavu wa miundombinu hali ambayo inaathiri utoaji wa elimu nchini. Kamati imeshuhudia baadhi ya majengo na miundombinu ya Taasisi za Elimu kuwa chakavu na kutokidhi mahitaji yake. Ukosefu wa Mabweni ya wanafunzi wa kike kwenye vyuo imekuwa ikidumaza elimu ya watoto wa kike nchini. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu lakini pia ukarabati kwa ile iliyochakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tuzo ya Udhadini ya Rais (*Presidential Scholarship Award*) kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikishauri juu ya umuhimu wa kuanzisha Tuzo ya Udhadini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kuwa na ufaulu wa juu. Lengo ni kuwawezesha kujiunga na vyuo vizuri duniani ili kupata elimu bora ambayo itakuwa na manufaa kwa Taifa lakini pia italeti chachu kwa wanafunzi wengine kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu umekuwa na matokeo mazuri kwa nchi za wenzetu. Kwa mfano, Korea ya Kusini ilifanikiwa kutokana na kupelekea wanafunzi wengi katika vyuo vizuri duniani kama Havard, *MIT*, *Oxford* na kadhalika. Pamoja na majibu ya hoja hii ambayo yamekuwa yakitolewa na Wizara, Kamati inaona bado kuna umuhimu wa kuanzisha tuzo hii kwa maendeleo ya watoto wetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefarijika kusikia Wizara imepokea ushauri wa Kamati iliutoa Mwaka 2019 wa kusoma ripoti ya Tume iliyoundwa na Rais wa 40 wa Marekani, Ronald Reagan Mwaka 1983 kwa lengo la kuiga mazuri yaliyomo kwenye taarifa hiyo ambayo ndiyo ilikuwa historia ya mabadiliko ya Mfumo wa Elimu. Pamoja na hiyo, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuangalia upya mfumo wetu wa elimu ili kuwezesha kuzalisha wahitimu wanaoweza kujijiri badala ya kusubiria ajira za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. Johh Pombe Magufuli kwa uamuzi wa kutoa elimu malipo. Ni ukweli ulio wazi kuwa wanafunzi wengi wamepata fursa ya kusoma kutokana na utaratibu huu. Katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba, 2015 hadi Februari, 2020, Serikali imetumia zaidi ya shilingi trilioni 1.01 kugharamia elimu bila malipo katika Shule za Msingi ikiwemo miundombinu. Kamati inapongeza sana Serikali kwa jitihada hizi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuboresha miundombinu hiyo ili wanafunzi waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia yetu kwa sasa inaelekea kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (*4<sup>th</sup> Industrial Revolution*). Kama ilivyoelezwa na Kamati mwaka, 2019. Suala la mitaala kuendana na mapinduzi haya ni muhimu sana. Tanzania haiwezi kubaki kama kisiwa kama ambavyo hatujawahi kuwa kisiwa katika masuala yoyote ya maendeleo. Ni kwa msingi huo, Kamati inaishauri Serikali ianze kuandaa nchi na hususan mifumo yetu ya elimu ikijumuisha mitaala ili kuweza kutoa Elimu ambayo itasaidia kupambana katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa namna ambavyo imewezesha kuleta maendeleo ya Sekta ya Elimu katika Miradi ya *EP4R*. Miradi hii imesaidia sana katika kuboresha miundombinu ya Elimu nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto za uchaguzi wa Shule zenye mahitaji kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati kutokana na suala hili kuhusisha Wizara zaidi ya Elimu. Kamati

inashauri Wizara ya Elimu iangalie mfumo wa uchaguzi wa shule zinazopaswa kuboreshewa miundombinu ili kuhakikisha kunakuwepo haki na usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Sekta Binafsi katika Sekta ya Elimu nchini. Itakumbukwa kuwa miaka ya nyuma kati ya mwaka 1980 - 2000 wazazi wengi walikuwa wanapeleka watoto wao nchi jirani kusoma kutokana na elimu za huko kuwa bora zaidi. Hata hivyo, baadhi ya Watanzania Wazalendo waliona umuhimu wa kupunguza gharama kwa Watanzania na kuanzisha shule hizo nchini. Kutokana na umuhimu huo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kushirikiana na wadau hawa ili kusukuma mbele gurudumu la Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; nakushukuru sana kwa fursa hii kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kuwashukuru sana wajumbe kwa kufanya kazi kwa umakini hususan wakati wa uchambuzi wa bajeti hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa. Naomba orodha ya wajumbe wa Kamati iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru, lakini pia kukupongeza kwa uongozi wako shupavu ambao umewezesha kuliongoza Bunge la 11. Aidha namshukuru Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wote Wabunge kwa kuendesha vyema vikao vya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Tata Ole Nasha, Naibu Waziri kwa ushirikiano ambao tumeujenga na kuwa nguzo katika ufanyaji kazi wetu. Aidha napenda kuwashukuru sana Makatibu Wakuu wa Wizara hii wakiongozwa na ndugu Dkt. Leonard Akwilako, Katibu Mkuu; Profesa James Mdoe, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Ave Maria Semakafu, Naibu Katibu Mkuu; na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa kamati yetu hata wakati wa uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano anaopa Kamati wakati wa kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake bila kukwama. Napenda pia kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto; Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu, Ndugu Gerald Magili, kwa ushirikiano wanaopa Kamati wakati wote. Aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Palangyo na Ndugu Nyamwanja Chilemeji kwa ushauri na utaratibu mzuri wa shughuli za Kamati pamoja na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali, liridhie na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Fungu namba 46 kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, shilingi trilioni 1. 24 na Tume ya *UNESCO*, Fungu namba 18 shilingi bilioni 2.23 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ina wajibu wa kushughulikia Bajeti ya Wizara inazosisimamia kama ilivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya kuchambua Bajeti, Kamati ilipata wasaa wa kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ulioisha kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo. Shughuli hiyo ilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

## **2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

### **2.1 UKUSANYAJI WA MADUHILI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) ilijiwekea Makadirio ya kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 553. 739**. Hadi kufikia Februari 2020, Wizara ilikuwa imekusanya **asilimia 52.9** ya makadirio ya makusanyo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 18 (Tume ya UNESCO) katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ilikadiria kukusanya Shilingi Milioni 27 hadi kufikia mwezi Februari 2020 ilikusanya **Shilingi 8,500,000.00** sawa na **asilimia 31.48** ya lengo.

### **2.2 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA MWAKA**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) iliidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi Trilioni 1.4** kwa ajili ya kutekeleza mipango na majukumu yake. Hadi kufikia Februari 2020 Wizara ilifanikiwa kupokea Jumla ya **Shilingi Bilioni 808.63** sawa na **asilimia 57.5** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 2.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika fedha za Miradi zilizopatikana **Shilingi Bilioni 421.953** sawa na **asilimia 91.9** ni fedha za ndani. ***Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha zake za ndani kwa ajili ya utekelezani wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara.***

### **2.3 MAELEZO NA MATOKEO YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA**

**Mheshimiwa Spika**, Kuanzia tarehe 13 – 17 Machi, 2020 Kamati ilifanya ziara ya kutembelea, kukagua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ziara za Kamati kwa kipindi hiki zilifanyika katika Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro ambapo jumla ya Miradi 2 ilitembelewa na kukaguliwa na Kamati pamoja na kupokea Taarifa ya Mradi mmoja. Aidha Kamati ilishindwa kufanya Ziara katika Mkoa wa Dar Es Salaam kufuatia kuahirishwa kutokana Ugonjwa wa Mafua unaotokana na Virusi vya Corona. Miradi iliyotembelewa na Kukaguliwa na Kamati ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

### **2.4 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa Maoni 12 yaliyotolewa na Kamati Mwaka 2019 na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maoni hayo. Kamati inapongeza sana Serikali kwa utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji huo mzuri, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya maoni utekelezaji wake unahitaji uwepo wa wa fedha za kutosha. Ni imani ya Kamati kuwa maoni hayo yatafanyiwa kazi hasa ikizingatiwa kuwa bado hatujafika mwisho wa Mwaka wa Fedha. Wizara ya Fedha isaidie kutoa fedha za Wizara hii kwa kuzingatia kuwa Elimu ni kila kitu kama ambavyo mwazuoni Benjamin Franklin alivyowahi kusema ***“An Investment in Knowledge Pays the Best Interest”.***

**3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**3.1 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2020/21 Wizara imepanga kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 525.93** kutoka katika vyanzo mbaimbali kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 4

**3.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia **Fungu 46** inakadiria kutumia Jumla ya **Shilingi Trilioni 1. 24**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 491.04** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara na Taasisi na **Shilingi Bilioni 750.65** ni kwa ajili ya kutekeza Miradi ya Maendeleo. Kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 5.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Tume ya UNESCO (Fungu 18), Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.23** kinaombwa kwaajili ya kutekeleza majukumu ya Tume. Kati ya Fedha hizo, mishahara inaombewa kiasi cha **Shilingi Milioni 706.88** na Matumizi Mengineyo yanaombewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.53**.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Tume imeongezeka kwa **asilimia 3.7**. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Tume hii.**

**4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-



#### 4.1 MAONI YA JUMLA

##### a)Uhaba wa Watumishi

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto ya uhaba wa Watumishi katika Sekta ya Elimu ni kubwa kwani karibu kila Taasisi ambayo Kamati iliitembelea kwa ajili ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilieleza changamoto hii. Uhaba huu umefanya Taasisi hizi na Sekta kwa ujumla kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kutokana na hali hiyo, **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa vibali vya Ajira vya Watumishi wa Sekta ya Elimu na hususan wa Taasisi ya Nelson Mandela, Chuo cha Ushirika Moshi na Chuo cha Ufundi Arusha.**

##### b)Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo siyo wa kuridhisha kama ilivyoonyeshwa kwenye Uchambuzi wa Kamati. Kamati imekuwa inashauri mara kwa mara ni bora kutenga miradi michache ambayo kutakuwa na uhakika wa upelekaji fedha. ***Kamati inaendelea kushauri utekelezaji wa ushauri huu ni muhimu ili kuondoa changamoto hii.***

##### c)Uhaba na Uchakavu wa Miundombinu

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi Nyingi za Elimu zinakumbana na uhaba na uchakavu wa Miundombinu hali ambayo inaathiri utoaji wa Elimu nchini. Kamati imeshuhudia baadhi ya majengo na miundombinu ya Taasisi za Elimu kiwa chakavu na kutokidhi mahitaji yake. Ukosefu wa Mabweni ya wanafunzi wa kike kwenye Vyuho imekuwa ikidumaza Elimu ya Watoto wa Kike nchini. **Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu lakini pia ukarabati kwa ile iliyochakaa.**

#### 4.2 Tuzo ya Udhhamini ya Rais (*Presidential Scholarship Award*)

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikishauri juu ya umuhimu wa kuanzisha Tuzo ya Udhhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kuwa na ufaulu wa juu. Lengo ni kuwawezesha kujiunga na Vyuo vizuri Duniani ili kupata Elimu bora ambayo itakuwa na manufaa kwa Taifa lakini pia italetta chachu kwa wanafunzi wengine kufanya vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu huu umekuwa na matokeo mazuri kwa nchi za wenzetu. Kwa mfano Korea ya Kusini ilifanikiwa kutokana na kupelekea Wanafunzi katika Vyuo vizuri Duniani kama Havard, MIT, Oxford n.k Pamoja na Majibu ya Hoja hii ambayo yamekuwa yakitolewa na Wizara, **Kamati inaona bado kuna umuhimu wa kuanzisha Tuzo hii kwa maendeleo ya watoto wetu na Taifa.**

#### 4.3 Mfumo wa Elimu

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefarijika kusikia Wizara imepokea ushauri wa Kamati iliutoa Mwaka 2019 wa kusoma ripoti ya Tume iliyoundwa na Rais wa 40 wa Marekani Ronald Reagan Mwaka 1983 kwa lengo la kuiga mazuri yaliyomo kwenye Taarifa hiyo ambayo ndiyo ilikuwa historia ya mabadiliko ya Mfumo wa Elimu Marekani. **Pamoja na hiyo, Kamati inaendelea kusesitiza Serikali kuangalia upya mfumo wetu wa elimu ili kuwezesha kuzalisha wahitimu wanaoweza kujajiri badala ya kusubiria ajira za Serikali.**

#### 4.4 Elimu bila malipo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. Johh Pombe Magufuli kwa uamuzi wa kutoa elimu malipo. Ni ukweli ulio wazi kuwa wanafunzi wengi wamepata fursa ya kusoma kutokana na utaratibu huu. Katika kipindi cha miaka minne kuanzia Disemba 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya Shilingi trilioni 1.01 kugharamia Elimu bila Malipo katika Shule za Msingi

ikiwemo miundombinu. **Kamati inapongeza sana Serikali kwa jitihada hizi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuboresha miundombinu hiyo ili wanafunzi waweze kusoma vizuri.**

#### **4.5 Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4<sup>th</sup> Industrial Revolution)**

**Mheshimiwa Spika**, Dunia yetu kwa sasa inaelekea kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. Kama ilivyoelezwa na Kamati Mwaka 2019, Suala la Mitaala kuendana na mapinduzi haya ni muhimu sana. Tanzania haiwezi kubaki kama kisiwa kama ambayo hatujawahi kuwa kisiwa katika masuala yoyote ya maendeleo. **Ni kwa msingi huo, Kamati inashauri Serikali ianze kuandaa nchi na hususan mifumo yetu ya elimu ikijumuisha Mitaala ili kuweza kutoa Elimu ambayo itasiadia Watasaidia kupambana katika Soko la Dunia.**

#### **4.6 Miradi ya EP4R**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa namna ambavyo imewezesha kuleta maendeleo ya Sekta ya Elimu kupitia Miradi ya EP4R. Miradi hii imesaidia sana katika kuboresha Miundombinu ya Elimu nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini uwepo wa changamoto za uchaguzi wa Shule zenye mahitaji kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati kutokana na suala hili kuhusisha Wizara zaidi ya Elimu. **Kamati inashauri Wizara ya Elimu iangalie mfumo wa uchaguzi wa Shule zinazopaswa kuboreshewa miundombinu ili kuhakikisha kunakuwepo haki na usawa.**

#### **4.7 Umuhimu wa Sekta Binafsi kwenye Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Sekta Binafsi katika Sekta ya Elimu nchini. Itakumbukwa kuwa miaka ya nyuma kati ya Mwaka 1980 - 2000 Wazazi wengi walikuwa wanapeleka watoto wao nchi jirani kusoma kutokana na Elimu za huko kuwa bora zaidi. Hata hivyo, baadhi ya Watanzanai Wazalendo waliona umuhimu wa kupunguza gharama kwa Watanzania na

kuanzisha Shule hizo nchini. **Kutokana na umuhimu huo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kushirikiana na Wadau hawa ili kusukuma mbele gurudumu la Sekta ya Elimu.**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa kufanya kazi kwa umakini na hususan wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii muhimu kwa Mustakabali wa Taifa. Naomba orodha ya Wajumbe wa Kamati iingie yote kwenye hansard.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kukushukuru lakini pia kukupongeza kwa uongozi shupavu ambao umwezesha kuliongoza vyema Bunge letu la 11. Aidha, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kwa kuendesha vyema vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, namshukuru Prof. Joyce Ndalichako (Mb)-Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. William Tata Ole Nasha (Mb) - Naibu Waziri kwa ushirikiano ambao tumeujenga na kuwa nguzo katika ufanyaji kazi wetu. Aidha, napenda kuwashukuru sana Makatibu Wakuu za Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Leonard Akwilapo - Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe- Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Ave Maria Semakafu Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano amabo wamekuwa wakiipa Kamati na hata wakati wa uchambuzi wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano anaoipa Kamati wakati wote na kuhakikisha Kamati inatekeleza Majukumu yake bila kukwama. Napenda pia kumshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Gerald Magili kwa kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, nawashukuru sana Makatibu wetu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Nyamwanja

Chilemeji kwa ushauri na uratibu mzuri wa shughuli za Kamati pamoja na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali, liridhie na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 **Shilingi Trilioni 1. 24** na Tume ya UNESCO (**Fungu 18**) **Shilingi Bilioni 2. 23** kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono Hoja.

Peter J. Serukamba, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA  
MAENDELEO YA JAMII**

24 APRILI, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Waheshimiwa Wabunge sasa ni saa ya Msemaji wetu lakini ameelekea Msekwa wakati akijiandaa kutusomea hiyo taarifa yake, nami nimekwishaipitia na kwa mwongozo ambao ulishatolewa hapa sehemu (f) sijui kama Mheshimiwa Susan Lyimo ameshafika Msekwa. Wataalamu wetu waliopo kule.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo sehemu (F) kwa maana ya aya ya 53 mpaka aya ya 57 zinaenda kinyume na kanuni zetu, kwa hivyo sehemu hiyo hautasoma. Msemaji wa Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Susan Lyimo, karibu.

Mheshimiwa Haonga hili ni Bunge la mwisho, tafadhali sana tuheshimiane, haya mambo yamesharudiwa mara kadhaa humu ndani yakielezwa, kama hujasikia kuhusu taarifa hii kuanzia tarehe Mosi Aprili, mpaka leo hilo unalolitafuta safari hii tafadhali, Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya Uhai na kunijalia afya njema kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili. Pili, napenda pia kutumia nafasi hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe kwa kuendelea kuniamini na kunitaua mara tano mfululizo katika nafasi hii kama Waziri kivuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Waziri Kivuli wa Elimu kabla ya Bunge la 11 kuisha na kwa kuwa tuko katika janga la *corona* ambalo limeadhiri sekta ya elimu kwa asilimia 100 hotuba yangu itajikita zaidi kwenye kuishauri Serikali kuchukua hatua za kukabiliana na janga kwa kubuni njia mbadala za utoaji wa elimu wakati huu ambapo wanafunzi hawapo shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maoni ya Kambi kuhusu bajeti ya wizara hii napenda kutumia fursa hii kuwatia moyo Watanzania hususan wanafunzi na watumishi wote wa sekta ya elimu nchini, Walimu na wasio Walimu kufatia janga la *corona* lililokumba nchi yetu. Nawasihi waendeleo kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu kama ilivyoelekezwa na wataalam wa afya na waendeleo kuishi kwa matumaini wakiomba Mungu aepushe Taifa hili na balaa hili ambalo halijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule na taasisi za elimu binafsi zinategemea ada za wanafunzi kulipa mishahara kwa Walimu na watumishi wengine wasio Walimu ni dhahiri kwamba kufungwa kwa shule na taasisi hizo

kutaadhiri uwezo wa shule na taasisi hizo kulipa mishahara kwa watumishi na tayari baadhi ya shule na taasisi zimetoa barua za likizo ya bila malipo kwa watumishi wao jambo ambalo linapelekea maisha kuwa magumu kwa Walimu na watumishi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke pia shule na taasisi binafsi za elimu zimeanzishwa na wawekezaji ambao walikopa benki lakini pia kwa mujibu wa sheria wanapaswa kuwalipa wafanyakazi stahiki zao zikiwa ni pamoja na kodi kama vile *Pay As You Earn, NSSF, Workers Compensation Fund* na kadhalika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba ili kunusuru kuanguka kwa sekta binafsi kwenye utoaji wa elimu, Serikali ione ni jinsi gani itazisaidia shule hizi kipindi hiki cha *corona* hasa mishahara kwa Walimu ama kuwakopesha bila riba au kutumia mifuko ya akiba kwa ajili ya kuwasaidia katika kipindi hiki ambacho hatujui ni lini janga hili litaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ya *corona* iko kuanzia ukurasa wa nne na athari zake kuanzia ukurasa wa nne hadi wa 16 lakini nitasema kwa kifupi kwa sababu ya muda. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingani kabisa na uamuzi wa Serikali wa kufunga shule na taasisi nyingine za elimu kama hatua ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya *corona*. Hata hivyo ni vyema kama Taifa tukawa na uelewa pamoja kuhusu madhara yanayoweza kutokea kwenye sekta ya elimu ikiwa shule zitaendelea kufungwa. Kwa kuwa Mkutano huu wa Bunge ni maalum kwa ajili ya kuidhinisha bajeti ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Bajeti ya Elimu ipangwe kwa namna tofauti na miaka mingine ili kuzingatia hali halisi ya ugonjwa wa *corona* ambao umeathiri sekta ya elimu kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa kutumia teknolojia ya elimu kufidia masomo yaliyokosekana kwa kipindi ambacho shule zilikuwa zimefungwa si jambo jepesi kwa kuwa nchi haikuwa imejiandaa na janga hili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inatambua pia kwamba si rahisi kwa kila kaya kuweza kuwa na vifaa vya kiteknolojia kama vile simu janja (*smart phones*) au *computer*. Aidha uwezo wa kuwa bna vifurushi vya *data* kwa ajili ya kupakua(*download*) kwa mada za kielimu pamoja na vitabu vya kiada na ziada ni changamoto kwa kaya nyingi kutokana na hali ya uchumi. Kwa sababu hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia bajeti hii kuanzisha mpango madhubuti wa muda mfupi na wa muda mrefu wa kuhakikisha kuwa vifaa vya kiteknolojia vya kujifunzia katika shule na vyuo ambavyo vinaweza kusaidia kutoa elimu ya masafa yaani *distance learning* ikiwa ni pamoja na nyenzo za kufundishia na kujifunzia (*educational materials*) ili kufidia muda wa masomo uliopotoea kama zilivyofanya baadhi ya nchi mbalimbali kama ambavyo zinajionyesha kwenye *speech* yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuandaa mpango wa muda mfupi na mrefu kwa ajili ya kutatua changamoto hizo kielimu na hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja itengwe bajeti ya kuendesha vipindi vya kitaaluma katika redio na *television* kwa kuanzia *Television* ya Taifa yaani *TBC1* na *TBC* Taifa zitumike kurusha vipindi hivyo kwa hatua ya baadaye. *Television* na redio binafsi kwa hatua baadaye zinaweza kuomba kuingizwa kwenye mpango huo ikiwa itaonekana kwamba *television* na redio ya Taifa havikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa mifano kama ambavyo imeainishwa hapo chini lakini la pili tunasema itengwe bajeti kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa watoa huduma za *internet* ili kupunguza gharama za upakuaji wa mada, machapisho na vitabu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ambako kuna hitaji kubwa la kutumia mfumo wa elimu masafa (*distance learning*) kutokana na *corona* Serikali inatakiwa kuchukua hatua na kujadiliana na wadau mbalimbali na kutenga bajeti na kutoa ruzuku kwa watoa huduma hizo ili kupunguza



gharama za *downloading* za mada, machapisho kwa wanafunzi, Walimu na wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za mamlaka ya Mawasiliano *TCRA*, mtandao wa *internet* ulikuwa umesambaa nchini kwa asilimia 43 kufikia mwaka 2018. Huu ukiwa na asilimia 48 ya watumiaji wa simu wanaounganishwa na mtandao wa *internet*. Hii ni sawa na kusema kwamba kati ya watu milioni 43 wanaotumia simu angalau watu milioni 23.1 walikuwa ni watumiaji wa mitandao ya *internet*. Kwa hiyo tunaomba Wizara kupitia Serikali Kuu ione umuhimu sasa wa kutenga bajeti kwa muda huu mfupi ili waweze kusaidia wananchi ili watoto waweze kusoma kupitia *distance learning*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili kuwapunguzia mzigo wa gharama wanafunzi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Fedha kukaa pamoja na kuandaa mpango wa ruzuku wa matumizi ya mtandao wa *internet* pamoja na vipindi vya taaluma na machapisho yatakayohusika na ruzuku hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunajifunza na kupata uzoevu kutoka kwa nchi zilizokumbwa na *corona* ili tuweze kuboresha mazingira yetu ya utoaji elimu ni lazima kama Taifa tujiulize, Wizara yetu ya elimu mpaka sasa imefanya nini kutatua changamoto ya kukosa masomo hasa kwa kipindi ambacho shule shule zimefungwa na hatujui zitafunguliwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba zipo taasisi za kitaaluma chini ya Wizara hii, hata hivyo, tungependa kujua Wizara ya Elimu imetumia vipi utaalum wa taasisi zake hususan taasisi za uvumbuzi kwa mfano *COSTECH* wamefanya nini mpaka sasa hivi na vyo vyetu vya teknolojia ili kusaidia kutatua tatizo hili la mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunahitaji bajeti ya elimu msingi iongezwe ili kuongeza vifaa vya TEHAMA. Kufatia mlipuko wa ugonjwa huu Serikali ione haja ya kuongeza bajeti ya maendeleo ya elimu msingi ili kuweza kutatua changamoto za mazingira magumu ya kujifunza hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya *Corona*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza nyongeza hiyo ya fedha iwekezwe katika teknolojia ya elimu na elimu ya masafa ili wanafunzi waweze kuendelea kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msisitizo uliowekwa na sera ya elimu ya mwaka 2014 kuhusu umuhimu wa matumizi ya TEHAMA, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshutushwa sana na Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI ya mwaka huu Aprili kwamba kati ya shule 3,742 za umma ni shule 153 sawa na asilimia nne tu zinazofundisha TEHAMA. Wanafunzi 36,101 tu ndio wanasoma TEHAMA kati ya wanafunzi zaidi ya milioni moja na nusu ya shule za Serikali. Tunaendaje kwenye uchumi wa viwanda bado tuko nyuma kiteknolojia? Ni rai yangu kuwa ugonjwa huu utatufungua fikra zetu zione mbali zaidi na kutenga bajeti zaidi kwenye TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunapendekeza Serikali ipunguze kodi kwenye simu za mikononi na vifaa vingine vya kieletroniki kwa ajili ya kufundisha na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia itenge bajeti kwa ajili ya mafunzo na matumizi ya TEHAMA kwa Walimu na uhamasishaji wa umma kuhusu matumizi ya TEHAMA. Mara nyingi tunakuwa na simu za mikononi na vifaa lakini wengi hatujui matumizi halisi kwa hiyo ni muhimu pia katika kipindi hiki Walimu na wanafunzi wapate mafunzo hayo ili waone jinsi gani wanaweza kutumia vifaa vyao vya simu katika kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa madarasa na matundu ya vyoo bado ni changamoto inayokabili elimu. Kwa miaka yote Kambi Rasmi ya Upinzani imeshauri kuwe na mpango maalum wa ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo. Ujio wa elimu bure umeongeza uhaba mkubwa wa

vyumba vya madarasa hivyo tulishauri kuwa kwa kuwa Serikali ina takwimu za watoto wanaoingia darasa la kwanza kila mwaka na pia inajua *approximation* ni wanafunzi wangapi watafaulu darasa la saba ni muhimu fedha zitengwe kwa kila mwaka kwa ajili ya madarasa na vyoo kwa idadi ili ndani ya miaka mitano tatizo liwe limepungua au limekwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake baadhi ya wanafunzi waliofaulu kukaa nyumbani zaidi ya miezi mitatu kusubiri madarasa wengine wakienda kwa *shift*, hii sio sawa kabisa na ubora hapa hauwezi kupatikana. Kwa takwimu hizi ni lazima basi Serikali ikiri kwamba upungufu wa vyumba vya madarasa ni jinamizi lingine linalonyemelea kunyonga elimu yetu na haingii akilini kuwa wanafunzi wetu takribani 200,000 wameshindwa kuingia kidato cha kwanza kwa miaka miwili iliyopita. Hivyo basi, ni muhimu kama tunavyosema kuwe na mpango mahususi na mpango maalum ambao utawezesha kutengwa kwa fedha na madarasa kiasi fulani au matundu yaliyo kiasi gani kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na adha hii ya upungufu wa vyumba na madarasa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuandaa mkakati na mpango wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa shule za msingi ambapo kuna upungufu wa vyumba zaidi ya 100,000 Serikali inatakiwa itenge bajeti ya takribani shilingi trilioni 1.5 kwa maana ya shilingi milioni 15 kwa darasa moja kwa hiyo wakiweza kutenga kila mwaka bilioni 300 ina maana kwa miaka mitano tatizo hili litaweza kwisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia itenge bajeti ya ajira za Walimu; nakumbuka kwamba tumeona kuna tatizo kubwa sana la ajira za Walimu na kwa maana hiyo tunaomba kama ile ahadi ya Naibu Waziri ya mwaka jana kwamba kila mwaka atakuwa anatenga ajira 10,000 basi jambo hilo lifanyike ili Walimu waweze kuwafundisha watoto wetu na uwiano wa wanafunzi kwa watoto uweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kupata fungu lake; jambo hili tumelizungumza muda mrefu na nakumbuka mwaka jana tulivyoongea Bungeni, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliahidi kwamba katika bajeti hii Bodi ya Mikopo itakuwa na *Vote* yake pekee, lakini cha kushangaza mpaka leo hatuoni na hakuna huo utaratibu. Tunasema hivi kwa sababu ukiangalia bajeti ya Wizara ya Elimu tunajua kwamba Bodi ya Mikopo iko kwenye fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha za maendeleo mwaka huu bilioni 857, Bodi ya Mikopo imepata bilioni 464 sawa na asilimia 57, lakini wote tunajua fedha hizi ni fedha za ndani zote za Bodi ya Mikopo. Kwa hiyo kwa fedha za ndani tulizonazo ambazo ni shilingi bilioni 600 na hawa wamepata 464, maana yake ni kwamba Bodi ya Mikopo imepata fedha za ndani asilimia 76.5. Haiwezekani asilimia 23.5 tu ndio zibaki kwa sekta nzima ya elimu kwa maana ya Wizara ya Elimu ukizingatia kuna vyuo vikuu, kuna taasisi za vyuo vya elimu na mengine mengi na hasa *quality assurance* kwa maana ya udhibiti ubora. Kwa hiyo tulitegemea kwamba ingekuwa na *Vote* yake Bodi ya Mikopo walau Serikali ingejipanga vizuri zadi kuhakikisha kwamba hizi idara nyingine nazo zinapata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo cha kusimamia elimu; tunambua kwamba mfumo wetu wa elimu hauna chombo chochote isipokuwa Serikali ndio inasimamia elimu hapa Tanzania, lakini vilvile tutambue kwamba Serikali yenyewe ina shule zaidi ya asilimia 85, haiwezekani Serikali hiyo hiyo yenye shule za umma, Serikali hiyo hiyo isimamie shule binafsi na Serikali hiyo hiyo iwe ndio kocha, mchezaji na vilevile iwe Tamisaa. Kwa hiyo tunaendelea kusititiza kwamba ni muhimu kuwe na chombo maalum au chombo huru ambacho kitakuwa kinasimamia elimu na kwa kweli hiki kitasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhamini wa vijana wanaofanya vizuri; tayari Mwenyekiti wa Kamati yangu naye amelizungumzia hili jambo, nataka kusisitiza tu ni muhimu sana

wale wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi kidato cha sita ni muhimu wakagharamiwa kila kitu, lakini wakasoma nje ya nchi ili kuweza kupata *exposure*, lakini vilevile kuja na teknolojia ili waweze kuja kutusaidia huko siku za baadaye. Kwa hiyo tunaomba sana jambo hili lifanyike ili tuweze kupata wataalam wazuri zaidi, kwa sababu sisi kama nchi tumekuwa na wahitimu wa masomo ya sayansi kwa miaka toka 1970s lakini bado ukiangalia hata kwenye *Stieglie's Gorge* au kwenye *SGR* unakuta ile *management team* wengi wanatoka nje. Kwa hiyo ni muhimu sana sisi kama taifa tuweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu wa sayansi na teknolojia; hakuna Taifa lililoendelea bila kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia. Hivyo basi, tunaomba Serikali iendelee kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia kwa sababu ukiangalia hata bajeti ya mwaka huu; ubunifu, sayansi na teknolojia imetengewa asilimia 0.5 tu ya fedha za maendeleo, kwa maana ya shilingi bilioni 5.1. Hatuwezi kuendelea mbele kisayansi kama hatutawekeza kwenye sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipatia Tume hii fedha za kutosha katika kipindi hiki cha *corona* ili waweze kusaidia kwenye elimu mtandao yaani TEHAMA. Haiwezekani kasma 8001 inayohusu sayansi na teknolojia na ubunifu ipate asilimia 1.4 tu ya bajeti ya maendeleo ya Wizara yaani shilingi bilioni 12 kati ya bilioni 857. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua umuhimu wa sayansi na teknolojia na kwa maana hiyo inategemea kwamba wataendelea kuwapa fedha za kutosha ili Taifa letu liweze kusonga mbele kisayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa Wahadhiri katika vyuo vikuu; jambo hili liko wazi vyuo vyetu vya elimu ya juu kwa kweli bado vina upungufu mkubwa sana wa Wahadhiri na jambo hili limeendelea kuwa kubwa zaidi baada ya Mheshimiwa Rais kuwa anateua Wahadhiri wengi kwenye nafasi za kisiasa. Jambo hilo ni jema lakini bado linaadhiri sana vyuo vyetu vya elimu ya juu na kwa maana hiyo tunaomba pale ambako kunakuwa na uteuzi basi kuwe na

*replacement* kwa sababu tunajua mtu mpaka kupata *PhD* inachukua muda mrefu, kwa hiyo ni muhimu sana kuwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na wahadhiri wa kutosha kwa maana wa *PhD* na wale wa *Masters* katika vyuo vyetu vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; hotuba hii imezungumzia kwa kirefu sana namna Sekta ya Elimu ilivyoathirika na Janga la Corona.

Aidha, imetoa mapendekezo na ushauri mwingi kwa Serikali juu ya matumizi ya mbinu mbadala za kutoa elimu kwa kipindi hiki ambacho shule na vyuo vya elimu vimefungwa. Sambamba na mapendekezo hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kupanga bajeti ya elimu kwa kuzingatia athari za Corona ambazo zimeelezwa kwa kirefu kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela, aliwahi kusema *no country can really develop unless its citizens are educated* ikiwa na maana kwamba hakuna nchi inaweza kuendelea kama wananchi wake hawajaelimika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa elimu ndiyo kila kitu kwenye mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Changamoto karibu zote ambazo nimezieleza kwenye hotuba yangu zinahusiana moja kwa moja na changamoto za kisera, usimamizi wa elimu na mfumo wa upangaji wa usimamizi wa bajeti katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama Taifa tunahitaji kuelewa nini falsafa ya elimu yetu, nini malengo makuu ya elimu yetu na tuwe na mikakati ya kuhakikisha

mfumo wetu wa elimu unalenga kutoa elimu jumuishi, elimu inayotoa fursa kwa watoto wote wa Tanzania kupata elimu bora na elimu inayolenga kumlinda na kumuendeleza mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora kwa kila mtoto wa Tanzania ndiyo itakayosaidia Tanzania hii kupata maendeleo. Ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa Serikali itayachukua na kuyafanyia kazi mapendekezo tuliyoyotoa kwa mustakabali mwema wa elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaamini Serikali itatekeleza kwa vitendo suala zima la Corona kuhakikisha kwamba wale wamiliki wa shule binafsi wanapatiwa msaada haraka sana kwa ajili ya kuwalipa walimu na wafanyakazi kwa sababu wote tunajua walimu na wafanyakazi wanategemea ada kutoka kwa wazazi na ada hizo haziwezi kupatikana kwasababu watoto wametoka shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa aibu Spika, kwa hiyo, ufanywe utaratibu wa haraka jinsi gani ya kuweza kuwasaidia watoto hawa kwa sababu sisi wenyewe tuliamua kwamba Serikali yenyewe haiwezi kuwa na shule zake peke yake tukakubali kuwe na shule za binafsi ambazo zinasaidia watoto wa Kitanzania, sio watoto wa nje ya Tanzania.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Serikali italichukua hili kama njia mbadala ya kuweza kusaidia kwa sababu vinginevyo hawa waimu tunakwenda kuwapoteza, na sisi wote tunajua kwamba tuna tatizo kubwa la walimu lakini wote tunajua kwamba hizi shule binafsi zimeleta maendeleo makubwa ya elimu hapa nchini. Kwa hiyo, ni matumaini yangu jambo hilo litashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA  
NA UFUNDI, MHESHIMIWA SUSAN ANSELM JEROME LYIMO  
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA  
UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2020/2021 – KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kwa zawadi ya uhai na kunijalia afya njema kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili la 11. Pili, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ninatoa salamu za rambirambi kwako Mheshimiwa Spika na kwa Wabunge wote kufuatia kifo cha Mbunge Mwenzetu, Marehemu Mchungaji Getrude Rwakatare ambaye Mwenyezi Mungu alimtwaa katika dunia hii tarehe 20 Aprili, 2020. Salamu hizi ziwaendee pia ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya Marehemu na kipekee kwa waumini wa Kanisa la Mlima wa Moto ambako Marehemu alikuwa akitoa huduma za Kichungaji. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina!

**2. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa imani kubwa aliyo nayo kwangu; kwa kuendelea kuiteua mfululizo kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho kama Waziri Kivuli wa Elimu kabla ya Bunge hili la 11 kufikia ukomo wa uhai wake, na kwa kuwa tuko katika janga la Corona ambalo limeiathiri sekta ya elimu kwa asilimia 100; hotuba yangu itajikita zaidi kwenye kuishauri Serikali kuchukua hatua za kukabiliana na janga hili kwa kubuni njia mbadala za utoaji wa elimu wakati huu ambapo wanafunzi hawapo shuleni na vyuoni ili kuliepusha Taifa na madhara makubwa zaidi siku za mbeleni ya kuwa na kizazi kilichokosa elimu.



**4. Mheshimiwa Spika,** kabla sijatoa Maoni ya Kambi Rasmi kuhusu bajeti ya Wizara hii; napenda kutumia fursa hii pia kuwatia moyo Watanzania hususani wanafunzi kufuatia janga la Corona liloikumba nchi yetu. Ninawasihi waendeleo kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya na waendeleo kuishi kwa matumaini wakimwomba Mungu aliepushe Taifa na balaa hili ambalo halijawahi kutokea katika historia ya nchi yetu.

**5. Mheshimiwa Spika,** neno la faraja ninalolitoa kwa wanafunzi, ninalitoa pia kwa watumishi wote wa sekta ya elimu nchini (walimu na wasio walimu) kwamba waendeleo kuwa na subira na pia waisaidie Serikali kubuni njia mbadala za utoaji wa elimu ikiwa ugonjwa huu utaendelea kwa muda mrefu. Rai yangu kwa Serikali, ni kwamba iendeleo kuwatunza watumishi wa sekta ya elimu kwa kuwapatia stahili zao zote katika kipindi hiki kigumu kwa kuwa kada hii ndiyo inayojenga maarifa na ujuzi katika Taifa – mambo ambayo ndio msingi wa maendeleo endelevu.

**6. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa shule na taasisi za elimu za binafsi zinategemea ada za wanafunzi kulipa mishahara kwa walimu na watumishi wengine wasio walimu; ni dhahiri kwamba kufungwa kwa shule na taasisi hizo kutaathiri uwezo wa shule na taasisi hizo kulipa mishahara kwa watumishi; na tayari baadhi ya shule na taasisi zimetoa barua za likizo bila malipo kwa watumishi wao jambo ambalo linapelekea maisha kuwa magumu kwa walimu na watumishi hao.

**7. Mheshimiwa Spika,** leleweke pia shule na taasisi binafsi za elimu zimeanzishwa na wawekezaji ambao walikopa benki, lakini pia kwa mujibu wa sheria wanapaswa kuwalipa wafanyakazi wao stahiki zao zikiwa ni pamoja na kodi kama vile PAYE, NSSF, Workers Compensation Fund na kadhalika. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba ili kunusuru kuanguka kwa sekta binafsi kwenye utoaji wa elimu, Serikali ione ni jinsi gani itazisaidia shule hizi kipindi hiki cha Corona hasa mishahara kwa walimu ama kwa kuwakopesha bila riba au kwa utaratibu wowote utakaofaa. Nasisitiza hivi

kwa kuwa mwanzo ilionekana ni tatizo dogo na wakapewa mwezi mmoja; lakini kwa mujibu wa Tangazo la Waziri Mkuu ni kwamba sasa shule na taasisi zote za elimu zitafungwa mpaka hapo itakapotangazwa vinginevyo.

## **B. UGONJWA WA CORONA NA ATHARI ZAKE KWENYE ELIMU**

**8. Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyoieleza hapo awali na kama ambavyo imetokea katika nchi nyingine, Tanzania nayo imepata pigo la kukumbwa na ugonjwa wa Corona. Kufuatia janga hili, Serikali tayari imefunga taasisi zote za elimu zikiwemo Shule za Msingi, Sekondari, Vyuvo vya Kati na Vyuvo Vikuu. Kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI ya Aprili, 2020 zaidi wanafunzi milioni 14 wa Shule za Msingi (12,034,577) na Sekondari (2,023,457) wamerudi majumbani na wataendelea kukosa masomo kwa kipindi chote ambacho shule zitakuwa zimefungwa kutokana na janga la Corona. Idadi hiyo inajumuisha pia wanafunzi ambao walikuwa wanakaribia kufanya mitihani yao ya Taifa.

**9. Mheshimiwa Spika**, Kufungwa kwa shule na taasisi nyingine za elimu kutokana na janga hili kutarudisha nyuma sana sekta ya elimu ambayo tayari ilikuwa na changamoto nyingi zikiwemo za ufaulu mdogo, viwango vya juu vya kuacha masomo (drop outs) na uhimilivu mdogo wa wanafunzi kubaki shuleni hadi kuhitimu.

**10. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kabisa na uamuzi wa Serikali wa kufunga shule na Taasisi nyingine za Elimu kama hatua ya kuzuia kusambaa kwa Virusi vya Corona. Hata hivyo, ni vema kama Taifa tukawa na uelewa wa pamoja kuhusu madhara yanayoweza kutokea kwenye Sekta ya Elimu, ikiwa shule zitaendelea kufungwa.

**11. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Mkutano huu wa Bunge ni maalum kwa ajili ya kuidhinisha Bajeti ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba bajeti ya elimu ipangwe kwa namna tofauti na miaka mingine ili kuzingatia hali halisi ya ugonjwa wa Corona ambao

umeathiri Sekta ya Elimu kwa asilimia 100. Ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Bajeti ya Elimu itazingatia uhalisia kwamba wanafunzi hawapo shuleni na vyuoni na masomo yamesimama. Katika mazingira kama hayo ni lazima upangaji wa bajeti uweke mkazo kwenye njia nyingine za kupata elimu kama vile elimu ya masafa (distance learning). Kwa msingi huo ni lazima kipaumbele cha bajeti ya elimu kwa sasa kiwe ni uwekezaji kwenye teknolojia ya elimu ili elimu iweze kuendelea kutolewa kupitia nyenzo na maarifa mengine tofauti na ilivyokuwa awali kwa wanafunzi kukusanyika kwenye darasa moja na kufundishwa.

**12. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa kutumia teknolojia ya elimu kufidia masomo yaliyokosekana kwa kipindi ambacho shule zilikuwa zimefungwa si jambo jepesi kwa kuwa nchi haikuwa imejiandaa na janga hili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua pia kwamba si rahisi kwa kila kaya kuweza kuwa na vifaa vya kiteknolojia kama vile simu janja (smartphones) au kompyuta. Aidha, uwezo wa kuwa na vifurushi vya data kwa ajili ya kupakua (downloading) mada za kielimu pamoja na vitabu vya kiada na ziada ni changamoto kwa kaya nyingi kutokana na hali duni ya uchumi.

**13. Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, na kutokana na mazingira tuliyonayo sasa hivi ya shambulio la COVID 19; ni lazima Serikali ianze kufikiria njia na mbinu nyingine za kutoa elimu kwa wanafunzi wetu tofauti na ilivyokuwa zamani. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia bajeti hii, kuanzisha mpango madhubuti wa muda mfupi na muda mrefu wa kuhakikisha kuwa kuna vifaa vya kiteknolojia vya kujifunzia katika shule na vyo ambavyo vinaweza kusaidia kutoa elimu ya masafa (distance learning); ikiwa ni pamoja na nyenzo za kufundishia na kujifunzia (educational materials) ili kufidia muda wa masomo uliopotea.

**14. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mazingira magumu yanayolikabili Taifa kwa sasa kufuatia gonjwa la Corona, Tanzania haina budi kujifunza kutoka nchi zilizokumbwa na

janga kama hili na ambazo zimeamua kutumia mfumo wa elimu ya masafa (distance learning) kama njia mojawapo ya kufidia muda wa masomo uliopotea baada ya shule kufungwa. Kwa mfano, nchi kama China, Italia, Ufaransa, Ujerumani na Saudi Arabia zimeamua kutoa elimu kwa njia ya mtandao (online learning). Nchi za Vietnam na Mongolia zinatumia simu za mkononi, runinga na redio kama nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji.

**15. Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuandaa mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu kwa ajili ya kutatua changamoto za kielimu zilizoababishwa na athari za COVID 19. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza mpango huo utengewe bajeti katika mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifutavyo:-

**i. Itengwe Bajeti ya Kuendesha Vipindi vya Kitaaluma katika Redio na Televisheni**

**16. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa hatujui COVID 19 itakwisha lini; Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba Serikali itenge fedha kupitia bajeti hii kwa ajili ya kulipia vipindi vya kitaaluma katika redio na televisheni ili wanafunzi waendeleo kupata masomo kipindi hiki ambacho shule zimefungwa. Kwa hatua ya sasa, Televisheni ya Taifa (TBC1) na Redio ya Taifa (TBC- Taifa) zitumike kurusha vipindi hivyo. Kwa hatua ya baadaye, televisheni na redio binafsi zinaweza kuomba kuingizwa kwenye mpango ikiwa itaonekana kwamba Televisheni na Redio ya Taifa hazikidhi mahitaji.

**17. Mheshimiwa Spika**, jambo hili linawezekana kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wanamiliki redio, televisheni au simu ya mkononi. Kwa mujibu wa tathmini ya bajeti kwa kila kaya (Household Budget Survey) kwa mwaka 2017 -2018 ni kwamba asilimia ya kaya zinazomiliki redio, televisheni na simu za kiganjani ni 43, 24 na 78 kwa mtiririko huo. Kwa hali hiyo, ni kwamba wananchi sasa wanaweza kusikiliza redio au kutazama vipindi vya televisheni kupitia simu janja, ving'amuzi

na pia Runinga zao. Kwa hiyo kipindi hiki ambacho inashauriwa watu kuwa mbali na wengine (social distancing) au kuwa katika zuio la kutoka nje (quarantine) kutokana na kujikinga na maambukizi ya COVID 19 au ikiwa kutatokea katazo la kutotoka nje kabisa (total lock down) elimu inaweza kuendelea kutolewa kwa kutumia vyombo vya habari kama vile redio na televisheni.

**18. Mheshimiwa Spika**, ni vema kama Taifa tukajipanga mapema na kubadili mfumo wetu wa elimu kwenda kwenye mfumo wa kidijitali kupitia redio na runinga. Kwa mujibu wa Taarifa ya Haki Elimu ya Aprili, 2020; mfumo huu umefanikiwa sana katika nchi za Honduras, Nicaragua, Papua New Guinea, Guinea, Liberia, Somalia, Cape Verde, Angola, Msumbiji, Guinea-Bissau, Afrika ya Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ufundishaji kwa njia ya redio na televisheni vitasaidia wanafunzi kujifunza wakiwa majumbani na hivyo kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona.

**ii. Itengwe Bajeti kwa ajili ya Kutoa Ruzuku kwa Watoa huduma za 'Internet' ili kupunguza gharama za upakuaji (downloading) wa Mada, Machapisho na Vitabu mbalimbali vya Elimu kwa Wanafunzi**

**19. Mheshimiwa Spika**, Kipindi hiki ambacho kuna hitaji kubwa la kutumia mfumo wa elimu masafa (distance learning) kutokana na Corona, Serikali inatakiwa kuchukua hatua ya kujadiliana na watoa huduma za Internet na kutenga bajeti ya kutoa ruzuku kwa watoa huduma hizo ili kupunguza gharama za upakuaji (downloading) wa mada, machapisho, vitabu na mihadhara ya moja kwa moja (live-streaming tutorials) kwa wanafunzi, walimu na pia wazazi.

**20. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) mtandao wa Internet ulikuwa umesambaa nchini kwa asilimia 43 kufikia mwaka 2018 huku kukiwa na asilimia 48.77 ya watumiaji wa simu waliounganishwa na mtandao wa Internet. Hii ni sawa na kusema kwamba kati ya watu milioni 43.62 wanaotumia simu, angalau watu milioni 23.14 walikuwa ni watumiaji wa mtandao wa Internet.

**21. Mheshimiwa Spika,** Ingawa matumizi ya mtandao wa internet kupitia simu yanaweza kusaidia kutoa elimu ya masafa (distance learning), lakini gharama za vifurushi vya Internet ni changamoto kubwa hasa kwa wananchi waishio vijijini kutokana na hali ngumu ya uchumi. Hii ni kwa sababu wastani wa gharama za kifurushi cha MB 750 ni shilingi 1,000 kwa siku (saa 24). Hii ina maana kwamba itahitajika angalau shilingi 30,000/= kwa mwezi kugharamia vifurushi vya Internet. Gharama hii ni kubwa kwa familia za kawaida zenye wanafunzi katika shule za umma kuweza kumudu.

**22. Mheshimiwa Spika,** Ili kuwapunguzia mzigo wa gharama wanafunzi, walimu na wazazi ambao watatumia njia mbadala ya mtandao kupata elimu baada ya katazo la mikusanyiko kufuatia tishio la Corona, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Fedha kukaa pamoja na kuandaa Mpango wa Ruzuku ya Matumizi ya Mtandao wa Internet pamoja na Vipindi vya Taaluma na machapisho yatakatyohusika na ruzuku hiyo.

**iii. Kukuza Ushirikiano wa Kielimu kati ya Taasisi za Umma na Binafsi ili kutatua changamoto ya Utoaji wa Elimu ya Masafa (Distance Learning)**

**23. Mheshimiwa Spika,** katika mazingira magumu ya utoaji wa elimu tunayokabiliana nayo kwa sasa, ni lazima Bunge hili lijadili na kuishauri Serikali namna ya kuweza kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika masuala ya elimu ili kusaidia utoaji wa elimu ya masafa hasa kwa wanafunzi washio katika mazingira magumu.

**24. Mheshimiwa Spika,** uzoefu unaonesha kwamba katika mataifa yaliyoathirika na virusi vya Corona kumekuwa na makundi na jumuiya mbalimbali zilizoanzishwa zikiwa na wadau kutoka katika tasnia na taaluma mbalimbali zikiwemo Serikali, wachapishaji, wataalam wa elimu, vyama vya kijamii (CSO's) watoa huduma za kiteknolojia, wamiliki na waendeshaji wa makampuni ya mawasiliano kwa lengo la kuunganisha taaluma na weledi wao ili kutumia teknolojia

ya kidijitali kama sehemu ya suluhisho la kupata elimu ya masafa baada ya athari za Corona kuharibu mfumo wa zamani.

**25. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Taarifa ya Haki Elimu ni kwamba Wizara ya Elimu ya China imeratibu zaidi ya taasisi 60 za elimu, wachapishaji (publishers) vyombo vya habari na wataalamu kutokana tasnia ya michezo na burudani wameweza kutoa bure vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile video zenye mihadhara ya elimu, mada za kufundishia, nyenzo za upimaji wa uelewa (utahini) na huduma za ushauri nasaha.

**26. Mheshimiwa Spika**, Wakati tunajifunza na kupata uzoefu kutoka kwa nchi zilizokumbwa na COVID 19 ili tuweze kuboresha mazingira yetu ya utoaji wa elimu, ni lazima kama Taifa tujiulize Wizara yetu ya Elimu mpaka sasa imefanya nini kutatua changamoto ya kukosa masomo hasa kwa kipindi hiki ambacho shule zimefungwa? Wizara ya Elimu imeshirikiana vipi na Wizara nyingine kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Habari, Michezo, Sanaa na Utamaduni na au Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili kurahisisha upatikanaji na utoaji wa elimu kwa njia mbadala?

**27. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba zipo taasisi za kitaalamu chini ya Wizara ya Elimu. Hata hivyo, tungependa kujua, Wizara ya Elimu imetumia vipi utaalumu wa taasisi zake zinazohusika na teknolojia kama vile Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Vyuo Vikuu ili kuja na suluhisho la kiteknolojia la utoaji wa elimu katika kipindi hiki cha janga la Corona?

**28. Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba Wizara ya Elimu, pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ziongoze kampeni ya kuhamasisha ushirikiano wa taasisi mbalimbali ili kusaidia utoaji wa elimu kwa watoto wetu kwa kutumia mbinu mbadala! Kwa muktadha huohuo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itenge fedha katika bajeti hii kwa ajili ya kuanzisha na kukuza ushirikiano

baina taasisi za umma na za binafsi kwa lengo mahsusi la kurahisisha upatikanaji wa elimu nchini ikiwa ni sehemu ya suluhiso la changamoto inayoikumba sekta nzima ya elimu kwa sasa (ya masomo kusimama) kufuatia janga la Corona.

**iv. Bajeti ya Maendeleo ya Elimu Msingi longezwe ili Kuongeza Vifaa vya TEHAMA Shuleni**

**29. Mheshimiwa Spika**, Mwenendo wa upangaji wa bajeti ya maendeleo ya Elimu Msingi umekuwa si wa kuridhisha. Kwa muda mrefu bajeti hii imekuwa ya wastani wa asilimia 10 ya bajeti nzima ya maendeleo katika sekta ya elimu. Mbali na ufinyu huo wa bajeti, bado fedha zilizotengwa zimekuwa hazitolewi kwa ukamilifu wake. Kwa sababu hiyo, bajeti hiyo imekuwa haitoshi kutatua changamoto za miundombinu katika shule za msingi na sekondari za umma.

**30. Mheshimiwa Spika**, kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Corona, Serikali ione haja ya kuongeza bajeti ya maendeleo ya elimu msingi ili kuweza kutatua changamoto ya mazingira magumu ya kujifunza hasa kwa kipindi hiki cha mlipuko wa Virusi vya Corona. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza nyongeza hiyo ya fedha iwekezwe kwenye teknolojia ya elimu na elimu ya masafa ili wanafunzi waweze kuendelea kupata elimu wakiwa majumbani.

**31. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na msisitizo uliowekwa na Sera ya Elimu ya mwaka 2014 kuhusu umuhimu wa matumizi ya TEHAMA katika kurahisisha kufundisha na kujifunza, bado zinahitajika jitihada za makusudi ili kuweza kufikia azma hiyo. Hii ni kwa sababu shule nyingi bado hazijaunganishwa na nishati ya umeme na pia hizina vifaa vinavyorahisisha matumizi ya TEHAMA kama vile kompyuta. Kwa mujibu wa takwimu za BEST 2018, idadi ya shule za awali ambazo hazijaunganishwa na chanzo chochote cha nishati ya umeme ni 10,346 ikiwa ni sawa na asilimia 59.1 ya shule zote za awali nchini. Kwa upande wa shule za msingi, kati ya shule 17,562 ni shule 7,322 tu sawa na asilimia 41.7 ndizo ambazo zimeunganishwa na angalau chanzo kimoja cha nishati ya umeme huku shule 10,240 sawa na asilimia 58.3 hazijaunganishwa na chanzo chochote.



**32. Mheshimiwa Spika**, ukiachilia mbali changamoto ya ukosefu wa nishati ya umeme; Takwimu za BEST 2018 zinaendelea kuonesha kwamba kuna vitabu vya kidijitali 14,794 kwa ajili ya kuhudumia jumla ya shule za msingi 17,533; kompyuta mpakato 7,237; tablets 830 na projekta 1,467 kwa ajili ya kuhudumia zaidi ya wanafunzi milioni 10 katika shule za msingi. Kutokana na hali hii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa bajeti ya maendeleo katika elimu msingi iongezwe angalau ifikie asilimia 40 ya bajeti ya Maendeleo ya sekta nzima ya elimu ili kuweza kumudu gharama vya vifaa vya TEHAMA na hivyo kuwezesha utoaji wa elimu ya masafa (distance learning) hasa kwa kipindi hiki cha janga la Corona lakini pia kwa siku za mbeleni ikiwa kutatokea janga lingine linalofanana na hili la Corona.

**33. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, imeshtushwa sana na hotuba ya Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI Aprili, 2020 kwamba kati ya shule 3,742 za umma ni shule 153 sawa na asilimia nne tu zinazofundisha TEHAMA; na ni wanafunzi 36,101 tu wanaosoma TEHAMA kati ya wanafunzi zaidi ya million moja na nusu wa shule za Serikali. Tunaendaje kwenye uchumi wa viwanda bado tuko nyuma hivi kiteknolojia? Ni rai yangu kuwa ugonjwa huu utatufungua fikra zetu zione mbali zaidi kwa kutenga bajeti zaidi kwenye TEHAMA.

**v. Serikali Ipunguze Kodi kwenye Simu za Mkononi na Vifaa vingine vya Kielektroniki kwa ajili ya Kufundishia na Kujifunzia**

**34. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, upo umuhimu wa kutumia njia mbadala na hasa kupitia teknolojia ya mawasiliano ili kukabiliana na mazingira magumu ya kufundisha na kujifunza yanayolikabili Taifa kwa sasa. Hata hivyo, kaya nyingi hazina uwezo wa kununua simu janja, runinga au kujiunga na vifaa vingine vya kielektroniki kwa ajili ya kusaidia kupata elimu ya masafa. Kwa mujibu wa Taarifa ya TCRA ya Disemba, 2019 ni watu milioni 25.8 tu sawa na asilimia 46 ndio ambao wamejiunga na huduma za kimtandao. Hii ina maana kwamba bado kuna idadi kubwa ya watu ambao hawana uwezo wa kumiliki simu janja,

runinga na au vifaa vingine vya ki-elektroniki kwa ajili ya kujiunga na mtandao wa Internet.

**35. Mheshimiwa Spika**, hali hii imesababishwa na hali ya umaskini nchini. Kwa mujibu Taarifa ya Utafiti wa Mwenendo wa Kibajeti katika Kila Kaya (Household Budget Survey 2017 – 2018) kiwango cha umaskini kinaonekana kupungua lakini idadi ya wananchi maskini haijapungua. Kati ya idadi ya watu nchini ambayo kwa sasa inakadiriwa kuwa watu milioni 55; watu milioni 14.5 sawa na asilimia 26.4 wako kwenye umaskini uliokithiri. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kupunguza kodi kwenye vifaa vya kielektroniki ili kupanua wigo wa matumizi ya TEHAMA katika kutoa elimu ya masafa (distance learning).

**vi. Serikali Itenge Bajeti kwa ajili ya Mafunzo ya Matumizi ya TEHAMA kwa Walimu na Uhamasishaji wa Umma kuhusu Matumizi ya TEHAMA.**

**36. Mheshimiwa Spika**, Imebainika kuwa idadi kubwa ya watu wanaomiliki simu janja hawazitumii ipasavyo hasa katika masuala ya kupata elimu. Kwa sababu hiyo, utoaji wa mafunzo kwa walimu na wazazi ni muhimu ili waweze kutumia simu na vifaa vingine vya kielektroniki katika kufundisha na kuwasadiwa watoto kujifunza.

**37. Mheshimiwa Spika**, Ili mafunzo hayo yaweze kutolewa inahitajika bajeti kwa ajili kuwapa walimu waliopo kazini (in-service teachers) mafunzo ya matumizi ya TEHAMA katika kusaidia kufundisha na kujifunza. Sambamba na hilo, Serikali haina budi pia kutenga bajeti ya uhamasishaji endelevu wa jamii juu ya mahitaji ya sasa ya kutumia njia mbadala ya TEHAMA katika kutoa elimu baada ya utaratibu wa zamani wa kutoa elimu kushindwa kutumika kutokana na janga la Corona ambalo limesababisha shule na taasisi za elimu kufungwa kwa muda usiojulikana!

**C. UHABA WA MADARASA NA MATUNDU YA VYOO BADO NI CHANGAMOTO KUBWA INAYOIKABILI ELIMU MSINGI**

**38. Mheshimiwa Spika**, Kwa miaka yote; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshauri kuwe na mpango maalumu wa ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo. Ujio wa elimu bure umeongeza uhaba mkubwa wa vyumba vya madarasa hivyo tulishauri kuwa kwa kuwa Serikali ina takwimu za watoto wanaongia darasa la kwanza kila mwaka na kwa kuwa pia wana idadi ya wanafunzi wa darasa la saba na wanajua idadi ya watakaofaulu (approximation). Ni muhimu fedha zitengwe kila mwaka kwa ajili ya madarasa na vyoo kwa idadi ili ndani ya miaka mitano tatizo liwe limeisha.

**39. Mheshimiwa Spika**, Kinachoshangaza hili halifanyiki na matokeo yake kila watoto wanapomaliza darasa la saba, viongozi wakuu akiwemo Waziri Mkuu, Mawaziri wa TAMISEMI, Wakuu wa Mikoa na kadhalika wanakuwa na kazi ya kuhimiza ujenzi wa madarasa. Swali ni je, wanafunzi wanasubiri madarasa au madarasa yanasubiri wanafunzi?

**40. Mheshimiwa Spika**, Matokeo yake baadhi ya wanafunzi waliofaulu hukaa nyumbani hadi miezi mitatu kusubiri madarasa wengine wakienda kwa shift. Hii sio sawa kabisa ubora utapatikanaje hapa? Bado tunashauri Serikali kuwa na mpango mkakati wa ujenzi kila mwaka ili tatizo hili liwe historia.

**41. Mheshimiwa Spika**, Ni matumaini yetu kuwa Corona itapita na shule zitafunguliwa; lakini ndani ya hayo matumaini mazuri upo ukakasi na uchungu mkubwa kwamba Taifa litajikuta tena kwenye mazingira yaleyale duni ya kufundisha na kujifunza. Hii inatokana na uhalisia kwamba bado kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari. Kwa mujibu wa Taarifa ya Haki Elimu 2020; shule za msingi za umma zina upungufu wa vyumba vya madarasa 82,200 wakati shule za sekondari za umma zina upungufu wa vyumba vya madarasa 4,647. Vyumba hivi vinahitajika ili kuweza kukidhi uwiano wa kitaifa wa darasa moja kwa wanafunzi 45. Upungufu huo unalikesha taifa fursa ya kuwa na rasilimali watu yenye weledi.

**42. Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Haki Elimu inaendelea kueleza kwamba kwa mwaka 2018 mathalani; jumla ya wanafunzi 24,433 waliofaulu mtihani wa taifa wa kidato cha nne hawakuweza kujiunga na kidato cha tano kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa. Kwa muktadha huo huo, mwaka 2019 na 2020 jumla ya wanafunzi 133,747 (18.24%) na 58,699 (7.73%) wa darasa la saba waliohitimu na kufaulu kujiunga na kidato cha kwanza kwa mfuatano huo, hawakupokelewa shuleni kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

**43. Mheshimiwa Spika**, Kwa takwimu hizo, ni lazima Serikali ikiri kwamba upungufu wa vyumba vya madarasa ni jinamizi lingine linalonyemelea kuinyonga elimu yetu! Haingii akilini kuwa watoto wetu takriban laki mbili wameshindwa kuingia kidato cha kwanza kwa miaka miwili iliyopita kutokana na kukosa madarasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleza Bunge hili hao watoto walioshindwa kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa wako wapi na wanafanya nini.

#### **D. MSONGAMANO WA KUTISHA DARASANI KUTOKANA NA UFINYU WA MIUNDOBINU**

**44. Mheshimiwa Spika**, Ni wazi kuwa miundombinu ya utoaji elimu hapa nchini hasa kwa shule za awali, msingi na sekondari haitoshelezi hususan ni madarasa, matundu ya vyoo, maabara na madawati. Wakati wastani wa darasa kwa wanafunzi ni 1:45-50 kwetu ni 1:96 = 12,034,577/125,719. Huku matundu ya vyoo ikiwa ni 1:20-25 kwetu ni 1:60. Hali hii haiwezi hata kidogo kuleta matokeo mazuri kwa vijana wetu. Pamoja na elimu bila malipo kuwa sehemu ya changamoto hii, bado hakuna mkakati mahsusi kwa kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi.

**45. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshauri mara nyingi kuwepo kwa bajeti (ring-fenced) kwa ajili ya miundombinu kwa kuwa Serikali ina takwimu zote za watoto wanoingia shule za awali hadi darasa la saba na vilevile ina makisio ya watakaofaulu kuingia kidato cha

kwanza. Hivyo, kwa mfano kila mwaka wakiwekeza fedha kwa 20% ya madarasa yote yanayohitajika ina maana kwa miaka mitano tatizo linakuwa limekwisha.

**46. Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa tuna wanafunzi wa msingi 12,034,599 na madarasa 125,719. Kama kila darasa mtachukua wanafunzi 50 maana yake tunahitaji madarasa 240,692. Hivyo, tuna upungufu wa madarasa 114,973. Hivyo basi kama tunakuwa na mpango wa kujenga madarasa haya ndani ya miaka mitano ina maana kila mwaka yajengwe madarasa 22,995 lakini huu utaratibu wa kujenga 2,000 mwaka huu na mwaka unaofuata 3,000 na pengine 1,000, kamwe hatutamaliza tatizo kwenye vyoo, madawati, maabara na nyumba za walimu. Kama Serikali ingesikiliza na kuufanyia kazi ushauri wa Kambi ya Upinzani na kujenga kwa utaratibu huu hakika tatizo la miundombinu lingekuwa historia.

**47. Mheshimiwa Spika,** Kwa takwimu za Hotuba ya Waziri wa TAMISEMI (2020) imeonesha kwa miaka minne 2016 (108,504) na mwaka 2020 (125,719) sawa na  $17,215/4=4304$  kwa mwaka. Hii ina maana ili tufikie madarasa 114,973 tutahitaji miaka 27 kukamilisha.

**48. Mheshimiwa Spika,** kwenye matundu ya vyoo ndio hatari zaidi. Sote tunajua kwenda haja ni lazima na hasa watoto wadogo ambao ni ngumu sana kujizuia. Wakati wastani wa tundu kwa wanafunzi; jinsia ya (Ke) na (Me) ni 1:25 lakini hapa kwetu ni 1:59 zaidi ya mara mbili ya wastani. Tuna matundu 205,663 tu na kibaya zaidi kwa miaka minne yamejengwa 7,922 tu sawa na 1980 kwa mwaka. Hivyo ni muhimu sana fedha zitengwe kwa idadi (fixed) itakayowekwa kila mwaka ili kutatua tatizo.

**49. Mheshimiwa Spika,** Ili kuondokana na adha hii ya upungufu wa vyumba vya madarasa; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuandaa makakati na mpango wa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kama ifuatavyo:-

**a) Kwa Shule za Msingi;** ambako kuna upungufu wa vyumba vya madarasa zaidi ya laki moja, Serikali inatakiwa itenge bajeti ya takribani shilingi trilioni 1.5 kuweza kujenga idadi hiyo ya madarasa. Gharama hii inatokana na makisio kwamba ujenzi wa darasa moja unagharimu shilingi milioni 15. Ikiwa Serikali itaweka mpango wa miaka mitano kukamilisha kazi hiyo, ina maana itahitajika kutenga bajeti ya takribani shilingi bilioni 300 – bajeti ambayo ina uwezo wa kujenga madarasa 20,000 kila mwaka wa fedha.

**b) Kwa upande wa Shule za Sekondari;** ambako kuna ongezeko kubwa la wanafunzi (wastani wa wanafunzi 200,000 wamekuwa wakijiunga na sekondari kwa miaka mitatu iliyopita) kutokana na sera ya elimu bure; bajeti ya ujenzi wa madarasa izingatie ongezeko hilo; sambamba na ujenzi wa takribani madarasa 4,000 ambayo ni pungufu kwa sasa.

## **E. SERIKALI ITENGE BAJETI YA AJIRA KWA WALIMU KUKABILIANA NA UPUNGUFU WA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI**

**50. Mheshimiwa Spika,** tatizo la upungufu wa walimu katika shule za msingi linafahamika na Serikali; ndiyo maana mwaka 2019 Serikali kupitia Naibu Waziri – TAMISEMI iliahidi kutenga bajeti ya kuajiri walimu kwa kila mwaka wa fedha ili kupunguza tatizo la uhaba wa walimu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutimiza ahadi hiyo na kwa kuanzia iseme imetenga kiasi gani cha fedha katika bajeti hii kwa ajili ya kuajiri walimu wapya.

**51. Mheshimiwa Spika,** tatizo la uhaba wa walimu bado ni kubwa. Sote tunatambua kuwa uwiano wa mwalimu na wanafunzi unakubalika kimataifa kwa shule za awali ni 1:25; lakini kwa mwaka 2018 uwiano wa mwalimu na wanafunzi kwa shule za awali za umma na za binafsi ulikuwa 1:114 (Ripoti ya Haki Elimu 2020). Kwa mujibu wa Ripoti ya Haki Elimu kuna walimu 9,127 tu wenye sifa za kuwa walimu wa shule za awali; wakati mahitaji ya kufikia uwiano wa 1:25 ni walimu 53,400. Pungufu ya zaidi ya walimu 47,000.

**52. Mheshimiwa Spika,** Kwa shule za msingi, uwiano wa mwalimu na wanafunzi ulikuwa 1:54 mwaka 2018. Hata hivyo

kulikuwa na baadhi ya mikoa iliyofanya vibaya katika hili. Mkoa wa Katavi mathalani ulikuwa na uwiano wa 1:75. Mkoa ulioongoza kwa uwiano mzuri ulikuwa ni Kilimanjaro ambao uwiano ulikuwa 1:34. Kama Serikali itaweka msisitizo wa uwiano wa 1:40 bado kutakuwa na upungufu wa walimu 65,000. Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuisisitiza Serikali kutenga bajeti ya kuajiri walimu ili kupunguza changamoto hii.

## [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

### **G. BODI YA MIKOPO IWE NA FUNGU LAKE LA FEDHA (VOTE)**

**58. Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ni nguzo kuu kwa wanafunzi wetu wa Elimu ya Juu. Hata hivyo, Bodi hii hupata zaidi ya asilimia 50 ya fedha yote ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu kwa mfano 2018/2019 bajeti ya Wizara ilikuwa shilingi bilioni 740.9 huku Bodi ya Mikopo ikitengewa shilingi bilioni 427.5 sawa na asilimia 57.7, mwaka 2019/2020 shilingi bilioni 862 huku Bodi ikipatiwa shilingi bilioni 450 sawa na asilimia 52 huku mwaka 2020/2021 Bodi ikipata shilingi bilioni 464 kati ya shilingi bilioni 857 sawa na asilimia 54.

**59. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Bodi ya Mikopo Fedha yake yote ni ya ndani na kwa kuwa jumla ya fedha yote ya ndani kwa Wizara hii ni shilingi bilioni 606.7, ina maana Bodi ya Mikopo imetengewa asilimia 76.5. Kambi ya Upinzani inaendelea kuisisitiza Bodi ya Mikopo iwe na vote yake ili kuondoa dhana kuwa Wizara ina fedha nyingi za maendeleo kumbe zaidi ya nusu zinaenda sehemu moja, huku idara nyingine nyingi kwa mfano, Ukaguzi “Quality Assurance” Walimu, Vyuvo vya Ualimu ambao ndio msingi wa elimu bora vikikosa fedha.

**60. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Waziri wa Fedha alishatoa ahadi kwa niaba ya Serikali kuanzisha fungu la fedha (Vote) kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu katika mwaka wa fedha, 2019/2020; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutimiza ahadi hiyo kwa kuanzisha Vote hiyo katika mwaka mpya wa fedha 2020/2021.

## H. CHOMBO CHA KUSIMAMIA ELIMU

**61. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi sasa nimekuwa nikiongeleasuala la uwepo wa chombo kitakachosimamia Elimu yetu. Sote tunajua kuwa tuna aina mbalimbali za shule na taasisi za Elimu hapa nchini. Tuna Shule za Umma/ Serikali, kuna shule za watu Binafsi, kuna za madhehebu ya dini na zile za kimataifa. Ukiacha za kimataifa shule zinazobakia zinasimamiwa na Wizara ya Elimuambayo nayo ina shule zake. Katika hali ya kawaida ya kibinadamu kwa wasiokuwa wa Serikali wataona wanaonewa. Malalamiko ya wamiliki wa shule na taasisi binafsi wamekuwa na malalamiko mengi ikiwemo vigezo vya kufungua shule, kodi na kadhalika.

**62. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumeshauri uundwaji wa chombo/Tume Huru itakayosimamia pamoja na mambo mengine mitaala, mfumo wetu wa elimu, vitabu vya kiada na kadhalika. Hii itasaidia sana kuboresha elimu yetu. Wizara ya Elimu inakosa mamlaka ya kimaadili (moral authority) kusimamia ubora wa elimu kwa kuwa na yenyewe inamiliki shule. Chombo hiki kitasaidia sana katika usimamizi mzuri wa elimu yetu tukiamini kitakuwa na wabobezi katika masuala ya elimu na kitakuwa huru. Haiwezekani Serikali yenye shule zake tena zaidi ya 85% bado isimamie shule binafsi. Hivyo basi tunaendelea kuishauri Serikali kuwa na chombo huru kusimamia elimu yetu kuendana na mabadiliko ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia.

## I. UDHAMINI WA VIJANA WANAOFANYA VIZURI KIDATO CHA SITA

**63. Mheshimiwa Spika**, Ni wazi kuwa kila binadamu ana uwezo na akili tofauti. Kuna watoto wenye uelewa mkubwa na wengine mdogo (slow learners). Pamoja na changamoto mbalimbali za mazingira, bado suala la utofauti tunapata watoto wenye daraja la juu kabisa la kwanza kwenye shule za pembezoni na pengine zisizo na walimu. Unajuliza mtoto kama huyu angepata mazingira bora zaidi angefaulu vipi? Hivyo, kutokana na ukweli huu wa utofauti wa uelewa (geneusness) ni muhimu kwa Serikali kuweka utaratibu walau



wa kutenga nafasi 20-50 kila mwaka kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita kwa 'combinations' zote bila kujali jinsi kwenda kusoma katika vyuo mashuhuri duniani na kuwaghamia kila kitu.

**64. Mheshimiwa Spika,** Hii itaongeza motisha kwa vijana wetu kusoma kwa bidii na malengo lakini pia itasaidia kama nchi kupata vijana wenye maarifa, upeo mpana na (exposure). Vijana hawa watarejea na kuja kubadili na kuongeza tija kwenye uchumi wetu. Leo hii baada ya 58 miaka ya Uhuru bado tunategemea rasilimali watu kutoka nje. Reli ya kati ya SGR, Stiglers Gorge kwa kiasi kikubwa management team na makandarasi wengi ni wa nje. Kwa nini sio wa kwetu na tumekuwa na wahitimu-wahandisi wetu toka mwaka 1970? Jibu sahihi ni ukosefu wa vitendea kazi na teknolojia. Hivyo vijana hawa wakienda nje kwa umri wao ni rahisi sana kuibadili nchi yetu.

## J. UBUNIFU SAYANSI YA TEKNOLOJIA

**65. Mheshimiwa Spika,** Hakuna Taifa duniani lililoendelea bila kuwekeza kwenye sayansi ya teknolojia. Wenzetu wanajua ni jinsi gani sayansi na teknolojia vinachangia sana katika maendeleo ya Taifa lolote. Mageuzi ya sayansi na teknolojia yanaleta hamasa ya ubunifu, pamoja na kuvutia zaidi ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza sayansi ya teknolojia na ubunifu. Ni wazi mageuzi haya yanahitaji fedha nyingi hasa za utafiti. Jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali haitoi fedha kwa ajili ya utafiti kwa mfano, Bajeti ya 2019/2020 sekta hii ilikuwa na upugufu mkubwa na hata baada ya agizo la tengeo la 1% la pato ghafi la Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kaisi gani cha pato ghafi la Taifa limetengwa?

**66. Mheshimiwa Spika,** Ni jambo la kusikitisha sana kuona COSTECH ambacho ndio chombo pekee cha kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu utafiti, sayansi na teknolojia na kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya Bunge ya mwaka 1986, haijaweza kupewa 1% ya pato ghafi la Taifa. Mathalani kwa mwaka jana 2019/2020; Serikali ilitengewa shilingi

6,574,177,540/= na mwaka huu shilingi 5,197,400,000/= sawa na 0.5% ya bajeti ya maendeleo. Swali ni je, kweli tunategemea kuwa na Taifa la sayansi?

**67. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipatia Tume hii fedha za kutosha katika kipindi hiki cha Corona ili waweze kusaidia kwenye elimu mtandao (TEHAMA). haiwezekani ***Kasma 8001 inayohusu Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ipate asilimia 1.4 tu ya bajeti ya Wizara ya maendeleo yaani shilingi bilioni 12.6 kati ya billion 857.5 za Wizara hii.***

**68. Mheshimiwa Spika**, Tulielezwa hapa COSTECH ilishauri kutoa mwongozo wa matumizi ya teknolojia ya kisasa itwaayo (Unmanned Aerial Vehicle - UAV) itumiayo helkopta zinazoendeshwa bila rubani (drones). Teknolojia hii ni muhimu sana kwa ajili ya udhibiti wa majangili kuandaa mipango miji, upimaji ardhi na katika matukio kama mafuriko. COSTECH ilishauri Serikali kuidhinisha teknolojia hii kama kipaumbele cha kufanya utafiti na hivyo Tanzania kuwa mstari wa mbele ikiwa taasisi zake zataitumia. Swali la kuuliza Serikali walitoa kiasi gani na mwongozo uko wapi kwani jambo hili halijagusiwa kabisa katika hotuba ya Waziri leo.

**69. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua umuhimu wa sayansi na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya nchi na imekuwa ikishauri mara kwa mara umuhimu wa taasisi mbalimbali za sayansi na teknolojia kama Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Taasisi ya Dar (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi ya Teknolojia cha Mbeya, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Chuo cha Teknolojia Arusha na COSTECH zipewe fedha za kutosha ili waweze kutekeleza mipango yao kabambe ikiwa ni pamoja na kuiweka nchi yetu kwenye sura ya kiteknolojia. Kwa masikitiko makubwa hata fedha tulizozipitisha mwaka 2019/2020 za baadhi ya vyuo hivi hazijapelekwa hata senti tano.

#### **K. UHABA WA WAHADHIRI KATIKA VYUO VIKUU**

**70. Mheshimiwa Spika**, wanazuoni wa masuala ya elimu wanatoa tafsiri ya Chuo Kikuu kwamba: ***“A University is an***

*Institution of Higher Learning where people's minds are trained for clear thinking, for independent thinking, for analysis and for problem solving at the highest level; is the Centre for Advancing the Frontiers of Knowled.*" Kwamba: Chuo Kikuu ni taasisi ya elimu ya juu inayoandaa watu kuwa na fikra pevu, fikra huru kwa ajili ya kuwa na uwezo mkubwa wa kiuchambuzi na kwa ajili ya kutatua matatizo kwa kiwango cha hali ya juu, ni kituo cha kuendeleza maarifa.

**71. Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri hiyo, ni dhahiri kuwa chuo kikuu kinatakiwa kuwa na wahadhiri wabobevu na wa kutosha ili kuweza kuakisi maana hiyo ya chuo kikuu. Wachambuzi wanaeleza kwamba sababu ya uchache wa wahadhiri ni ongezeko la vyo vikiu vipya ambalo limepelekea wahadhiri kuhama kutoka vyo vya zamani na kwenda kwenye vyo vipya ama kwa kuteuliwa kushika nafasi za uongozi katika vyo hivyo vipya au kutafuta mazingira bora zaidi ya kufanyika kazi ikiwemo kipato kikubwa zaidi.

**72. Mheshimiwa Spika**, Inaelezwa pia kwamba teuzi mbalimbali zinazofanywa na Mkuu wa Nchi kwa wahadhiri wa vyo vikiu kushika nafasi mbalimbali za kisiasa na kiutendaji Serikalini kama vile Wabunge wa Kuteuliwa, Makatibu Wakuu na Maafisa wengine Serikalini zimesababisha kupungua kwa wahadhiri katika baadhi ya vyo vikiu hapa nchini.

**73. Mheshimiwa Spika**, Tanzania kwa sasa ina wastani wa asilimia 25 ya wahadhiri wenye shahada ya uzamivu (PhD). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee kina asilimia 41 ya wahadhiri wenye shahada ya uzamivu. Uhaba wa wahadhiri umeathiri pia vyo vikiu vingine Kusini mwa Jangwa la Sahara isipokuwa vyo hivyo vina nafuu zaidi ukilinganisha na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Botswana ni 65%, Chuo Kikuu cha Cape Town 63%; Chuo Kikuu cha Ghana 50%; Chuo Kikuu cha Nairobi 46%; Chuo Kikuu cha Mauritius 42. Hivyo, pamoja na kwamba ninawapongeza wahadhiri walioteuliwa lakini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia vyo vikiu kutenga fedha

nyingi kwa ajili ya kusomesha wahadhiri ili kusiwe na ombwe kunapofanyika uteuzi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa vyuo vikongwe kutoa motisha kwa wahadhiri wao ili wasipate tamaa ya kuhamia vyuo vingine kwa ajili kutafuta maslahi.

## L. HITIMISHO

**74. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii imezungumzia kwa kirefu namna sekta ya elimu iliyoathirika na janga la Corona. Aidha, imetoa mapendekezo na ushauri mwingi kwa Serikali juu ya matumizi ya mbinu mbadala za kutoa elimu kwa kipindi hiki ambacho shule na vyuo vya elimu vimefungwa. Sambamba na mapendekezo hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani imeitaka Serikali kuona umuhimu wa kupanga bajeti ya elimu kwa kuzingatia athari za Corona ambazo zimeelezwa kwa kirefu kwenye hotuba hii.

**75. Mheshimiwa Spika**, Baba wa Taifa la Afrika ya Kusini; Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema kuwa “No country can really develop unless its citizens are educated” ikiwa na maana kwamba “Hakuna nchi inayoweza kuendelea kama wananchi wake hawajaelimika.”

**76. Mheshimiwa Spika**, hata Kambi Ramsi ya Upinzani Bungeni, inaamini kuwa elimu ndio kila kitu kwenye mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Changamoto karibu zote ambazo nimezieleza kwenye hotuba yangu zinahusiana moja kwa moja na changamoto za kiseru, usimamizi wa elimu na mfumo wa upangaji na usimamizi wa bajeti ya sekta ya elimu. Tanzania kama Taifa tunahitaji kuelewa nini falsafa ya elimu yetu, nini malengo makuu ya elimu yetu na tuwe na mikakati ya kuhakikisha mfumo wa elimu yetu unalenga kutoa elimu jumuishi, elimu inayotoa fursa kwa watoto wote wa Tanzania kupata elimu bora na elimu inayolenga kumlinda na kumuendeleza mtoto. Elimu bora kwa kila mtoto wa Tanzania ndiyo itakayosaidia Taifa hili kupata maendeleo.

**77. Mheshimiwa Spika**, ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa Serikali itayachukua na kuyafanyia

kazi mapendekezo tuliyotoa kwa mustakabali mwema wa elimu yetu.

**78. Mheshimiwa** Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)

**WAZIRI KIVULI WA ELIMU NA MSEMaji MKUU WA KAMBI  
RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU,  
SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

24 Aprili, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Susan Lyimo. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa mawasilisho, sasa tutaanza uchangiaji. Nianze kwa kuwataja Waheshimiwa Wabunge watakaochangia kutokea Msekwa; Mheshimiwa Ester Mahawe kama yupo humu ndani aelekee Msekwa, Mheshimiwa Oscar Mukasa atachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Zacharia Issaay atachangia kutoka Msekwa na Mheshimiwa Charles Mwijage.

Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili naye atachangia kutoka Msekwa na kwa kuwa Mheshimiwa Susan Lyimo tayari yuko Msekwa atachangia kutoka Msekwa. Tutaanza na Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge ajiandae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata fursa hii kuongea katika sekta hii muhimu kwa Taifa letu na baada ya mkutano wetu huu Bunge tutakuwa tumemaliza Bunge letu la Kumi na Moja kwa hiyo wakati huu ni mzuri wa kuangalia kutoka tulipoanza na Bunge letu hili mpaka hapa tulipofika tume-*achieve* nini na mbele tunategemea kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda sana nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe

Magufuli, kwa kazi nzuri sana aliyofanya katika sekta hii. Amefanya kazi nyingi lakini moja ambayo ni muhimu tuiangalie na kuenzi ni kutoa elimu bure; kwamba Serikali yetu ili kutekeleza jambo hili imekuwa inatoa shilingi bilioni 22 kila mwezi kuhakikisha kwamba watoto wetu wote wanaweza kupata elimu ya msingi na elimu ya sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne. Haya ni mambo ambayo ni makubwa na inabidi tuipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukachanganya sasa na yale mambo makubwa ambayo yamefanywa kwa sekta mbalimbali utakaa uone katika Bunge letu hili la Kumi na Moja kumekuwa na mabadiliko makubwa, maendeleo makubwa, na tumshukuru sana Rais wetu, ahsante sana Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwapongeze sana viongozi ambao wanaongoza Sekta hii ya Elimu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Dkt. Joyce Ndalichako na Naibu wake na watendaji wake wamefanya kazi nzuri sana lakini kazi hii bado inaendelea.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Wamefanya kazi nzuri sana katika kupanua elimu katika ngazi zote.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Maghembe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Ahaa, vizuri.

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninapenda kumpa taarifa tu mzungumzaji kwamba Mheshimiwa Ndalichako ni Profesa, siyo *doctor*. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Maghembe.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ingewezekana ningempa taarifa kwamba maprofesa wote wana *PhD*, kwa hiyo Dkt. Ndalichako ni sawasawa ni Profesa lakini pia ni daktari, tena wa kusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Ndalichako kwa kweli kwa kazi nzuri sana ambayo amefanya katika Sekta ya Elimu. Mheshimiwa Prof. Ndalichako na wasaidizi wake wote wamefanya kazi nzuri sana na wamefika hatua nzuri ambayo wamefanya upanuzi katika nchi yetu wa elimu, kwamba kila mtoto wetu sasa anaweza kupata elimu ya msingi kwa maana ya *primary education* na *secondary education*; hii ni kazi kubwa. Lakini pia kumekuwa na upanuzi mkubwa katika ngazi ya *A-Level*, katika ngazi ya vyuo vikuu; hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo iko mbele yetu sisi ni kuboresha elimu. Kuboresha sasa hao watoto wengi ambao wanaingia kwenye Sekta ya Elimu, sasa elimu yao iwe ya kiwango cha juu sana. Sisi tuna imani kubwa sana na timu ambayo unayo Mheshimiwa Profesa Ndalichako katika kufanya kazi hiyo. Tutakupa mawazo mengi sana lakini ninawaomba muwe imara sana mfanye kile ambacho mnaamini kwamba hiki kweli kitatupeleka mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu mtapewa mawazo, mtapewa ushauri wa kila aina, hata watu wasioitakia mema nchi yetu watawapa mawazo. Watu wengi wanaamini kwamba labda sasa imefika wakati tufundishe masomo yote tangu mwanzo mpaka chuo kikuu

kwa Kiswahili, wakasema wamefanya utafiti kwelikweli, lakini hawajaangalia jinsi Hesabu inavyofundishwa katika shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hesabu darasa la kwanza mpaka la saba inafundishwa kwa Kiswahili lakini ufaulu wa mtihani wa darasa la saba wa Hesabu hapa nchini unasikitsha kwelikweli. Ni asilimia 17 ya watoto wetu wanafaulu mtihani wa Hesabu na unafundishwa kwa Kiswahili. Sasa kusema tubadilishe na haya masomo mengine yote yafundishwe kwa Kiswahili katika ngazi zote ni kama yule daktari ambaye anapata mgonjwa wa Malaria badala ya kumtibu vidudu vya Malaria anatibu joto na vidudu vinaendelea kumla mgonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashauri sana wajenge umahiri wa walimu wetu katika kila ngazi ili waweze kufundisha masomo yetu hayo ya Hesabu ambayo watoto hawafanyi vizzuri, masomo ya Kiingereza ambayo watoto hawafanyi vizuri na kuwapa umahiri katika maeneo ambayo yatawafanya watoto wetu wajiamini na kwenda kifua mbele na kumudu masomo na elimu yetu kuwa na uimara na *quality* ile ambayo inatakiwa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambao ni muhimu kulifanya, tuhakikishe kwamba tunazijengea shule zetu zote za sekondari maabara. Ninajua kwamba wananchi wanaendelea kuyajenga hayo maabara lakini sasa tumefika miaka kumi wananchi wanajenga, na wamefikia asilimia 30 peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumepata nataka niwapongeze sana, kulikuwa na yule mtume wa bahati mbaya aliyekuwa anataka kutuletea bahati mbaya aseme tusipewe na pesa za ku-*improve* elimu huko kwenye Benki ya Dunia, naona ameshindwa, na wangesema wale watu wanaosemea kwenye misikiti huko washindwe kwa jina la Mwenyezi Mungu.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba tujenge sasa maabara ya shule zetu zote kwasababu shule zetu za sekondari zimejengewa maabara kwa asilimia 30 peke yake, asilimia 70 ya maabara yanayohitajika bado hayajakamilika au hata hayajaanza kujengwa. Kwa hiyo, sasa tumefika wakati ambapo ni lazima tukamilishe jambo hili haraka iwezekanavyo ili watoto waweze kujifunza Sayansi kwa msingi ambao ni wa kidunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni muhimu zaidi kwasababu nimeelezwa kwamba Baraza letu la Mitihani linaelekea kufuta ule mtihani unaitwa *Alternative to Practicals*, watoto wote watafanya *practicals*. Sasa kama asilimia 70 ya maabara hayapo kwa kweli ina maana kwamba hata watoto wanaosoma kwenye shule zetu zile za kata watakuwa wote wa kufeli mtihani. Kwa hiyo, jambo hili la kujenga maabara tuliharakishe na tuombe Wizara isiharakishe kuondoa *Alternative to Practicals*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine muhimu sana ambalo ninataka kulisema ni suala la mikopo ya elimu ya juu. Kama Bunge tulikaa hapa tukaangalia ile sheria ya kutoa mikopo na utaratibu wa kutoa mikopo na ile bodi inafanya juhudi kubwa kufuata huo utaratibu na kutoa mikopo kwa njia hiyo. Lakini ukifika kule jimboni wakati unakutana na wananchi na shida zao, watu wengi wanaokuja ambao wamekosa mikopo wanaingia chuo kikuu wamekosa mikopo ni wale watoto maskini wa maskini, na hao ni wengi kwelikweli wanakuja kuomba ni namna gani watapata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inamaana kwamba umefika wakati lazima tuangalie upya namna gani tunatoa mikopo kwa watoto wetu... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Jambo la muhimu ningependa nimalizie hapa kwamba lazima tutafute

njia ambayo tutawapa watoto wote wa Tanzania wapate mikopo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mheshimiwa Khadija Nassir ajiandae.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu, Dkt. Ave Maria Semakafu pamoja na Prof. James Mdoe kwa hotuba nzuri lakini vilevile kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ni mkutano wa mwisho katika Bunge la Kumi na Moja, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge ndg. Kagaigai kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mwanamke wa shoka, humu ndani tunakuita mama kanuni, pamoja na kwamba hii ni *term* yako ya kwanza Bungeni lakini kanuni zote ziko kwenye *fingertips*, zote ziko kichwani. Kwa hiyo, sisi kama wanawake wenzako tunafurahia na tunajivunia kazi nzuri unayoifanya ndani ya Bunge na hata kazi unayoifanya nje ya Bunge na hasa ukiwa kule Mbeya. Tunaomba wakuone na wakurudishe hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ndugai, hili Bunge amelitoa kwenye *analog* tunakuja humu na rundo la makaratasi sasa hivi tunakwenda ki-*digital*, vishakwambi mkononi, basi tunamshukuru sana kwa kutufikisha hapa. Tunampongeza kwasababu ya uongozi ulotukuka, kwa kweli Bunge sasa limetulia na linafanya kazi nzuri kwasababu ya utulivu uliopo. Yeye ni kiongozi ametuonesha upendo, amekuwa msikivu na mvumilivu, na alikuwa anawajali sana watu wake na hata ukiugua alijitahifi sana kuhakikisha kwamba unapona unarudi

humu unaendelea kuchapa kazi. Kwa hiyo, tunawaomba wale watu wa Kongwa kule wamuone wamchague tena awe Mbunge arudi humu Uspika ataukuta unamsubiri hapahapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii miaka minne kuna maendeleo makubwa sana katika Sekta ya Elimu. Nimeisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mikopo ya elimu ya juu imeongezeka sana, madarasa ya shule, hasa za sekondari, yamejengwa mengi sana, vifaa vya maabara katika shule vimeongezeka, lakini vilevile tumeona fedha nyingi zinaingia katika shule kwasababu ya elimu bila ada. Lakini vilevile tumeona *enrollment*, wanafunzi wanaonaza darasa la kwanza wanaongezeka kwasababu ya elimu bila ada.

Mheshimiwa Nabu Spika, najua haya yote yametokea kwenye mkoa yote lakini naomba nitoe mfano katika mkoa wangu ninaotoka wa Kagera. Mkoa wa Kagera katika kipndi hiki cha miaka minne tumeweza kupata bilioni 46.9 kwa ajili ya elimu bila malipo, zimeingia Mkoani Kagera. Serikali imetusaidia kukarabati shule zetu zilizoharibiwa na tetemeko; lyungo Sekondari na Nyakato, ukifika lyungo sasa hivi utafikiri ni chuo kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imetuletea milioni 898 kwa ajili ya kukarabati Shule kongwe ya Kahororo, mmetuletea zaidi ya milioni 872 kukarabati Shule kongwe ya Rugambwa, mmetuletea zaidi ya 1,481,000,000 kwa ajili ya karabati shule kongwe ya Bukoba Sekondari. Vilevile tunaendelea kujenga shue nyingine kule Ngara tunajenga shule ya Murusagamba mmetuletea milioni 265, pale Muleba tunajenga Shule ya Nyailigamba mmetuletea milioni 310. Lakini vilevile kwa watu wa Mkoa wa Kagera walivyojitolea wakajenga maboma, kwa hiyo, Serikali imeweza ku-*support* hizo nguvukazi za wananchi mkatuletea zaidi ya milioni 600 tukamilishe yale maboma yaliyo katika shule za msingi na shule za sekondari, tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hiyo tu, vilevile kule Karagwe tunajenga Chuo cha VETA chenye thamani ya

bilioni nne na zaidi. Nawashukuru sana Wizara a Elimu, mmesikiliza kilio ha muda mrefu cha Wabunge wa kutoka Mkoa wa Kagera. Tumekuwa tukiomba tujengewe Chuo cha VETA kikubwa cha Mkoa sasa hivi mnatujengea chuo kikubwa chenye thamani ya bilioni 22; tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mkoa wa Kagera nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Olenasha, nakupongeza Mheshimiwa Prof. Ndalichako. *Actually* kuna shule tumeiita Ndalichako kwetu kwasababu ya kazi nzuri uliyoifanya kwenye Wizara ya Elimu na tuko tunaangaliaangalia tunatafuta sasa ni ipi tuiite Olenasha. Tunawaomba huko mnakotoka wawaone na Mwenyezi Mungu awajalie muweze kurudi Bungeni na Rais awateue muendeleo kuendeleza kuwa Mawaziri ndani ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo yote, unajua ukishapata upanuzi mkubwa namna hii lazima kutatokea changamoto. Sasa katika Mkoa wa Kagera tuna upungufu mkubwa wa walimu. Tunaomba tupatiwe walimu zaidi ya 6,570 wa shule za msingi. Tupatiwe walimu zaidi ya 1,060 wa masomo ya Sayansi katika sekondari na vilevile tusaidiwe kujenga maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kufikia uchumi wa viwanda kama hatutakuwa na wataalamu katika sayansi na teknolojia. Naomba Wizara tuweke mkakati kwamba kila shule ya sekondari iwe na maabara zote, ya fizikia, kemia, baiolojia, jiografia na *computer*, ili wanafunzi wetu waweze kusoma masomo kwa njia ya matendo pamoja na nadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Corona* ipo, tusiwe na hofu, tusikilize ushauri wa Serikali. Nataka kukubaliana na waliotangulia kusema kwamba Wizara ya Elimu imeathirika sana. Tuna watoto ambao wako kule hawajui cha kufanya, tuna watoto ambao ni madarasa ya mitihani, mtu alitegemea kufanya mtihani wa *form six, form four, form two*, darasa la saba na la nne, tunaomba sasa Wizara kila wiki angalau muwe mnatoa maneno ya faraja kwa hawa vijana

kusudi wasije wakapata msongo wa mawazo. Pia kuna kule ambapo hata redio hazifiki, tunafanyaje kuwafikia hawa watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hizo *private schools* ambazo sasa hivi hawana karo, kwa hiyo, wanawalipaje sasa watumishi wao? Napendekeza kwa Serikali Wizara ya Fedha itengeneze ka-*stimulus package*. Hapa tunazungumzia *private schools* lakini kuna sekta nyingine zimeathirika, tuangalie tunawasaidiaje waendeleo kulipa angalau mishahara kidogokidogo hata posho kwa hawa watu ambao wamesimamishwa kazi sasa hivi ili waweze kuwasaidia katika kipindi hiki cha *Corona*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Nasri, Mheshimiwa Esther Mahawe ajiandae.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye mkopo wa Serikali wa Dola za Kimarekani milioni 500 ambazo Serikali imepata kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha elimu ya sekondari, hususan kuwarudisha watoto wa kike waliofukuzwa shule kwa kupata ujauzito. Katika mchango wangu nimefanya rejea kwenye nyaraka mbalimbali na kama ukitaka basi naweza kuzi-*table* Mezani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kila mwaka takribani wanafunzi 60,000 wanaacha shule kwa sababu mbalimbali. Kati ya hao 5,500 ni watoto wa kike wanaofukuzwa shule kwa sababu ya kupata ujauzito. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *World Bank Facts Sheet* inasema, Serikali inasema kwamba haiwafukuzi watoto wa kike wa kitanzania ambao wanapata ujauzito wakiwa shuleni, hii siyo kweli. Mimi nimesoma Shule ya Wasichana Msalato iko hapa Dodoma, tulikuwa tunapimwa na wanafunzi wanaopatikana na ujauzito walikuwa wakifukuzwa shule, kwa hiyo, mimi ni shahidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tarehe 22/06/2017, Rais alitoa tamko kwamba watoto wakike wanaopata ujauzito wasirudi shuleni. Pia tarehe 03/04/2020, Msemaji Mkuu wa Serikali aliandika kwenye *account* yake ya *twitter*, naomba nimnukuu alisema: *"Ufafanuzi wa Mkopo wa Elimu wa Benki ya Dunia. Suala la wanafunzi wanaopata ujauzito kutoendelea na masomo haukuanza leo, ni msimamo wa Serikali kwa miaka yote."* Swali langu ni kwa nini Serikali mmeidanganya Benki ya Dunia? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkononi mwangu hapa ninayo *guideline* au mwongozo unaoitwa *Guideline on how to enable pregnant school girls to continue with their studies*, 2009. Mpango huu ulikuwa...

## TAARIFA

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, Msekwa huku.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa kutoka Msekwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa mzungumzaji, hivyo anavyohisi kwamba ndiyo tusipewe mkopo kwa hayo maneno yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge endelea na mchango wako.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Ninao mwongozo hapa wa Serikali wa mwaka 2009 uliokuwa unaelezea vizuri ni jinsi gani watoto wanaopata ujauzito wanaweza kurudi shule. Mwongozo huo unasema miezi sita baada ya kujifungua mpaka mwaka mtoto wa kike anaweza kurudi shule kwa mfumo rasmi kuendelea na masomo. Swali langu, je, Serikali inatambua mwongozo huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini natambua wataalam mbalimbali wa Wizara walisafiri nchi karibia sita za Afrika kwenda kupata *experience* au uzoefu wa jinsi gani ya kutekeleza mwongozo huu. Walitumia pesa za walipa kodi lakini sasa hivi ni miaka 11 mwongozo huu haujatekelezwa. Napenda kujua ni kwa nini pesa za Watanzania zimetumika kuandaa mwongozo huu lakini haujatekelezwa mpaka leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo Sheria ya Zanzibar inaitwa *The Spinster and Single Parent Childhood Protection Act* ya 2005 ambayo inamwezesha mwanafunzi aliyepata ujauzito akiwa shuleni kuweza kurudi kwenye mfumo rasmi wa masomo na kuendelea na masomo kwenye shule za umma. Napenda nichukue fursa hii kwanza kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza sheria hii na hii imesababisha kupungua kwa mimba za utotoni Zanzibar kwa 7%. Napenda kufahamu ni kwa nini kama sisi ni nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upande mmoja wa Muungano unaweza kutekeleza sera moja ya elimu na mwingine usiweze kutekeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna 53% ya mimba za utotoni kwa maana ya Tanzania Bara, ikiongozwa na Katavi ikifuatiwa na Mkoa wa Tabora. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jambo zuri na ni vizuri na sisi tukafanya kwa sababu haiwabagui watoto wa kike katika kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina nyaraka nyingine hapa inaitwa *Project Aprisal Document* au *PAD*, nafahamu Mheshimiwa Waziri unaifahamu vizuri hii *document*. Ukisoma *document* hii inaonesha kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaenda kuwanyima watoto wa kike fursa ya kupata elimu kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuwapeleka kwenye mfumo mbadala ambao wao wameuita *Alternative Education Pathways* ambao ni mfumo duni na nitaenda kueleza kwa nini nasema ni mfumo duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 15 mpaka wa 18 na ukurasa wa 84 wa hii *document* inayoitwa *PAD* wanasema wanakwenda kuwarudisha wanafunzi shule kwa mfumo wa elimu mbadala na umegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza linaitwa *Government Education Centres* na wanasema kuna vituo 151 ambavyo viko chini ya elimu ya watu wazima, 25 viko Dar-es-Salaam na 126 viko mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina *joining instructions* ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Mkoa wa Dar-es-Salaam, inaonesha wana vituo viwili tu. Napenda kufahamu hivyo vituo 23 viko wapi? Serikali iweke wazi kwa majina na *physical address* ya vituo hivi ili watoto wa Watanzania wajue wanaenda kupata wapi hii elimu ya mfumo mbadala. Pia vituo hivyo 126 tunataka kujua viko mikoani na wilaya gani ili tuweze kufuatilia na watoto wetu waende wakapate elimu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mkononi kwangu nina *document* ambayo inaitwa *Open Schools* na ambayo ninyi pia mmeelezea kwamba watoto hawa watakaofukuzwa shule baada ya kupata ujauzito watakwenda kusoma kwenye hizo *open schools*. Kwa utafiti wangu nimegundua hizi *open schools* ni ile elimu ya jioni ambayo wanafunzi huwa wanakwenda kusoma kwa kutumia majengo ya shule za msingi na nina *list* hapa. Naomba Serikali iweke wazi hivi vituo ni vipi na vinaendeshwa na nani, vinamilikia na nani na ni *government* au ni *private*? (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda ukurasa wa 87 wa *PAD* kuna *table* ambayo inaonesha wanafunzi walioacha shule wakirudi kwenye huu mfumo mbadala wataenda kufanya mtihani unaitwa *QT*. Watasoma miaka miwili, *form one* na *form two* watasoma mwaka mmoja, *form three* na *form four* mwaka mmoja na watakwenda kufanya mtihani wa Taifa. Hii ni *QT* tunayoifahamu au ni kitu kingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu *QT* wanafanya mitihani kama *private candidates*. Sasa mkopo huu unawanufaisha vipi watoto wa kitanzania ukizingatia kwenye Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima pamoja na hii *QT* wanalipa ada?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninyi wenyewe mmekiri kwenye hii nyaraka kwamba walimu wale hawana *qualification*, kwanza hawaitwi *teacher's* wanaitwa *tutors*, lakini *sylabus* siyo hii ambayo wanasoma watoto wengine. Huu ni mfumo duni na huu ni ubaguzi wa watoto wa Kitanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namna nyingine ya pili ambayo Serikali wameeleza wanaenda kutoa elimu ni kupitia *Folk Development Centres* au Vyuo vya Stadi za Kazi. Mmekiri kwamba kuna vyuo 30 vya stadi za kazi ambavyo viko chini ya Wizara ya Elimu. Cha ajabu ni kwamba mradi huu wa stadi za kazi inaenda kupewa taasisi binafsi ambayo inaitwa *Karibu Tanzania Organisation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu kama *procurement procedures* zilifuatwa kumpata huyu *service provider*, lakini anatoa mafunzo ya cherehani pamoja na kucheza soka. Tunachukua shilingi trilioni moja kwenda kuwafundisha watoto cherehani? Wakasome elimu ya jioni au *QT* kwa *expense* ya kodi za Watanzania ambazo zinakwenda kulipa mkopo huu?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aeleze kinagaubaga anavyosema *Alternative Education Pathways* anamaanisha nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Nassir, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Mahawe, Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kuwatakia Waislamu wote nchini kheri ya...

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Khadija Nassir.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wa CCM wanaochangia kuanzia sasa wanachangia kwa dakika 7. Mheshimiwa Khadija Nassir endelea.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa napenda kutumia fursa hii kuwatakia Waislamu wote nchini kheri ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Nawaomba tutumie muda huu wa mwezi Mtukufu kumwomba Mwenyezi Mungu atuinge na majanga ambayo yanatukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Serikali kupitia Wizara hii ya Elimu imekuwa ikifanya mambo makubwa sana. Napenda kuipongeza kwa usimamizi wa Sera ya Elimu Bure nchini lakini pia kwa uboreshaji wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na maboresho ya miundombinu mbalimbali katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuwaambia Serikali bado tunahitaji mfumo wa elimu mbadala, umekuwa ni suluhisho kwetu lakini pia kwa wale wanafunzi ambao walikuwa wamekosa fursa ya kuendelea na elimu. Elimu

mbadala imetuwezesha hata humu ndani kuweza kunufaika. Tukianza kuulizana humu nani na nani ambaye ameweza kufaidika tutajikuta ni wengi sana. Kwa hiyo, tufanye maboresho katika mfumo huo lakini uendelee kwa sababu umekuwa na tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi hii hayawezi tu kutegemea Watanzania wachache ambao wameweza kupata fursa ya kusoma vizuri na kufaulu kwenye masomo yao. Maendeleo ya nchi hii ili yaweze kupiga kasi lazima tuweze kuwatumia Watanzania ambao waliweza kufaulu vizuri, lakini wale ambao walikatisha elimu yao kutokana na sababu mbalimbali kwa hatua ya kati na wale ambao waliweza kupata elimu tu ile ya awali. Kwa kuchanganya nguvu, mawazo, fikra ya makundi yote haya matatu ndiyo sasa tunaweza kwenda kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo. Uzuri ni kwamba makundi yote haya matatu yako chini ya Wizara ya Elimu kwa jukumu la kuwalea na kuwaandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kifanyike? Nina ushauri, suala la kwanza, Wizara iweze ku-*design* mfumo utakaowezesha wanafunzi kujitegemea na kukabiliana na changamoto za kimaisha. Mfumo wetu umekuwa ukileta *confusion* kubwa sana ndani ya jamii, hatuna uwezo wa kuchanganua mwanafunzi au Mtanzania ambaye ameweza kumaliza elimu yake vizuri na yule ambaye hakupata fursa. Hili limesababisha kushusha morali ya vijana wetu kufanya vizuri kwenye masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili, Wizara iweze kufanya maboresho ya mitaala kwa kuanzisha masomo ya stadi za kazi na ujasiriamali kuanzia ngazi ya awali ili kujenga nguvu imara. Nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi sana na kupitia rasilimali tumekuwa na uwezo wa kuzalisha ajira ambazo sio rasmi. Sasa ili tuweze kuona umuhimu wa kuzalisha ajira ambazo siyo rasmi kwa wingi zaidi, lazima wanafunzi waweze kupata ujuzi wa stadi za kazi na ujasiriamali kuanzia hatua ya awali ili hata mwanafunzi asipoweza kufanikisha

kufika chuo kikuu awe na uwezo wa kujajiri na kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa tatu, Wizara lazima iendeleo kuboresha maandalizi bora ya walimu wetu kwa kuwapandishia stahiki zao, kuwajengea miundombinu rafiki lakini kuwapa motisha mbalimbali. Walimu ndiyo kitovu au *source* kuu ya kuweza kuboresha elimu hapa nchini. Kwa kuwaandalia mazingira mazuri nao wataweza ku-*concentrate* kuwasomesha wanafunzi na ku-*produce* wale wanafunzi ambao wanaweza kuja kuwa na tija kubwa sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, napenda kuongelea kidogo sekta ya elimu kwa wale wenzetu ambao wana mahitaji maalum. Hapa nina ushauri tu kidogo ambao nitautoa kwa harakahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza, Serikali iweze kuona namna ambayo itaweza kuboresha mwongozo wa kujifunza na kufundishwa kwa wenzetu ambao wana mahitaji maalum. Pili, Serikali iweze kutofautisha mitihani wakati wa kutunga, kusahihisha na kutoa alama kwa wenzetu kwa sababu, wamekuwa wakipata changamoto kubwa sana ya kuweza ku-*cope* na mfumo huu ambao upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa tatu, tutoe motisha kwa walimu ambao wanasomesha wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa kweli, mazingira ni magumu sana kuweza kum-*coach* mtoto ambaye ana mahitaji maalum mpaka aweze kufikia ile hatua ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, napenda kushauri mwongozo wa kijifunza na kufundishwa uwe wa tofauti. Hii itasaidia ufaulu wa wenzetu ambao wana mahitaji maalum uweze kidogo kupanda na wao waweze kufaidika na haya matunda ya elimu bure ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Esther Mahawe, atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi ajiandae.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Ester Mahawe, atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi ajiandae.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi yake kubwa na iliyotukuka ya kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kusema mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, najua hata muda wangu hautatosha, lakini itoshe tu kusema naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano na Chama changu cha Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza Ilani kama ilivyokusudiwa na kama ilivyokuwa matazamiao ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kabisa juhudi zinazoendelea kufanywa na Wizara ya Elimu chini ya Profesa Ndalichako pamoja na Naibu Waziri na timu yote ya Wizara ya Elimu juu ya kuboresha elimu yetu. Wote tumeshuhudia mambo yaliyofanyika katika nchi yetu kwa kipindi hiki cha miaka mitano, ni makubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu tu kupitia hotuba hii ya Wizara ya Elimu, kazi iliyofanywa kupitia mpango wa *EP4R* ambao ni wa kulipa kulingana na matokeo; mpango huu umeweza kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo mbalimbali, umeweza kununua magari kwa ajili ya wadhhibiti ubora wa kanda pamoja na wilaya mbalimbali nchini, umejenga ofisi zaidi ya 100 kwa ajili ya kuboresha

udhibiti wa ubora wa elimu nchini. Hii kazi ni kubwa sana, kwa hiyo, ninaomba sana kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko kwetu Manyara ilikuwa ni changamoto kuwa na kidato cha Tano na Sita, lakini katika Awamu hii tumefanikiwa kupata shule nyingi tu za kidato cha tano na sita. Naipongeza sana Serikali na niendeleo kuiomba iendeleo kuongeza bidii ili wanafunzi wengi wa jamii hii ya kifugaji waweze kupata elimu hasa watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoka katika jamii ya kifugaji na mkoa mzima wa Manyara ni jamii ya kifugaji. Naiomba Serikali kupitia huu Mpango wa *EP4R* kama walivyofanya kwenye mambo mengine mengi, watusaidie tuendeleo kufanikiwa kupata hasa shule zenye mabweni kwa ajili ya watoto wetu wa kike ili kupunguza majanga ya mimba na vitu vingine vya namna hiyo. Napongeza juhudi ambazo tayari zimeonekana. Fedha zilizopelekwa katika Mkoa wa Manyara ni nyingi kwa ajili ya elimu bila malipo na matokeo chanya yameonekana. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapojadili haya, ninajua katika mikakati na malengo ya Wizara ya Elimu, lengo namba tisa ni pamoja na kuhakikisha kwamba udhibiti ubora wa elimu unakaa sawa sawa. Zipo changamoto ndogo ndogo za kimaslahi, za mishahara na posho zile za utendaji wa wadhibiti ubora Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba tu Wizara iangalie. Kuna maombi ambayo yameelekezwa na Waraka Na. 3 wa 2014 wa watendaji hawa ambao unaelekeza kupewa posho ya majukumu, lakini hili halijafanyika. Kama tunahitaji kuboresha elimu, hawa watu wasiishi kwa manung'uniko. Najua Serikali imefanya mambo mengi makubwa, lakini wajaribu wakati muda utakaporuhusu Mungu akipenda, basi kuangalia maslahi mapana ya Wadhibiti Uboora Wakuu wa ngazi ya Wilaya ili kwamba tuweze kufanikiwa kwa kadri ya malengo tunayojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la TEHAMA. Najua Serikali inaendelea kuwekeza vizuri katika masuala mazima ya teknolojia na jambo hili nimelizungumza tena huko nyuma kwamba kwa bahati mbaya hatuna mtaala wa TEHAMA katika *A'Level* kwa maana ya *Form V and VI*. Tunakutana tena na TEHAMA katika *level* ya Vyuho Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba tu Serikali yangu Sikivu, ione namna gani TEHAMA itaendelea kufundishwa katika vidato hivi vya Tano na Sita ili kuweze kuwa na mwendelezo ambao unaeleweka kutoka Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, Tano na Sita hadi Vyuho Vikuu na hata Vyuho vya Ufundi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tuna janga kubwa la *Corona*. Nampongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Ummu Mwalimu na Wizara ya Afya na hapa nawapongeza Watendaji wote wa Afya kwa jinsi wanavyopambana na janga hili. Janga hili limeleta taharuki kila mahali. Naomba ku-*declare interest* kwamba nami ni mdau wa elimu katika sekta binafsi ambapo kwa kiwango kikubwa kwa kweli tuna wafanyakazi walio walimu na wasio walimu ambao kwa sasa wanaendelea kuathirika sana kwa sababu mapato ya wamiliki wa shule yanatokana na ada ama makusanyo yanayolipwa na wazazi. Kwa sasa wateja hao ambao ni wanafunzi wako nyumbani, kwa hiyo, hakuna *income* yoyote inayoingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Rais wangu kwa maana ya kwamba yeye mwenyewe ameomba juzi *World Bank* ione namna ambavyo itaweza kusamehe madeni ya nchi yetu na nchi zetu za Afrika katika kipindi hiki na vitu vya namna hiyo. Sisi hatuna pa kupeleka ombi letu, namwomba sana Mheshimiwa Rais aweze kusema na mabanki yaliyoko nchini ambapo wadau wa elimu wamekopa huko na wana marejesho makubwa. Pia kama inawezekana tukapata aidha ni *soft loans* kipindi hiki kwa ajili ya mishahara ya walimu na wafanyakazi wasio walimu ili

waendeleo ku-*survive* wao pamoja na familia zao mpaka pale janga la *Corona* litakapokuwa limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo wadhibiti ubora wa *level* ya Kata kwa maana ya Maafisa Elimu Kata ambao Serikali imewapatia vyombo vya kurahisha kazi zao kama pikipiki. Hawa ni wale wanaofuatilia shule kwa karibu kutoka shule moja kwenda nyingine. Jiografia ya maeneo mengi ya Tanzania inatofautiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie tu mfano wa Mkoa wa Manyara, maeneo ya Kiteto, Simanjiro, Hanang na Mbulu, kuna kilometa nyingi kutoka shule moja kwenda nyingine. walihidiwa hela ya mafuta shilingi 122,000 kwa mwezi ikiwa ni pamoja na matengenezo kidogo. Yako manung'uniko kidogo kwamba hawajafanikiwa kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zingeangaliwa pia wakati zinatolewa, kuna zile Wilaya ama Halmashauri ambazo kidogo wenyewe hawana umbali mkubwa kutoka shule moja kwenda nyingine kama ilivyo Simanjiro, Kiteto na maeneo mengine, basi waweze kuwatazama walimu hawa kwa sababu unakuta shule moja ina kilometa 50 mpaka 80 kutoka shule hadi shule. Ukisema huyu mtu ajiwekee mafuta mwenyewe pamoja na kwamba ana chombo hicho, tutachelewa kuimarisha masuala mapana ya uboreshaji wa elimu katika maeneo yetu. Kwa hiyo, naomba hawa watu pia watazamwe kwa namna ya tofauti ili waweze kusimamia elimu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Serikali, nakumbuka mwaka juzi tulikuwa tuna changamoto kubwa ya matundu ya vyoo katika shule zetu. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano, tunavyozungumza sasa vyoo zaidi ya 9,712 vimejengwa katika maeneo mbalimbali nchini na yote haya ni kusaidia watoto wa kike na wa kiume. Kwa hiyo, naipongeza sana juhudi hii, siyo ya kubeza hata kidogo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*



**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali na zaidi sana niendeleo kuiomba Serikali kujaribu kutafuta namna ya kutega miundombinu ya maji kwa ajili ya usafi wakati wa matumizi ya vyoo hivi kwa sababu siyo maeneo yote tayari yamefikiwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mengi ya kusema, lakini kubwa kuliko yote niendeleo kuipongeza Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kengele imeshagonga. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Oscar Mukasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi na Mheshimiwa Rose Tweve, ajiandae.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu leo kwenye Wizara ya Elimu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kuendelea kutulinda na dhoruba inayoendelea, lakini nawashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kuwa nami katika shughuli hii ambayo tunaelekea kuikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, kwa sababu muda hautoshi, naomba Mheshimiwa Ndalichako na Mheshimiwa Olenasha muiwakilishe Serikali kuchukua pongezi zote kwa kazi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahsusi kwa Biharamulo, tunashukuru, kuna mambo yamefanyika kule ambayo kwa kweli tuna wajibu wa kusema na kushukuru. Vyumba vya madarasa, maboma yale 20 kwa Shule ya Msingi yametusaia sana, 12 kwa Shule za Sekondari na maabara nne na usajili wa shule mpya. Najua watu wanaweza kudhani ni wajibu wa Serikali, ni kweli, lakini hasa kwenye usajili tunawapongeza kwa sababu siyo tu wamesajili, lakini katika ule mchakato walikuwa wanafanya ile *supportive service*.

Siyo tu kukuvizia ukosee ili ushindwe, lakini walikuwa wanaelekeza, hiki fanya hivi, hiki fanya hivi ili twende mbele. Kwa hiyo, nawapongeza sana katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida ya Biharamulo, upungufu wa walimu wa sayansi ni mkubwa sana. Najua ni tatizo la Kitaifa lakini lazima niseme Biharamulo halafu tuzungumzie Tanzania. Upungufu wa walimu 155 wa sayansi; kwa dunia ya sasa tunakokwenda kwa hali hii hatutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najiuliza, hivi hatuwezi kutumia walimu wastaafu wa sayansi ambao wako kule? Tuone namna gani tunaweza tukawatumia, tunaweza kwenda kwenye mifuko ya hifadhi tukaweka pesa kidogo ambapo mbali na *pension* yake pale mwishoni kuna kitu fulani kiliongezwa ambacho atapokea *pension* yake lakini utaongeza kitu Fulani ambacho...

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Ndiyo. Aah, karibu. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Naona kuna taarifa kutokea Msekwa.

## T A A R I F A

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka nimpe Taarifa mchangiaji, asiwaze kuchukua waliostaafu. Wapo *freshers from schools* na hawajaajiriwa hao walimu wa sayansi. (*Makofi*)

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Haya, tuendeleo Mheshimiwa Naibu Spika. Walimu ambao wamestaafu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni nzuri, hamna shida. Shida ni kwamba tunafahamu Serikali

inapata shida kwenye *payroll*. Sasa wakiweka walimu waliopo ni vizuri kabisa, lakini kama wanashindwa kama *alternative*, walimu wastaafu hawakuongezezi mzigo kwenye *payroll*, badala yake unafanya ubunifu ambapo kule nyuma kwenye mifuko ya hifadhi kuna kitu unaongeza kinawabeba unaendelea kuwa-*sustain* na ina faida zaidi ya ajira.

Mhshimiwa Naibu Spika, uko utafiti hapa unasema mtu aliyestaafu asipofanya *physical and mental activities*, anakufa haraka. Uko huo utafiti, wameandika wanasayansi. Kwa hiyo, tutafute namna tuwatumie hata kama tunaendelea kutumia walimu waliopo, hakuna shida. Kwa hiyo, naomba tutafute namna ya kuwatumia hao walimu wakati tunajipanga kuwekeza kwenye *payroll* kwa ajili ya walimu ambao ni wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyakanazi, tumejenga shule tatu sasa za msingi lakini bado hazitoshi. TAMISEMI wanafahamu, wametuahidi mara kadhaa watakuja pale kuona namna gani tunashirikiana nguvu zetu Halmashauri na za Kitaifa ili tutatue tatizo hili. Huo ni mfano tu mmoja wa miji ambayo inakua kwa kasi.

Mheshimiwa Waziri, ushauri wangu mwingine ni ile asilimia moja ya *GDP* ya Taifa kwa ajili ya utafiti na ubunifu. Hapa ndipo nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu wekeza nguvu kubwa kwa sababu siku zote zinawekezwa nguvu kubwa pale ambapo pana tija sana na baada ya maelekezo ya Rais ya Serikali mwaka 2012 habari ya *one percent* ya *GDP* Serikali iliweka shilingi bilioni 19 kwenye *cost* kwa kazi hiyo, baadaye ikaweka shilingi bilioni tano mwaka mmoja uliofuata lakini zikapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushahidi kwamba hizo pesa kidogo zilizowekwa zilizozaa ile *return on investment* ilikuwa kubwa sana. Mifano michache, mmojawapo ni *Max* malipo ambayo ni matunda ya uatamizi wa *COSTECH*. Watu waliokwenda kufanya pale uatamizi kwa muda fulani *Max* Malipo imejibu sana mara tatu ya kile kilichowekezwa na Serikali kwa hiyo miaka miwili na ushahidi upo na Serikali

inafahamu. Kwa hiyo, tuwekeze kwenye uatamizi na ububifu, ndiko dunia inakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwa habari ya *Corona*, tunakwenda kubadilika kabisa. Tunaomba tuwekeze kwenye maeneo ambayo yanajibu haraka. Ubunifu siyo kwenye sayansi ya juu peke yake (*high tech*) hata *social science* kuna ubunifu wa *social innovation*, tuna ushahidi mambo yamefanyika sana. Umoja wa Tanzania, Sweden na Netherlands waliwahi kushirikiana ikaingia bilioni 1.2 kwa ajili ya *innovation* lakini imekufa, haiendelei na hili ndiyo eneo ambalo tunapaswa kuwekeza na Tanzania ikatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa mfano juzi juzi hapa, ubunifu wa chombo cha maji Nelson Mandela; ule ukichukuliwa una faida kwa Wizara ya Afya na Wizara ya Maji. Wakinywa maji masafi, vifo vya watoto vinaweza kushuka kwa zaidi ya mara mbili na ushahidi upo. Mtanzania ametengeneza chombo, ukikitumia kile, ukakiingiza kwenye *policy environment* kitaokoa, watoto watakunywa maji masafi na utaondoa vifo. Sasa hivi tuondokane na elimu ya *knowledge* peke yake ya kufahamu tu, twende na elimu ya kubuni na kutatua matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Corona*, wamesema waliotangulia. *Private Sector* hasa kwa upande wa shule tuwasaidie. Huwezi kuilaumu Serikali, wala kumlaumu mtu, unamlaumu *Corona* tu, lakini lazima tukae tujipange tuone tunafanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa mwanafunzi mmoja wa *masters* tena ni mfanyakazi wa Bunge hapa, ananiambia naye haendi shule kwa sababu ya *Corona*. *Masters!* Kuna namna ambavyo *Open University* na watu wengine wanasoma tu kwa mtandao. Hawa wa *undergraduate* ndiyo wengi lazima tuwaondoe. *Masters* na *Ph.D* hebu fanyeni haraka warudi wasome. Kuna mitandao, *Open University* wana mifumo inafanya kazi vizuri sana. Nelson Mandela leo naambiwa wanaendelea kusoma kwa sababu pale ni *Masters* na *Ph.D*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu ambacho siyo huria asilimia 70 ya wahadhiri ni *full time, thirty percent part time*. Huwezi kupata *total loss*, walipwe hawa kwa kufindisha *masters* na *Ph.D* kipindi hiki, waendeleo tusipate *total loss*. *Open University* ndiyo asilimia 30 *full time, 70, part time*. Kwa hiyo, huwezi kupoteza kwa asilimia 100 wakati kuna asilimia fulani unaweza ukaokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwa Mheshimiwa Waziri; *innovation*. Hii elimu ya kusoma tu kujua moja, mbili, tatu, nne bila kubuni, hatutaiondoa Tanzania kwenye hali iliyopo. Tuondoke kwenye kusoma na *knowledge* peke yake twende kwenye ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Tweve na Mheshimiwa Fatmah Toufiq ajiandae.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Elimu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku ya leo kunipa afya njema, kuchangia Wizara hii. Namshukuru Mheshimiwa Spika japokuwa hayupo, wewe binafsi Mheshimiwa Tulia, umetulia kama jina lako, Mwenyezi Mungu aendeleo kukulinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wenyeviti wote ambao mlisaidiana nao kwa kipindi chote mlichoniongoza katika Bunge hili ambalo nimekaa muda wa miaka miwili na miezi saba mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri wetu Mkuu japokuwa hayupo, lakini salamu zitamfikia na Mawaziri wenzake na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano ambao wamenipa kwa kipindi ambacho nilikuwa hapa na nilipokuwa nikiwaomba msaada wao katika mambo ya shughuli zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wote wa Bunge kwa msaada ambao wametupa. Mwenyezi Mungu awabariki sana. Wa kuwashukuru ni wengi, hata Makatibu Wakuu wa Wizara na Wasaidizi wao, nawashukuru sana, wametusaidia sana katika kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampa pole Mwenyekiti wangu wa Taifa wa *CUF* kwa msiba uliotupata katika chama chetu kuondokewa na Katibu Mkuu wetu, Mheshimiwa Khalifa Seif Khalifa na wanachama wote wa *CUF*. Nasema pole sana. Vile vile nawapa pole sana familia ya Mheshimiwa Getrude Rwakatare, Watangazaji wa Redio Tanzania. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema Peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najikita katika kushauri. Mimi natokea Mkoa wa Kagera. Mkoa huu una upungufu wa walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Kwa upande wa Sekondari ni walimu wa mafunzo ya sayansi. Walimu 6,935 ni shule za *primary* na Sekondari katika Mkoa wa Kagera tuna upungufu wa walimu 495. Ninaishauri Serikali iajiri walimu wa kufundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nitajikita katika kushauri. Naishauri Serikali iwajengee walimu nyumba za kukaa hususani vijijini. Walimu wanatembea mwendo mrefu hawana nyumba za kukaa pale shuleni. Ninaomba Serikali iwajengee nyumba za kukaa wawe karibu na maeneo wanapofundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninaishauri Serikali, Serikali ijenge maktaba mashuleni kwa kuwa hawaba maktaba za kutosha hasa vijijini. Mimi najikita sehemu za vijijini. Sehemu za mjini bahati nzuri wana maktaba, wana shule nzuri, kama Mheshimiwa Mama Mushashu alivyotangulia kusema. Shule zilizokuwa zimeanguka zote wakati wa tetemeko la nyuma, naishukuru Serikali imezijenga zote ziko katika *standard* nzuri kabisa. Nawashukuru sana, lakini shule za vijijini hawana maktaba, wala vitabu. Naishauri

Serikali ilifanye jambo hilo kusudi watoto wetu wapate maktaba za kujifunzia na vitabu vya kujifunzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naishauri Serikali ni kuhusu Walimu, stahiki zao hazitoshi. Wawaongezee mishahara yao maana Walimu na wenyewe ni binadamu, wana mahitaji mengi sana, wanapaswa wapate mishahara, watulize akili zao. Kamshahara wanakopakata ni kadogo mno, wakitoka vijijini maana wanatembea wengine mwendo mrefu na wengine wanapanda magari hapa na pale, akija kufika mjini na kurudi vijijini huku mishahara umshaisha. Naomba Serikali iwaongezee mishahara ili nao wakidhi mahitaji yao, akili zao zitulie waweze kutufundishia watoto wetu kwa kutulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naishukuru Serikali...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakimsemesha Mzungumzaji bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Bwana mimi msinizingue. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijenge shule mahali ambapo shule hazitoshi, iwajengee shule wanafunzi kusudi wasitembee mwendo mrefu, watembee mwendo mfupi ili wakisoma masomo yaweze kutua vichwani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami katika wachangiaji waliopita huu ndio mchango pekee uliopata kutokea Msekwa na humu ndani na amepigiwa makofi na watu wote, mchango bora kabisa kwenye Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ahsante sana Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Rose Tweve, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo ajiandae.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye wizara muhimu sana hii Wizara ya Elimu. Awali ya yote naomba nitumie fursa hii kwa kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa *commitment* na *dedication* kubwa ambayo ameionyesha kwenye wizara hii kuhakikisha Watanzania wanapata haki yao ya msingi hasa kwenye upande wa elimu bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zaidi, nipongeze sana wasaidizi wake Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ambao wamehakikisha hii kiu ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na *access* ya elimu inafikiwa na matunda haya yanajidhihirisha dhahiri. Utaangalia kwenye *enrollment* kwenye ngazi zote kuanzia shule ya awali kumekuwa na ongezeko kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na ufaulu kwenye mitihani ya Kitaifa kwa kweli inatupa moyo na la zaidi ya yote ambayo Awamu ya Tano itakumbukwa na Watanzania ni kuhakikisha tunawapa *access* watoto wote kupata elimu hasa watoto wetu wa kike. Ukiangalia kwa takwimu, kwa Taifa zima sasa hivi *enrollment* ya mtoto wa kike inafika 50 kwa 50. Ukifika kwa mfano Mkoa wa Iringa sasa hivi hadi namba zinakwenda zaidi ukilinganisha na zile za watoto wa kiume. Kwa hili, niipongeze Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nina mambo machache ambayo napenda kushauri ili tuweze kufika mbele. Kama Taifa tumekuwa na malengo ya kuhakikisha tunaweza kujitegemea na kufikia uchumi wa kati. Katika nchi ambayo imependelewa, *Tanzania is one of them*. Tukianza kwenye hizi *natural resources, you name it* Tanzania



tunayo, ukija kwenye rasilimali watu zaidi ya asilimia 50 ni nguvu kazi ya vijana ambayo ingeweza kutusaidia kufika kwenye malengo yetu, ardhi tunayo ya kutosha *and above all* tuna Rais ambaye yupo *dedicated* kuhakikisha sisi kama Taifa tunafikia huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matamania haya yote na hizi *resources* ambazo tunazo lakini bado tumekuwa na changamoto ya kufikia yale malengo yetu na *piece of the puzzle* ambayo ina-*miss* hapa ni kubwa ambayo nyie wenzetu Wizara ya Elimu mnetusaidia kufikia hayo malengo, ni kuhakikisha tuna-*invest heavily* kwenye *science, technology* na *innovation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo, Bunge lako Tukufu lilifanya agizo kuhakikisha tunakuwa na tume chombo maalum cha kuhakikisha tuna-*coordinate* na ku-*promote* masuala yote ya *research* na *technology* hapa nchini, tukaanzisha chombo kinaitwa *COSTECH*. Cha kusikitisha, chombo hiki pamoja na umuhimu wake kimekuwa kinapewa *funding* ndogo sana. Nadhani tulikuwa tumepanga wapate *8.5 billion*, mpaka sasa hivi wana uwezo wa kupata *only five billion*.

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tukiangalie chombo hiki kwa umuhimu wake. Kama nilivyosema hii ni *one of the piece of the puzzle* ambayo ina-*miss* ili tuweze kufikia malengo yetu kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto imekuwa kubwa sana, sisi kama Kamati tulipata nafasi ya kuweza kutembelea vyuo mbalimbali ikiwemo chuo chetu mahiri sana Chuo cha Mandela. Tukakuta pale kuna majengo mazuri, wanafunzi wazuri na kuna *innovation* kubwa ambayo inaendelea kwenye hiki chombo chetu. Changamoto kubwa ambayo tumeikuta pale ni uwezo wa vyuo hivi kufanya uendelezi wa ule ugunduzi ambao wanafunzi wetu wa vyuo wanakuwa wamegundua hasa gunduzi hizi ambazo zinazoweza kutatua changamoto mbalimbali ambazo sisi kama Taifa tunazipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja tu, tulikuwa tumekuta binti mmoja pale Chuo cha Mandela anaitwa Cecilia, yeye ni mmoja wa wanafunzi wa Shahada ya *PhD* ambaye ameweza kugundua magome ya miti na udongo ambao unapatikana hapa nchini ambao anaweza akachakata na kuweza kutengeneza ngozi ili tuweze kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na ugunduzi huo. Changamoto kubwa kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri hatuna *funds* za kuhakikisha ugunduzi huu ambao umefanywa na hawa vijana wetu tuweze kuufikisha mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa ndipo ambapo Mheshimiwa Waziri na Serikali yote kwa ujumla ningependa kuhakikisha tunakuwa na *innovation fund*, kama Taifa hatuwezi kukwepa hapa. Tuna vijana ambao wapo tayari kujifunza lakini changamoto kubwa kama nilivyosema hakuna hizi *funds* ambazo zinaweza kufanya sasa mwendelezo wa kile ambacho wamejifunza ili kuweza kutatua changamoto mbalimbali ambazo tunakwenda kuzipata kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, / *know* Mheshimiwa Waziri *is competent*; najua kama Taifa tumepitia changamoto kubwa na wizara ambayo ipo *affected* sana ni Wizara ya Elimu. Najua watakuwa na kazi kubwa ya kujipanga kuhakikisha ni jinsi gani kama Taifa tunaweza sasa kuwarudisha watoto wetu vyaoni na shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamesema Sekta ya Elimu hasa hizi *private schools* na vyo wana mchango mkubwa sana wa kuhakikisha wanasomesha hawa watoto wetu, kwa sababu hawa watoto wanaosoma pia ni watoto ambao wataendelea kufanya kazi hapa nchini kwetu. Wengine wamesema *terms* ya *funding* sijui na nini, mimi naomba twende *further*, tuwaite tu tupate kuongea nao tujue mawazo na changamoto zao, ni jinsi gani sasa wataweza kurudi shuleni salama kuendelea kuwafundisha hawa vijana wetu. Hilo ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niwatakie heri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara katika utekelezaji wa bajeti yao. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Fatma Toufiq...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq naomba usubiri kidogo, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ningependa tu kupata ufafanuzi au sijajua kama kuna matatizo ya kiufundi, kwa sababu hotuba yetu ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani haipo kwenye mtandao. Naamini kama kitu ambacho kinatakiwa kisiwepo ni kile ulichokitolea *ruling* peke yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hapa kwangu inaonekana, hebu tujaribu kwenda kwenye kile kitufe kilichoandikwa *refresh*; twende kwenye kile kitufe kiliichoandikwa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge, twende kwenye kitufe kilichoandikwa *refresh* halafu utaiona itajitokeza hapo.

Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Fatma Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo na Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza

kuchangia bajeti ambayo ni ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sambamba na hilo, naomba nitumie fursa hii nikushukuru sana wewe kwa kunipa fursa hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wote kwa kumpongeza Waziri wangu wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, lakini sambamba na hilo Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Wakuu, lakini pia na watendaji wote ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu sana kwa kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya elimu katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa tatu wa hotuba hii, Mheshimiwa Waziri ameeleza kuhusu wanafunzi kuendelea kupata elimu katika kipindi hiki ambacho kuna janga hili kubwa la *corona*. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu vipindi kupitia redio maalum na *television*, napongeza sana hatua hii.

Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo ambapo *television*, redio na hizi *online media* hawaoni, naomba nitoe ushauri kwamba katika yale maeneo ambayo vitu vyote hivi haviwezi kuonekana, basi ufanyike utaratibu wa kuweza kupata au vitini au *material* mbalimbali ili kusudi wazazi na walezi wa watoto hawa waweze kupata *materials* haya hatimaye yaweze kuwasaidia hawa watoto pamoja na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa pindi itakapotokea janga hili likawa limepungua au likawa limekwisha na hizi shule pamoja na vyo vikafunguliwa, basi ufanyike utaratibu wanafunzi hawa wapimwe kwa jinsi walivyosoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupongeza mambo yote ambayo yamefanyika katika udhibiti ubora wa elimu. Hotuba imezungumza kwamba wamejenga ofisi, wamenunua vitendea kazi, lakini pia hata sisi katika Mkoa wa Dodoma tumeweza kufaidika kwa kujengewa ofisi za wadhibiti ubora katika Wilaya nne za Mkoa wa Dodoma na vifaa vingine kama magari na kadhalika. Hata hivyo, naomba tu nitoe ushauri kwamba, magari yapo lakini tatizo la bado madereva hakuna. Kwa hiyo Wizara ione inalifanyiaje kazi hili ili kusudi mwisho wa siku waweze kupatikana au waajiriwe madereva kwa ajili ya kuweza kuendeleza hili gurudumu la elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu Wadhibiti Ubora wa Elimu, wenzangu wengi wamelizungumzia lakini pia naomba nihusishe pia ule Waraka wa mwaka 2015 ambao ulikuwa umebainisha *DEOs, REOs*, Wadhibiti Ubora wa Elimu wa Wilaya na Kanda walipwe kwa ngazi ya *LSSE*. TAMISEMI wametekeleza jambo hili, lakini kumekuwa kuna malalamiko kwa baadhi ya Wadhibiti Ubora wa Elimu; sasa hebu basi wizara ione inalifanyia hili kazi ili kusudi kuweza kuboresha maslahi ya hawa Wadhibiti Ubora wa Elimu, kwa sababu inawezekana katika kipindi hiki kuna baadhi ya Wadhibiti Ubora ambao wameshastaafu, sasa je stahiki zao wanalipwa vipi? Kwa hiyo, naomba hili waweze kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa ushauri kuhusu mfumo mpya wa kukagua katika shule, mfumo ambao unaotumika na Wadhibiti Ubora wa Elimu kwamba anakagua somo lolote lile. Nashauri kwamba hebu Wizara iangalie upya kwamba hawa Wadhibiti Ubora waende kwa viwango vile vya elimu ambavyo wao wamesoma. Kwa mfano, kama amesome *English*, Kishwahili au amesomea masomo ya sayansi, basi akague kwa jinsi ya ile taaluma yake aliyonayo, kwa sababu utakapokwenda kumwambia Mdhhibiti Ubora ambaye amesomea *English* au Kiswahili akakague *Biology* mimi naona inakuwa ni mtihani kwake. Kwa hiyo, naomba hili jambo waweze kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nipongeze sana kwenye ukurasa wa 82, wamezungumzia kuhusu uendelezaji yaani kuna wanafunzi wa Kichina 10 ambao wamepewa ufadhili kusoma Kiswahili. Naona hii bado ni namba ndogo, basi hebu Wizara ione tunawezaje kuongeza idadi kubwa zaidi ili kusudi sasa tukipata wengi wakajifunza Kiswahili, basi ina maana kwamba Kiswahili kitaweza kuzungumzwa dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda sio rafiki sana, basi kwa uchache, naomba nichangie hayo na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Zacharia Isaay ajiandae.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Tunatambua kwamba elimu ndio kila kitu, kwa kuwa huu ni uchangiaji wangu wa mwisho kwa Bunge hili, ningependa kusema mambo machache. Nchi yetu tunaamini katika suala zima la usawa wa kijinsia na kila Waziri anapoanza au anapoandaa hotuba yake, mara zote wanasema/tunasema hotuba hii inafuata/ inaongozwa na Dira ya Maendeleo lakini vilevile inaongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 52(2) inasema kwamba itahakikisha kuwa wasichana wote wa elimu msingi wanaoacha shule kwa sababu ya ujauzito wataendelea na masomo, hii ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020.

Sasa nataka kujua kama mlituahidi mwaka 2015 kwamba watoto wa kike wanaopata ujauzito watarudi shule, ni kwa sababu gani sasa hivi jambo hilo halifanyiki huku tukitambua kwamba katika fedha zitakazotolewa na *World Bank* dola milioni 500, sawa na trilioni 1.2 ni pamoja na kusaidia watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika barua yake aliyoandika tarehe 6 Aprili, 2020 kama *public notice* ameeleza wazi kwamba katika hizo fedha dola milioni 500 ni pamoja na kusaidia watoto zaidi ya milioni 6.5 walio-*drop out* lakini ni pamoja na watoto waliopata ujauzito. Sasa nilitaka kujua *statement* hii ya Waziri, moja; inaenda sawasawa na kauli ya Mheshimiwa Rais kwa sababu hatujaona mahali popote ambapo kuna maandalizi ya kuhakikisha kwamba watoto hawa watarudi shule. Kwa hiyo, naomba tuelewe kwamba mtoto wa kike anapokosa shule maana yake ni kwamba hata kile kiumbe kitakachozaliwa kinakosa shule, kwa sababu tafiti zinaonesha wazi zaidi ya asilimia 90 ya watoto waliokosa shule kwa sababu ya ujauzito au vyovyote vile, ni vigumu sana watoto wao wanaowazaa wakaendelea na shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimba inakaa tumboni, haikai kichwani; tumeshuhudia baadhi ya Wabunge ndani ya Bunge lako wamejifungua na wameendelea na kazi vizuri, wengine ni Mawaziri; kwa nini tunawanyima watoto wa kike shule? Tunaomba jambo hili lifanyiwe utafiti na Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni mwanamama ahakikishe kwamba watoto hawa wanarudi shule na hizi fedha zitakapotolewa na *World Bank* tuone utekelezaji wake, vinginevyo tutakataa. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la *corona* na shule za *private*. Ni wazi kwamba kama ambavyo nimeongea kidogo kwenye hotuba yangu, lakini tuelewe pamoja na kwamba kuna sekta nyingi za binafsi lakini hizi sekta nyingine za binafsi ni za uzalishaji kwamba wanapata fedha kutoka kule lakini hizi shule za binafsi, wanategemea fedha za kuwalipa mishahara watumishi wao kutoka kwenye ada za wazazi, sasa hawa watoto wapo nyumbani, wazazi hawawezi kutoa ada wakati mtoto yupo nyumbani. Kwa hiyo, tunaomba, tunajua ni jambo gumu, lakini naamini Serikali ina mambo mengi, lakini ina vyanzo vingine vingi vya fedha; wanaweza wakachukua mikopo wakawapa waajiri wa hizi shule ili baadaye waweze kuwalipa mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke wazi kwamba kuna sheria za kazi maana yake ni kwamba sasa hivi hawa walimu wanaweza kabisa wakawashtaki waajiri wao kwa sababu hawajawalipa. Pia tuna ile mifuko ya akiba, tunadhani inaweza ikasaidia. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue jambo hili *very serious* ili kuokoa hawa watumishi wa sekta binafsi.

## TAARIFA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, kuna taarifa kutokea ukumbi mwingine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa Mheshimiwa Susan Lyimo taarifa kwamba mwaka 2018 tulipofanya marekebisho ya Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Serikali kwa mantiki ya utumishi wa umma na watumishi wa sekta binafsi, pamoja na mambo mengine tulianzisha kitu kipya ambacho kinaitwa *unemployment benefit* ambapo kifungu husika kilikuwa kinatoa nafasi kwa watumishi ambao watakosa ajira kwa kipindi cha muda fulani kuweza kulipwa fedha ama kulipwa pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nampa taarifa hiyo ili sasa Mawaziri wakati wanatujibu waseme kipindi hiki cha *Corona* wakati ambapo watumishi wa sekta binafsi ambao wamekidhi vigezo vya michango ya miezi 18 na zaidi, je, watalipwa kama sheria inavyosema ama la? Kwa hiyo, nilikuwa nampa tu taarifa ili kuboresha hiyo hoja nzuri na muhimu sana anayoizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo anazungumzia walimu sasa wewe umesema watumishi wote. Sasa ukisema watumishi tena tunarudi kule kwenye ajira. Yeye alitaka



mchango wake uwe kwenye walimu wa shule binafsi, ndiyo mchango wake yeye, sasa wewe umelifanya lote kwa pamoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hapana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa ili taarifa yako ikae vizuri na yule ajue namna ya kuipokea kwa sababu msije mkampa Waziri kazi ya kujibia Wizara nyingine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme hivi, mimi nazungumza kimapana kwa sababu *always* niko *broad* ila nachosema ni kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Sasa wewe si unampa taarifa mchangiaji, basi kaa Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Umenielewa eeh?

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo, nimeshakuelewa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, hiyo taarifa imechanganywa mambo mengi, wewe pokea ile inayokuhusu kama unataka kupokea.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee, naipokea taarifa hiyo, isipokuwa tu ieleweke kwamba walimu pia ni watumishi na kwa maana hiyo kama Serikali itaipanua kwa wote lakini hoja yangu ni kweli ilikuwa kwa walimu ambao ni muhimu sana wakasaidiwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendeleo kwenye suala la *Corona*, Wizara hii ni ya Elimu na ndiyo yenye sera. Leo tunavyozungumza wanafunzi wa mwaka wa tano wa *medicine* ambao wako kwenye *clinical rotation* wako nyumbani vilevile. Nadhani kwa sababu wanafunzi hawa

wa mwaka wa mwisho tayari hawaingii madarasani wanakuwa hospitalini wangeweza wakatumba hawa kuwasaidia madaktari katika janga hili hasa tukitambua kwamba Wizara ya Afya ina upungufu wa takriban 52% lakini tunaambiwa kwa madaktari ni zaidi ya 60%. Kwa hiyo, nadhani Serikali ingeweza kuona umuhimu wa kuwatumia hawa vijana walioko *clinical rotations* ili waweze kuwasaidia madaktari na wale *intense* kwa ajili ya kusaidia katika hili janga kubwa la *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie vilevile suala la upungufu mkubwa wa madarasa na vyoo na hili ni kwenye udhibiti. Najua haya masuala yako TAMISEMI lakini Wizara hii ndiyo yenye sera na ndiyo yenye udhibiti ubora (*quality assurance*). Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kweli hali ni mbaya sana. Najua wamekuwa wakitamba kwamba awamu hii inafanya vizuri lakini nitake kusema tu tuna upungufu wa vyumba vya madarasa zaidi ya 1,014,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa spidi wanayosema kwa miaka hii minne, kuanzia 2016 mpaka 2020 wameweza kujenga jumla ya vyumba 125, kwa hiyo, kuna upungufu huo, kwa maana kwamba kila mwaka ni wastani 4,300. Kwa hiyo, itatuchukua takriban miaka 27 kupata madarasa ya kutosha. Kwenye vyoo *is even worse* itatuchukua zaidi ya miaka 100 kama tutaenda na spidi hii ya matundu ya vyoo 3,000 kila mwaka kwa sababu tuna upungufu mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kwamba uwiano wa tundu na wanafunzi kwa watoto wa kike ni 1:20 na watoto wa kiume 1:25. Hata ukichukua kwa 1:25 bado tuna upungufu mkubwa sana wa zaidi ya matundu 300,000. Kwa hiyo, tunaomba sana na tunajua wote kwamba watoto wadogo ni lazima waende chooni, ni muhimu sanasana kuhakikisha kwamba matundu ya vyoo yanajengwa kwa wakati ili watoto waweze kusoma vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nizingumzie pia kidogo suala la vijana wanaofanya vizuri. Vijana wanaofanya

vizuri katika nchi hii ni wengi lakini tunasema wale wanao-*excel*, wale *top 10* au *top 20* bila kujali jinsi yao lakini wamefanya vizuri na nina hakika kutakuwa na wasichana na wavulana waende wakasome nje ya nchi kwa sababu kule watakuwa na *exposure* na teknolojia kubwa wakija hapa Tanzania inakuwa ni rahisi sana kuweza kuendeleza nchi. Pia italeta motisha kwa wale ambao wako *form five* na huko chini kuhakikisha kwamba nao wanafanya vizuri ili waweze kusoma nje. Vilevile tunasema hawa sasa Serikali iwagharamie kwa kila kitu siyo Bodi ya Mkopo, iwagharamie ili iweze kuwaletae wenzao motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sayansi na teknolojia, Mheshimiwa Rose Tweve ameliongea vizuri, niseme tu kwamba kwa kweli sasa hivi kuna kila sababu, kama ni 4% tu ya shule zetu ndiyo wanasoma TEHAMA, hili ni tatizo kubwa. Sasa hivi tunaenda kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia, kwa hivyo, naomba sana tuendelee kuwekeza katika sayansi na teknolojia ili tuweze kulipeleka taifa letu mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makoff*)

**NAIBU SPIKA:** Wahudumu walioko Msekwa wampatie maji ya kunywa Mheshimiwa Susan Lyimo.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Charles Mwijage atakayechangia kutoka Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay na yeye atachangia kutoka Msekwa halafu Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu. Bajeti ya leo inatupa taswira ya kazi kubwa tuliyoifanya kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye ndiye jemedari mkuu wa vita hii kwa namna alivyotuongoza kutekeleza shughuli

ya elimu. Kwa shukrani hizo na pongezi basi wasaidizi wake wote nimewataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee nitambue mchango mahsusi wa Wizara ya Elimu chini ya uongozi wa Prof. Ndalichako na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo. Kazi kubwa imefanyika na imeelezwa na kila mtu anatoka Tanzania hii anaweza kuona picha kila mahali anakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naipongeza Serikali nizungumze mahsusi kazi iliyofanyika kwenye Jimbo langu la Muleba ya Kaskazini. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa nguvu ulizoelekeza katika Jimbo langu tukaweza kupata Chuo cha Ufundi Ndolage VETA. Mheshimiwa Waziri ukipitia kwenye kitabu chako angalia Ibara ya 96, 98 na 99 yale uliyoahidi kwenye kitabu hayakuandikwa. Najua uliwaambia watendaji wako wakasahau kuyaandika, kwa hiyo, warekebishe Ibara ya 96 Ndolage haipo, 98 Ndolage haipo na 99 Ndolage haipo, hapo ni kwenye nyumba na mabweni uliyoahidi kuongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Wizara kwa kuweza kutusaidia kufungua shule zetu tano. Sisi katika kipindi cha miaka mitano Jimboni kwetu Muleba Kaskazini tumeweza kujenga shule tano mpya kwa nguvu za wananchi Serikali ikaja kutusaidia kwenye kufungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kushirikiana na TAMISEMI na nguvu za wananchi tumeweza kujenga vyumba vya madarasa 179. Kuna hesabu zinafanyika kwamba itatuchukua miaka 100 kumaliza vyumba vya madarasa na vyoo, haitatuchukua miaka 100. Baada ya kutengeneza msingi kinachofuata ni kuchupa. Msingi tumeshauweka sasa tunakwenda kuchupa kusudi kazi imalizike kabla ya 2025. Tunachupa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujua utaratibu wa kujenga vitu hivi kama walivyofanya Wilaya ya Muleba wanakonunua vitu kutoka viwandani kwa *bulk procurement* tutakachofanya sasa tunaiomba Serikali nendeni mkakope,

kama mmekopa shilingi trilioni 1.1 kakopeni hata shilingi trilioni 5 mtuletee tumalize biashara ya kujenga kusudi tuende mbele. Haitatuchukua miaka 100, wala mitano haifiki tunakwenda kukopa. Hakuna mwananchi atakayeilaumu Serikali kwa ajili ya kukopa kuja kujenga shule, hiyo hutalaumiwa hata riba hawatakuuliza nenda kakope uje ujenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie jambo moja, hata wasichana wanaopata mimba kopa jenga mabweni wafungie shuleni hawatapata mimba. Wanaopata mimba wanatoka nyumbani wanakutana na bodaboda, tuwafungie shule wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao wameshaolewa achana nao, mtu aliyekwishaolewa amezaa huwezi kumrudisha shule akaelewa, kule kwenye kuolewa kuna matatizo kule.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuwekeza nguvu kwa wale walioko nyumbani tuwajengee mabweni kusudi waweze kuendelea na shule yao. Sitaki kuingia kwenye *debate* hizo wala siyo mtaalamu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ualimu Katoke. Ametujengea shule yetu kwa gharama kubwa ya shilingi karibu milioni 800, akatuletea gari na akahimiza kwamba lile gari litumike vizuri na inatumika vizuri na tunashukuru kwa *computer*. Hata hivyo, kwetu wanasema ukishampelekea mtoto ndizi lazima umpelekee na njugu mawe, kwa hiyo, tunakusubiri ulileta ndizi lete na njugu mawe mjukuu kusudi mambo yaweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu hoja iliyotolewa na ...

## T A A R I F A

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, kuna taarifa kutoka kwa Ali Salim na yeye yupo Msekwa.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba tu nimpe taarifa mchangiaji kwamba walioolewa wakisomeshwa pia wanaelewa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hamna kwamba watu wameolewa hawaelewi. Watu wameolewa hapa, wengine wanasoma na wengine wanafanya kazi na wanafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa mchangiaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na taarifa aliyonipa Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, Serikali nenda mkakope mlete pesa hata akina mama wote wakasome, muwafundishe na urubani, mimi sina tatizo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mchango wa Kamati ya sekta husika. Mheshimiwa Serukamba amezungumzia awamu ya nne ya viwanda *(forth industrial revolution)*, niwaombe watendaji wa Serikali nendeni mkasome kitabu cha Ali Mufuruki cha *Tanzania Industrial Revolution Journey*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mbali na masimulizi haya kipindi tulichonacho kinakuja kuleta mabadiliko

ambayo hayatafuata huu mtiririko tuliouzoa wa kwenda uchumi wa kati au miaka 50 ijayo, mnaweza kuona mabadiliko ambayo yanaweza kuifanya Afrika kuwa China mpya. Sasa ili Afrika iwe China mpya tutahitaji watu wenye elimu walioandaliwa. Kwa hiyo, hali hiyo ambayo sasa ndiyo inazungumzwa katika kipindi cha miezi mitatu, minne mnapoona mtikisiko utaweza kuifanya Afrika ivamiwe upya, wanazuoni ndivyo wanavyoeleza. Sasa ili tuweze kwenda hivyo lazima Serikali iwekeze kwenye elimu ikimaanisha unapomaliza kuimarisha miundombinu ukimbie na kwenye rasilimaliwatu. Lazima walimu wetu wapewe uwezo mkubwa kusudi waweze kuhimili hali hii. Hatuwezi kukubali Afrika iende kwenye *industrialization* tukiwa sisi ni manamba, tunataka kuwa watu wa mstari wa mbele katika viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la shule binafsi. Jukumu la kutoa elimu ni la Serikali na suala la kutoa elimu unaweza kulilinganisha kama mzazi. Kwa wale waliotelewa zamani au waliozaliwa zamani mzazi ukizaa mtoto ulikuwa unampeleka kwa mtu akalee, sasa hizi shule binafsi ni walezi lakini mtoto ni wa Serikali. Unapopeleka mtoto wako kwa mlezi huyo mlezi anapoelemewa usimuachie mwanao. Ndiyo maana ukiangalia Serikali ya Zimbabwe pamoja na mitikisiko yake mfumo wa Zimbabwe ni imara kwa sababu kila mfanyakazi yeyote kwenye sekta ya elimu Serikali inajua umahiri wake na kuna kiasi fulani inampatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachoiomba Serikali wale wafanyakazi angalau mara moja kwa dhamana ya wenye shule; mmezisajili shule muwapatie kiasi fulani cha pesa hata 30%. Sisi Tanzania pesa tunazo hata kama hatuna benki tukakope. Watu wanaotoka kwenye migodi wanasema kuna dhahabu nyingi basi kachukueni dhahabu hiyo nenda sokoni kwenye soko la dunia kuna bei kubwa leta pesa muwape hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu walittoa kwenye aibu, watoto wa Tanzania walikuwa wanakwenda nchi jirani, wanasoma kwa shida, wanahangaika na wanajifunza tabia za ajabu lakini watu binafsi wakaja hapa

na kama nilivyosema shule hizi ni mali ya Serikali hawa wanalea tu lazima tuwasaidia. Sisi kwetu unampelekea ntukulu (zawadi) na usisubiri alie akuletee mtoto ameshakufa unakwenda kuangalia mtoto anaendeleaje. Sasa wewe mwenye mtoto ambaye ni Serikali mtoto wako kule analala njaa. Nenda kamchukue na kumchukua ni kumuwezesha huyu mtu aweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipowasaidia hawa wafanyakazi *by the time* tunarudi shule hazitakuwa na walimu na mfumo mzima utakuwa umeteketea, watoto tutawapelekea Uganda, Malawi au Kongo. Mtoto wako anatoka Kongo badala ya kusimulia mambo anakuchezea ndombolo na pesa zote ulizolipa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali wakati huu ni wa kusimama imara, pesa tunazo, kopeni muweze kuwasaidia watoto hawa kusudi watakapokuwa wanarudi shule wazazi waweze kukuta shule zipo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. JOHN P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipunguzia muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Zacharia Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nichukue nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote kwa miaka mitano ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano. Sisi ni waja wa Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu mafanikio makubwa kwa hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru kama maombi yetu ya kila siku.



Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuungana na Watanzania wote, viongozi mbalimbali kuliombea Taifa letu kwa janga hili la *Corona*. Ugonjwa huu ni tishio kwa dunia na kwetu sote tuna kila sababu ya kuungana ili kuweza kuliombea Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ana namna mbalimbali za kutukumbusha. Ni imani yangu hili ni kumbusho kutoka kwake na kila mmoja wetu anayo nafasi kwa namna mbalimbali kumrudia Mungu lakini pia kuwa na kauli ya pamoja ya kuliombea Taifa letu na dunia kwa ujumla. Rai yangu kwa janga la *Corona* ni kuwataka wadau mbalimbali kuendelea kutoa elimu kama sisi viongozi na vyombo mbalimbali lakini pia Serikali kuchukua jukumu la kupata vifaa kwa ngazi ya hospitali za kanda na hospitali za mikoa ili tuweze kukabiliana na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kwa kuwa ni Bunge na Mkutano wa mwisho, kwanza kabisa kwa namna ya pekee sana tuwaombe Watanzania wote waliotangulia mbele za haki. Mwenyezi Mungu ametuacha sisi amewaita ndugu zetu, anayo nafasi ya pekee sana ya kututaka sisi tujirudi na tujitazame kwa matatizo haya na majanga yanayotokea. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee tuwaombe ndugu zetu waliotangulia mbele za haki wakiwemo viongozi mbalimbali, Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzetu Mungu aendeleo kuwapokea na kuwarehemu katika nafasi yake kama muumba wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi kwa niaba ya Watanzania wote, Wanambulu kwa ujumla na kila mmoja wetu nimpungeze kwa jinsi alivyoliongoza Taifa hili. Nchi yetu ni hakika imepata nafasi kubwa sana chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Niwatake Watanzania tukubaliane kusiwe na uchaguzi wa Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

(Hapa kipaza sauti kilizimika)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay uhame kwenye hiyo sehemu *mic* yako imezima. Wataalam mliopo huko mpeni *mic* mojawapo zinayotembea ili kuepusha matumizi ya *mic* moja kwa Wabunge wawili. Kwa hiyo, mchango wako wa mwisho ulioshia neno uchaguzi haujasikia kwa hiyo uanzie kuanzia hapo ili Taarifa Rasmi za Bunge zikae vizuri. Mheshimiwa Zacharia Issaay. (*Makofi*)

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nimesema, kila mtanzania anakiri kuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli anafanya kazi kubwa sana, na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na viongozi wengine wote na wandaamizi na Wabunge. Wote wametimiza wajibu wao na taifa limepata hatua kubwa ya maendeleo, tungepaswa kusema kwamba Mheshimiwa Rais wala hana sababu ya kuchaguliwa tena tuendelee kuwa na Rais Dkt. Pombe Magufuli kwa miaka mitano ijao, hayo ni mawazo yangu na ninayazungumza hapa nikiwa wazi wazi kwa sababu ya kazi nyingi zilifanyika, mfano wa wazi upo Jimbo la Mbulu Mjini.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay kuna taarifa nimechindwa kujua ni Mheshimiwa nani, Mheshimiwa Susan Lyimo.

## T A A R I F A

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa kwamba, Katiba yetu ipo wazi inasema Mheshimiwa Rais atachanguliwa kila baada miaka mitano na kwa maana hiyo Mheshimiwa huyu anataka kutuambia kwamba tuvunje Katiba. Kwa hiyo nilikuwa nataka kumpa

taarifa kwamba jambo hili haliwezekaniki kwa sababu liko kikatiba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, umepokea taarifa hiyo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe umeshafika wenye akili wamesikia na kubaliana na kwamba hakutakuwa na uchaguzi kwa imani yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipoteze muda naomba nilindie muda wangu. Jambo la kwanza kabisa nitakalopenda kusema Mheshimiwa Ndalichako na Naibu Waziri na viongozi wengine wote. Naomba yafuatayo yaweze kuzingatiwa, tuboreshe elimu bila malipo kwa kuwa nchi yetu sasa tumepata mafanikio makubwa kwenye elimu bila malipo basi kunahitajika miundombinu na walimu. Lakini pia tuboreshe majengo mbalimbali ya shule yakiwemo yale ambayo yanachukua nafasi kwa walimu kama nyumba za walimu na madarasa kwa sababu uandikishaji umekuwa mkubwa kwa hiyo itahitaji walimu wengi na mchango mkubwa utatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalopenda kuzungumza katika ukatabati wa shule kongwe, kuna shule takribani tano katika halmashuri ya mji wa mbulu zimejengwa kati ya mwaka 1910 mpaka 1922 hususani shule za msingi. Tunaomba shule hizo ziratibiwe ili ziingizwe kwenye utaratibu wa kukarabati shule kongwe nchini, ili kujenga mazingira mazuri ya utoaji wa elimu katika taifa letu na halmashuri ya mji wa mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalotaka kusema katika halmashuri ya mbulu tulijenga madarasa ya *computer*, madarasa 14 hadi sasa sita hazijapata vifaa kwa maana ya *computer*. Kwa hiyo, tunaiomba serikali itume wataalam ili itupatie *computer* kwa ajili ya zile shule na shule zingine nchini wa ajili ya kuboresha mifumo ya TEHAMA kwa shule zetu na shule za misingi kwa ajili ya mahitaji ya wakati wa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamefanyika na serikali ya Awamu ya Tano, kila mmoja anakubishia hapa ni ubishani wa utashi kisiasa. Lakini yote yanaoneka mbele ya watazania na mbele ya wapenda maendeleo niitake Serikali ya Awamu ya Tano, na nimuombe Mwenyenzi Mungu aweze kuwarudisha tena viongozi hawa katika madaraka yao akiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wote kwa sababu wametembea nchi zima na mbulu wameitendea haki katika kutatua changamoto za wananchi kwa kila sekta. Mwenyenzi Mungu aendelee kulibariki Taifa letu tuendelee kuwa wa moja na Mwenyenzi alihepushe janga hili la corona Tanzania na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nashukuru kwa muda huu niliopewa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ajiandae.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kuniwezesha kunipa pumzi hizi, ambazo zimeniwesha mpaka leo nipo katika Bunge hili na ninaendelea vizuri. Lakini vilevile napenda kutoa pole kutoka na msiba wa Katibu Mkuu wetu Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa pole nyingi zimfikie mwenyekiti wetu, wanachama wetu, pamoja na familia ya marehemu. Hatuna cha kusema ila tunasema *Inna Lillah wa Inna Ilyhirajjun.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia vilevile napenda kutoa pole kwa familia ya Mama Rwakatare ambaye naye amekwisha tangulia mbele ya haki, tunasema Bwana ametoa na Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kushukuru Taifa kwa juhudi zake zinazofanya kutokana na janga hili lililotufikia la corona, kwa hiyo, tunatakiwa na sisi yale

tunayopewa na maelekezo ya watalaam tuyafuate. Lakini pia tumeshaambiwa kuda dawa za mitishamba tutumie majungu yale kujifukiza, tusiwe twajifukiza wakati tukienda kwa waganga wa kienyeji tukaenda kuomba mambo ya kiibilisi, lakini tujifukize ili tuweze kuepukana na gonjwa hili hatari la corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala zima la mitaala, sasa hivi katika shule za msingi kuna mtaala wa somo la ujasilimali. Kwa kweli somo la ujasiliamali ni nzuri na linamuandaa vizuri mwanafunzi pindi atakapokamaliza elimu yake aidha ya msingi, ya sekondari au na kuendelea. Lakini tatizo linakuja katika hilo somo la ujasiliamali utakuta kwa shule za msingi walimu hawana mwongozo, huwezi kufundisha bila ya kuwa na mwongozo. Kwa hiyo, tunaomba wizara ihakikishe kuwa inatoa mwongozo kwa somo hili la ujasiliamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vitendea kazi hakuna, wa mfano mwanafunzi anatakiwa labda ajifunise kushona, kupinda lesa, lakini mwalimu hana kitambaa, hana uzi, hana sindano. Je, mwalimu atalifundishaje somo hilo? Inamaana masomo yanafundishwa nadharia tu sio vitendo kwa hiyo tunaomba serikali ihakikishe tunapotoa mitaala ya masomo mapya kuwepo namiongo ambayo itaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la vitabu, katika Bunge lililopita tulipata taarifa au tulisoma au tulishangia vilevile kuhusu vitabu ambavyo vilikuwa havifai kwa ajili ya wanafunzi kusomea, vitabu vile vikaambiwa visitumike tena madarasani. Lakini cha kushangaza vitabu hivyo hivyo vinatumika shuleni kama vitabu vya ziada. Sasa napenda kuiuliza wizara je hivyo vitabu vimeshatolewa hayo makosa mpaka vikawe vitabu vya ziada? Si wanafunzi vilevile watakuwa wanajifunza vitu ambayo sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba wizara ihakikishe kuwa kama ilivyosema kuwa vitabu hivyo havifai basi visiwepo kuwa kama vitabu vya ziada. Kwasababu

mwanafunzi anapotumia kitabu cha ziada ana *material* anayopata ili viweze kumsaidia. Lakini vilevile katika uandaaji huo wa vitabu, wakati vitabu viliyokuwa vinatungwa walihusika watu wengi, kulikuwa na wataalamu kulikuwa na wahariri, kulikuwa na wachoraji picha, kulikuwa na wataalamu kutoka vyuo vikuu, walimu kulikuwa na kamati labda ya kamishina wa elimu na kadhalika katika kuvianda vitabu hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kilichotokea kutoka taasisi ya elimu kuna baadhi ya wafanyakazi waliochishwa kazi kutokana na ubovu wa vitabu hivyo. Watu wale wameachishwa kazi na mpaka leo wapo nyumbani na wengine bahati mbaya wamepata maradhi, wamepata *stroke* wengine vilevile wamekufa. Lakini katika hilo jopo la watu wote waliandaa wahariri na nini na nini kuna baadhi wanaendelea na kazi. Sasa ni kigezo gani kilichotumika kuwarudisha wengine kazini na kuwafanya wengine wasiwepo kazini na wakakosa haki zao. Tunataka waziri atuambie ni lini watu hao watapewa haki zao, ili weweze kujikimu kimaisha. Kwa sababu wapo waliofanya kazi miaka 10, 20 kuna ambao walikuwa karibu wanastaafu lakini watatu hao wameachishwa na hakuna walichokipata chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuzungumzia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nuru Bafadhili kengele imeshagonga. Ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mheshimiwa William Ole Nasha ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia jioni ya leo. Kwanza binafsi nipende kupongeza Wizara hii ya Elimu kwa kazi kubwa wanazozifanya, ikiwa ujenzi wa Madarasa na

Mabweni nchi nzima, ujenzi wa VETA Nchi nzima maeneo mbalimbali kwa kweli ni kazi nzuri nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda kwasababu muda wangu pia ni mchache. Nilikuwa napenda nichangie kwenye sekta hii ya elimu kwa uchache wake.

Kwanza tunapenda kuipongeza Serikali kwa kutu-*support* kwasababu tumejenga shule mpya tano za msingi na wametupa fedha kwa ajili ya kuziendeleza. Tumezisajili shule tano mpya lakini pia tunajenga shule saba za sekondari mpya ambazo mpaka sasa tumepata usajili shule tatu na zingine ziko mbioni kupata usajili nimuombe tu Mheshimiwa Waziri zile ambazo zipo katika Ofisi yake atufanyie wepesi ili sasa tuweze kuhakikisha kwamba wanafunzi ambao tunao walio wengi wasitembee umbali mrefu kuzifuata zile shule zingine kwasababu wanafunzi wanatoka kata moja kwenda kata nyingine ambako wanaweza kutumia karibu kilomita 12 mpaka 15. Kwa hiyo niombe tu Mheshimiwa Waziri alichukue kwa uzito wake kuhakikisha kwamba tunalitaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nilikuwa nataka kuchangia katika suala zima la *VETA*. Nakumbuka mwaka 2015 wakati wa Kampeni Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu alikuja pale katika Mji wetu wa Choma Chankola na akaahidi kuipanua na kuiendeleza ile *VETA* ambayo imejengwa na *World Vision* na nashukuru baada kuchaguliwa mwaka mmoja nilikuja kumuona Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Ndalichako kumuambia kuhusu hili la *VETA* yetu ya pale Choma, na alituma Timu ya Wataalamu ambao walikwenda kukagua na kwenda kuiona na kutoa baadhi ya mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliniita akaniambia Mheshimiwa Gulamali ile *VETA* yako ambayo ulikuwa unaihangaikia kwa muda mrefu sasa tumepata fedha 1.5 billion tunapeleka kwa ajili ya kupanua *VETA* hiyo ili iweze sasa kuendelea kutoa huduma kwa wakazi wa maeneo yenu hususan Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kwamba baada ya taarifa ile aliniambia niwasiliane na Mkurugenzi Mkuu wa VETA. Niliwasiliana naye na bahati nzuri pia Naibu Waziri alikuja kutembelea maeneo ya kwetu kule kujiridhisha ile VETA ambayo ilikuwa tayari imeshajengwa na alitembelea maeneo yote ambako aliona kwamba pale Choma Chankola panastahili kuendelezwa na alijiridhisha kwa asilimia zote kwasababu alimuuliza Mkuu wa Wilaya kwamba Je, Mkuu wa Wilaya VETA hii ya hapa Choma au tukaanzishe VETA mpya ipi tufanye? Lakini majibu aliyopewa na Mkuu wa Wilaya alisema hatuwezi tukaacha VETA hii tukaenda kuanzisha VETA mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini swali langu hapa nisaidie Mheshimiwa Waziri, kwamba watu hawa wa *World Vision* wamejenga VETA yenye madarasa manne pale katika Mji wa Choma. Lakini wamejenga jengo la ghala la mazao, wamejenga jengo la mashine ya kukamua alizeti, wamejenga jengo la mashine ya kukoboa mpunga, wamejenga nyumba ya watumishi, wamejenga kibanda cha mlinzi, wameweka kibanda na jenereta, lakini bado kuna wanafunzi wanasoma mpaka muda huu wako pale wanasoma, na mwalimu ameajiriwa ni wa Serikali wanafundishwa. Lakini cha kusikitisha wameanza kwenda kujenga VETA eneo lingine kabisa sababu tunawauliza ni nini wanasema lile eneo lilikuwa halitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika pale aliwauliza wenye VETA mna ukubwa gani wa VETA yenu wakasema tuna ekari 60. Yaani ekari wanazotaka wao VETA ni ekari 50 lakini hii VETA ya *World Vision* waliyojenga ina hekari 60. Sasa najiuliza tunaenda kujenga mpya eneo lingine unaacha hili kwasababu tu ya *influence* ya wafanya biashara ili waweze kufanya biashara zao za pale kwenye majumba yao. Nilikuwa nataka kumuomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati suala hili, aweze kulitatua kwa uharaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *otherwise* fedha zenyewe mlizotoa kwa awamu ya kwanza ni milioni 250 mnaenda



kujenga porini tumeanza kukata majani. Tumeanza moja halafu mnaacha huku majengo *infrastructure* haya tutayatumia kwa kazi gani. Kuna yule meneja wetu wa VETA pale Mkoani, hakuwahi hata kuja kukutana na mimi lakini kwa *record* ni huwa ana migogoro migogoro sana sio kwetu tu kuna sehemu nyingine alipotoka tena aliweka migogoro ya mivutano ambayo sio ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili hata wallkohamishia hakujawahi kukaa Baraza la Madiwani, likaamua VETA ikajengwe huko, sasa nashangaa nataka kumuambia Mheshimiwa Waziri katika kufanya *windup* yake hapa aweze kutuingilia kati atoe maelekezo kwamba ile VETA ambayo nilikuwa nikifuatilia kwa muda mrefu aielekeze kwasababu bado hatujafika mbali ndio kwanza tunafyeka mapori. Twende tukaendeleze kule ambako tayari hizi taasisi ambazo zimejitolea zinachukua fedha za Mataifa ya nje maana yake wanaondoka watayaacha haya majengo ambayo yatakuwa hayana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri hii VETA hii ambayo imejengwa na hawa watu wa Taasisi hii ya *World Vision* isipotee bure, majengo yasipotee bure, *infrastructure* ni nyingi ambazo zimewekezwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninyi kama Serikali muendeleze kwasababu wale *World Vision* wamewakabidhi ninyi kama Serikali, eneo la ukubwa wa ekari 60, majengo madarasa manne, nyumba za watumishi, majengo mengine ya mpunga, alizeti na kila kitu na majenereta makubwa kama hakuna umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walisema kwamba hakuna maji kuna mradi wa maji wa Ziwa Victoria unakwenda pale unataka nini. Tuna kituo cha Afya cha kutoa huduma sasa niombe tu Wizara waliangalie suala hili, tusiende kwenye migogoro. Lakini hata hivyo fedha zenyewe walizozitoa ya awamu ya kwanza milioni 250 hatuwezi kukimbia wala chuo hakiwezi kufanguliwa, sana tunapoteza ile hela na mwakani

tunaweza kupata au tusipate na mwaka unaokuja tunaweza tupate au tusipate. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bora kuweka pale ambapo tumeanzisha tuendeleze kuliko kwenda kuanza moja ambapo hatuna hakika kama tutafika mwisho.

Mheshimiwa naibu Spika, mwisho naunga hoja bajeti ya hii ya wizara hii kazi ni nzuri zinaonekana tunameona shule kongwe zimeboreshwa, tumeona veta zinajengwa, tumeona madarasa yanaongezwa niombe tu wizara iingilie tatizo ili itatue ili haya maisha mengine yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante sana kwa kunipa muda wako kuchangia jioni ya leo. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ajiande Mheshimwa William Tate Olenasha

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa nafasi pia naomba niwapongeze viongozi wetu Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake kwa kweli mmefanya kazi nzuri, natambua mjenga vyuo vya ualimu 26 hapa nchini, lakini pia natambua mjenga nyumba kwa ajili ya *staff* wetu wa udhibiti ubora 100, 55 zipo *under way* lakini natambua zaidi wapo walipeza kwamba hatuoni mkijenga matundu ya vyoo hakuna chochote kilichofanyika lakini natambua na nina wapongeza kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa kujenga matundu 9,712 kwa shule zote za nchi hapa Tanzania, ninawapongeza kwa kuwajali watoto wakike mmewajengea matundu ya vyoo 5539 na Me *character* umewajenga matundu ya vyoo 3645. Lakini walimu mmewajengea matundu ya vyoo 528 hongereni sana hizi ni juhudi ambao haipaswi kubezwa hongereni sana viongozi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza lakini kwasababu hii ni hotuba yangu ya mwisho au uchangiaji

wangu wa mwisho ninakupongeza na sana Mheshimiwa wangu Prof. Ndalichako kaka Mheshimiwa Olenasha nyie mmekuwa ni walezi kwangu. Lakini mmekuwa ni walezi kwasababu mmekuwa tayari kuvumilia hata yale tuliyougea nje ya utashi wetu au nje ya maadili yetu ya kazi. Mmlikuwa na vifua vipanda vya kupokea maoni yetu tuliwakasilisha hatukuchukia mliyachukua yote. Kwa kweli binafsi nawapongeza sana ahsante kwa kazi nzuri ya malezi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda nichangie kama ifuatavyo:- nitapenda nianze na suala la corona kwasababu ndilo lililopo ninaishukuru serikali kwasababu ilitambua nguvu kazi ya Taifa hili ni vijana, na wakaaza kufunga shule za misingi lakini namba mbili walifunga vyyo vikuu ninawapongezeni sana kwa kujali nakutambua nguvu kazi ya vijana.

Mheshimiwa naibu Spika, lakini katika suala hili la corona, sijui kila mtu ameguswa kwasababu sisi hata sisi tumefiwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Rwakatare ambaye ni mdau mkubwa kwenye sekta ya elimu. Lakini binafsi ni muhanga pia. Mdogo wangu jana ndiyo tumefanya *birthday* yake ya siku 14 kutoka *Magufuli Campas*, kwa kweli hata mimi ni mtu ambaye siweze kubeza haya yote tunayochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nina shida moja ambayo nilitamani sote tuielwe, iko hivi changamoto ziko nyingi na *Corona is real* yaani ni kitu ambacho kipo, ni kweli kila mtu ameguswa. Lakini suala langu liko mahali pamoja, Mheshimiwa Salome, tulia, suala langu liko sehemu moja. Kuna suala la malaria, nitapenda Bunge lako litambue *WHO* mwaka 2018 ilitoa taarifa ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Malaria kwa Tanzania, tumepata maradhi haya kwa wananchi milioni 11 kutokana na repoti ya *WHO* ya mwaka 2018, lakini katika hayo maambukizi ya Malaria tumepoteza nguvu kazi ya Taifa hili, Watanzania 80,000 walifariki mwaka 2018. Kwa hiyo, nikiangalia hili naona ni tatizo kubwa kuliko. Nafikiri basi

tunapoongelea *Corona* tusiache na hili kwa sababu hili ni janga namba moja kwa nchi ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi 32 za Afrika mwaka 2018 *WHO* imesema tumepata watoto ambao wanazaliwa *under birth* 875,000, yaani mtoto anazaliwa *pre-mature*. Kwa wamama sisi nilitamani tuchangie sana eneo hilo, lakini sioni. Naona tunavyokuwa *busy* kwenye *tweeter*, tunashindwa hata kutafsiri na kutoa miongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Rais ame-*recommend* hata kuna tiba, lakini huo Mkaratusi kule kijijini kwako inaitwa nini? Tuchukue nafasi hizo kutafsiri maelekezo ya Serikali tunayopewa kupeleka kwa wapiga kura wetu. Nilidhani hilo ndiyo jukumu letu la kwanza badala ya kukaa ku-*tweet*, kuhangaika, kutoa taharuki huku na kule. Nafikiri tupunguze hapo, tuchukue na haya ambayo tunaona ni kweli kabisa yanaua Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongee jambo lifuatalo: kwenye suala hili la *Corona* ninasikitika sana ninaposimama hapa mbele yako, kwanza samahani naomba nianze kwenye suala ambalo liliongelewa upande wa kule sikumbuki, lakini liliongelewa pale. Walisema kwamba *re-entry* ndiyo *big deal* yaani ndiyo njia ya kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliongozana na Mheshimiwa Lucy Magereli, naomba ikiwa nitasema uongo nipewe adhabu yoyote katika Bunge hili. Nilienda Namibia ambayo ni *one amongst the best countries* zinazo-*practice* hayo masuala ya *gender mainstreaming*. Mimi Nili-*lead delegation* lakini pia nili-*lead delegation* kwenda Kenya; nilienda kukaa chini tukajifunza *representation roles* za Wabunge Wanawake Kenya na nilikaa na *KEWOPA*, nili-*lead* hiyo misafara miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Namibia tukawaambia hebu tuambieni, kwa nini mmeshindwa ku-*achieve* hizi tatu? Wao wame-*achieve* 47% wakasema tunasikitika sana Chama Pinzani, *I mean Opposition* wanawalalamikia *Rulling Part*. Wao

walipeleka Muswada Bungeni wa kutaka *re-entry*. Sasa *opposition* inawaumiza sana, wakasema sasa hivi tunaandaa Muswada binafsi kwenda kupinga mawazo ya *Ruling Part*, wanatupoteza. Watoto kule hawasomi, imekuwa ni sehemu kama *nursery*, yaani hakuna kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yupo rafiki yangu mpendwa alinisimamia *Kitchen Party* yangu, Mzanzibar, nilimwuliza shoga yangu niambie, uliniambia kwamba unaenda kwenye *re-entry*, eeh vipi? Akaniambia shoga yangu nimeishia kukosa cheti na mume pia nimekosa. Akasema mimba tunabeba tumboni lakini mimba hiyo ya sisi Wabunge kweli tunabeba tumboni, lakini kwa hao wanafunzi msifikiri mimba yao wanaibeba tumboni, wao wanabeba mimba zao humu kichwani ndiyo kwenye shida. Huwezi ku-*concentrate* kutumikia mabwana wawili kwa wakati mmoja, haipo dunia kote. Tunataka *fifty fifty*; tutaipataje? Uteme mate, ubebe michanga, ubebe sijui udongo, nani kasema? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipinga sana, ninaipinga mno. Nilikuwa mshabiki, baada ya kutembea nchini Afrika, nimejiona nilikuwa mjinga sana. Kwa hiyo, naomba, Mheshimiwa Anatropia Theonesta yupo hapo, lakini Mheshimiwa Khadija yupo pale, mwulizeni Mheshimiwa Lucy Magereli, huko wanalia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijielekeze kwenye suala la *Corona* kwenye Chuo Kikuu cha Bungando...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mmasi, nadhani kuna taarifa kutokea Msekwa, sijaweza kujua ni sauti ya nani. Mheshimiwa Yosepher Komba.

## T A A R I F A

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimpe taarifa Mzungumzaji dada yangu

Mheshimiwa Ester. Tunapotetea watoto wa kike kurudi shuleni, hatumaanishi warudi na mimba zao, tunamaanisha wajifungue, waache watoto nyumbani uandaliwe utaratibu wa kuendelea na masomo yao. Kwa hiyo, kutema mate siyo shule, watajifungua majumbani, wataacha watoto au watatengenezewa utaratibu. Kwa hiyo, hilo linawezekana. Unapokuwa mama, unakuwa akili imetulia, unakuwa *serious* na masomo kuliko kitu kingine. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mmasi, unaipokea taarifa hiyo!

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu. Mheshimiwa Komba ambaye yuko Msekwa ni rafiki yangu mpendwa sana, lakini niseme tu kwamba siwezi kuipokea taarifa hiyo kwa sababu kwanza sikuwa naye kwenye msafara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa nchi ya Namibia wao walikuwa hawaendi na mimba, kulikuwa kuna kituo maalum (*re-entry*) yaani mtu akishajifungua ndipo anaenda kule shuleni. Ukifika mchana analetewa mtoto amnyonyeshe, sijui amfunge *pampers*, sijui afanye nini wakawa wanailaumu sana, imewapotezea muda wao. Unakuta mtu anagawa 80% ya muda wake kum-*attend* mtoto, 20% anaitoa kwenye shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea hapa, wenzenu wa huko wapo na ninasema *Hansard* inaandika, mje hapa mni-*correct* wakiwa hao wenzenu nilioenda nao kwenye hizo nchi. Sitaki kupoteza muda wangu kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Bugando, Chuo cha Bugando na St. Joseph nasikitika sana. Jana nimefuatwa na Mwenyekiti wa *TAHLISO* nchini Tanzania nyumbani kwangu saa nne usiku. Kilichopo Bugando leo, baada ya wanafunzi kutolewa madarasani kuambiwa kwamba mkapumzike

mpaka tutakapoonna hali ya *Corona* inaendeaje; leo hii wanafunzi wamelazimishwa kurudi mashuleni walipe *full fees*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo nikaenda kuhoji, *guideline* yenu iko wapi? Nilienda St. Joseph, nikaomba *guideline* ya kuwarudisha wanafunzi lakini naomba pia *permit* na nijue ni utaratibu gani ambao nyie mnautumia kutengua kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mikaambiwa kwamba watalipa ada (*full payment*) ya mwaka mmoja lakini ufundishwaji wake ni kwenye *WhatsApp group* kwamba Mwalimu huyo ataingizwa kwenye *group* hii, kama niki ni kipindi gani ataingizwa humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujiunga kwenye *group* la *WhatsApp* Bugando na St. Joseph ni shilingi milioni mbili mpaka tatu. Inasikitisha sana. Nasikitika mno kwa sababu hatukumaanisha hivyo. Mheshimiwa Waziri Mkuu hakutoa maelekezo ya hivyo. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapo mbele na *TAHLISO* niko nao hapo getini, nafikiri hata nyie waliwapigia simu; hili suala limeleta *crisis*. Hivi ninavyoongea, kumekuwa na sintofahamu na taharuki kubwa sana kwenye hivi vyuo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda niongelee suala la *research and development*...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mmasi, kengele ilikuwa imegonga, nilitaka umalizie hoja yako hiyo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu. Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shule za binafsi, Mheshimiwa Waziri kumekuwa na sintofahamu kwa waliokuwa shule hizi binafsi kutowalipa mishahara walimu kipindi hiki cha likizo ya magonjwa hasa Corona, kwa mfano tu ni Shule ya *Gods Bridge Mbalizi Primary, Caanani Secondary School* huko Mbozi, hii ni mfano mchache sana kati ya uongozi wa wamiliki wengi wa shule binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mimba za utotoni, tunaomba sana wanafunzi ambao waliacha shule asiwepo hata mmoja wa kutoingizwa kwenye programu ambayo Serikali mmekubali kusaini na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mabweni, bado kuna shida kubwa ya uwepo wa mabweni ya watoto hasa watoto wa kike kwa kukosa mahali pa kulala ukizingatia wengi wanatoka mbali na maeneo ya shule. Kumekuwa na kujitolea kwa wazazi wengi kujenga maboma na Serikali kushindwa kumaliza juhudi za wazazi, hivyo tunaomba Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madai ya walimu, kumekuwa na madai ya walimu hasa kupanda kwa mishahara, upandaji wa madaraja na pesa za likizo. Tunaomba sana Wizara iwatazame walimu kama hii ni haki yao ya msingi na ione kwa kutofanya hivi ni kupoteza *morale* ya kazi. Walimu wengi sana wamebadilishiwa vituo na madaraja kwa walimu hasa wale walikuwa shule za sekondari kupelekwa shule za msingi bila malipo ya mizigo na kuhakikishiwa malazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya vyuo; kumekuwa na ugumu wa upatikanaji wa mikopo hasa masomo ya sayansi kwa watoto wa kike kama Ilani ya Chama Tawala ilivyoahidi, kumekuwa na kuachia ngazi njiani kwa wanafunzi wa udaktari tunaomba sana Wizara hii isimamie.



Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri watoto wote wapate mikopo sawa kama raia wa Tanzania ili tusiwe na matabaka.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Uongozi Wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza Mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya elimu hasa kuboresha ufaulu na hata miundombinu ya madarasa na mabweni. Pia kwa kusimamia vizuri, ufaulu kwa elimu ya msingi na sekondari kwa Mkoa wa Mbeya umeongezeka na kuwezesha Mkoa kuwemo kwenye kundi la tano bora. Halmashauri ya Mbeya imekuwa inafanya vizuri kwa kuongoza kimkoa katika ufaulu wa elimu ya sekondari na pia kumekuwepo na mafanikio makubwa katika ujenzi wa sekondari mpya nne ikiwemo Sasyaka, Iyela, Inyala na Galijembe ambayo ni shule ya bweni kwa wasichana. Pamoja na hizo shule mpya, pia katika shule ya sekondari kumeanzishwa kidato cha tano na sita na kukamilisha *high school*/kwa kila Tarafa zote tatu za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, walimu bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa majengo ya nyumba za kuishi. Napendekeza Serikali kuendelea kushirikiana na wananchi

katika ujenzi wa nyumba za walimu iende sambamba na ujenzi wa maboma na pia madawati kwa wanafunzi wote. Ni muhimu kuhakikisha motisha kwa walimu ili kuboresha taaluma iwe ya kiushindani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na hata Afrika. Napendekeza pia Serikali itoe kipaumbele kwa kulipa madai ya malimbikizo kwa walimu ili kupunguza muda wa kufuatilia malipo yao na badala yake waelekeze muda zaidi kwenye kufundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la *Corona Virus (Covid-19)*, tumejifunza umuhimu wa teknolojia katika kufanya kazi na hata kwenye elimu. Napendekeza Serikali iongeze msukumo kwenye mafunzo ya teknolojia na pia elimu yetu ilenge mafunzo ya wahitimu wetu kuzalisha ajira badala ya kutafuta ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuboresha elimu nchini kwetu. Katika muda mrefu Serikali ilizitelekeza shule kongwe za Serikali bila kufanyiwa ukarabati wowote. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kufanya uamuzi wa busara wa kukarabati shule zote za sekondari na vyuo vya elimu na sasa majengo yamekuwa mazuri masafi na yanapendeza. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni Serikali iongeze katika upangaji wa mitaala uzingatie hali halisi ya mazingira ya ukosefu wa ajira hivyo basi mtaala ujikite katika elimu ya kujitegemea ambayo itamsaidia kijana anayehitimu mafunzo ya chuo atakuwa ana uwezo wa kujitegemea na kujijiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu maalum, kwa kweli sasa Serikali imesimamia vizuri kwani katika Mkoa wa Dar es

Salaam elimu jumuishi katika kila shule za msingi kumekuwa na watoto wenye ulemavu na hasa ulemavu wa akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na kubwa mno aliyofanya kwa nchi yetu kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Ndalichako, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri mno ya kuitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa shule kongwe na vyuo nchini; Serikali hii ya Awamu ya Tano imefanya kazi nzuri sana kuhakikisha shule kongwe nchini zinakarabatiwa zikiwepo za Mkoa wetu wa Iringa kwa shule za Ifunda, Lugalo, *Iringa Girls*, Malangali na Tosamaganga. Hii imesaidia sana kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi wetu na kufanya vizuri zaidi kuongeza na ufaulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wadhibiti Ubora wa Elimu, nipongeze Selikali kujenga Ofisi kwa Wadhibiti Ubora katika Manispaa 100 nchini. Ni imani yangu Halmashauri zote zitapatiwa ofisi. Lakini Idara hii ina changamoto kubwa sana katika Mkoa wetu wa Iringa na haina vitendea kazi kama *computer* na magari. Mkoa wetu una miundombinu mibovu sana wakati wa msimu wa masika na kufanya barabara nyingi kutopitika hivyo Wadhibiti Ubora wa Elimu wanashindwa kufanya kazi zao vizuri. Vilevile bado Idara hii ina uhaba wa wafanyakazi. Hivyo nilikuwa naomba Wizara itoe kipaumbele kwa Idara hii ili elimu yetu iendelee kuwa bora zaidi. Sijaelewa vigezo gani huwa vinatumika kupunguza hizi changamoto nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, gonjwa la Corona; niipongeze Serikali kwa kutoa tamko la kufunga shule zote

na vyuo nchini mpaka hali itakapotengemaa. Ningependa kupata ufafanuzi wa masuala yafuatayo:-

Moja, Serikali imetoa maelekezo kuhusu wanafunzi wawapo majumbani wasome kwa njia ya mitandao, *television* na radio. Je, kwa wale wanafunzi wasio na uwezo na kuwa na hivyo vyote wanajifunzia vipi?

Pili, je, kwa watu wenye ulemavu wanajifunza vipi? Kwa kuwa ulemavu wao unatofautiana?

Tatu, je, kuna mafunzo yoyote yatatolewa kwa watakoendesha mafunzo hayo ya njia ya mitandao?

Nne, je, kwa wanaotegemea kufanya mitihani yao ya mwisho utaratibu utakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa mabweni vyuoni na katika shule za sekondari; wanafunzi wetu kuishi nje ya vyuo au shule wamekuwa wakipata changamoto kubwa sana ukiwepo na kusumbuliwa na wamiliki wa nyumba walizopanga mitaani kutokana na kupandishiwa kodi na bili za maji, umeme na kadhalika na mimba nyingi sana hasa katika shule za sekondari zinaweza kusababishwa na ubakaji na kuathirika na gonjwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya elimu ya juu na elimu bila malipo; niipongeze sana Serikali kwa kutoa elimu bila malipo imefanya Watanzania wote waweze kupata elimu bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe pongezi nyingi kwa kuendelea kutoa mikopo kwa vijana wetu wanaosoma elimu ya juu. Kumekuwa na changamoto ya kukosa mikopo kwa vijana wanaosomea masomo ya sanaa, je, matatizo ni nini kwa sababu wote ni Watanzania. Vilevile hata hawa vijana wanapohitimu masomo yao kupata ajira imekuwa ni changamoto sana hata kama walibahatika kupata mikopo. Sasa hawa vijana wanarudisha vipi mikopo yao?

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe na iongeze madarasa ya kutosha kwa kuwa wazazi wamehamasika na elimu bila malipo ambapo imepelekea ongezeko la wanafunzi hivyo kusababisha upungufu wa vyumba vya madarasa. Hivyo Serikali itenge fedha za kutosha ili kujenga madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika mitaala hususan ya sekondari iwe ambayo ina fani za kuwafundisha wanafunzi hasa kwa vitendo, kwa mfano ushonaji, uashi, makenika, upishi na kadhalika ili wanafunzi hao wanapomaliza kidato cha nne wawe na uwezo wa kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika shule zetu nyingi hazina maktaba pia vitabu vya kujisomea, hivyo itenge fedha za kutosha kujenga maktaba na kuweka vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa walimu wa shule za binafsi iweze kutenga fungu la dharura ili kuweza kuwalipa mishahara kwa kuwa mishahara yao inategemea ada ambazo kwa sasa wazazi hawawezi kulipa sababu ya Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iajiri walimu wa kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji makubwa ya walimu katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijenge mabweni ya kutosha hususan katika vyuo vikuu ili wanafunzi

waweze kukaa katika maeneo ya chuo na kujisomea bila bugudha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri Serikali iboreshe miundombinu katika shule za msingi, sekondari na vyuo vyetu vyote hapa nchini ili viweze kutoa elimu bora na sio bora elimu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi nchi nzima kwenye shule *almost* zote. Shule ya sekondari inakuwa na mwalimu mmoja au wawili kwa madarasa saba. Tunawezaje kuhamasisha watoto wasome masomo ya sayansi wakati hakuna walimu wa sayansi? Tunawezaje kwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda wakati wanafunzi hawafundishwi sayansi shuleni? Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha walimu wa sayansi walioko mitaani wanaajiriwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na idadi ya wanafunzi watakaopata mikopo kuongezeka kufikia 54,000 bado wanafunzi wengi maskini wanakosa kupata elimu kwa sababu ya kukosa mikopo ya elimu ya juu. Watoto wengi wana ndoto za kufika mbali kitaaluma lakini wanaishi vijijini wakisononeka kwa kukosa mikopo. Ni lini Serikali itahakikisha watoto wote wa Tanzania maskini wenye ndoto ya kusoma wanasoma kwa kupata mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya mrejesho ya mikopo bado *speed* ni ndogo sana na hili ni tatizo sana kwani wangekusanya zaidi wangeongeza idadi ya wanaohitaji mikopo. Nini kikwazo kinachosababisha kukusanywa kwa mikopo? Nini mkakati wa uhakika wa Serikali kukusanya mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetenga shule moja kila Wilaya kwa ajili ya kupokea watoto wenye mahitaji

maalum (walemavu) tangu mwaka 2017. Mpaka leo hizo shule hazina mazingira rafiki kwa watoto hao. Ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya shule hizi ili hawa watoto wapate elimu kama wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi hazina walimu wenye taaluma ya kutoa elimu maalum kwa watoto wenye mahitaji maalum. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inaonesha walimu wa kutosha kwenye *specialization* ya mahitaji maalum?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na janga la Corona wanafunzi wamerudi nyumbani na haijulikani lini watarejea mashuleni, ni vema Serikali ikabuni mfumo wa kutoa elimu kwa watoto wetu kwa njia ya redio na *television* ili watoto waendeleo kuelimika kwa njia mbadala na hasa wale ambao walikuwa kwenye mwaka wa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kaliua kwa muda mrefu tumeomba tujengewe Chuo cha *VETA* ndani ya Makao Makuu ya Wilaya yetu ili kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ufundi na stadi za kazi. Nini mkakati wa Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Kaliua?

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la walimu wanaojiendeleza kimasomo wanaporudi hawapandishwi madaraja wala kurekebisha mishahara yao. Wapo walimu wamekaa tangu mwaka 2013 mpaka leo hawajawahi kupandishwa hata hatua moja, hili linawakatisha tamaa na kuffisha juhudi za kazi yao ngumu yenye changamoto kibao na mbaya zaidi ndani ya Wilaya ya Kaliua kuna walimu walipandishwa vyeo mwaka 2017 lakini mwaka 2019 walinyang'anywa barua zao bila maelezo yoyote. Naomba Serikali ifuatilie kwa karibu na kutoa ufafanuzi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuatilie kwa karibu ukaguzi unaofanywa kwenye shule za *private*. Kumekuwepo na tabia ya wakuu na walimu wa shule hizi kuwapanga wanafunzi wafiche madhaifu mengi ya shule zao pale wanapokuja wakaguzi. Hili ni tatizo kubwa sana.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Corona na matokeo mabaya yajayo baada ya Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kifupi, sote tunaelewa janga hili la Corona kila kona ya nchi shule zinafungwa na zinaendelea kufungwa, naomba Serikali hii itenge bajeti ili kunusuru matokeo mabaya yajayo ukizingatia hali ya Corona, watoto wengi hawajisomei kutokana na hali ya maisha ni ngumu na wazazi wako *busy* kutafuta pesa ili kulisha familia katika kipindi hiki cha Corona ambacho hali ya uchumi ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenge bajeti kunusuru wanafunzi bajeti kusaidia kuendesha programu za kielimu kwa watoto waliopo majumbani kupitia *TBC* na Redio Tanzania zisaidie kuwarudisha watoto kupitia *tv* na redio itakayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe ahueni ya kupunguza kodi kwa wamiliki wa mitandao ya simu ili kupunguza gharama za bando ili wanafunzi wapakue na kusomea kupitia simu za kiganjani.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja na kumpongeza sana *comrade* Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba hii yote sijaona katika mpango wa uanzishwaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi (*VETA*) Wilaya ya Wanging'ombe. Katika ziara ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Njombe Aprili, 2019 alikubali ombi letu wananchi wa Wanging'ombe kutoa majengo ya mradi wa ukarabati kipande cha barabara Makambako/Igawa yaliyopo Wanging'ombe kuwa Chuo cha *VETA*. Nilikuandikia na ukatuma watalaam wako. Nilitarajia kuona kitu kwenye hotuba yake.



Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri unipe jibu ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa lini. Tayari Wizara ya Ujenzi kupitia Meneja wa *TANROADS* walishakabidhi majengo hayo.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwako kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia sehemu moja tu, nayo ni juu ya elimu ya ufundi. Elimu ya ufundi ni elimu muhimu sana katika nchi kama ya Tanzania ambayo inaelekea kwenye ujenzi wa viwanda. Hivyo natoa ushauri kwa Serikali yetu kuimarisha Vyuo vya Ufundi kila Wilaya ili kufikia azma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuongeza fedha kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndlichako pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa William Ole Nasha kwa kazi kubwa wanayofanya katika jukumu zima la kusimamia utoaji wa elimu bora nchini bila kuwasahau Dkt. Akwilapo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Naibu Katibu Mkuu wote pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu wanafanya kazi nzuri sana. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, napongeza sana. Kuna tatizo kwa baadhi ya wanafunzi wengi kukosa mikopo na mbaya zaidi vijana wengi ambao wanakosa mikopo wanatoka kwenye familia ambazo

hazina uwezo, baadhi yao wamekuwa wakiacha kuendelea na masomo na kurudi nyumbani. Nashauri ni mhimu kupitia vizuri fomu zao za rufaa za mikopo ili kuwabaini hawa watoto wa maskini au turudi kwenye kigezo cha ufaulu yaani *division one* kwa masomo ya sanaa na angalau *division two* kwa masomo ya sayansi. Hii itawasaidia vijana wetu kujua mapema kwamba ana sifa ya kuomba kuendelea na masomo ya chuo kikuu au watafute vyuo vingine visivyo vya *degree*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la ugonjwa wa *Corona viruses 2019* ambalo limeathiri ratiba za masomo na masomo kwa wanafunzi wa ngazi zote na mpaka sasa haijulikani Corona itaisha lini ili wanafunzi wetu warudi mashuleni au vyuo. Shule zetu na vyuo vyetu vingekuwa vimeunganishwa na mtandao wa *internet* na wanafunzi wote wangukuwa na ujuzi wa kutumia *computer* na *internet* wangeweza kufundishwa *online* wakiwa nyumbani kama nchi za wenzetu zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nashauri sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha kuwa shule na vyuo vyetu vinakuwa na somo la *computer* na vijana wetu wajue kutumia na kuanza kuwatumia mazoezi na kazi mbalimbali kwenye *email* zao na wakishafanya hizo kazi zitumwe *online*. Hii itasaidia kama njia mbadala kunapotokea tatizo kama hili la Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo la Corona baadhi ya wamiliki wa shule binafsi wameshawaandikia walimu wa shule zao kuwa hawatawalipa mishahara walimu kwa kuwa hawapo kazini na kuna waajiri wamewapa walimu wao likizo bila malipo, hii ni unyanyasaji. Wanafunzi wanaosoma katika shule hizo wamelipa ya robo muhula au nusu muhula sasa ni kwa nini walimu wasilipwe mshahara wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kama ifuatavyo; kwa kuwa shule zimefungwa na shule za binafsi wanategemea ada za wanafunzi ndio walipe walimu mishahara na sasa ada hizo hazipo, naomba Serikali iwasaidie ili wapate mikopo kutoka kwenye mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa udhibiti ubora wa elimu wa Halmashauri ya Mji wa Njombe hawana gari naomba Serikali iwapelekee gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba Serikali iwaongeze walimu mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi hoja ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana Mungu kwa uzima na afya aliyotupa mpaka sasa hivi, maana hata sasa Mungu ametusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maongozi yake na maelekezo kwa Wizara hii na hatimaye kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kujitoa kikamilifu na kwa dhati kuitumikia nchi hii kupitia Wizara hii. Mawaziri hawa si watu wa kusemasema sana, lakini ni Mawaziri wa vitendo na ndio maana kuna mabadiliko makubwa kwenye Wizara hasa kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule na usimamizi wa ubora wa elimu yetu. Hongereni nyingi sana pamoja na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeze Wizara kwa kutupa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Cuo cha Maendeleo ya Wananchi Malampaka, ujenzi unaendelea, kasi tu sio ya kuridhisha sana kwa maana ujenzi huu umeanza muda mrefu na pengine ujenzi ungekuwa

umeshakamilika sasa. Niwapongeze pia kwa kutukamilishia jengo letu la Udhhibiti Ubora Wilaya ya Maswa, lakini bado ofisi hii ina uhitaji mkubwa wa vifaa kama vile *photocopy machine* na vifaa vingine. Pia gari lililopo kwa ajili ya ufuatiliaji ni la zamani sana na linaharibika mara kwa mara. Naomba Serikali iangalie kutupa gari na vifaa kwa ajili ya ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mradi wa huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni, pesa zilitolewa kwa kila shule kwa ajili ya mradi huu bado hazijatumika kwa sababu wataalam wetu huko Wilayani wanashindwa kuziingiza kwenye mfumo wa matumizi unaojulikana kama *FAS* kwa sababu zilikuja nje ya bajeti. Pesa hizi ni muhimu zitumike ili kuondoa tatizo la miundombinu ya maji, afya na mazingira kwa shule zetu. Naomba tatizo hili litatuliwe haraka ili fedha hizi ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapunjo kwa walimu; walimu waliopandishwa madaraja Juni, 2014 walirekebishiwa mishahara yao Novemba, 2014 lakini hawakulipwa mapunjo yao kwa miezi ya Juni, Julai, Agosti, Septemba na Oktoba. Mpaka sasa walimu hawa hawajalipwa mapunjo hayo. Naomba walimu hawa walipwe stahili zao. Pia kuna walimu waliostaafu, lakini nao hawajalipwa pesa za kurudi kwao, naomba walimu hawa pia walipwe kama utaratibu unavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa walimu; Wilaya ya Maswa tuna upungufu mkubwa wa walimu kwa sababu ya kuhama, ama kustaafu au kuachishwa. Mfano kwa upande wa shule za sekondari mahitaji yetu ya walimu Kiwilaya ni walimu 739 lakini tulionao ni 493. Upungufu ni walimu 246 ambapo walimu wa sayansi wanaokosekana ni 146 na walimu wa sanaa ni 100. Shule za msingi ni hivyo hivyo tuna upungufu mkubwa. Naomba Serikali itakapoajiri walimu wa sekondari ione umuhimu wa kutupangia walimu ili kupunguza upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali pia irejeshe utaratibu wa Wilaya kuridhia kuhama kwa walimu. Utaratibu wa sasa kwamba Wilaya hairuhusiwi kuzuia uhamisho wa walimu utaendelea kufanya baadhi ya maeneo ya nchi yetu yaendeleo kuwa na upungufu wa walimu kwa sababu ya maeneo hayo kutokuwa rafiki sana kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena na naunga mkono hoja.

**MHE. WILLY Q. QUAMBALO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru Wizara hii kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi chini ya mpango wa *EP4R* - Endabash Sekondari (jengo la utawala), Gongali Shule ya Msingi (madarasa), Welwel Sekondari (bweni), Banjika Sekondari (madarasa), Mangola Sekondari (madarasa na nyumba za walimu). Miundombinu hiyo imesaidia sana wanafunzi na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, eneo la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu bado kuna changamoto ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaostahili. Bado kuna wanafunzi wanaotoka kwenye familia duni. Wako wanafunzi wa familia hizo wanasoma kwa shida sana kwa kukosa mikopo. Niishauri Serikali inapotoa mikopo izingatie vigezo na watoto wanaotoka kwenye kaya hizo waangaliwe zaidi

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, udhibiti wa ubora wa elimu ni jambo muhimu sana na niishukuru Wizara kwa kujenga jengo la wataalam wa ubora wa elimu Wilayani Karatu. Niombe idadi ya wataalam hao iongezwe ili kufikia shule nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, watoto wa kike wanaopata bahati mbaya ya kupata ujauzito mashuleni wapewe fursa ya kurudi darasani kuendelea na masomo. Kinyume na hapo wasichana hao watakuwa wamepoteza nafasi ya kujenga maisha yao.

**MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri pamoja na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza kwa kupanga kuachana na utaratibu wa *alternative to practicals*. Utaratibu huo umedumaza ukuaji na ufundishaji wa sayansi katika shule zetu. Utaratibu huo pia ulikuwa hauwezi kuwafanya wanafunzi kuelewa sayansi badala yake uliwaandaa kukariri!! Haiwezekani kusoma sayansi kwa kukariri, hata ubunifu hauwezi kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna watu wana vipaji vingi sana vya ubunifu. Hata katika kipindi hiki chenye changamoto ya Corona kuna kijana anaitwa Brighton Katabazi amebuni na kutengeneza roboti ya kukaa mlangoni kunawisha mkono watu na kuwafungulia mlango. Tatizo ninaloona ni *COSTECH* kutokuwa na *outreach programme* au mbinu za *extension* kuvifikia vipaji vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ianzishe utaratibu wa kuwatambua, kuwafuata na kuwasaidia. Nitaomba Mheshimiwa Waziri aweke utaratibu wa kuwafuata wabunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, kwanza, Serikali ipeleke fedha za wadhibiti ubora. Mwaka 2018/2019 ilikuwa ni bilioni 1.5 na bajeti ya 2019/2020 zilitengwa bilioni moja. Kuna changamoto nyingi huko kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tuliomba kuwe na *separate vote* kwa Bodi ya Mikopo na bado haijatekelezwa. Nashauri itekelezwe kwani Wizara inabakiwa na fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, utekelezaji hafifu wa fedha za maendeleo. Ukiangalia randama fedha za nje uletwaji wake si mzuri ni 13.2% tu hadi Machi, 2020. Ningependa kujua sababu ni nini. Pia nashauri basi fedha za maendeleo zingetoka katika vyanzo vya ndani kwa kuwa miradi mingi haitekelezwi. Kwa mfano mwaka wa fedha huu kati ya miradi 40, ni miradi mitano tu imepata fedha hadi 50%. Miradi 24 haikupata kabisa fedha. Hii ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kutokana na janga la Corona, Serikali itenge bajeti ya dharura kwa ajili ya sekta hii kwa ajili ya miundombinu ya madarasa na miundombinu ya teknolojia. longezwe zaidi ya 30% ya bajeti. shule za Serikali wamekuwa waathirika wakubwa; itenge fedha kwa ajili ya ku-*subsidize* kwenye sekta za habari kwa mfano *tv*, redio na *bundle* kwenye *online* na visimbuzi ili walimu na wanafunzi na wazazi ili waweze kuimudu na ufundishaji na ujifunzaji uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwekeza pia kwenye *distance learning* kwa kutumia *flash*, redio za *solar* pia na kanda za kaseti kwa kujifunzia, punguzo kwa simu janja liangaliwe.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni yangu juu ya Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nina mambo machache ya kuishauri Serikali hasa namna ya kuboresha masuala yanayohusu elimu hasa kipindi cha janga la Corona lililoikumba dunia na hasa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza athari za ugonjwa wa Corona kwenye elimu, kufungwa kwa taasisi zote za elimu msingi mpaka chuo. *About* milioni 14 ya wanafunzi wa msingi na sekondari wapo nyumbani kwa sasa na hawajui hatima yao ya kurudi mashuleni. Nashauri Serikali iandae elimu mtandao ili wanafunzi waweze kuendelea kusoma wakiwa majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara iko tayari kutenga bajeti kwa ajili ya elimu mtandao? Stahiki za walimu hasa wa shule za *private*, tunafahamu wamiliki wa shule za *private* wanategemea ada ili waweze kulipa mishahara. Nashauri Serikali iwakopeshe wamiliki wa shule na iwawekee dhamana kwenye taasisi za fedha ili wapate fedha ili wakawalipe walimu mishahara yao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari kwa watoto wenye ulemavu au wenye wazazi wenye ulemavu; Wizara ina mpango gani kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata elimu wakiwa majumbani kupitia mitandao na TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa walimu; uwiano kimataifa ni 1:25, lakini repoti ya HakiElimu inaonesha uwiano ni 1:114, kuna upungufu wa walimu 47,000 kwa shule za .... tu. Hali ni mbaya sana hata kwa wahadhiri wa vyuo, Tanzania ina 25% ya wahadhiri wenye Shahada ya Uzamivu (*Ph.D*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali itenge fedha na utaratibu wa kuhakikisha inaongeza ajira kwa walimu kwa kuhakikisha ajira mpya zinatangazwa kila mwaka kisheria.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki kuanzia mabweni kwenye shule za sekondari za Nelson Mandela, Mkuyuni na Ngerengere, uboreshaji na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari, Matuli madarasa mawili na maabara tatu, Ngerengere madarasa nane, maabara tatu, Mkuyuni vyumba vya



madarasa kimoja vitatu vya ukarabati, shule ya sekondari madarasa mawili na nyumba ya walimu ya familia sita, ujenzi wa madarasa na maabara katika shule za sekondari za Mikese, Kinole, Kirika, lwata, Mkulazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashukuru kwa uboreshaji wa vyumba vya madarasa vya shule za msingi kadhaa katika Jimbo kama vile Fulwe, Newland, Mikese, Mkuyuni, Mgumbwe, Kiruna, Madamu, Kirke, Njia Nne, Matera, Kidunda, Baggio, Hewett, Gozo, Mheshombeho, Subways na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizo naomba kushauri Serikali ilinifanye kazi zaidi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tunaomba ujenzi wa Shule ya Ufundi VETA katika Halmashauri ya Morogoro katika Kijiji, Kata na Tarafa ya Ngerengere kwa kuwa tuna zaidi ya hekta 300 kwa ajili ya miundombinu ya elimu tuliyopewa na Serikali yetu baada ya maombi ya Mbunge wao Mheshimiwa Mgumba kukubali na Serikali. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kujali watu wa Jimbo langu kwa kutoa ardhi hiyo ambayo kulikuwa na habari kutokana na ufinyu wa ardhi Ngerengere.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba Serikali iendelee kutuunga mkono wananchi wa Jimbo hili katika ujenzi wa mabweni kwenye shule zetu za kata zote 14 kwa kuwa watoto wanatoka mbali sana kutokana na hali ya kijijografia ya maeneo yetu. Mfano umbali wa kutoka .... mpaka Makao Mkuu ya Kata Kidugalo ni zaidi ya kilometa 65, umbali wa Kidunda mpaka Makao Mkuu ya Kata ni zaidi ya kilometa tatu, Usungura Kidunda zaidi ya kilometa 50, Mbarangwe na Tununguo ni zaidi ya kilometa 20 na inatenganishwa na Mto Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, pia naomba Serikali ikague haraka na kutoa kibali cha kuanza kidato cha tano na sita katika shule yetu ya Nelson Mandela ili kuanza kidato

cha tano na sita na pia kumaliza vyumba vya madarasa vya kidato cha tano na sita katika Shule za Sekondari za Mkuyuni na Ngerengere ambazo ni Makao Makuu ya Tarafa ili na sisi tuwe na angalau shule tatu katika Jimbo na Halmashauri yetu ya Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna hata shule moja ya kidato cha tano na sita katika Jimbo zima ambalo lina shule za sekondari zaidi ya 30. Nimenza mimi na wananchi wenzangu ujenzi wa madarasa hayo na katika hali hiyo, nimeshapeleka matofali 8700 za *block*, mifuko 100 kila shule illi kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango katika suala hili la Corona. Naomba kushauri shule zetu za umma kutoa mitihani kwa njia ya mawasiliano ya magazeti, mitandao ya kijamii, redio na *tv* kila wiki au kila mwezi ili kuwaweka na shughuli watoto wetu na kuwapima uwezo wao wa kujifunza majumbani, hasara ya kuwaacha muda mrefu bila kufahamu huko nyumbani kama wanachosoma kinawasaidia na kina tija katika masomo yao kwani hatujui huu ugonjwa utaisha lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kushauri wanafunzi wa elimu ya juuu wa Shahada ya Pili na ya Tatu kuendelea na masomo yao kupitia elimu ya mtandao kwani kuna madarasa ya elimu mbalimbali na walimu wao kupitia mtandao ili kupunguza hasara kwa Serikali ya kuwa na wahadhiri bila kazi na pia kuwapa nafasi wahitimu wetu kuendelea na masomo na kuwapunguzia muda mrefu wa kumaliza kozi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa elimu kwa Watanzania walio wengi na hasa kwa uongozi na maelekezo yake katika kipindi hiki cha Corona na kuwatia moyo wa kuendelea kuchapa kazi ili kujenga nchi yetu na vipato vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa maandishi kwenye hoja iliyoko mezani ya hotuba ya bajeti ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Naibu wake Mheshimiwa William Ole Nasha; Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu; pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kuifanya katika kuboresha mazingira ya utoaji elimu na mazingira ya kujifunzia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba nichangie hoja iliyoko mezani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa janga la ugonjwa wa Corona limepelekea shule zote nchini kufungwa kwa muda, nashauri Serikali iwekeze katika matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano ya kielektroniki kutoa elimu kwa wanafunzi wa ngazi zote wakiwa majumbani wakati huu wa ugonjwa wa Corona. Nashauri redio, televisheni na mifumo mingine ya mawasiliano ya mitandao ya jamii itumike kuwafikishia wanafunzi wetu masomo wakiwa majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo hata shule binafsi zinafanya sasa hivi na sioni kwa nini Serikalil isichukue uzoefu kutoka shule binafsi na kuwaagiza walimu wetu ambao kwa sasa wanaendelea kulipwa mishahara wakati wanafunzi hawako mashuleni kusoma, waandae na kutoa elimu kwa njia za kielektroniki kwa kadri itakavyowezekana. Nashauri TBC 1 redio na TBC1 tv ambavyo ni vyombo vyetu vya umma vitumike kuandaa na kutoa elimu kwa kurusha vipindi ili wanafunzi wajifunze wakiwa majumbani wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba pia nichangie kuhusu suala la elimu ya awali. Katika bajeti iliyopita nilichangia pia kwamba Serikali iwekeze kwa nguvu zote katika utoaji wa elimu stahiki katika ngazi ya elimu ya awali (*Early Childhood Development Education - ECD*) kwa watoto wadogo wanaoishi mbali na shule za msingi vijijini na ambao wanasoma kwenye shule za awali zilizoanzishwa na wazazi bila kuwa na walimu wenye ujuzi. Katika shule hizi za awali, kuna tatizo kubwa la walimu wanaofundisha bila kuwa na taaluma ya elimu ya awali. Wazazi ndio waaajiri wao na huwatumia vijana wao (wa kike na wa kiume) ambao ni *failures* wa darasa la saba au kidato cha nne na ambao hawajapata mafunzo yoyote ya ufundishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iwekeze katika kutoa elimu kwa walimu hawa ili waweze kuwa na ujuzi wa kuwaandaa ipasavyo watoto wadogo kujunga na shule za msingi.

Nashauri katika kila eneo (iwe kitongoji ama kijiji ama mtaa) palipo na shule ya awali ambayo haishikani na shule ya msingi au shikizi yenye walimu wa Serikali waliosomea, Serikali ichukue jukumu la kuwajengea uwezo, hata kama ni kwa kupitia mafunzo ya muda mfupi wakiwa kazini ama wakati wa likizo (*on the job training*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nashauri Serikali iwape shule hizi za awali vitendea kazi kama vitabu vya kiada na ziada na izisimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba pia niipongeze Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa elimu msingi bila ada. Kwa kuwa mpango huu umekuwa na tija kubwa sana katika kumpa kila mtoto wa Tanzania fursa ya kupata elimu hadi kidato cha nne bila ada; naomba sasa Serikali iende mbele zaidi na kupanua elimu bila ada hadi kidato cha sita ili wazazi maskini wenye watoto wanaofaulu pia waondokewe na mzigo wa ada kwenye ngazi hiyo ya elimu ya sekondari. Watoto wanaofaulu *A-Level*, elimu ya chuo kikuu wataipata kupitia mpango wa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne na mwisho, naomba niishauri Serikali waongeze bajeti ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mashuleni kuanzia madarasa, nyumba za walimu, maabara, mabwalo ya kulia, maktaba, majengo ya utawala sambamba na kutoa usafiri kwa shule za sekondari zilizoko katika mazingira magumu kama ilivyo kwa shule nne za Jimbo langu la Longido ikiwa ni pamoja na lekule girls secondary school, lake natron flamingo, Matale na Enduimet.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na ahsante kwa kupokea mchango wangu.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Ndalichako pamoja na timu yake, kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ufanisi na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika uhaba na uchakavu wa miundombinu, kwanza niipongeze Serikali yangu tukufu kwa kutoa fedha kwa baadhi ya shule za msingi na sekondari kwenye Jimbo langu la Lushoto. Naishukuru sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Mwenyezi Mungu ampe siha njema na umri mrefu ili aendelee kuwatumikia Watanzania. Kwani Rais wetu huyu ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Ahsante Mungu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi kubwa inayofanywa na Serikali ni imani yangu kubwa sasa kuwa katika Jimbo la Lushoto maboma, *hostel* na maabara zitatengewa fedha za kutosha kwenda kujenga na kumalizia katika shule zifuatazo; Sekondari ya Malibwi haina hosteli na maabara; Sekondari ya Gare haina hosteli, maabara pamoja na maboma; Sekondari ya Ubiri, hosteli, maabara pamoja na kuongeza maboma; Sekondari ya Kitara, hosteli, maabara pamoja na kuongeza maboma; Sekondari ya Lushoto hosteli, maabara pamoja na maboma; Mkuzi Juu Sekondaro hosteli na maabara; Kwai Sekondari hosteli na maabara; Kwemashai

Sekondari, hosteli na kumaliza maabara; Mariamu Mshangama Sekondari hosteli na maabara; Ngwelo Sekondari hosteli na maabara; Mlongwema Sekondari hosteli na maabara; Mdando Sekondari hosteli na maabara na Mbwei Sekondari hosteli na maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lushoto lina sekondari zaidi ya 25 na hizi nilizoziorodhesha ni baadhi tu ya shule ambazo zikipata hosteli tutakuwa tumewasidia sana watoto wetu hasa watoto wa kike kwani ndio wanaopata majanga ya mimba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali yangu tukufu iongeze walimu katika mashule yetu na tunaposema tunaelekea mapinduzi ya nne ya viwanda lazima tuandae miundombinu yetu ya majengo ya madarasa, maabara zetu ziwe na vifaa, hosteli zetu ziwe za kisasa pamoja na walimu wawe wa kutosha, yakikamilika haya yote tutakuwa na uhakika wa kuandaa watu ambao wapo tayari kwa kwenda na kasi ya mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ipokee maoni na ushauri wanaotoa Wabunge kutokana na changamoto wanazokutana nazo kwenye mashule ambayo yapo katika majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali yangu tukufu iwape vifaa vya kutosha Ofisi ya Udhhibiti Ubora wa Elimu kwani watu hawa wanafanya kazi nzuri sana, lakini wanapata changamoto ya vifaa hasa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia uhai na leo kuniwezesha kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa

hatua anayoendelea kuchukua katika mapambano haya ya janga la Corona, hakika mwongozo wake unaendelea kutujengea imani na kutuondolea hofu kubwa inayoikumba jamii yetu. Vilevile nimpongeze kwa kuwapatia vijana wetu elimu bila ya ada, hatua ambayo imetuongezea uwezo wetu wa kupambana na adui ujinga. Kwani sasa watoto wa wanyonge wengi wameweza kumudu kupata elimu itakayowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.

Mwisho naomba pia kumpongeza Mheshimiwa Ndalichako - Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuonesha uwezo mkubwa katika kusimamia wizara hii, sambamba na watumishi wote katika Wizara hii, hasa Baraza la Mitihani kwa kudhibiti uvujaji wa mitihani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada za pongezi zangu hapo juu sasa naomba kuishauri Serikali yangu mambo yafuatayo kwa maslahi mapana ya nchi yetu na kwanza ni suala la upungufu wa walimu. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali katika kuboresha miundombinu ya shule nyingi nchini, bado tunalo tatizo kubwa la uhaba wa walimu hasa kwa shule za msingi zilizo vijijini mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Lakini katika hili wapo walimu ambao Halmashauri huwatumia kuziba mapengo wale waliohitimu na hawajapata ajira. Naishauri Serikali kufanya mawasiliano na Halmashauri zetu pale inapotaka kuajiri basi walimu hawa wanaojitolea katika mashule yetu wangepewa kipaumbele katika ajira mpya. Walimu hawa wameonesha uzalendo mkubwa, lakini ajira zinapotoka hawafikiriwi na hivyo kuwakatisha tamaa katika kuendelea kutoa mchango wao katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ya maabara, ili kuwa na Taifa lenye uchumi wa kati utakaoakisi uwepo wa viwanda nchini, ni ukweli usiopingika kuwa tunauhitaji mkubwa wa wanasayansi ambao ndio nguvu kazi za viwandani. Hivyo basi umuhimu wa kuwa na maabara za kisasa zenye vifaa vya kutosha ni mkubwa sana. Lakini hadi sasa kuna shule nyingi za sekondari nchini hazina vyumba vya maabara na pale ambapo vyumba vipo, vyumba hivyo havina vifaa vya maabara. Mfano katika Halmashauri yangu

ya Liwale katika shule za Mirina, Miruwi, Hangai Mlembwe, Mkutano, Nicodemus Banduka, shule zote hizo hazina vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya *VETA*; sekta hii ni muhimu sana kwa sasa ambapo nchi yetu inaelekea kuwa nchi ya viwanda. Hivyo basi naiomba Serikali kuja na sera itakayohakikisha kuwa kila Wilaya nchini inakuwa na shule au kituo cha *VETA*. Vituo vingi tulivyonavyo sasa vingine viko mbali sana na baadhi ya Makao Makuu ya Wilaya, hivyo wazazi wengi wanashindwa kupeleka vijana wao katika vituo hivyo. Mfano katika Wilaya ya Liwale ambayo iko umbali wa zaidi ya kilometa 300 kutoka Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi ambako ndiko kuna kituo cha *VETA*. Hivyo naiomba Serikali ifikirie kuwasongezea huduma hii wananchi hawa ambao wanaelekea kuachwa nyuma katika Taifa Iijalo Taifa la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine katika hili naishauri Serikali kuja na mitaala ya vyo hivi vya veta ili viweze kwenda na teknolojia ya kisasa, na hivyo kuwa nguvu kazi ya kutosha katika viwanda tunavyo vijenga. Kwani elimu inayotolewa sasa bado kwa kiwango kikubwa haiakisi na ujio wa viwanda vinavyo kuja na tekinolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu ya watu wazima, sekta hii ya elimu ya watu wazima kwa sasa inahitaji msukumo mpya kwani kuna kila dalili ya Taifa letu kuwa na ongezeko la watu wasiojua kusoma na kuandika. Hii inatokana na watu wengi kukosa elimu kwenye mfumo rasmi. Vituo vya elimu ya watu wazima kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya havipo kabisa na kama vipo basi havifanyi kazi kabisa. Hivyo naiomba Serikali kuja na msukumo maalum ili kukabiliana na janga hili linalolinyemelea Taifa letu la kuwa na idadi kubwa ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo mashuleni; sekta ya michezo mashuleni ni muhimu sana, michezo ni afya na michezo ni ajira. Hivyo basi naiomba Serikali kuimarisha



michezo mashuleni ili kusaidia kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali nchini. Katika hili ni lazima Serikali kuanza kuandaa walimu wenye taaluma ya michezo, kwani shule zetu nyingi hazina walimu wa michezo. Walimu hawa ni bora wakaandaliwa toka vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shule binafsi, kwa kuwa wazazi wengi hulipa ada kila robo ya mwaka, kwa robo hii ya pili wazazi hawajalipa ada hivyo kupelekea shule binafsi kushindwa kujiendesha na sasa walimu hawalipwi mishahara. Tunaomba Serikali iingilie kati kwa kuwapatia fedha wamiliki wa shule ili waweze kulipa walau mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi waliopata ujauzito kurudi shule, mmepokea fedha za *WB* kwa ahadi kuwa warudi shule lakini mpaka sasa hakuna mwongozo wa Wizara juu ya hili. Nataka kauli ya Serikali juu ya wasichana waliopata ujauzito kurudi shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtaala wa vyuo vikuu, Serikali itambue kwa mfumo uliopo sasa haumsaidii mhitimu kuwa mbunifu na kujijajiri zaidi unamtengeneza kutegemea kuajiriwa. Serikali ipitie upya mtaala tutengeneze watu watakaouza akili kuliko nguvu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kwa njia ya mtandao; dunia imeshahamia kwenye dijitali. Serikali ianze kufikiria namna ya kutoa elimu rasmi na isiyo rasmi (*VETA, SIDO*) kwa njia ya mtandao. Hii itaongeza shauku ya kujifunza na shauku ya matumizi ya kompyuta. Hebu fikiria tungekuwa tumeanzisha mfumo huu tangu zamani, huenda tusingekuwa tunaongea tunayoongea kwa kipindi hiki cha Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wa wanafunzi waliopo majumbani sababu ya Covid-19 kwa hatua ya dharura Serikali ipeleke *computer* na *photocopy machine*

walau kwa kila Mratibu Elimu Kata. Ofisi hiyo itoe nakala za mitihani na *reading materials*, zigawiwe kwenye shule zote na wazazi waitwe kufuata mashuleni wawapelekee watoto waweze kujisomea kwa kipindi hiki ili wasisahau masomo na kujikuta wanajiingiza kwenye tabia za ajabu. Watoto ni Taifa la kesho, ni gharama kubwa kuwapa maelezo bora lakini ni lazima tuinge gharama hizo ili kutengeneza Taifa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia TBC iongeze vipindi vingi vya masomo badala ya kuweka mambo ya kikubwa hasa mida ya mchana. Hiyo ni televisheni na redio ya wananchi lazima iwanufaishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara. Naomba nishauri katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Wilaya ya Ukerewe kama moja ya maeneo ya pembezoni, kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi hali inayoathiri ndoto ya Tanzania ya viwanda hasa kwenye eneo la Ukerewe. Nashauri kuwa katika mgao wa walimu ujao basi Wilaya hii ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashukuru kwa pesa zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi/upanuzi wa Chuo cha Ualimu Murutunguru. Naomba Wizara itoe kiasi kilichobaki ili mradi ule ukamilike na kuweza kutoa huduma kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, nashukuru pia kwa kutoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha *VETA* pale Ukerewe, niombe Serikali ihakikishe mahitaji yanayotakiwa ili chuo hiki kuanza kama nyumba za watumishi na vifaa viwepo ili mpango wa chuo hiki kuanza ifikapo mwishoni mwa mwaka huu uweze kufanikiwa.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waziri na Naibu Waziri wa Elimu na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kiwango cha kutukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, pongezi kwa kikosi kizima cha Chama cha Mapinduzi kikiongozwa na Mtendaji Mkuu Dkt. Bashiru na wasaidizi wake wote, uongozi mzima wa ngazi za juu na wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kustahili kupita kifua mbele popote ndani na nje ya nchi kwa kuwa na Ilani nzuri na iliyotekelezwa bayana na kwa kiwango cha mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mchango wa hoja na mafunzo kwa vitendo. Wanafunzi wa vyuo vya *DIT* na *MIST* waliopata fursa za mafunzo kwa vitendo ni 667. Ni vema idadi ya wanaopata fursa ikaongezeka. Kimsingi, wote wanaokuja na uhitaji huo kulingana na mafunzo yao wapate fursa hiyo. Miradi mikubwa yote itumike kwa mahitaji haya kwa utaratibu utakaowekwa. Serikali itenge fedha za kutosha lakini pia wenye viwanda na miradi wachangie gharama kwa kuwa wanafunzi hao licha ya kujifunza wanafanya pia kazi zinazozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi – *VETA*, umuhimu wa ujenzi wa vyuo hivi hauhitaji kurudiwarudiwa kuutaja. Nashauri Serikali itafute fedha za kutosha na iweke mtawanyiko bora zaidi wa fursa hii kwa Watanzania wote. Vyuo vya mikoa ni sawa. Vyuo vya Wilaya viangalie umbali kutoka chuo cha jirani. Kwa mfano Wilaya ya Tunduru ambayo ni ya pembezoni, kubwa kieneo pia ina ujirani wa Chuo cha *VETA* takribani kilometa 194 kule Namtumbo na zaidi ya kilometa 100 kule Mangaka, Masasi au hata kilometa 400 kule Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, haja ya kuboresha zaidi lengo la *training by objective* hususan katika kada za uhandisi; Serikali iimarisha utekelezaji wa lengo la Taifa kuwa na rasilimali watu mahiri katika uwiano bora. Kama

ilivyoelekezwa katika Dira ya Taifa 2025 na Ilani ya CCM kuwa uwiano wa Wahandisi, Mafundi Sanifu Uhandisi (*Engineering Technicians*) na Mafundi Stadi Uhandisi (*VETA graduates*).

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hotuba za 2018/2019 na 2019/2020 zote zina uwiano wa udahili unaosababisha uwiano uwe wa kuzalisha wahandisi wengi zaidi kuliko wasaidizi wao yaani *engineering technicians* na *artisans*. Nimesoma zaidi kwa vyuo vitatu, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha *MIST* na *DIT*. Kwa utendaji wenye tija zaidi kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani uwiano unapaswa kuwa au kuharibika 1:5:25 kwa mhandisi mmoja, *technicians* watano na *artisans* 25 ili tija ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha *ATC* kiko vizuri katika eneo hili. Vyuo vingine vielekezwe hivyo na vyuo vitizamwe kwa ujumla wake katika kuzalisha wataalam hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, udanganyifu katika mitihani ufuatiliwe kwa karibu katika ngazi zote za elimu na kuchukuliwa hatua stahiki kwa kuwa athari ya jambo hili katika uchumi na ustawi wa Taifa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika kuchukua hatua ni vema wahusika halisi wakapatikana na hao ndio wachukuliwe hatua kali. Pia katika ngazi ya shule za msingi uwekwe utaratibu wa kuzingatia umri wa watoto hao na uwezekano wa kushawishiwa kufanya kosa hili. Kuna taarifa ya baadhi ya watoto kupokea maelekezo kutoka kwa walimu wao wanaopenda sifa ya kufaulisha, wakati mwingine watoto hao ni wale wenye uwezo wa kufaulu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa kichunguzi ufanyike, wenye makosa dhahiri waadhibiwe lakini walioingizwa huko kwa kuwa *influenced* au kulazimishwa wasamehewe. Lakini pia kanuni iliyopo ya kuwaadhibu kwa kuwazuia kabisa kupata elimu katika mfumo rasmi wa Serikali uangaliwe upya. *Destiny* ya watoto hawa inafungwa milele kwa kuwa wengi hawawezi kuimudu *private route*. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru pekee ina wanafunzi wa

aina hii 173. Tunaomba Serikali ipitie upya. Ikiwa baadhi ya wahalifu watu wazima husamehewa kwa sababu mbalimbali, je, haiwezekani kuwafikiria watoto hawa?

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano na Baraza lake la Mawaziri kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 kwa kiwango kikubwa cha kuridhisha. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako na timu yake yote kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nina ushauri kidogo katika mambo yafuatayo kwa uboreshaji wa sekta ya elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kutokana na matokeo ya mitihani katika kidato cha nne kwa miaka mingi mfululizo tumeshuhudia kuanguka kwa kiwango cha ufaulu kwa vijana wetu toka katika shule za Serikali almaarufu shule za kata. Kwa uzoefu wangu mdogo katika elimu, moja ya kisababishi cha kutofanya vizuri kwa vijana hawa ni tatizo la lugha la kiingereza. Ushauri wangu kwa Wizara ni kuwa tuweke utaratibu wa kuwaweka vijana hawa darasa lingine kwa mwaka mzima kabla ya kuendelea na masomo ya sekondari baadae akimaliza darasa la saba, yaani tuwe na darasa la *pre-form one* ili tuyajengee msingi bora katika lugha ya kiingereza na hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kiwango cha Watanzania wasiojua kusoma wala kuandika kwa Tanzania kinaendelea. Sijaona Serikali kupitia bajeti hii ya elimu tunayojadili hakuna mkakati au mpango wowote kimkakati katika bajeti inayozungumzia elimu ya watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wilaya ya Malinyi ni miongoni mwa Wilaya zenye ufinyu mkubwa wa miundombinu ya mabweni au *hostel*/hususan kwa wasichana. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii walimu na TAMISEMI waiangalie Wilaya hii ya Malinyi kwa miradi ya ujenzi wa

mabweni au *hostel* kwani kwa Wilaya nzima ina shule moja tu yenye mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu wa dakika saba naomba kuishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali iwe na mpango wa kutafuta hela kujenga madarasa na nyumba za walimu kwa kuwa uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na kitengo cha wadhhibi ubora kwa ngazi ya Mkoa kwa sababu shule za sekondari za Serikali zimekuwa nyingi kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, utaratibu wa shule kongwe nchini utazame ili kuwa na uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja 100% na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Tate Olenasha, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu. Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kunateua katika nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka mitatu ambayo Mheshimiwa Rais ameniteua katika nafasi ya Naibu

Waziri katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia nimekuwa shuhuda wa mageuzi makubwa na mapinduzi ya kihistoria yaliyofanyika katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembea katika maeneo mengi ya nchi yetu na katika miaka hiyo nimeona sura ikibadilika kutokana na uwekezeji mkubwa ambao umefanyika katika Sekta ya Elimu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwaletea Watanzania maendeleo na hususan Watanzania wale wengi ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakipata changamoto za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushauri na maelekezo yao muhimu katika utendaji wangu wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia wewe pamoja na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima, busara na weledi mkubwa. Nashukuru pia Kamati inayosimamia Wizara yetu; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ambayo nimekaa Serikalini kama Naibu Waziri lazima nikiri kwamba hii ni moja kati ya Kamati bora kabisa ambazo nimewahi kuziona ambayo Wajumbe wake wengi wana uelewa mpana wa masuala ya elimu na kwa hakika wamekuwa ni washauri wakubwa. Mafanikio ambayo tunayo hatuwezi tukaacha kurasibisha na ushauri wao ambao wametupa kwa muda wote huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa uongozi wake thabiti, uongozi wa mfano ambao umefanya Wizara yetu iwe na mafanikio makubwa. Kule tunamwita mama, hana mchezo. Kwa kweli mafanikio ambayo tunayo ni kwa sababu ya uongozi wake

usiotetereka, lakini pia uadilifu mkubwa; eeh, mtu ambaye tunasema anaweka *cross* kwenye T na kuweka *dot* kwenye I, wewe ukiona kosa moja yeye anaona mia moja. Namshukuru sana, nimepata malezi makubwa sana chini yake, kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Prof. Ndalichako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mafanikio ambayo tunayo kwa kweli lazima tuseme ni kwa sababu ya kuwa na Katibu Mkuu Dkt. Akwilapo pamoja na Manaibu Katibu Wakuu Prof. Mdoe na Dkt. Avemaria Semakafu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Taasisi zake, hawa wamekuwa ni msaada mkubwa. Hatuwezi tukasema tuna mafanikio tukawasahau wao kwa sababu wao ndiyo watendaji wa kila siku. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini kwa vyovyote vile siyo kwa umuhimu, naishukuru sana familia yangu kwa upendo na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro kwa imani yao kubwa kwangu na ushirikiano ambao umesaidia Jimbo letu kupiga hatua kubwa katika kipindi kifupi cha Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache ya utangulizi naomba sasa nitumie muda uliobaki kujielekeza kwenye baadhi ya hoja ambazo zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge katika mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia pamoja na kwamba muda ulikuwa mfupi, lakini niseme tu kwa ujumla kwamba hoja zao zote tumezichukua, inawezekana tusipate muda wa kujibu yote, mengine tutayaleta kwa maandishi lakini naomba tu kwa muda niliopewa nijibu machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja imetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi tena kwa nguvu na msisitizo



mkubwa kuhusiana na mikopo ya elimu ya juu kwamba ibadilishiwe fungu badala ya kubakia kwenye fungu la sasa la 46. Hoja hii ambayo pia imezungumziwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hoja hii kimsingi imejishehenesha katika kusema kwamba mikopo siyo maendeleo, ni matumizi ya kawaida au basi ni *re-current expenditure*, kwa hiyo basi, haitakiwi ikae kwenye fungu la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kwamba utoaji wa elimu ya juu ni moja kati ya majukumu ya msingi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara inawajibika kusimamia shughuli za ugharamiaji wa elimu ikiwa ni pamoja na kuzalisha nguvu kazi muhimu inayohitajika katika shughuli mbalimbali za uzalishaji. Kwa hiyo, *human resource development* ni moja kati majukumu makubwa ambayo Wizara imekabidhiwa katika hati ya kiidhini. Kwa hiyo, suala la mikopo ni kitu muhimu sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu ifahamike kwamba Serikali katika miaka tokea Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ianzishwe imeshatumia shilingi trilioni 4.3 fedha ambazo imeshawasaidia Watanzania 529,466 kuweza kumaliza shahada mbalimbali za kwanza katika fani mbalimbali. Ni uwekezaji mkubwa katika nguvu kazi ya Taifa kwa sababu kama tunataka tujenge uchumi lazima tuwe na nguvu kazi yenye weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uwekezaji katika kuendeleza nguvu kazi kwa vyovyote vile haiwezi ikawa ni *recurrent expenditure*. Ni jambo la kimaendeleo kwa sababu Wizara na Serikali inaona kwamba bado ni muhimu kuendelea kuchukulia jambo hili kwamba ni la kimaendeleo. Kwa sababu hiyo tunaendelea kushauri kwamba fedha ya mikopo ibakie katika fungu la 46. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo imebuliwa tena kwa nguvu na kwa ushawishi mkubwa na Waheshimiwa Wabunge walio wengi ni hoja ya namna gani tunajaribu kuhakikisha kwamba elimu yetu inazingatia

masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Kwa kutambua umuhimu wa maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya utafiti na ubunifu kadiri ya uwezo wa mapato ya Serikali yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huu Serikali ilishaanzisha Mfuko Maalum unaoitwa Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (*MTUSATE*) ambapo kupitia Mfuko huu fedha hutengwa kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ya Watanzania. Mfuko huu unaratibiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) na hadi kufikia mwaka 2019/2020 jumla ya shilingi bilioni 50.55 zimeshatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu Serikali kwa mwaka wa pili sasa imekuwa ikiendesha mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (*MAKISATU*) kwa lengo la kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu na ugunduzi wa teknolojia mbalimbali unaofanywa na Watanzania hususan wale wa ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tokea mashindano yaanze mwaka 2019 jumla ya wabunifu wa teknolojia 1,036 wameibuliwa na kutambuliwa. Wabunifu mahiri kati yao 130 wanaendelezwa hivi sasa na Serikali ili ubunifu wao uweze kubiasharishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na changamoto zilizopo tayari Serikali inalifanyia kazi jambo hili na tayari kuna vijana wetu wabunifu mahiri kabisa wa sekta mbalimbali wanaendelezwa, wanapatiwa fedha kuna wabunifu 130. Tayari Mheshimiwa Mwijage alishatoa mfano wa Max Malipo, huyo ameshaenda kwenye *level* ya uzalishaji sasa huduma iko sokoni. Kuna wengine wengi wako kwenye *queue*, baada ya muda mtaona huduma mbalimbali ambazo zinatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii na jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea wako 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru kwa dhati tena kwa mara nyingine Kamati yangu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa mchango mzuri ambao wameutoa na kwa ushauri ambao wamekuwa wakiutoa. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Kivuli kwa hotuba yake Mheshimiwa Susan Lyimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa huu ni Mkutano wa mwisho, naomba nichukue nafasi hii tena kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipatia katika kipindi cha miaka mitano ambayo nimehudumu katika nafasi hii kama Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hakika Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na upendo mkubwa, wamekuwa na michango mizuri, nami nasema Mwenyezi Mungu awabariki sana katika malengo yenu yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Mawaziri wenzangu ambao Mheshimiwa Rais alitupa dhamana ya kumsaidia, hakika tumeifanya kazi hii kama timu kwa moyo wote chini ya Jemadari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akisadiwa na mama yetu shupavu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri Mkuu mchapa kazi na mfuatiliaji. Hakika tuliyoyafanya

Watanzania wanayaona na mafanikio ni makubwa, mwenye macho haambiwi tazama. Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano yanaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuzishukuru Taasisi za Elimu za Serikali na Zisizo za Serikali, lakini na wamiliki wa shule binafsi kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa katika miaka mitano, hakika tumefanya kazi vizuri. Nawashukuru kwa dhati Wahadhiri wote wa Vyuo Vikuu, walimu, wanafunzi, Serikali za Wanafunzi kwa ushirikiano ambao wamenipa, lakini pia kwa kujituma. Ndiyo maana tumeshuhudia hata viwango vya ufaulu vikiwa vinaongezeka mwaka hadi mwaka kwa sababu wamekuwa wakijituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunipa utulivu kwa upendo na kwa ushirikiano. Kipekee naomba nitoe shukrani za dhati kwa mama yangu mzazi ambaye pamoja na matatizo yake ya kiafya, lakini kwa kweli amekuwa ni nguzo muhimu kwangu. Amekuwa akiniombea na naweza nikasema kwamba maombi ya mama yangu yamekuwa ni nguzo kubwa kwangu kuniwezesha kusimama imara katika kazi yangu. Namwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee sina budi kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kigoma na hasa ndugu zangu wa Kasulu kwa upendo mkubwa ambao wamekuwa wakinionesha. Hakika ndugu zangu wa Kasulu wamekuwa wakinionesha upendo mkubwa, kwanza wamekuwa wakifuatilia kazi zangu ninazozifanya, wamekuwa wakinipa maoni na ushauri na naweza kusema wazi kwamba maoni yao na upendo ambao wamekuwa wanaufanya na kufuatilia kwao kazi kumenifanya niwe imara, nijitume na niwe na bidii zaidi katika kazi, na nawaaambia nawapenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa, naomba nijielekeze katika hoja na niwahakikishie

Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zenu zote zitajibiwa kwa maandishi kwa sababu ya muda, naomba nizungumze machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza na hili suala ambalo ni janga la kitaifa, suala la ugonjwa wa *corona* ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza. Kwa mara nyingine naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge jambo hili viongozi wetu, Rais wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akiliongea, lakini nami kwa nafasi yangu naomba niseme kwamba Serikali iko kazini, Serikali haijalala tangu ugonjwa huu umeingia, Serikali iko kazini kuhakikisha kwamba kwanza inatoa miongozo kwa Watanzania namna ya kujikinga na kujiepusha na maradhi haya ya *corona*. Pia Serikali inaendelea kufanya tathmini katika sekta zote ikiwemo na Sekta ya Elimu kuangalia madhara yanayosababishwa na virusi vya *corona* na Serikali itachukua hatua muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara yangu hatujalala, kwanza baada ya shule kufungwa tarehe 17 Machi, 2020 hatua ya kwanza ambayo kama Wizara ya Elimu tulichukua kwa ajili ya wanafunzi ilikuwa ni kuwezesha wanafunzi kuweza kupata machapisho kwenye Maktaba ya Taasisi ya Elimu Tanzania bila malipo. Kawaida ile maktaba ili iweze kupata machapisho ilikuwa inatakiwa kulipa hela, sasa kwa kutambua kwamba wanafunzi wako nyumbani, wanahitaji kusoma tuliondoa zile gharama za kupata *materials*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo narudia kusema kupitia Maktaba ya Taasisi ya Elimu Tanzania wanafunzi wanaweza wakapata vitabu vya kuanzia elimu ya awali, darasa la kwanza mpaka la saba, kidato cha kwanza mpaka cha nne mpaka kidato cha sita. Hata hivyo, tuliona hiyo haitoshi kwa sababu tunatambua wapo baadhi wanafunzi wanatoka katika maeneo yenye changamoto za mitandao kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hatua nyingine ambayo tuliifanya ni kuandaa vipindi kwa ajili ya televisheni na vipindi kwa ajili ya redio. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 20 Aprili, 2020, Wizara yangu imezindua rasmi vipindi vya redio na vipindi vya televisheni na tunashirikiana na TV mbalimbali kama vile *Azam Tv, Channel Ten, TBC*, pia tumefanya ushirikiano na redio za kijamii zaidi ya 34 na tuko tayari kuendelea kushirikiana na redio za kijamii kwa sababu tunatambua pia kuna changamoto ya usikivu. Kwa hiyo tumeweka katika mifumo mbalimbali na niwahakikishie kwamba tutaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akizungumza kwa Watazania, naomba nitoe hofu kwa wadau katika Sekta ya Elimu. Watu wamekuwa wakitumia ugonjwa wa virusi vya *corona* kutiana hofu na wapo watu ambao wamekuwa wakiwatia hofu wanafunzi, kwamba mtakapofungua shule tu mnakutana na mitihani. Naomba niwatoe hofu wanafunzi Serikali iko makini, Serikali inafuatilia kitu kinachoendelea na pia Serikali inaangalia wanafunzi watakaa muda gani. Baada ya Serikali kujiridhisha kwamba sasa hali ni shwari, shughuli zinaweza zikaendelea, mikusanyiko inaweza kuendelea, Serikali itakaa chini na kuangalia utaratibu ambao utatumika katika kuhakikisha kwamba tunafidia zile siku wasizoenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo napenda kuwaambia kwamba, hakuna cha mtihani siku ya kufungua shule, wala hakuna cha *test* siku ya siku ya kufungua shule bali Serikali itaweka utaratibu mzuri. Kwa hiyo, niwaombe wazazi, niwaombe wanafunzi sasa hivi elekezeni akili zenu katika kujikinga na virusi vya *corona*, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu mrudi shuleni mkiwa salama na tutaweka utaratibu mzuri, watu wasiwatie *pressure* bila sababu yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa kuhusiana na suala la *corona* ni suala la mchango ambalo Mheshimiwa Esther Mmasi amezungumza kwamba vipo baadhi ya Vyuo na Taasisi ambavyo

vinawaambia kwamba wafungue shule. Hii ni kinyume kabisa na maelekezo ya Serikali, aliyetoa tangazo la kufunga shule ni Waziri Mkuu na msemaji kuhusiana na suala la *corona*, tumeshapewa maelekezo kwamba aidha atakuwa ni Mheshimiwa Rais ama Waziri Mkuu, ama Waziri wa Afya, ni nani sasa ambaye ametoa maelekezo ya hivyo vyo ambavyo vimefunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi kama Serikali tutasimama kuhakikisha kwamba maelekezo ya Serikali yanazingatiwa na taasisi zote. Naomba wazazi mumpuuze mtu yeyote ambaye anatoa tangazo kuhusiana na maelekezo kuhusu *corona* kama siyo Rais, kama siyo Waziri Mkuu ama siyo Waziri wa Afya, naomba kabisa mumpuuze na huyu anayetoa hayo matangazo ashindwe na alegee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzngumzia suala la *corona*, naomba sasa pia nizungumzie suala la Mradi wa Benki ya Dunia. Nakumbuka suala hili nililizungumza wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini labda kwa sababu aidha, Waheshimiwa wengine hawakuwepo au kwa sababu zozote zile ni jukumu letu kuendelea kutoa ufafanuzi kadri ambavyo inahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Dunia kwa kukubali andiko la nchi yetu ya Tanzania la kuomba mkopo wa kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kuendeleza elimu ya sekondari. Kama ambavyo nilisema ndani ya Bunge lako na naomba nirudie kusema, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli inaheshimu mikataba na makubaliano ya kimataifa. Kwa hiyo, mkopo huo utatekelezwa kwa kuzingatia makubaliano yaliyopo, haiwezekani mtu akupe dola milioni 500 yaani hivi hivi tu, tulikuwa na andiko ambalo limewekwa, limechambuliwa, lina mashiko, wameridhika, wameidhinisha, tutapokea zile fedha, tutazisimamia kwa kuzingatia yale ambayo yameandikwa. Nirudie kwa mara nyingine kuwahakikishia Watanzania kwamba, tuko hapa kutoa elimu

kwa watoto wote, nchi hii haina ubaguzi. Kwa hiyo mkopo huu utaenda kunufaisha watoto wa kike na watoto wa kiume. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimrekebishe tu kidogo dada yangu Susan Lyimo, naona takwimu zake kidogo alijichanganya. Tunaposema fedha hizi zitanufaisha watu milioni 6.5 ni wale wanufaika wote wa mkopo ikiwemo wale ambao wanaenda katika utaratibu wa kawaida na wale ambao wanaacha shuleni na kurudi. Kwa hiyo, hii siyo namba ya watu wanaoacha shule bali ni namba ya watu ambao tunategemea ndani ya miaka mitano ya utekelezaji wa huu mkopo watanufaika na huo mkopo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwahakikishie kwamba hayo mambo ambayo watu wanayazungumza ni mambo mepesi mepesi tu kwamba sijui *statement* ya Waziri, *statement* ya Rais, mimi na Rais wangu tunawasiliana sana. Kwa hiyo, siwezi nikatoa *statement* ambazo zinapishana, tuna masiliano yaani *network* iko vizuri kabisa. Kwa hiyo, nilichokiandika na kilichokubalika ndicho ambacho kitatekelezwa na hata *statement* yangu someni vizuri, nimesema tutatekeleza kwa mujibu wa makubaliano, kama makubaliano hamyajui basi rudieni kusoma mara tatu, mara nne, lakini habari ndiyo hiyo, mkopo umepita, tutatekeleza kama ambavyo imekubalika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzia ni suala la uhaba wa Wahadhiri na kwamba Mheshimiwa Rais anachangia katika kuleta uhaba wa Wahadhiri kwa sababu anawateua Wahadhiri kwenda kushika nafasi mbalimbali Serikalini. Kwanza nadhani tungempongeza Rais wetu kwamba anatoa fursa yale ambayo wanakuwa wanayatoa darasani wanahubiri tukifanya hivi nchi itakwenda, anawapa nafasi ya kwenda kuyatekeleza. Sijaona tatizo lolote katika hilo kwa sababu unapooni kiongozi amefanya bustani yako ndiyo mahali pa kwenda kuchuma tunda, kazi yako wewe mtunza bustani ni kuimwagilia, kuiwekea mbolea ili hata kesho akitaka kwenda kuchuma tunda lingine akute matunda yameiva. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kazi yetu sisi kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunatoa ufadhili na ndiyo maana katika hotuba yangu nimesema kwamba Serikali inasomesha Wahadhiri 620; ambapo kati yao 196 wanalipiwa na Serikali wanasoma Shahada ya Uzamili na 424 wanasoma Shahada ya Uzamivu, ili kiongozi akitaka kuchuma tunda tena akute na hao wengine aje tu achume, yaani Mheshimiwa Rais aje hata kesho achukue, sisi tuko imara wala hatutatetereka na tutahakikisha kwamba hizi fursa ambazo anazitoa ili ile nadharia yao ikaingie Serikalini iende kwa vitendo, tusukume kwa kasi maendeleo ya nchi yetu, nadhani ni jambo jema na ni jambo la kupongezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la matumizi ya TEHAMA. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hii inafanya kazi katika kuhakikisha kwamba suala la TEHAMA tunalipeleka shuleni na mojawapo ya sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa *World Bank* ni kuendeleza TEHAMA katika shule za sekondari. Kwa hiyo, wakati mwingine watu wanakuwa wanapinga vitu, lakini hao hao ndiyo wanasema ni mahitaji, sasa Serikali imekaa, ikaandika andiko, limekubaliwa. Kwa hiyo mojawapo ya *component* ya ule mradi wa *World Bank* itakuwa ni kuendeleza masuala la TEHAMA katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunaendelea pia kuendeeza TEHAMA kupitia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mfuko wa Mawasiliano Sawa kwa Wote unatoa pia suala la TEHAMA shuleni na wanatoa mafunzo kwa Walimu, pia wanatoa vifaa vya TEHAMA shuleni. Kwa sababu siyo Wizara yangu na suala limejitokeza katika michango sina takwimu kamili, lakini nafahamu kwamba wameshafikia zaidi ya shule 500 na mwaka jana mimi mwenyewe nilikuwa mgeni rasmi katika kufunga mafunzo kwa Walimu zaidi 1,500 wa shule za msingi na sekondari ambayo walifadhiliwa na Mfuko wa Mawasiliano Sawa kwa Wote. Kwa wanapokuwa wanaingalia Serikali waiangalie kwa mapana yake, siyo mtu anaangalia tu bajeti ya TAMISEMI, halafu kwa sababu hajaona kwenye bajeti ya TAMISEMI, anasema ndiyo hapo

hapo, Serikali ina taasisi nyingi, kwa hiyo unapotaka kuangalia jambo angalia katika taasisi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara ya Elimu tumefanya kazi kubwa na kama ambavyo nimeeleza kwenye hotuba yangu katika kuhakikisha kwamba tunawaandaa Walimu katika masuala ya TEHAMA kwa sababu mwisho wa siku tukipeleka TEHAMA shuleni lazima tuwe na Mwalimu ambaye tumemwandaa, huko tunafanya vizuri na umeona takwimu ya vifaa vya *computer, servers* ambazo tumeweka nadhalika ambavyo tunaweka kwa ajili ya kuwaweka vizuri. Kwa hiyo, suala la TEHAMA shuleni linafanyika na litaendelea kufanyika kwa kasi kubwa kupitia Mradi wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la Mapinduzi ya Viwanda na Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanataka kuona ni jinsi gani kama nchi tumejipanga kukabiliana na mapinduzi ya nne ya viwanda. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali iko makini na taasisi zetu zinafanya vizuri katika kuhakikisha kwamba zinakuwa zinajifunza hata kupitia kwa taasisi nyingine kwanza, taasisi zetu nyingi zina ushirikiano na taasisi za nje, pia na zenyewe ziko mbele katika kuhakikisha kwamba zinaangalia machapisho.

Kwa hiyo, hatuko nyuma, kwenye suala la mapinduzi ya nne ya viwanda tayari kuna taasisi zetu zimeanza kutoa kozi kwa mfano Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam inazo kozi ambazo zinaiandaa nchi katika mapinduzi ya nne ya viwanda, Taasisi ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia - Mbeya na vyo vingine. Kwa hiyo, sana sana tunachotakiwa kufanya ni kuongeza kasi ili tuweze kutoa fursa nyingi zaidi na ukienda kwa mfano kama Nelson Mandela, ukienda *DIT* tayari hata tunayo *super computer* ambayo zote hizo zinachangia katika kufanikisha masuala ya *Fourth Industrial Revolution*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo nimeona nilitolee ufafanuzi hapa ambalo liliongelewa nafikiri

na Mheshimiwa Nuru Bafadhili, kuhusiana na vitabu ambavyo Serikali ilikuwa imeviondoa lakini vinatumika shuleni. Vitabu vilivyoondolewa shuleni mwaka 2017 vyote viliteketezwa, sasa kama kuna mtu ameenda kuvifukua, ameenda kuchukua majivu au amevipata kwa namna yoyote hiyo, hiyo ni kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mheshimiwa Nuru Bafadhili anisaidie, kama tunaweza tukapata ushahidi wa mahali gani vinatumika, basi huyo anayefanya hivyo ni mhalifu kama wahalifu wengine, anastahili kuchukuliwa hatua kwa sababu vitabu hivyo ni batili na ili vitabu vitumike shuleni kuna taratibu zake. Kwa hiyo naomba sana niwahakikishie kwamba Serikali iko makini, tulivyosema tunaondoa vitabu, haiwezekani tuwe na Serikali hiyo hiyo ivirudishe vitabu kwa mlango wa nyuma, hivyo vile vitabu ni batili, havipaswi kutumika shuleni kwa sababu ambazo Serikali tayari ilishazieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia hatua ambazo zilichukuliwa kuhusiana na wafanyakazi ambao kwa kweli waliidhalilisha Serikali kwa kuandika vitabu vya ajabu ajabu. Tunafahamu kwamba nchi yetu inaendeshwa na utawala wa sheria na mtumishi anapewa haki ya kusikilizwa. Kwa hiyo, hatua zilizochukuliwa ziliendana na uzito wa makosa baada ya watumishi kupewa nafasi ya kujieleza. Kwa hiyo, kama mtumishi ambaye labda anaonekana pengine alishiriki inawezekana labda kulikuwa hakuna uthibitisho wa moja kwa moja kama yeye ndiye aliyechangia makosa katika kitabu ambacho kipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia hayo ni mambo ambayo ni suala la kiutaratibu na mtumishi anaruhusiwa kukata rufaa. Nafahamu hata hawa watumishi walishakata rufaa na wameshindwa. Kwa hiyo, kama mwingine ambaye labda anaona ameonewa, nishauri tu afuate zile taratibu za kiutumishi, lakini kama Serikali tusingeweza kuwahukumu watumishi wote bila kuwapa fursa ya kuwasikiliza, bila kuchambua maelezo yao na kuona sasa nani mwenye hatia na nani ambaye hana hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele imeshalia, kwa hiyo naomba nihitimishe hoja yangu kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, hakika limekuwa ni Bunge zuri, tumekaa vizuri na naamini tutaendelea kukaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kwa heshima kubwa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Fungu 18 na Fungu 46 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana.

### HOJA ZA KISERA

**NAIBU SPIKA:** Sasa ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanahitaji ufafanuzi wa mambo mbalimbali kwenye mshahara wa Waziri, mambo ya kisera, Mheshimiwa Mary Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo. (*Makofi*)

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Vyuho vya Ualimu katika nchi yetu ikiwemo cha *Korogwe TTC*, tuna wafanyakazi wa kawaida, tuna Walimu katika vyuo, lakini tuna Wakufunzi. Sasa wapo ambao wanaitwa Walimu wana miaka kumi wengine hadi 20, lakini wako Walimu ambao wamekuja, wametoka vyiuni wamekuja pale kufundisha, wanaitwa Wakufunzi, hata miaka minne anaitwa Mkufunzi, lakini huyu aliyekaa miaka

10, 20 na ameweza kupata mafunzo ya aina mbalimbali, semina mbalimbali, bado anaitwa Mwalimu. Sasa napenda nipate ufafanuzi lini sasa mtafanya angalau marekebisho ya muundo angalau hao watu wamekwenda miaka 10, 20 wanazeeke, wanakutwa na vijana wanaitwa Wakufunzi wao bado wanaitwa Walimu, lini sasa mtarekebisha muundo huo ili angalau na wenyewe waweze kuitwa Wakufunzi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nimshukuru dada yangu Mary Chatanda, mpambanaji wa Korogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake kuhusiana na muundo kwamba wengine wanaitwa Walimu na wengine Wakufunzi niseme kwamba labda ni swali mahususi zaidi kuliko la kisera, lakini itoshe tu kumwambia kwamba Mheshimiwa nimelipokea na tutaenda kulifanyia kazi ili tuweze kuangalia kikwazo kiko wapi na kama kuna marekebisho ya kufanyia kwa ujumla ni kwamba tumelipokea na Serikali tutaenda kulifanyia kazi. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda niungane na wachangiaji wenzangu kumpongeza Waziri Mama Ndalichako kwa kazi nzuri anayoifanya, Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo dogo ambalo natakiwa nipate ufafanuzi na kwa hatua iliyofikiwa kwa kweli inahitaji huruma ya mama Ndalichako. Mwaka 2019 ni kama miaka mingine kule nyuma ambapo wanafunzi wa darasa la saba wamekuwa wakifanya mitihani ya kumaliza elimu yao ya msingi.

Sasa kumejitokeza sintofahamu katika mwaka 2019, baadhi ya wanafunzi walifanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, lakini walifutiwa matokeo ya mtihani katika Mkoa wetu wa Ruvuma limejitokeza hilo na naomba nitolee mfano shule moja Shule ya Msingi Muungano ambapo wanafunzi 103 wamefutiwa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo hili limeleta sintofahamu kwa wazazi na wanafunzi wenyewe. Naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Wizara na kama nilivyosema kwa hatua iliyofikia linahitaji huruma ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu ili asaidie wale watoto waweze kuendelea na masomo. Nafahamu kwamba jambo hili si jambo geni limewahi kujitokeza huko nyuma na njia mbalimbali zimeweza kutumika pengine kurudi kuwasaidia wale watoto kufanya mitihani upya. Bahati nzuri nilimwona Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nilimwona; naomba nipate ufafanuzi tunafanyaje katika kuwasaidia wale watoto ili waendeleo na masomo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ni kweli kwamba Mheshimiwa Chikambo amekuwa akifuatilia suala hili tena kwa bidii kubwa. Napenda wapiga kura na wananchi wake wafahamu kwamba amelifuatilia mara nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi na udanganyifu katika mitihani ni kosa katika mfumo wetu wa elimu. Mara nyingi athari zake kwa kweli zinawezekana zisipendeze sana lakini ndio sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanafunzi anayepatikana kufanya udanganyifu katika mitihani ya darasa la saba sheria yetu imeweka wazi kwamba adhabu pekee iliyopo ni kumfutia yaani ku-*nullify* kana kwamba hajafanya mtihani na hakuna *remedy* nyingine. Kwa hiyo,

ikigundulika kulikuwa na udanganyifu, kwa mfano, wanafunzi wamekutwa wakibia mtihani, adhabu yake ni kwamba wale wanafunzi ule mtihani itachukuliwa kama hawajafanya, hawana matokeo na hawataweza kuendelea na shule za sekondari za Serikali. Isipokuwa watapata vyeti vyao vya darasa la saba yaani *certificate* ile ya kumaliza darasa la saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaweza wakaendelea katika shule za sekondari za za binafsi. Kwa hiyo, tungependa sana kumsaidia na kwa vyovyote vile Serikali ina huruma lakini tunaangalia vilevile athari ambazo zinaweza zikatokea tukiendelea kuruhusu udanganyifu katika mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ukiacha hiyo adhabu ambayo imetolewa kwa wanafunzi lakini Serikali vilevile inaendelea kuwafuatilia wahusika wote ili sheria iweze kuchukua mkondo wake. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo kutokea Msekwa.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini niseme kwamba baadhi ya majibu hasa ya Waziri hata hayajaniridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na hoja moja. Wabunge wengi sana wamezungumzia suala zima la *Corona* na jinsi gani Wizara itasaidia shule za *private* lakini Waziri ameliruka kabisa kama vile halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna zaidi ya wafanyakazi/walimu 90,000 kwenye sekta binafsi lakini tuna na wafanyakazi ambao wote wanategemea ada na shule zilifungwa mwezi wa tatu ambapo wanafunzi hawa au wazazi wanalipa ada kwa *quarter* au kwa *term*. Sasa tayari walishalipwa labda mpaka mwezi wa tatu, mwezi huu wa nne na kuendelea ndio hivyo haijulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara baada ya kuona tatizo hili na hasa ikizingatiwa kama alivyosema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mwijage kwamba hawa watoto ni wa Serikali ya Tanzania, hizi shule ni kama walezi tu na kwa sababu tayari imetolewa tangazo, haijulikani hili tatizo litaisha lini, nilitaka kujua wana mpango gani wa muda mfupi na wa haraka wa kuwasaidia? Tukisema na watumishi wengine siyo sahihi. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi kwa mfano hospitali binafsi, ndiyo kipindi ambacho wanaweza wakapata hela nyingi sana kwa sababu hata hizi barakoa tumevaa zinauzwa ghali, kwa hiyo, wanapata hela lakini hii ni kutoa huduma wanategemea ada za wazazi. Kwa hiyo, nataka kujua ni mpango gani Serikali inakuja nao kuwasaidia hawa wafanyakazi na waajiri wa shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na kama sitaridhika nitaomba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Susan Lyimo amesema kwamba katika majibu yangu sikueleza labda pengine bahati mbaya tu hakusikia lakini nadhani hili suala nimelieleza vizuri na ilikuwa ni hoja ya kwanza kuitolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kusema ambacho nilikisema kwamba suala la athari ambazo zinajitokeza katika sekta ya elimu kutokana na ugonjwa wa *Corona*, Serikali inafanya tathmini ya athari katika sekta zote. Ndiyo jibu ambalo nililisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema kwamba katika kuangalia hizi athari Serikali itazingatia maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, majibu ndiyo hayo kwamba Serikali inafanya tathmini ya athari katika sekta zote na pia itazingatia maoni na ushauri wa Wabunge. Nimeeleza vizuri zaidi kwamba jambo hili lina wasemaji.



Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili kutoka Ukumbi wa Msekwa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi niliulizia kuhusu wale wafanyakazi wa taasisi walioachishwa kazi na Mheshimiwa Waziri alijaribu kuniambia vigezo vilivyotumika. Hata hivyo, CAG alipofanya ukaguzi aligundua kwamba Mwongozo wa Tathmini ya Ukaguzi wa Vitabu kutoka Taasisi ya Elimu haukuzingatiwa. Je, wale waliosimamishwa kazi Serikali au Wizara inawafikiriaje kuwapa angalau kitu kidogo kwa sababu wameondoka kama walivyokwenda na ndivyo walivyorudi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Nuru Bafadhili kwa kuendelea kufuatilia na kuhakikisha kwamba haki za wafanyakazi zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia ukaguzi wa CAG na suala la Mwongozo lakini hapa tunazungumzia hatua zilizochukuliwa kwa watu ambao waliandika vitabu vyenye makosa ambavyo humu Bungeni ilikuwa kila mtu anacheka, ni makosa ambayo yako wazi kabisa. Kwa hiyo, taratibu za kiutumishi zilizingatia kwamba umesomea ni taaluma yako na ni vitu ambavyo kwa kweli ilikuwa ni *gross negligence* ambayo ilijitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la haki na stahiki za watumishi, mtumishi yeyote anapoachishwa kazi, anapoacha kazi yeye mwenyewe kuna haki zake za kiutumishi ambazo zimeainishwa katika Mwongozo wa Utumishi wa Umma na Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, napenda tu kuwasihia watumishi wafuate sheria na Kanuni ambazo zipo ili waweze kupata haki zao kwa sababu

hata ukiniambia mimi Waziri lakini na mimi ninabanwa na sheria, kanuni na taratibu. Kwa hiyo, kwa kutumia hizo sheria, kanuni na taratibu kama kuna mtu ambaye anastahiki na hakupata stahiki yake, nawasihi watumishi ni haki yao waweze kuzingatia taratibu ili haki yao isije ikapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Suala nililotaka ufafanuzi limefafanuliwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, sina haja tena ya kuendelea kutaka ufafanuzi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tutamalizia na Mheshimiwa Oscar Mukasa, kutokea Msekwa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mimi suala langu lipo kwenye ubunifu. Nimefurahia majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Mfuko wa Ubunifu lakini na idadi kwamba watu kama 130 hivi wamefuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba ufafanuzi namna gani tunatoka kwenye ubunifu kwenda kwenye sera na kutumia. Tuna mfano pale Nelson Mandela (*non-filter*) imepata *certification* ya WHO na kwingine duniani lakini imekaa pale na ina *potential* kubwa ya kusaidia nchi hii. Tuondoke kwenye kuwasaidia kwa ngazi ile ya chuoni tupeleke kwenye mfumo wa viwanda na mazingira ya sera tutatue matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo yake kuhusu namna ya ku-link kinachotokea pale na *policy environment* na viwanda, tutumie tuondokane na matatizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Mukasa amekuwa akisisitizia kwa muda mrefu tu kuhusiana na umuhimu wa kutoka kwenye hatua ya kutamia *innovation* kwenda kwenye hatua ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mukasa kwamba Serikali inatambua kwamba ukiachia *innovation* ibakie kwenye hatua ya kutamia inawezekana isiwe na msaada sana katika jamii. Kwa hiyo, Wizara kitu ambacho imefanya ni kwamba Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) imekuwa ikiwaunganisha wabunifu pamoja na viwanda, wafanyabiashara na watu wengine ambao wanaweza wakaingia nao ubia ili kuweza kuwapeleka kwenye hatua ya pili sasa ya kwenda kwenye *production* badala ya kuishia kwenye *prototypes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumekuwa tukijaribu kuhakikisha kwamba wakati tunawaunganisha na wafanyabiashara na viwanda haki miliki zao zinalindwa. Kwa sababu kuna wengine ukishamuunganisha unakuta ananunuliwa na haki yake ile inapotea na wafanyabiashara wakubwa na viwanda vinachukulia kwamba wenyewe ndiyo wamefanya ile *innovation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tayari Serikali inawaunganisha na wazalishaji wakubwa. Shukrani sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa ufafanuzi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu zetu nimeangalia hapa Wabunge ambao wamekwisha kupiga kura idadi yao ni kubwa na wengi wamesema ndio kwa bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Kwa namna hiyo Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa

mwaka wa fedha 2020/2021 imepitishwa rasmi na Bunge.  
(Makofi)

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha  
2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 46 – Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia.....Sh. 491,049,151,000

Fungu 18 – Tume ya Taifa  
ya UNESCO.....Sh. 2,239,181,000

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 46 – Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia.....Sh. 857,514,224,000

**NAIBU SPIKA:** Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji walio chini yenu kwa kazi nzuri mnayoifanya. Mmepata pongezi nyingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge lakini pia Kamati imetambua kazi nzuri mnayoifanya, kwa hiyo, nawapongeza sana. (Makofi)

Pia niishukuru Kamati kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuisimamia Wizara hii na kwa ushauri wao ambapo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekiri kwamba Kamati ya Bunge inafanya kazi nzuri ya kuwashauri mambo mbalimbali ambayo yamewasaidia katika kuboresha utendaji kazi wao. Kwa hiyo, tunawashukuru Kamati. (Makofi)

Vilevile tunawashukuru Wabunge ambao wameshiriki kutoa michango yao, naamini yale mengine ambayo yalikuwa ni mapendekezo yatafanywa kazi na upande wa Wizara na yataweza kutusaidia sisi kama Taifa kusogea mbele.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji wa haya ambayo mmetuahidi mnaenda kuyafanyia kazi baada ya Bunge hili kuridhia makadirio haya ambayo mmeyaleta mbele yake. Tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji.

Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili; la kwanza ni la kifupi tu kuhusu *Corona* na uvaaji wa hizi barakoa. Mimi siyo daktari wa binadamu lakini nawaona Waheshimiwa Wabunge wengi wengine wanashusha hapa halafu anairudisha tena. Sasa ukishashusha hapa na sisi ni kioo cha jamii, ukaanza kuzungumza watu wanafikiri unaweza kushusha ile halafu ndiyo uanze kuzungumza.

Kimsingi ukivaa barakoa maana yake unataka kumlinda yule unayezungumza naye lakini hata anayezungumza na wewe. Kwa hiyo, usitoe barakoa ama kama unaitoa basi fuata utaratibu ule wa kuitoa barakoa. Toa kutokea nyuma kwa sababu hapa mbele hutakiwi kuwa unaigusa ukishavaa. Ukishavaa barakoa usiiguseguse hapa mbele unaipandisha, unataka kushusha kwa sababu sasa kama ni kweli imeingia hivyo virusi maana yake wewe mwenyewe unajiambukiza badala ya kukulinda inakuwa tayari unaeneza wewe mwenyewe.

Kwa hiyo, kama mtu anatoa, atoe kutokea nyuma kwenye hizi kamba na siyo hapa mbele kuishika na kuishusha kidevuni. Huo ndiyo uvaaji wa barakoa. Kwa hiyo, tuzivae vizuri ili zitusaidie. Nadhani elimu itaendelea kutolewa.

Kwa wale wanaovaa barakoa zinazoitwa *surgical masks*, nadhani kwa sasa tumeshajua angalau ni zipi, hizi ambazo upande wa ndani ni nyeupe upande wa nje ni za *blue*, hazitakiwi kuvaliwa kuanzia asubuhi mpaka jioni na unaongea kila wakati. Kwa sababu unakuwa umeshaitumia kwa muda, kwa hiyo, imeshapata unyevu. Sasa usije ukapata jambo lingine ambalo hukulikusudia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukumbuke ule muda ambao wataalamu wetu wanatushauri kwamba hizi ambazo kwa ndani ni

nyeupe, kwa nje ni za *blue* usivae kwa muda mrefu sana hasa wewe ambaye unaitumia hapa Bungeni kwa sababu muda mwingi unakuwa unazungumza kwa hiyo inaweza kupata unyevu.

Waheshimiwa Wabunge, hilo lilikuwa ni la jumla tu kuhusu matumizi ya hizi barakoa. Niwaombe sana, yule anayeona hawezi kuzungumza na barakoa basi aitoe kwa kamba huku nyuma ili awe ametoa vizuri kama wataalamu wetu wanavyotushauri.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa ya Mheshimiwa Spika hapa nayo ni taarifa kuhusu kifo cha Mbunge wa zamani wa Jimbo la Peramiho, Dkt. Damas Mbogolo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anachukua fursa hii kuwataarifu kifo cha Mheshimiwa Mbunge wa zamani wa Jimbo la Peramiho, Dkt. Damas Mbogolo ambaye amefariki tarehe 22 Aprili, 2020 katika Hospitali ya Peramiho Songea. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, Dkt. Damas Mbogolo alikuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1985 mpaka 1995 ambapo baada ya yeye Mbunge aliyefuatia ni Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi na sasa ni Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

Wakati akiwa Mbunge, Dkt. Damas Mbogolo aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango na pia Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku. Aidha, kwa nyakati tofauti aliwahi kufanya kazi zifuatazo: Alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Kamishna wa Uchumi na Mipango, Ofisi ya Rais; Kamishna wa Sensa ya Taifa; na Mwanzilishi wa Taasisi ya *Wilima Community* ambayo ilizaa Sekondari ya Wilima.

Aidha, baada ya kustaafu, Dkt. Damas Mbogolo alikuwa ni Mhadhiri katika Vyuo Vikuu vya Dodoma na SAUT, Tawi la Songea. Marehemu Dkt. Damas Mbogolo ambaye kitaaluma ni Mchumi atazikwa kesho siku ya Jumamosi tarehe

25 Aprili, 2020 katika Kijiji cha Wino, Jimbo la Madaba. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa nane kamili mchana.

*(Saa 11.57 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 27 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*